

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Arobaini na Sita – Tarehe 15 Juni, 2020

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae, tunaendelea na Mkutano wetu wa 19, Kikao cha 46, bado kimoja tu cha kesho. Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2020 (*The Finance Bill, 2020*).

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 (*Monetary Policy Statement for the Financial Year 2020/2021*).

MHE. ALBERT N. OBAMA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2020 (*The Finance Bill, 2020*).

**MHE. RHODA E. KUNCHELA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA
KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA
NA MIPANGO:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya fedha wa mwaka 2020 (*The Finance Bill, 2020*).

**MHE. DKT. TULIA ACKSON - MAKAMU MWENYEKITI WA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KANUNI ZA BUNGE:**

Azimio la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kanuni za Bunge kuhusu Marekebisho ya Kanuni za Bunge

SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Naibu Spika, Katibu

MASWALI NA MAJIBU

(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtando)

Na. 426

Migogoro ya Mipaka

MHE. MARIAM N. KISANGI aliuliza:-

Kumekuwepo na migogoro mingi ya mipaka katika ngazi za Mitaa, Kijiji, Kata, Wilaya na hata Mkoa hali inayosababisha maeneo husika kutotambua vizuri wakazi wake:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura 287, Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura 288 na Sheria ya Mipango Miji, Na.8 ya mwaka 2007 zimeweka utaratibu wa kuzingatia wakati wa kuanzisha na kusimamia Maeneo ya Utawala (Mitaa, Vijiji, Kata, Wilaya na hata Mikoa). Utaratibu huo, pamoja na mambo mengine, unahusisha kuandaa Matangazo ya Serikali (*Government Notice-GN*) yenyenye maelezo ya mipaka ya ardhi ya kila eneo la utawala hasa wakati wa uanzishaji wa mamlaka hizo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kumekuwepo na changamoto kadhaa ikiwemo: Kutotafsiriwa vyema matangazo hayo ya Serikalini ardhini jambo linalosababisha wananchi kutotambua vizuri mipaka hiyo na hivyo kuleta migogoro na wananchi kutozingatia ipasavyo mipaka kama ilivyobainishwa kwenye Matangazo ya Serikali. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inapitia na kuboresha Mwongozo wa Uanzishwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2014 ambao utapaswa kuzingatiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zote wakati wa kuanzisha maeneo mapya au kupandisha hadhi maeneo ya utawala.

Mheshimiwa Spika, katika utaratibu huo, kusudio la kuanzisha eneo jipya la utawala (Kijiji, Kata, Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa au Jiji) lililojadiliwa na vikao stahiki lazima liambatane na Rasimu ya Ramani inayoinishwa mipaka ya kijirofia ya mamlaka inayopendekezwa kuanzishwa pamoja na rasimu ya ramani ya mamlaka inazopakana nazo. Aidha, ili kuondoa migogoro, uhakiki wa ramani hizo uwandani utafanyika kabla ya Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kutoa kibali cha uanzishaji wa mamlaka hizo.

Mheshimiwa Spika, katika Mamlaka za zamani (zisizo mpya), Serikali kuitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeendelea kutatua migogoro ya mipaka kwa kuitia na kutafsiri ardhini Matangazo mbalimbali ya Serikali yaliyoanzisha Wilaya na Mikoa husika na kuondoa mkanganyiko wa mipaka. Pia, Ofisi ya Rais, TAMISEMI

inaandaa mfumo wa usajili wa maeneo ya utawala kwa njia ya kielektroni unaoitwa *Administrative Areas Registration System-AReS* ambao utazuia mwingiliano (*overlapping*) wa mipaka na hivyo kupunguza migogoro.

Na. 427

Hitaji la Gari la Wagonjwa Kituo cha Afya Bwisya

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA aliuliza:-

Kituo cha Afya cha Bwisya kilichoko Kisiwani Ukara kimekarabatiwa kwa kiwango kikubwa na kuwa na hadhi ya hospitali; Serikali iliahidi kupeleka gari la wagonjwa toka mwaka juzi lakini bado gari hilo halijapelekwa:-

Je, ni lini gari la wagonjwa litapelekwa katika Kituo hiki?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Kamilembe Julius Lwota, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kulingana na mazingira ya kituo hiki, kuna hitaji la usafiri kwa ajili ya wagonjwa kutoka kisiwa cha Ukara kwenda maeneo mengine hususan Hospitali ya Nansio ambayo iko kwenye Kisiwa cha Ukerewe. Kwa kuwa visiwa hivi vimetanganishwa na maji, Serikali imeona umuhimu wa kutengeneza *boat ambulance* mpya kwa ajili ya Kisiwa cha Ukara badala ya kununua gari. Boti hiyo imekamilika na inatumika.

Na. 428

Mradi wa Maji wa Lwakajungu – Karagwe

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI aliuliza:-

Mradi wa maji Ziwa Lwakajungu uliopo Wilayani Karagwe, Mkoani Kagera unaoanza Kata ya Bweranyange mpaka Nyashozi ulianza tangu mwaka 2005 lakini mpaka sasa hakuna jitihada zinazoonekana:-

Je, ni lini Serikali itawapatia wananchi hao maji ya uhakika na kuwatua ndoo kichwani wanawake wa wilaya hiyo?

WAZIRI WA MAJI aliibuu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Alfredina Apolinaria Kahigi, Mbunge wa Viti Maalum, Kagera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya India imeingia Mkataba wa Mkopo wa masharti nafuu kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maji na Usafi wa Mazingira katika miji 28 ukiwemo Mji wa Kayanga/Omurushaka ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe. Mwezi Mei, 2019 Wizara ya Maji iliingia Mkataba na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina wa miradi katika miji hiyo ukiwemo Mji wa Kayanga.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa taratibu za manunuzi ya Wakandarasi zinaendelea ambapo ujenzi wa miradi unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2020. Mradi huu utakapokamiliika unatarajiwa kunufaisha wananchi wapatao milioni nne kwa kuanzia na wananchi milioni sita ifikapo mwaka 2040 katika miji 28.

Na.429

Uchakavu wa Mitambo – Skimu ya Maji Makonde

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA aliuliza:-

Skimu ya Maji ya Makonde inakabiliwa na tatizo kubwa la uchakavu wa mitambo na umeme usio wa uhakika na hivyo kushindwa kusambaza maji hadi Mji wa Nanyamba.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo?

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, eneo la Mamlaka ya Maji Makonde ina jumla ya watu 510,975 wenyewe mahitaji ya maji mita za ujazo 766,462 kwa mwezi. Maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya maji yana wakazi wapatao 275,928.00 wenyewe mahitaji ya maji mita za ujazo 413,892 kwa mwezi sawa na asilimia 54 ya mahitaji ya wakazi wote wa Mamlaka ya Maji Makonde. Miundombinu iliyopo inaweza kuzalisha maji mita za ujazo 482,400 kwa mwezi kiasi ambacho kinakidhi mahitaji ya watu wote waliofikiwa na mtandao wa maji.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji na matengenezo, uwekezaji umepangwa kuelekezwa kwenye chanzo cha Mitema kwani chanzo hicho kina gharama za umeme nafuu zaidi katika uzalishaji maji na uwezo wa chanzo hiki ni mkubwa kuliko vyanzo vingine na unaotosheleza mahitaji ya wakazi wote na kijiografia kiko katikati ya eneo la Mamlaka ya Maji Makonde.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wananchi wanaoishi maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka ya Maji Makonde wanapata huduma ya maji, Serikali kuititia Wizara ya Maji ikishirikiana na Wadau wa Maendeleo imetoe kipaumbele katika uboreshaji wa huduma ya maji katika Mamlaka hiyo. Katika kipindi kilichoanzia mwaka 2015 hadi 2020, miradi yenye thamani ya Shilingi 13,436,000,000 imetekelizwa na miradi mingine inaendelea kujengwa.

Aidha, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni jitihada za kukabiliana na tatizo la uchakavu wa mitambo, miundombinu na umeme usio wa uhakika kwa kufanya marekebisho ya mitambo iliyopo pamoja na kutoa kipaumbele katika matumizi ya nishati jadilifu na hatimaye kupunguza gharama za uendeshaji kwa wananchi.

Na. 430

Hitaji la Baraza la Ardhi la Wilaya

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI aliuliza:-

Wilaya ya Busega haina Baraza la Ardhi na hivyo kupelekea kesi za ardhi za wilaya hiyo kupelekwa wilaya za jirani: -

Je, ni lini Busega watapatiwa Baraza la Ardhi la Wilaya?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hadi sasa imeunda jumla ya Mabaraza 111 ambapo kati ya hayo, Mabaraza 55 yanatoa huduma na Mabaraza 56 hayajaanza kutoa huduma kutokana na changamoto za uhaba wa rasilimali watu na majengo ya ofisi. Ili Baraza liweze kutoa huduma linahitaji kuwa na jengo la ofisi pamoja na watumishi, yaani angalau Mwenyekiti wa Baraza mmoja, Katibu Muhtasi, Msaidizi wa Kumbukumbu, Msaidizi wa Ofisi, Dereva na Mlinzi.

Mheshimiwa Spika, taratibu za ajira kupata watumishi zitakapokamilika, wananchi wa Wilaya ya Busega watapewa kipaumbele kwa kufungua Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ili kuondokana na adha ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya liliopo Maswa. Aidha, natoa rai kwa uongozi wa Wilaya ya Busega waweze kuandaa na kutoa jengo litakalofaa kutumika kwa matumizi ya Ofisi ya Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya, tukiwa tunasubiri upatikanaji wa watumishi wa kuhudumia Baraza hilo.

Na. 431

Upatikanaji wa Chanjo ya Mama na Mtoto – Katavi

MHE. TASKA R. MBOGO aliuliza:-

Katavi ni Mkoa wa mwisho katika upatikanaji wa chanjo kwa mama na mtoto:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha akinamama na watoto wa Mkoa wa Katavi wanapata chanjo.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekuwa ikinunua na kusambaza chanjo kwa ajili ya mikoa, halmashauri na vituo vyote hapa nchini kulingana na idadi ya walengwa katika maeneo husika. Wizara imeendelea kusambaza chanjo katika Mkoa wa Katavi na mikoa yote nchini ili kuhakikisha kuwa akinamama na watoto wanakingwa dhidi ya magonjwa yanayozuulika kwa chanjo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikinunua chanjo za *Tetanus Toxoid (TT)* kwa ajili ya kuwakinga mabinti wa umri wa kuzaa na wanawake wajawazito dhidi ya ugonjwa wa pepo punda. Aidha, chanjo mbalimbali za kuwakinga watoto na magonjwa yanayozuulika kwa chanjo zimekuwa zikinunuliwa, ikiwemo chanjo ya *Pentavalent* kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya donda koo, kifaduro, uti wa mgongo na homa ya ini; *PCV-13* kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya nimonia na uti wa mgongo; *BCG* dhidi ya ugonjwa wa kifua kikuuu; *BOPV*na *IPV* dhidi ya ugonjwa wa kupooza; *MR* dhidi ya ugonjwa wa surua; *rubella Rota* dhidi ya ugonjwa wa kuhara na *HPV* dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi kwa

wasichana wa umri wa miaka 14. Katika mwaka 2019, Mkoa wa Katavi ulitoa chanjo kwa watoto 38,468 na wajawazito 43,665 ikiwa ni kiwango cha asilimia 100 na hivyo kuzidi lengo la uchanjaji kimko.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma za chanjo ni kipaumbele cha kwanza cha Wizara ya Afya, Serikali ya Awamu ya Tano ambapo kwa mwaka 2019/2020 imetenga jumla ya shilingi bilioni 30 ili kuboresha upatikanaji wa chanjo katika maeneo mbalimbali hapa nchini ukiwemo Mkoa wa Katavi. Aidha, kupitia Bunge hili, Serikali inawaagiza Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kuhakikisha usambazaji wa chanjo unafanyika kwa wakati na kwa kiwango cha kutosheleza mahitaji ya vituo vyote vya kutolea huduma za afya ili kuwakinga akinamama na watoto wachanga wote pamoja na mabinti wote wanaofikisha umri wa miaka 14 dhidi ya magonjwa mbalimbali yanayozuillika kwa chanjo.

Na. 432

Changamoto ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu

MHE. GRACE V. TENDEGA aliuliza:-

Kumekuwa na changamoto kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu kupata mikopo ya elimu ya juu:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto hizo?

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wahitaji na wenye sifa wanapata mikopo hivyo kutimiza ndoto zao za kupata elimu ya juu na

kushiriki katika shughuli za maendeleo ya Taifa kikamilifu. Ili kutimiza dhamira hiyo, Serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya fedha za mikopo ambayo imeongeza idadi ya wanufalka kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, bajeti ya fedha za mikopo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 348 mwaka 2014/2015 hadi kufikia shilingi bilioni 450 mwaka 2019/2020 ambayo imeongeza idadi ya wanufalka kutoka jumla ya wanafunzi 101,036 mwaka 2014/2015 hadi wanafunzi 130,072 mwaka huu 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongeza bajeti, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imeendelea kuimarisha utendaji ikiwemo kuboresha mifumo ya TEHAMA na kuendesha programu za elimu ya uombaji mikopo kwa usahihi kwa wanafunzi wa shule za sekondari ili kuongeza uelewa wao. Kwa mfano, kati ya mwezi Aprili – Juni, 2019, programu hizi zillendeshwa katika shule mbalimbali nchini na katika Kambi zote 17 za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ambapo jumla ya wanafunzi 46,669 walifikiwa. Programu hizi zinatarajiwा kuendeshwa tena kuanzia mwezi Aprili – Juni mwaka huu 2020 na zitahusisha shule za sekondari, vyuo vya stashahada, Kambi za JKT na watoa huduma za intaneti ambazo hutoa huduma kwa waombaji mikopo.

Mheshimiwa Spika, lengo la jitihada zote hizi ni kuhakikisha wanafunzi wanafahamu sifa, vigezo na utaratibu wa kuwasilisha maombi ya mikopo kwa usahihi ili wale wote wenye sifa wapate mikopo na kutimiza ndoto zao za kupata elimu ya juu kama Serikali ilivyolenga wakati wa kuanzisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Na. 433

**Ujenzi wa Barabara ya Kinyanambo – Rujewa Kwa
Kiwango Cha Lami**

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA aliuliza:-

Kumekuwa na ahadi nyingi za ujenzi wa barabara ya kutoka Kinyanambo “A” – Isalavano – Sadani – Madibira mpaka Rujewa.

Je, ni lini ujenzi wa barabara hii muhimu utaanza?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kinyanambo Ä"- Isalavano – Sadani – Madibira mpaka Rujewa yenye urefu wa kilomita 152 ni barabara ya mkoa inayosimamiwa na Wizara kuitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mikoa ya Iringa na Mbeya. Barabara hii inayounganisha Mikoa wa Iringa (Kinyanambo) na Mikoa wa Mbeya (Madibira) ni ya kiwango cha changarawe na inapita katika maeneo muhimu yenye kilimo cha mahindi na mpunga.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) imefanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami. Kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina na kuandaa nyaraka za zabuni tayari imekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, barabara hii imetengewa kiasi cha shilingi milioni 3,380 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii imeendelea kutenga fedha za matengenezo mbalimbali ambapo katika mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya shilingi milioni 215.940 zilitengwa na katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya shilingi milioni 829.268 zimetengwa ili kuhakikisha barabara inapitika majira yote ya mwaka.

Na. 434

Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Mbinga - Mbamba Bay

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO aliuliza:

Mhe. Rais, Dkt. John Magufuli wakati wa kampeni katika Jimbo la Nyasa, Kata ya Lituhi, aliahidi akiingia madarakani ifikapo mwezi Aprili, 2016 bababara ya Mbinga – Mbamba Bay itajengwa kwa kiwango cha lami:-

(a) Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

(b) Kwa kuwa barabara ya Chiwindi – Mbamba Bay hadi Lituhi ni barabara iliyoko mpakani, Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Sikudhani Yassin Chikambo Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mbinga - Mbamba Bay yenye urefu wa kilometra 65 ni sehemu ya barabara kuu ya Songea – Mbinga - Mbamba Bay ambayo ina jumla ya kilometra 165. Kati ya urefu huu, Serikali imekwishakamilisha ujenzi wa kilometra 100 kwa kiwango cha lami kutoka Songea hadi Mbinga. Aidha, kwa sehemu ya Mbinga – Mbamba Bay, Mkandarasi yupo katika eneo la mradi anaendelea na kazi ya ujenzi. Hadi mwezi Machi, 2020, kazi ya ujenzi ilifikia asilimia 54 na mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo Januari, 2021.

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara za Chiwindi – Mbamba Bay na Mbamba Bay – Lituhi ni barabara ya mpakani. Baada ya Serikali kulitambua hilo, tayari imeanza maandalizi ya kujenga barabara hizo kwa kiwango cha lami. Hadi Aprili, 2020, Wizara ya Ujenzi kuititia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANRAODS*), imekamilisha upembuzi yakinifu,

usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa sehemu ya Mbamba Bay – Lituhi. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2020/2021 barabara ya Chiwindi – Mbamba Bay hadi Lituhi imetengewa jumla ya Shilingi bilioni 1,317.45 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ili iweze kupitika majira yote ya mwaka.

Na. 435

**Barabara ya Mwasonga – Tundwi – Songani Hadi
Kimbiji (Km 48)**

MHE. LUCY S. MAGERELI aliuliza:

Barabara ya Kibanda – Mwasonga – Tundwi Songani hadi Kimbiji katika Wilaya ya Kigamboni imekuwa katika mipango ya bajeti ya Serikali toka mwaka 2016/2017 kwa kujengwa kwa kiwango cha lami:-

Je, ujenzi wa barabara hiyo upo katika hatua gani na ni lini utakamilika?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Lucy Simon Magereli, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*)imekamilisha usanifu wa kina kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kibada – Mwasonga - Tundwi Songani hadi Kimbiji (kilomita 48) mwezi Julai, 2019. Nyaraka za zabuni kwa ajili ya manunuzi ya Mkandarasi wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami zinapitiwa na wataalam wa Wizara yangu ili kujiridhisha kabla ya kutangaza zabuni.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2019 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Ahsante sana; Katibu ameshatusomea shughuli ambayo tunaiendea ambayo ni hoja za Serikali. Nilitaka kuwaambia tu mapema kabla sijamuita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha kwamba leo tuna shughuli nyingi kweli kweli kwa pamoja.

Kwa hiyo, naomba ushirikiano wenu kabisa ili tuweze kuzitendea haki na siku ya leo iweze kwenda kama ilivyopangwa ili tutoe na nafasi ya kesho pia kwenda kama ilivyopangwa. Kwa hiyo, mambo ni mengi lakini kwa pamoja tunaweza. Moja kwa moja nimuite sasa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, robo saa, baada ya hapo mtoa hoja nusu saa.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kukushukuru sana wewe kwa kunipa fursa hii njema kwa ajili ya kuchangia hoja iliyowekwa Mezani na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyetuwezesha kufika siku hii ya leo na tunaweza kuhitimisha hoja hii ya Serikali ndani ya kipindi chetu cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, kwasababu ya muda naomba niende moja kwa moja kwenye hoja na nianze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa hoja kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani ambayo walijitahidi sana

kulipotosha Bunge lako pamoja na wananchi wetu kwa ujumla. Naomba niweke sawa ili Watanzania waelewe nini tunafanya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na jemedari na mzalendo namba moja, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja yenye walieleza, na kwa ufupi naomba ninukuu maneno yao machache, walisema Mpango wa II wa Taifa wa Maendeleo umefeli kwa kuwa tuko kwenye mwaka wa mwisho wa utekelezaji wake ikiwa malengo makubwa hayajafikiwa hata kwa robo. Wakaendelea kusema, lengo kuu la Mpango wa II lilikuwa ni kuhakikisha Tanzania inaingia katika uchumi wa kipato cha kati. Serikali iwaambie wananchi ni viashiria gani vya uchumi wa kipato cha kati vimeanza kuonekana ikiwa fursa na ajira kwa wafanyabiashara na wakulima zimebanwa.

Mheshimiwa Spika, hii hoja imepotoshwa kwa kiwango kikubwa sana. Nasema imepotoshwa kwanza kwa pointi ya kwanza kabisa, lengo kuu la Mpango wa II wa Maendeleo halikuwa kulifikisha Taifa letu kwenye uchumi wa kipato cha kati. Hili naomba Watanzania waelewe waziwazi, kwamba lengo la Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati lipo kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2020 - 2025.

Mheshimiwa Spika, Dira ya Maendeleo ya Taifa inatekelezwa kupitia mipango mitatu ya maendeleo ya miaka mitano mitano. Mpango wa kwanza tumeutekeleza kuanzia mwaka 2011/2012 hadi mwaka 2015/2016, na dhima yake kuu ilikuwa ikisema ni kufungulia fursa *features* za ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano tumeliona Taifa letu likifunguka kwa miundombinu ambapo ndilo lilikuwa lengo kubwa. Taifa letu limeunganishwa.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka Mheshimiwa Rais wetu akiwa Waziri wa Ujenzi aliwahi kuwaambia Watanzania anapomaliza kazi yake kama Waziri wa Ujenzi, mtu atasafiri

na *saloon* carkutoka Ruvuma hadi Kagera, na yaliwezekana. Kwa hiyo, kwa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo tulifanikiwa kwa asilimia 100, na Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kuwaaminisha Watanzania kwamba hatukufika hata asilimia 50 ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Pili wa Maendeleo tumeanza kuutekeleza mwaka 2016/2017 hadi tutakamilisha 2020/2021. Dhima yake ni nini; sivyo kama wanavyojaribu kupotosha Taifa letu. Dhima kuu ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochaea mageuzi ya kiuchumi na maendleo ya watu. Hili ndilo lengo kuu la Mpango wa Pili wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana; juzi ulisema kwa miaka mitano mlimi na Mheshimiwa Waziri wangu tumejaribu kufundisha darasa la uchumi ndani ya Bunge lako Tukufu na ninaona limeeleweka kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Spika, ninasema limeeleweka kwa sababu safari hii mwanzo mwisho hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani hawakuongelea Serikali ya vitu, tumeelewesha vizuri sasa wameelewa maana ya Serikali ya vitu ni nini na Serikali inayojali wananchi ni nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dhima hii ya Mpango wa Pili wa Maendeleo Serikali yetu imefanya makubwa, na viashiria wanavyojaribu kuuliza kwamba tuwaeleze Watanzania ni vishiria gani basi vyta uchumi wa kipato cha kati ambavyo Taifa letu limeanza kufikia. Nitaje viashiria viwili tu ambavyo ni viashiria vyta kimataifa. Kiashiria cha kwanza ni wastani wa pato la mwananchi (*per capita income*) la mwananchi mmoja mmoja la kiwango cha kati ya Dola za Marekani 1,026 hadi 3,995.

Mheshimiwa Spika, wapi Watanzania tupo; pamoja na kwamba bado tuna miaka sita ya kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa letu hadi mwaka 2025, sasa hivi wastani wa pato la mwananchi mmoja ni Dola za Kimarekani 1,021.

Mheshimiwa Spika, tumbakiza dola ngapi kuingia kwenye pato la uchumi wa kati? Tumbakiza dola tano tu. Bado tuna miaka sita ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo. Kwa hiyo niwaambie wapinzani hoja hakuna, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli anachapa kazi na Watanzania wameelewa hizi dola tano ni imani yangu kwa usimamizi imara wa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi mwaka mmoja uliobaki wa utekelezaji wa Mpango wetu wa Miaka Mitano tutazikamilisha dola hizi tano ili kuliingiza taifa letu katika taifa la kipato cha uchumi wa kati. Hivyo naomba Watanzania waendelee kuchapa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumemuelewa sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli katika jambo hili na sote Watanzania tunachapa kazi. Hao wanaosema kwamba hawana mlo mmoja maisha hayafanani, hata nchi zillizoendelea Marekani wapo wananchi wanalala na mlo mmoja na wengine wanalala njaa. Kwa hiyo, wala hilo tusishangae lakini tumepeiga hatua kubwa ya kimaendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kiashiria cha pili ambacho nataka waelewe, na Watanzania wameelewa – naamini ni Kambi Rasmi tu ya Upinzani ndiyo ambayo hajiajewa, Watanzania wameelewa. Kiashiria cha pili ambacho kinatolewa na *Human Development Index*, tunaondoka sasa kwenye namba tunakwenda kwenye hali halisi ya utoaji huduma ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nini tumefanya, na huduma zinazotajwa katika *Human Development Index* ziko nne; ya kwanza ni ubora wa huduma za afya, ya pili ni ubora wa huduma za elimu, ya tatu ni ubora wa huduma za maji. Ndiyo viashiria vitatu ambavyo tunatakiwa tuangalie kwenye maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nini Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, chini ya Dkt. John Pombe Magufuli tumefanya; kwa ufupi tu naomba niseme kwa upande wa afya tumewafikia Watanzania. Tumewafikia Watanzania

kwasababu tumeweza kuboresha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya. Mheshimiwa Waziri wa Afya, dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu amekuwa akieleza vizuri; vifo vimepungua. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo wala halihitaji kuingia darasani ni jinsi Taifa letu lilivyopambana na janga la *COVID-19*. Bila huduma bora za afya tungeumia sana lakini hii inaashiria kwamba tumefanya kazi kubwa na tukirudi kwenye takwimu kama wachumi tunaangalia namba, nini tumefanya.

Mheshimiwa Spika, tumeweza kujenga zahanati 1,198 kwa muda wa miaka minne ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Wananchi wamefikiwa angalau kila kata ina zahanati moja, kila tarafa ina kituo cha afya. Hizi ndiyo *Human Development Index* zinazomuelezea Mtanzania kwamba amefikiwa na huduma za afya. Kwa mara ya kwanza tunaona Taifa letu likijenga hospitali 71; nini tunataka Watanzania? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, huduma za operesheni zinatolewa mpaka vijiini kwasababu umeme umefika, nishati ya umeme imefika na sasa tumewafikia Watanzania kule walipo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu nini tumefanya; Serikali yetu imeendelea kugharamia utoaji wa elimu msingi bila malipo ambapo kwa miaka hii minne tayari tumetoa shilingi trilioni 1.03. Na tunaona ufaulu umeongezeka wa darasa la saba, ufaulu umeongezeka wa kidato cha nne, vijana wetu wanaojunga chuo kikuu wanapata mikopo yao kwa wakati kwa hiyo, zile hoja zao za kudandia kwa vijana wa vyuo vikuu zimepotea. waseme nini sasa? (*Makofii*)

WABUNGE FULANI: Hakuna. (*Vigelegele*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, hakuna wanachoweza kutueleza Watanzania. Chama Cha Mapinduzi chenye Serikali imara na ambacho ndani ya

miaka 50 ijayo tutaendelea kuistaajabisha dunia. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za maji, ameleeza vizuri Mheshimiwa Waziri wangu wa Fedha, kwamba kwa mijini tumefika asilimia 70.1, kwa vijiji ni tumefika asilimia 84; haya yamewezekana. Tusipotoshe sana, mtu anaposimama kwamba kwenye jimbo langu, hilo unaongelea sehemu moja ndani ya Taifa lenye majimbo zaidi ya 380. Tuangalie *in its generality* nini Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imefanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumewafikia akina mama, zile hoja za wale watu tunaowafahamu wakieleza kwamba akinamama wanapoteza muda mwingi sasa kwenda kuchota maji, hilo halipo sasa. Nitoe mfano mmoja; unaifahamu Kondoa, Kondoa sasa hatuna shida ya maji, maji yamefika maeneo yote, ni imani yangu na kule Kongwa ndani ya mwaka mmoja ujao hatutakuwa tena na shida ya maji, tutamalizia kwa uhalisia wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu katika hoja yao hii haina mashiko, Watanzania wamemuelewa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na kazi njema imeweza kufanyika. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye hoja nyingine ambayo pia walijaribu kupotosha; kazi yangu ni kunyoosha kulikopotoshwa, Mheshimiwa Waziri atajibu hoja nyingine. (*Makofii/Vigelegele*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walishangilia)

MBUNGE FULANI: Nyoosha, nyooosha! Wanyooshe hao.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, walikuja na hoja kwamba Serikali imekuwa haitoi taarifa kuhusu pato la wastani la Mtanzania mmoja mmoja. Hii ni aibu kubwa kuja kupotosha Bunge Tukufu kama hili tuliloaminiwa na Watanzania.

WABUNGE FULANI: Waambiee!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Walieleza wazi kwamba kwa mwaka 2018 nini kimefanyika wakasema kwa mwaka 2019 hadi wanaandaa taarifa yao pato la wastani la Mtanzania lilikuwa halijaelezwa wazi.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze nini tumefanya Serikali ya Awamu ya Tano; tunapowasilisha Mpango wa Maendeleo ambao tayari Mheshimiwa Waziri wa Fedha alishauwasilisha tangu mwezi Machi tulishaeleza, na ninaomba waende kwenye Kitabu cha Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2020/2021 ukurasa wa sita katika aya ya 2.2.3.2, nini Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imewaeleza Watanzania, hatuna cha kuficha kwa sababu tunajua kilichofanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulisema yafuatayo; katika kitabu chetu tukasema kwa mwaka 2019 pato la Taifa kwa bei za miaka husika lilikuwa shilingi 139,893,804 ikilinganishwa na shilingi 129,043,901 kwa mwaka 2018.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Malizia tu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hakuna cha kuficha kwa sababu tuna uhakika nini tunafanya ndani ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniamini kwa miaka mitano. Leo naweza kukamilisha ndani ya hotuba hii na ninauona utukufu wa Mwenyezi Mungu kuititia imani hii ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ya kuniamini katika utendaji wangu wa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie wapiga kura wa Kondoa, walimsikia vizuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kasema, wamewasikia vizuri Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wamesema tuliyoyafanya Kondoa ndani ya

miaka mine, ni sawa na yaliyotendeka Tanzania na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ndani ya miaka minne. Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi amesema, wanaokwenda kwenye Majimbo yenyewe watu makini wajitafakari kwanza kabla hawajashika fomu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru sana familia yangu, mume wangu mpenzi Dkt. Muhamid Kachwamba, amekuwa ni nguzo kubwa kwangu. Amesimama nami kwa miaka yote, kwa nguvu zote na ninamtakia mema. Naijua dhamira yake na jamaa wale wa *Bukoba Town* wanajua nini anakwenda kufanya. Tunaweletea kifaa, atatenda kwa nguvu zake zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana tena Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuweza kutuonesha Watanzania kwamba yeye ni mchumi. Nitashangaa sana Vyuo Vikuu vya Tanzania visipompattia Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli Shahada ya Udaktari ya Heshima ya Uchumi. Amedhihirisha yeye ni mchumi. Mataifa yote yametetereka kiuchumi kwenye janga hili, yeye hajatetereka na bado tumesimama imara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa wana-Kongwa, kaka yangu Mheshimiwa Job Ndugai yuko makini. Wamemtikisa ndani ya Bunge hili kwa uimara wake na kwa busara yake. Nami nitakuja kule Jimboni; sitarajii na hakuna mtu atakayechukua fomu kwa ajili ya Jimbo la Kongwa. Utarudi kwa kishindo tuendelee kuwatumikia Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa hii adhimu. Naendelea kumshukuru Mheshimiwa Waziri wangu, amenilea, nimekomaa sasa, tuko tayari kwa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge, makofi hayo hayatoshi. Ahsante sana baada ya utumishi uliotukuka. (*Makofi*)

Sasa kabla sijamwita Mto Hoja, Waheshimiwa Wabunge ninao wageni kwenye *Gallery* yangu na *Gallery* ya upande wangu wa kulia. Hawa sio wengine isipokuwa kwenye *Gallery* yangu pale ni Viongozi wa Klabu ya Yanga. Naomba msimame Viongozi wa Yanga. Kwa upande wa *gallery* yangu ya kulia ni wachezaji na baadhi ya viongozi pia wa Klabu ya Yanga. (*Makofi/Vigelegele*)

Karibuni sana hapa Bungeni. Karibuni sana, tunafurahi sana kuwa nanyi, hili ni Bunge lenu. Sasa mnaweza mkakaa. Waheshimiwa Wabunge wanauliza tu mchezaji mmoja, sijui nani! Sijui anaitwa Moson sijui! (*Kicheko/Makofi*)

Naomba asimame Morrison. Yupo? Yupo eeh! Hayupo bwana! Hayupo, hayupo. Basi naomba Waheshimiwa Wana-Simba, hebu wasalimieni, wapeni salamu kidogo kwa makofi. (*Makofi/Kicheko*)

Hizo ni salamu tu kwa Yanga kwamba ule mkuki mmoja ule tunaukumbuka sana. Mtakapokutana tena na Simba mjiaandae kisawasawa maana itarudi mikuki kadhaa. (*Kicheko/Makofi*)

Karibuni sana Yanga, karibuni Klabu ya Wananchi. Karibuni sana Bungeni kwenu. (*Makofi/Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, pitisha bakuli. (*Kicheko/Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa moja kwa moja nimkaribishe Mto Hoja, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango. Karibu sana Mheshimiwa.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, tarehe 11 Juni, 2020 niliwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2019, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2020/2021 na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka ujayo wa fedha, 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kuendesha mjadala huu vizuri sana na mjadala huu utahitimishwa hivi leo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutambua michango iliyotolewa na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Kawe kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni upande wa Wizara ya Fedha na Mipango na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza au kwa maandishi hapa Bungeni. Ninawashukuru wote kwa michango yenu.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Wabunge 98 wamechangia hoja niliyowasilisha, na kati ya hao 87 wamechangia kwa kuzungumza na 11 kwa maandishi. Naomba niseme kwa niaba ya Serikali, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mliyoitoa juu ya Bajeti hii ya Serikali ambayo mnawakilisha maoni ya wananchi wenu. Nawashukuru pia wananchi wote ambao walitoa maoni na ushauri juu ya Hotuba hii ya Bajeti ya Serikali kupitia majukwaa mbalimbali na vyombo vyahabari.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kabisa kuwa hoja na michango mbalimbali iliyotolewa kwa siku hizi tatu na Waheshimiwa Wabunge ni vigumu kuzifafanua zote kwa muda wa nusu saa. Hivyo, kama ilivyo ada, napenda kuliahidhi Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itatoa ufanuzi wa kina wa hoja zote na tutaziwasilisha kwa maandishi kupitia kwa Katibu wa Bunge kwa ajili ya rejea ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, napenda pia, nitumie nafasi hi kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kufafanua vizuri hoja ambazo zilihusu sekta wanazozisimamia.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba uniruhusu nianze kufafanua hoja tatu muhimu, halafu nitaendelea na nyingine.

Kwanza kulikuwa na suala kuwa mapato ya *TANAPA, TAWA* na Ngorongoro kukusanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania na kupelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Hoja ilikuwa kwamba, Serikali ifafanue nia hasa ya uamuzi huu ni nini? Kwa kuwa, hatua hii inakuja kipindi ambacho mamlaka hizi zimeathiriwa kwa kiwango kikubwa na ugonjwa wa *Covid-19*; mapato yake yameshuka, lakini kwa miaka ya nyuma wamekuwa na ufanisi mkubwa katika ukusanyaji wa mapato yao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na athari za *Covid-19* ambazo ziliathiri uendeshaji wa hizi taasisi, *TANAPA, TAWA* na Ngorongoro, taasisi hizo hazina uwezo tena wa kutekeleza majukumu yake ya msingi ya uhifdahi na kudhibiti ujangili kwa kutumia mapato yao ya ndani. Kutokana na changamoto hiyo, Serikali imechukua hatua ya makusudi kuzinusuru hizi taasisi kwa kuziweka kwenye kipindi cha mpito kupitia Bajeti ya Msajili wa Hazina na tulitumia kasma inaitwa *Parastatal Rehabilitation/Contingent Liabilities*.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huo unatokana na ukweli kwamba *Corona* ilijitokeza baada ya mchakato wa maandalizi ya bajeti kwa mwaka ujao wa fedha kukamilika na hivyo, ilishindikana kujumuishwa kwenye bajeti ya Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo ni Fungu 69. Katika kipindi cha mpito tutafanya mapitio ya bajeti yake na kuwasilisha mapendekezo ili tuweze kujumuisha bajeti za hizo taasisi kwa mujibu wa matakwa ya Kifungu cha 43 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na pia Kifungu cha 12(7) cha Kanuni za Sheria ya Bajeti. Serikali pia itahakikisha kuwa taasisi hizo zinaendelea kutekeleza majukumu yake kisheria bila kuathiri ufanisi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Wabunge wanisikilize vizuri. Utaratibu ambao unapendekezwa unalenga kuhakikisha uendelevu wa shughuli za uendeshaji wa taasisi hizo, ikiwa ni pamoja na ulipaji wa mishahara kwa watumishi wa mamlaka zote za uhifadhi, shughuli za uhifadhi na miundombinu yake na pia kuhakikisha kwamba, utalii unaendelea vizuri pale panapotokea majanga kama

ilivyotokea kwa *Covid* na pia madhara ya mvua nygingi ambayo yaliharibu miundombinu. Haya yote yalisababisha kuwa nje ya hizi mamlaka tatu ambazo tunazzungumzia.

Mheshimiwa Spika, sasa hatua hiyo inalenga kwanza kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya taasisi hizo. Kwa hiyo, tutaziunga na mfumo wa *GePG*, lakini pia tutakwenda kutumia mifumo ya Serikali kwa ajili ya ku-audit hii mifumo ya ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, lengo la pili ni kusimamia vizuri zaidi matumizi ya mamlaka za hifadhi ambayo kwa kupitia kaguzi mbalimbali ambazo tumefanya yameonekana yana upungufu mkubwa sana. Lengo lingine ni kusimamia idadi kubwa ya watumishi walioko kule kwenye taasisi hizi, takribani watumishi zaidi ya 3,000. Ni muhimu kwamba mamlaka husika iweze pia kusimamia ajira ya mamlaka hizi kwa maana ya Idara Kuu ya Utumishi.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapoanzisha utaratibu huo, Hazina, Wizara ya Maliasili na Utalii na Mamlaka za Hifadhi zenyewe zitakaa pamoja kuandaa taratibu za kuhakikisha kwamba shughuli nyeti za uhifadhi hazikwami. Kwa hiyo, shughuli kama *operation* za dharura kukabiliana na ujangili, hizi zote na shughuli nyingine fedha zake zitakuwa *ring fenced*; tutazilinda.

Mheshimiwa Spika, tunafanya hivyo, kama ambavyo tunafanya pia kwa ajili ya vyombo vya ulinzi na usalama vingine vyote ambapo posho zao kwa ajili ya shughuli maalum zinalindwa. Utaratibu huu siyo mpya, ndiyo unaotumika Mamlaka ya Mapato Tanzania; Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*TAA*)na inatumika kwa ufanisi. Kwa hiyo, ufanuzi ulioombwa ndiyo huo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ilikuwa kuhusu janga hili la *Covid-19* kwamba limekuwa na athari kwenye utekelezaji wa bajeti ambayo tunaimalizia sasa na bajeti inayokuja. Kwa kuwa, Bunge lilipitisha mpango na ukomo wa bajeti mwezi Desemba na ugonjwa huu haukuwepo, angalau

katika nchi yetu, kwa hiyo, ilishauriwa kwamba kuna haja ya kufanya tathmini na mapitio ya mafungu ya bajeti tuliyoyapitisha ili kuweza kufanya *internal reallocation* kuakisi uhalisia.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe ufanuzi kwamba, hotuba yangu ya Bajeti nilieleza kwamba tulifanya tathmini ya kiuchumi kati ya Januari na Aprili mwaka huu 2020 na ilionesa kwamba nchi yetu hajaathiriwa sana na ugonjwa huu wa *Corona*, ikilinganishwa na Mataifa mengine. Ni muhimu nieleze pia kwamba kwa mujibu wa uchambuzi wa kiuchumi uliofanywa na *OECD*, ile hatua ya kuwafungia watu ndani illathiri sana ukuaaji wa uchumi kwa takribani asilimia 20. Ndiyo *OECD* wanavyoonesha. Ila kwa upande wa Tanzania tunachoona; nilijaribu kueleza kwenye hotuba ile ya bajeti, hatuoni hizo athari zikiwa ni kubwa kama hii Taarifa ya *OECD* inavyooneshwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nilieleza kwamba, kwa mfano, tukiangalia mapato ya ndani kwa ujumla, kwetu sisi badala ya kupungua, yameongezeka kutoka shilingi triliioni 6.3 mpaka triliioni 6.8 katika kipindi hicho. Vile vile nilisema utoshelevu wa chakula katika nchi bado uko vizuri kwa asilimia 118. Mauzo ya dhahabu yaliongezeka kutoka takribani shilingi bilioni 743.8 hadi shilingi triliioni 1.5 ukilinganisha na mwaka 2019 na 2020. Sekta ya kibenki ambayo nchi nyingi ndiyo zinaathirika zaidi na ugonjwa huu, sisi tunaona imeendelea kuwa imara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, haya ambayo yamebainika kwenye tathmini tuliyofanya kwamba madhara hapa Tanzania siyo makubwa hivyo, kwa kweli yanatokana na maono ya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ambaye alizua *lock down* kwa kuwa haiendani kabisa kabisa na maisha ya wananchi wetu ya kila siku katika kujitafutia kipato kukidhi mahitaji yao na familia zao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Balozi Kamala alifafanua kwa umahiri kabisa hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali ili kupunguza kasi ya uchumi wetu kudorora na

nileleza vizuri kwamba hatua zilizochukuliwa na Serikali ni kupunguza kasi ya uchumi wetu kudorora na nilileleza vizuri kwamba hatua zilizochukuliwa ni ili kuongeza *aggregate demand*. Mnaona kabisa kwamba, tumefanya uamuzi wa makusudi, mwaka ujao wa fedha kuanzia Julai mosi hatuungezi kabisa ushuru wa bidhaa (*excise duty*), pia tumeshusha kiwango cha *Skills Development Levy* na tumefuta tozo nyingi, takribani tozo 60. Yote haya tumefanya katika kuhakikisha kwamba mfukoni wananchi wetu wanakuwa na fedha zaidi za kujikimu wao na familia yao katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kufuatilia mwenendo wa viashiria vya uchumi na utekelezaji wa bajeti kwa ujumla. Kama itabainika kutakuwa na haja ya kufanya marekebisho ya bajeti, yaani *adjustment* ya bajeti, tutafanya hivyo wakati wa mapitio ya nusu mwaka (*Mid Year Review*) mwezi Desemba.

Mheshimiwa Spika, hoja nyininge ambayo nitapenda niieleze kwa urefu kidogo, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri ameifafanua vizuri sana, lakini nitataka niongezee kwa sababu sikupenda sana ilivyoelezwa humu ndani. Ni ile hoja kwamba Serikali imeshindwa kabisa kufikia malengo yaliyowekwa katika Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na ikitolewa mifano kwamba hakukuwa na ongezeko la pato la wastani kwa mwananchi, miradi ya maendeleo haikutekelezwa kwa kuwa Serikali haipeleki fedha, lengo la kupungua kiwango cha umasikini hakijafikiwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa majibu ya Serikali ni hivi, madai hayo kwa kweli wanisamehe nitatumia lugha ambayo sina mazoea kuitumia, madai hayo ni ya uzandiki! Nawashangaa sana waliotoa hoja hiyo dhaifu wakati Watanzania wanashuhudia mafanikio ya kishindo ya Serikali ya Awamu ya Tano. Wananchi hawa jamani wanaona kabisa mafanikio makubwa, sasa wanahudumiwa na zahanati 1,198 zilizojengwa; wanahudumiwa na vituo vya afya 487; wanahudumia na hospitali mpya 71 za wilaya nchi

nzima; na hospitali za rufaa. Vile vile wanaona pia miradi ya maji Mheshimiwa Nsanzugwanko alieleza vizuri miradi ya maji kule katika Jimbo lake la Kasulu na Wabunge wengine. Watoto wetu wanafaidi elimu bila ada, vijana wetu walioko katika Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu wanafaidi sana mikopo. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, vijiji vyetu pia sasa vinawaka umeme. Hata *satellite* zinaonesha sasa Tanzania imebadilika, miundombinu ya barabara na madaraja iko kila mahali. Reli ya zamani jamani imefufuliwa, wenzangu wa Moshi si wanaona? Reli imefufuliwa, inakarabatiwa, kwenye maziwa yetu kuna meli mpya, kuna vivuko, Serikali sasa iko Dodoma, jamani! Hivi mtu anawezaje kusema Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano haujatekelezwa? (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Hawana hoja.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nilikuwa namwangalia, naona amekuja, huwa namwona Mheshimiwa Halima Mdee ana macho mazuri, sikufikiria kwamba ana makengeza. Labda pengine ndiyo maana wenzetu wanakimbiwa na watu kila kukicha na nitashangaa kwa macho hayo kama wengine watarudi mwezi Novemba. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kuongezea uzito tu kwa kusema tulikubaliana ndani ya Bunge hili tathmini ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano itafanyika kwa kutumia *independent evaluator* na kazi hiyo bado iko katika hatua za maandalizi. Bado tuna mwaka mzima wa kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Sasa hiyo tathmini sijui wameipata wapi. Kwa hiyo nitaiacha hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine tuliambiwa tuongeze jitihada katika usimamizi wa taasisi na mashirika ya umma ili kuongeza ufanisi na kufikia malengo ya kuanzishwa kwa taasisi hizo. Napenda niseme kwamba Serikali imeendelea kusimamia mashirika na taasisi za umma

kuhakikisha zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu ili tuweze kuongeza ufanisi. Tumechukua hatua kufuatilia, tunafanya mapitio ya mikataba ya wanahisa, mikataba na kimenejimenti hata mikataba ya misaada ya utaalalm katika makampuni.

Mheshimiwa Spika, tumeepata mafanikio makubwa sana katika usimamizi wa taasisi na mashirika ya umma. Tumeongeza hisa za Serikali katika Kampuni ya Simu *Airtel* kutoka asilimia 40 mpaka 49 na kuanza kutoa gawio kwa Serikali. Tumeanzisha Kampuni ya Twiga *Minerals Corporation* ambayo sasa tunamiliki kwa ubia. Tuna asilimia 16 kama Serikali na *Barrickwana* asilimia 84. Tumerejesha hisa za Serikali katika kampuni ya *UDA* na *UDART* mpaka zimefika asilimia 85. Tumerudisha umiliki wa hisa ya kampuni ya *MECCO* na zote hizi ni jitihada za kuimarisha usimamizi wa taasisi na mashirika mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba Benki za Serikali zinakuwa zinafanya vibaya na *TPB Bank PLC*, imeanza kufanya vizuri lakini tuna longeza benki nyingine ambayo inafanya vibaya zaidi. Tulianza kuongeza Twiga na Benki ya Wanawake na kwa hiyo hofu ni kwamba tutaisababishia benki hiyo nayo kufanya vibaya au kufa.

Mheshimiwa Spika, tumechukua uamuzi wa kuunganisha *TPB Bank PLC*, na *TIB Corporate* ili kuboresha utendaji wa taasisi za fedha ambazo zinamilikiwa na Serikali ili tuweze kuwa na benki moja imara ya kibiashara na kabla ya hatua hii, *TIB Corporate* ilikuwa inahudumia wateja wakubwa yaani *corporate banking* na *TPB Bank* ilikuwa ikijikita kwa wateja wadogo wadogo na wa kati (*Retail banking*). Sasa muungano huu unalenga kuleta mageuzi makubwa ya kiutendaji, kimfumo na kimundo na hata kitaswira ili benki iweze kuhimili ushindani kwenye Sekta ya Fedha. *TPB Bank PLC*, imeimarika zaidi baada ya kuunganishwa na benki nyingine na imeongeza wateja waliokuwa kwenye hizo benki nyingine. Kwa hiyo katika zoezi la kuiunganisha *TPB* na *TIB Corporate* limeifanya *TPB Bank PLC*, kuwa na amana za wateja kufikia bilioni 743 kutoka bilioni 449. *Assets*,

zimeongezeka kutoka bilioni 657.5 kwenda triliuni 1.002 na hivyo kukidhi matakwa ya msimamizi wa mabenki kwa sababu benki hii sasa iko kwenye *tier number one* ya mabenki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaendelea kuimarisha benki zinazomilikiwa na Serikali zilizobaki na hususan Benki ya Maendeleo ya Kilimo lakini pia *TIB Development* kwa kuwapatia mtaji kadri itakavyoonekana inafaa. Vile vile tutaendelea kuimarisha pia usimamizi wa mashirika na taasisi ili tuhakikishe zinaendeshwa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu na hatimaye ziweze kuongeza mchango wao kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba kwa mujibu wa Ibara ya 135(1) ya Katiba, makusanyo yote ya Serikali yanatakiwa yawekwe kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, lakini licha ya maelekezo hayo, imebainika kuwa utaratibu huo haufuatwi. Naomba nisisitize kwamba Ibara hiyo ya Katiba inamatamka kweli fedha zote zinazopatikana kwa njia mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano isipokuwa fedha za aina iliyotajwa katika Ibara ndogo ya (2) ya Ibara hiyo zitawekwa katika Mfuko mmoja maalum ambao unaitwa Mfuko Mkuu wa Hazina. Ibara ndogo ya pili inaeleza na naomba ninukuu kwamba:

"Fedha ambazo hazitawekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ni zile zote ambazo zimetajwa na sheria kwamba zitumike kwenye shughuli maalum au ziwekwe katika Mfuko Mkuu mwengine kwa ajili ya matumizi maalum."

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kutekeleza na kusimamia matakwa haya ya Katiba na kuhakikisha kuwa fedha zote zinazotakiwa kuwekwa Mfuko Mkuu zinawekwa huko na matumizi ya zile zinazotakiwa kuwekwa kwenye Mifuko maalum zinatakiwa kwa mujibu wa sheria zitumike kwa shughuli maalum ambazo zinasimamiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, labda nisemee pia hoja nyininge kuwa kwa kuwa Serikali imepunguza kiwango cha riba katika Benki za Biashara kwa kiwango cha asilimia mbili kwamba,

je, Serikali haioni umuhimu wa kupunguza kiwango cha riba kwa wananchi wanaokopa katika Benki za Biashara kwa kiwango hicho hicho? Ni kweli, kinachosemwa kuititia Benki Kuu tumepitia riba ambayo Benki zinatoza zinapokopa Benki Kuu kutoka asilimia saba mpaka tano na hii ilifanyika ili kupunguza athari za *Covid19*, lakini tulitaka tupunguze gharama ambazo benki wanatakiwa kulipa wanapokopa Benki Kuu na kuongeza ukwasi kwa ajili ya kutoa mikopo kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Kwa hiyo, matarajio yetu kama Serikali ni kwamba Benki za Biashara nazo zitashusha riba zao kutokana na hii hatua ambayo imechukuliwa na Benki Kuu na bahati nzuri nilieleza kwa mfano *Exim Bank* na baadhi ya Benki nyingine, sio *Exim Bank* peke yake. Baadhi ya Benki tayari zimeshusha riba kwa baadhi ya mikopo yake na hii ni kuitikia utekelezaji wa hatua hii ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa kwamba, tuangalie namna ya kutatua suala la *VAT* kwa bidhaa zinazonunuliwa Tanzania Bara na kwenda kutumika Zanzibar. Kwa kuwa, kuna mifumo bora sasa ya kusimamia kodi wanafikiri kwamba sasa hili linawezekana. Naomba tu niseme kwamba Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) sio kodi ya Muungano na hivyo wafanyakishara ambao wana usajili Zanzibar wanaponunua bidhaa katika viwanda viliwyoko Tanzania Bara ili kwenda kuviuza Zanzibar wanauziwa bidhaa hizo bila *VAT*, hivyo kodi kwenda kulipiwa kule Zanzibar. Aidha, kwa taasisi ambazo sio za kibiashara ambazo zinanunua bidhaa katika masoko ya kawaida, hao wanalipia kodi kwa sababu wanahesabika kama ni walaji wa mwisho na ni vigumu kutofautisha ni bidhaa zipi zitakazotumika hapa Bara na zipi zitakwenda kutumika Zanzibar. Kwa hiyo, tunashauri ili kuepuka adha ya ulipaji wa kodi ya *VAT*mara mbili, ni vizuri bidhaa hizo zikanunuliwa viwandani ambako ni rahisi kuzitofautisha.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ningependa kuitolea ufanuzi ni kwamba, tumepeata msamaha uliotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*)

kwa Serikali iendelee kuwasiliana na taasisi kama hizi ili tuweze kupata ahueni zaidi kuwa na uwezekano wa kupata misamaha zaidi.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kama nilivyoeleza tulipata msamaha wa dola za Marekani milioni 14.3, sawa na shilingi bilioni 32.6 kutoka *IMF* chini ya ule mpango wa *catastrophic containment and relief trust* na huu msamaha unaweza kuongezeka hadi kufikia bilioni 58.6. Pia Serikali imepokea msaada wa dola za Marekani milioni 15.16 ambazo ni shilingi bilioni 34.8 kutoka *Global Partnership for Education* kwa ajili ya kuboresha mazingira ya elimu katika kipindi cha ugonjwa huu wa *Covid19* na msaada huu utatumika kujenga madarasa, kununua vitabu, kutengeneza mazingira mazuri ya kusomea.

Mheshimiwa Spika, msaada huu wa *Global Partnership For Education* umeidhinishwa kutambua uongozi na nia ya Serikali na jinsi inavyopambana na madhara ya Covid katika Sekta ya Elimu. Kwa hiyo na hii itatusaidia pia katika *recovery upande* wa elimu. Pia, Serikali imeshawasilisha ombi la msaada Benki Kuu ya Dunia kupertia dirisha ambalo linaitwa *pandemic emergency financing facility* ambapo tunataraja dola za Marekani milioni 3.98 lakini tumeendelea pia kushawishi nchi nyingine ambazo zinatukopesha kwa masharti nafuu kwa utaratibu ule ule wa kuahirisha ulipaji wa madeni (*Debt payment suspension initiative*) lakini vile vile, tumewasilisha maombi kwenye *Pandemic Emergency Financing Facility* ya Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niseme tu kwamba Serikali haijalala inaendelea kutafuta vyanzo vingine vya mapato ili tuweze kupunguza makali ya bajeti ya Serikali kutumika kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha nataka kuzungumzia pia hoja kwamba Serikali iangalie uwezekano wa suala la kuangalia watumishi wa umma kuhusu nyongeza za mshahara kwa kuwa bajeti hii ni ya mwisho. Napenda nisisitiza kwamba Serikali imeendelea na ulipaji wa madeni

mbalimbali yaliyohakikiwa ikiwa ni pamoja na madeni ya watumishi ambapo toka Serikali hii ilipoingia madarakani mpaka mwezi Aprili mwaka huu, tumekwishalipa shilingi zaidi ya bilioni 382 kwa madeni mbalimbali na haya ni yale yanayohusu malimbikizo ya mishahara na madeni yasi ya kimshahara. Dhamira yetu ni kuhakikisha kwamba tunalipa madai haya ambayo yamewasilishwa na kuhakikiwa na hii ni kwa mujibu wa sheria ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu nyongeza ya mshahara, Serikali imekuwa ikishughulikia suala hili ili kuboresha mishahara ya watumishi kwa njia mbalimbali. Njia mojawapo ni kupandisha vyeo ambayo tumeendelea kufanya. Kutoa nyongeza ya mwaka (*annual increment*) lakini pia kupunguza kodi kwenye mishahara hadi kufikia kima cha tarakimu moja. Katika mwaka ujao wa fedha kama nillivyosema tumependekeza kuongeza kwango cha mapato yasiyotozwa kodi (*threshold*) kutoka Sh.170,000 mpaka Sh.270,000 kwa mwezi. Pia kubadilisha makundi mengine ambayo yamebainishwa kwenye jedwali 1(b) la hotuba yangu. Mapendelekezo haya yanalenga kuleta unafuu wa kikodi kwenye mapato ya wafanyakazi na hivyo kuwaongezaa kiasi cha mshahara ambacho wanaweka mfukoni (*take home*). Kwa hiyo, Serikali imefanya jitihada kulingana na hali halisi ya kiuchumi kuwajali wafanyakazi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa uniruhusu nihitimishe. Kabla ya kuhitimisha maelezo yangu napenda nichukue fursa hii kulipongeza sana Bunge lako Tukufu kwa kufanya mambo makubwa ya maendeleo kwa manufaa ya nchi yetu. Bunge lako limeweka alama kubwa katika nchi yetu kwa kuitisha sheria na maazimio mbalimbali ambayo ni ya manufaa kwa wananchi wa Tanzania. Mtakumbuka sana Waheshimiwa Wabunge jinsi ambavyo mmeunga mkono juhudzi za Rais wetu kusukuma mbele maendeleo ya Taifa letu. Mambo makubwa ni pamoja na kuitisha Sheria ya kuitambua Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi na walipigilia misumari kwa kuitisha Azimio la kuitaka Serikali isije kubadili uamuzi wa Jiji hili kuwa Makao Makuu ya nchi na shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, vile vile tukio la jana la kuchanga na kujenga shule ya kisasa kabisa ya wasichana katika nchi yetu kwa mara ya kwanza ni jambo la kihistoria. (*Makof/ Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya mambo makubwa na Serikali hii ya Awamu ya Tano itaendelea kufanya Mambo makubwa zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyooleza katika hotuba yangu, hatua ambazo zilipendekezwa kwenye hotuba ya bajeti zinalenga kuendelea kujenga misingi madhubuti ya uchumi wa viwanda lakini pia kupanua fursa za ajira na za kibashara. Sasa kufanikiwa kwa bajeti hii kunahitaji nidhamu ya hali ya juu katika kusimamia mapato na matumizi. Na ili tuweze tuweze kufikia adhima hii, juhudzi za pamoja kati ya Serikali na wadau wote zinahitajika ikiwa na pamoja na kuhamasisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika uchumi ili wawekeze zaidi katika maeneo ya kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe tena rai kwa kila Mtanzania kutimiza wajibu wake ili bajeti hii iweze kutekelezwa kama ilivyopangwa. Ninapenda pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge kuunga mkono hatua ambazo zinaongozwa na Serikali ya Awamu ya Tano kuhakikisha kuwa tunaimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani. Hao wajomba nao wana mambo yao; wamepigwa na *COVID - 19* na mambo yao mengine kwa hiyo ni lazima tuelekeze nguvu kukusanya zaidi mapato ya ndani lakini pia katika kusimamia matumizi na kuyaelekeza, kuelekeza fedha tunazopata kwenye maeneo yenye tija na manufaa kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha maelezo yangu, napenda nichukue tena fursa hii kuwashukuru tena watumishi wa Wizara ya Fedha na Mipango katika ngazi zote. Pia watumishi wote wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango lakini na viongozi Katibu Mkuu Doto James, Naibu Makatibu Wakuu Amina Shabani, Mary Maganga, Bwana Adolf Ndunguru kwa kweli mimi na Mheshimiwa Ashatu

wametupatia ushirikiano wa hali ya juu sana katika kutekeleza majukumu yetu katika kipindi chote cha miaka mitano; kwa kweli wamefanya kazi kubwa na kwa pamoja tumetenda tulyoyaweza kama timu moja, ninawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya ufanuzi wa hoja hizo chache kama nilivyosema, zilizobaki tutaleta ufanuzi zaidi kwa maandishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA JAMII:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge, makofi hayo ni kuashiria jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha amehitimisha hoja yake vizuri kabisa na kuhitimisha huko kwa kawaida kunafuatiwa na kuwahoji lakini shughuli ya leo ni tofauti kidogo na shughuli ya siku zote. Na kwa maana hiyo nawaomba sasa Waheshimiwa Wabunge wale mnaozururazurura hebu kila mmoja basi akae mahali pake, tuwe na utulivu kidogo tuweze kwenda pamoja.

Moja kwa moja nimuite *Sergeant-at-arms* ili agonge kengele kumualika kila Mbunge kuingia ndani ya ukumbi huu na kila mmoja kuwa mahali pake. Ningewaomba sana usikivu na maelewano, najua mlion wengi mnaagana agana na nini lakini nawaomba usikivu. Wengine hata ninavyoendelea kuongea nao wamesimama wana yao, naomba make, kila mtu akae mahali pake *please get seated*, tuelewane.

Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa tumehitimisha mjadala wa Makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na mtoa hoja kumaliza kuhitimisha hoja yake, tunatakiwa sasa katika hatua hii kufanya maamuzi kwa kuyapitisha Makadirio hayo. Kanuni ya 107(2) inaelekeza kuwa utaratibu wa kuidhinisha Makadirio ya matumizi ya Serikali kama ifuatavyo, nanukuu kwamba "Uamuzi wa Bunge wa kupitisha au kutopitisha Bajeti ya

Serikali utafanya kwa kupiga kura ya wazi kwa kutaja jina la Mbunge mmoja mmoja."

Ibara ya 94(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na Kanuni ya 77(1) ya Kanuni za Bunge pamoja na mambo mengine zinazelekeza kwamba akidi ya Kikao cha Bunge wakati wa kufanya maamuzi ni nusu ya Wabunge wote na hapa hata kwa macho tu tupo zaidi ya nusu ya Wabunge wote. (*Makofii*)

Sasa kwa vile wabunge wote 385 waliopo kabla ya kuanza zoezi hili la kupiga kura, tunatakiwa kuwa na Wabunge wasiopungua 192 ambaa ndiyo nusu ya Wabunge wote, hivyo Katibu wa Bunge atatumia utaratibu unaofaa kutuhakikishia kama tunazidi idadi hiyo Kikanuni, kwa kweli kama nilivyosema hata kwa macho tunaona kabisa kama tunazidi nusu ya Wabunge wote.

Kanuni ya 79(1) inafafanua kuwa mambo yote yanahitaji kuamuliwa na Bunge yataamuliwa kwa kufuata maoni ya Wabunge walio wengi waliohudhuria na kupiga kura Bungeni. Hivyo katika zoezi letu la leo tutafuata utaratibu ufuataao; kwanza kengele itapigwa na nimeshaelekeza tayari na Waheshimiwa Wabunge walio nje ya ukumbi waingie ndani, pili Katibu atahesabu Wabunge wote ili kuona kama akidi imetimia na nimeshaeleza tayari hamna haja ya Katibu kuhangaika tena.

Tatu, zoezi la kupiga kura litaanza ambapo Katibu atasoma majina ya Wabunge mmoja mmoja baada ya mwingine na kila anayeitwa atatoa uamuzi wake wa kura ya ndio au hapana au atanyamaza (*abstain*). Waheshimiwa Wabunge baada ya hapo kura zitahesabiwa kisha tutapatiwa matokeo ya kura hizo ambayo ndiyo itafanya uamuzi kuhusu Makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Waheshimiwa Wabunge sasa namkaribisha Katibu wa Bunge ili aanzishe zoezi sasa la kuanza kupiga kura na ukishapiga kura kama unataka kwenda kupata chai kidogo

canteen unaweza kufanya hivyo lakini msiwe mbali kwasababu mambo yanaendelea na kama nilivyoeleza leo mambo ni mengi na yote inabidi yakamilike leo.

Katibu tuendelee sasa na zoezi, naomba Waheshimiwa Wabunge tupeane ushirikiano, nafikiri tulipofikia sasa hivi nianze kutoa watu nje ili tuelewane, Mheshimiwa Khatibu au nani pale nitaanza sasa kuwatoeni nje lakini bado sijakutoa na wengine amba mnapigapiga kelele; mnavyotaka kuongea nendeni tu nje mkaongee sana tu, mbadilishane simu na nini lakini naomba utulivu humu ndani ili kila anayeitwa jina lake aweze kusikia.

Naomba tena Waheshimiwa Wabunge maana yake tumechoka kukumbushana, kelele ni nyingi kwa nini? Nendeni nje mkaongee, kuna shida gani? Tusikilizane ili kila mmoja asikie jina lake apilge kura kwasababu atakayeitwa na hasa ninyi wa upande huu wa kulia, usisikie jina lako halafu ukipiga kura hapa ndiyo umejimaliza hivyo. Kwa hiyo, zoezi hili ni muhimu, tusikilizane kwa makini. Na mnafahamu hatima ya jambo hili kwa mfano kama Serikali ikakosa kura za idadi inayotakiwa kupilisha bajeti hii, si mnafahamu matokeo yake, inabadilisha kabisa uwanja. (*Makof*)

Kwa hiyo, ni zoezi muhimu sana, naomba mnaotaka kuongea nendeni nje na hakika nitawatoa watu hapa nje. maana yake tunarudiarudia hamsikii, unataka kuongea na mtu nendeni tu *canteen* kule au mahali pengine mnaongea tu wala hakuna shida lakini hapa tusikilizane ili tufanye zoezi hili muhimu la Kikatiba; anayesema ndiyo aseme, anayesema hapana aseme na anaye-*abstain* aweze ku-*abstain*, Katibu tuendelee!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:
Mheshimiwa Spika, tunaanza kuita majina kama ifuatavyo:-

Mhe. Dkt. Tulia Ackson.....	Ndiyo
Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa	Ndiyo
Mhe. Dkt. Adelardus Lubango Kilangi.....	Ndiyo
Mhe. Andrew John Chenge.....	Ndiyo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mhe. Najma Murtaza Giga.....	Ndiyo
Mhe. Selemani Saidi Jafo.....	Ndiyo
Mhe. Capt. Mst. George Huruma Mkuchika.....	Hayupo
Mhe. Jenista Joakim Mhagama.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi.....	Ndiyo
Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa.....	Ndiyo
Mhe. William Vangimembe Lukuvi.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Harrison George Mwakyembe.....	Ndiyo
Mhe. Angellaah Jasmine Kairuki.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango.....	Ndiyo
Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako.....	Ndiyo
Mhe. Ummy Ally Mwalimu.....	Ndiyo
Mhe. Luhaga Joelson Mpina.....	-
Mhe. Dkt. Medard Matogoro Kalemani.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla.....	-
Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwele.....	Ndiyo
Mhe. Prof. Paramagamba John Aidan Mwaluko Kabudi.....	Ndiyo
Mhe. Doto Mashaka Biteko.....	Ndiyo
Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga.....	Ndiyo
Mhe. Innocent Lughha Bashungwa.....	Ndiyo
Mhe. Mussa Azzan Zungu.....	Ndiyo
Mhe. George Boniphace Simbachawene.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchomba.....	Ndiyo
Mhe. Josephat Sinkamba Kandege.....	Ndiyo
Mhe. Anthony Peter Mavunde.....	Ndiyo
Mhe. William Tate Ole Nasha.....	Ndiyo
Mhe. Abdallah Hamis Ulega.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji	Ndiyo
Mhe. Angeline Sylvester Mabula.....	Ndiyo
Mhe. Elias John Kwandikwa.....	Ndiyo
Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya.....	Ndiyo
Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni.....	Ndiyo
Mhe. Eng. Atashasta Justus Nditiye.....	Ndiyo
Mhe. Subira Khamis Mgalo.....	Ndiyo
Mhe. Jumaa Hamidu Aweso.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa.....	Ndiyo
Mhe. Juliana Daniel Shonza.....	Ndiyo
Mhe. Stella Ikupa Alex.....	Ndiyo
Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo.....	Ndiyo

Mhe. Omary Tebwete Mgumba.....	-
Mhe. Hussein Mohamed Bashe.....	Ndiyo
Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara.....	Hayupo
Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro.....	Ndiyo
Mhe. Mussa Ramadhan Sima.....	Ndiyo
Mhe. Constantine John Kanyasu.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel	-
Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa.....	Ndiyo
Mhe. Jasson Samson Rweikiza.....	Ndiyo
Mhe. Peter Joseph Serukamba.....	Ndiyo
Mhe. Vedasto Edgar Ngombale.....	-
Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni.....	Ndiyo
Mhe. Moshi Selemani Kakoso.....	Ndiyo
Mhe. Dunstan Luka Kitandula.....	Ndiyo
Mhe. Emanuel Adamson Mwakasaka.....	Ndiyo
Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq.....	Ndiyo
Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa.....	Ndiyo
Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka.....	Hapana
Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa.....	-Hayupo
Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki.....	Ndiyo
Mhe. Salum Mwinyi Rehani.....	Ndiyo
Mhe. Kemilembe Julius Lwota.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma.....	Ndiyo
Mhe. Abdallah Dadi Chikota.....	Ndiyo
Mhe. Mwanne Ismail Mcchemba.....	Ndiyo
Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri.....	Ndiyo
Mhe. William Mganga Ngeleja.....	Ndiyo
Mhe. Juma Selemani Nkamia.....	Ndiyo
Mhe. Zaynabu Matitu Vullu.....	Ndiyo
Mhe. Khalfan Hilaly Aeshi.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga.....	Ndiyo
Mhe. Hawa Mchafu Chakoma.....	Ndiyo
Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe.....	Hayupo
Mhe. John John Mnyika.....	Hapana
Mhe. Ester Amos Bulaya.....	Hapana
Mhe. Raphael Japhary Michael.....	Hapana
Mhe. Ruth Hiyob Mollel.....	Hapana
Mhe. Tunza Issa Malapo.....	Hapana
Mhe. Paschal Yohana Haonga.....	Hapana

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi.....Ndiyo (*Makofi/Vigelegele*)

MBUNGE FULANI: CCM!

MBUNGE FULANI: Kondoa.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

Mhe. Halima James Mdee.....Hapana
Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa.....Hapana
Mhe. Godbless Jonathan Lema.....Hapana
Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare.....-
Mhe. Esther Nicholaus Matiko.....Hapana
Mhe. Antony Calist Komu.....Hapana
Mhe. Susan Anselm Lyimo.....Hapana
Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi.....Hapana
Mhe. Qambalo Willy Qulwi.....Ndiyo
Mhe. John Wegesa Heche.....Hapana
Mhe. Grace Victor Tendega.....Hapana
Mhe. Cecilia Daniel Paresso.....Hapana
Mhe. Zubeda Hassan Sakuru.....Hapana
Mhe. Salome Wycliff Makamba.....-
Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki.....-
Mhe. David Ernest Silinde.....Ndiyo (*Makofi/Vigelegele*)
Mhe. Devota Mathew Minja.....-
Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda.....Hapana
Mhe. Zainab Mussa Bakar.....Hapana
Mhe. Frank George Mwakajoka.....Hapana
Mhe. Anatropia Rwehikila Theonest.....Hapana
Mhe. Lucy Simon Mageleli.....-
Mhe. Suzan Limbweni Kiwanga.....-
Mhe. Catherine Nyakao Ruge.....Hapana
Mhe. Jesca David Kishoa.....Hapana
Mhe. Joseph Leonard Haule.....Hapana
Mhe. Sabreena Hamza Sungura.....Ndiyo

MBUNGE FULANI: Weweee! (*Makofi*)

Mhe. Joyce John Mukya.....	Hapana
Mhe. Peter Ambrose Lijualikali.....	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mhe. Rhoda Edward Kunchela.....	Hapana
Mhe. Upendo Furaha Peneza.....	-
Mhe. Grace Sindato Kiwelu.....	Hapana
Mhe. Lucy Fidelis Owenya.....	Hapana
Mhe. Yosepher Ferdinand Komba.....	Hapana
Mhe. Hawa Subira Mwaifunga.....	Hapana
Mhe. Lucia Michael Mlowe.....	Hapana
Mhe. Rashid Ali Abdallah.....	Hapana
Mhe. Maida Hamad Abdallah.....	Ndiyo
Mhe. Hamida Mohamed Abdallah.....	Ndiyo
Mhe. Munde Tambwe Abdallah.....	Ndiyo
Mhe. Bahati Ali Abeid.....	Ndiyo
Mhe. Abdul-Aziz Mohamed Abood.....	Ndiyo
Mhe. Khadija Hassan Aboud.....	Ndiyo
Mhe. Lameck Okambo Airo.....	Ndiyo
Mhe. Abdallah Haji Ali.....	Hapana
Mhe. Jamal Kassim Ali.....	Ndiyo
Mhe. Khadija Nassir Ali.....	Ndiyo
Mhe. Khamis Mtumwa Ali.....	Ndiyo
Mhe. Mbarouk Salim Ali.....	Hapana
Mhe. Ally Saleh Ally.....	Hapana
Mhe. Hussein Nassor Amar.....	Ndiyo
Mhe. Wanu Hafidh Ameir.....	Ndiyo
Mhe. Zainab Mndolwa Amir.....	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mhe. Ussi Salum Pondeza Amjadi.....	Ndiyo
Mhe. Saul Henry Amon.....	Ndiyo
Mhe. Jaku Hashim Ayoub.....	Ndiyo
Mhe. Omary Ahmad Badwel.....	Ndiyo
Mhe. Nuru Awadh Bafadhili.....	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mhe. Faida Mohammed Bakar.....	Ndiyo
Mhe. Mbaraka Salim Bawazir.....	Ndiyo
Mhe. Innocent Sebba Bilakwate.....	Ndiyo
Mhe. Hamidu Hassan Bobali.....	<i>Abstain</i>
Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba.....	Ndiyo
Mhe. Abdallah Majura Bulembo.....	Ndiyo
Mhe. Halima Abdallah Bulembo.....	Ndiyo
Mhe. Selemani Said Bungara.....	-
Mhe. Felister Aloyce Bura.....	Ndiyo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mhe. Jerome Dismas Bwanausi.....	Ndiyo
Mhe. Marwa Ryoba Chacha.....	Ndiyo
Mhe. Josephine Tabitha Chagula.....	Ndiyo
Mhe. Lathifah Hassan Chande.....	Ndiyo (<i>Makof!</i>)
Mhe. Mary Pius Chatanda.....	Ndiyo
Mhe. Sikudhani Yassini Chikambo.....	Ndiyo
Mhe. Eng. Christopher Kajoro Chiza.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Rashid Mohamed Chuachua.....	Ndiyo
Mhe. Cosato David Chumi.....	Ndiyo
Mhe. Mbaraka Kitwana Dau.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. David Mathayo David.....	Ndiyo
Mhe. Makame Mashaka Foum.....	Ndiyo
Mhe. Tauhidha Cassian Gallos.....	Ndiyo
Mhe. Alex Raphael Gashaza.....	Ndiyo
Mhe. Pauline Philipo Gekul.....	Ndiyo
Mhe. Josephine Johnson Genzabuke.....	Ndiyo
Mhe. Boniphace Mwita Getere.....	Ndiyo
Mhe. Anna Joram Gidarya.....	Ndiyo (<i>Makof/Vigelegele</i>)
Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia.....	Ndiyo
Mhe. Seif Khamis Gulamali.....	Ndiyo
Mhe. Haji Ameer Haji.....	Ndiyo
Mhe. Mwantum Dau Haji.....	Ndiyo
Mhe. Othman Omar Haji.....	Hapania
Mhe. Khatib Said Haji.....	Hapania
Mhe. Azza Hillal Hamad.....	Ndiyo
Mhe. Juma Kombo Hamad.....	Hapania
Mhe. Juma Othman Hijia.....	Ndiyo
Mhe. Mansoor Shanif Hiran.....	Ndiyo
Mhe. Augustine Vuma Holle.....	Ndiyo
Mhe. Joram Ismael Hongoli.....	Ndiyo
Mhe. Yussuf Salim Hussein.....	Hapania
Mhe. Khalifa Mohamed Issa.....	Hapania
Mhe. Zacharia Paulo Issaay.....	Ndiyo
Mhe. Asha Mshimba Jecha.....	Ndiyo
Mhe. Emmanuel Papian John.....	Ndiyo
Mhe. Asha Abdullah Juma.....	Ndiyo
Mhe. Juma Ali Juma	Ndiyo
Mhe. Mwantakaje Haji Juma.....	Ndiyo
Mhe. Hamoud Abuu Jumaa.....	Ndiyo
Mhe. Jafar Sanya Jussa.....	Ndiyo

Mhe. Ritta Enespher Kabati.....	Ndiyo
Mhe. Risala Saidi Kabongo.....	Hapana
Mhe. Mgeni Jadi Kadika.....	Hapana
Mhe. John Peter Kadutu.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu.....	Ndiyo
Mhe. Alfredina Apolinairy Kahigi.....	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mhe. Haji Khatib Kai.....	Hapana
Mhe. Joseph George Kakunda.....	Ndiyo
Mhe. Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala.....	Ndiyo
Mhe. Vicky Paschal Kamata.....	Ndiyo
Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli.....	Ndiyo
Mhe. Maria Ndila Kangoye.....	Ndiyo
Mhe. Sebastian Simon Kapufi.....	Ndiyo
Mhe. Rukia Ahmed Kassim.....	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mhe. Zainab Athuman Katimba.....	Ndiyo
Mhe. Hassan Seleman Kaunje.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa.....	Ndiyo
Mhe. Kanali (Mst.) Masoud Ali Khamis.....	Ndiyo
Mhe. Yussuf Haji Khamis.....	Hapana
Mhe. Sadifa Juma Khamis.....	Ndiyo
Mhe. Ali Salim Khamis.....	Hapana
Mhe. Fakharia Shomar Khamis.....	Ndiyo
Mhe. Mohammed Juma Khatib.....	Hayupo
Mhe. Munira Mustapha Khatibu.....	Ndiyo
Mhe. Aida Joseph Khenani.....	Hapana
Mhe. Omari Abdallah Kigoda.....	Ndiyo
Mhe. Mendrad Lutengano Kigola.....	Ndiyo
Mhe. Omari Mohamed Kigua.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe.....	Hayupo
Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete.....	Ndiyo
Mhe. Salma Rashid Kikwete.....	Ndiyo
Mhe. Ali Hassan Omar King.....	Ndiyo
Mhe. Elibariki Immanuel Kingu.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa	Ndiyo
Mhe. Mariam Nasoro Kisangi.....	Ndiyo
Mhe. Jumanne Kibera Kishimba.....	Ndiyo
Mhe. Boniventura Destery Kiswaga.....	Ndiyo
Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga.....	Ndiyo
Mhe. Allan Joseph Kiula.....	Ndiyo
Mhe. Silvestry Francis Koka.....	Ndiyo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mhe. Dkt. Susan Alphonse Kolimba.....	Ndiyo
Mhe. Leah Jeremia Komanya.....	-
Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma.....	Ndiyo
Mhe. Saed Ahmed Kubenea.....	-
Mhe. Zuberi Mohamedi Kuchauka.....	Ndiyo
Mhe. Julius Kalanga Laizer.....	Ndiyo
Mhe. George Malima Lubeleje.....	-
Mhe. Riziki Said Lulida.....	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mhe. Kangi Alphaxard Lugola.....	Ndiyo
Mhe. Anna Richard Lupembe.....	Ndiyo
Mhe. Livingstone Joseph Lusinde.....	-
Mhe. Eng. Gerson Hosea Lwenge.....	Ndiyo
Mhe. Hamad Salim Maalim.....	Hapana
Mhe. Amina Idd Mabrouk.....	Ndiyo
Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula.....	Ndiyo
Mhe. Khamis Yahaya Machano.....	Ndiyo
Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe.....	Ndiyo
Mhe. Catherine Valentine Magige.....	Ndiyo
Mhe. Sonia Jumaa Magogo.....	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mhe. Ester Alexander Mahawe.....	Ndiyo
Mhe. Almas Athuman Maige.....	Ndiyo
Mhe. Ezekiel Magolyo Maige.....	Ndiyo
Mhe. Kunti Yusuph Majala.....	Hapana
Mhe. January Yusuf Makamba.....	Ndiyo
Mhe. Yussuf Kaiza Makame.....	Ndiyo
Mhe. Makame Kassim Makame.....	Ndiyo
Mhe. Eng. Ramo Matala Makani.....	Ndiyo
Mhe. Joel Mwaka Makanyaga.....	Ndiyo
Mhe. Amina Nassoro Makilagi.....	Ndiyo
Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.....	Ndiyo
Mhe. Anne Kilango Malecela.....	Ndiyo
Mhe. Angelina Adam Malembeka.....	Ndiyo
Mhe. Ignas Aloyce Malocha.....	Ndiyo
Mhe. Issa Ali Mangungu.....	Ndiyo
Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi.....	Ndiyo
Mhe. Sixtus Raphael Mapunda.....	Ndiyo
Mhe. Agness Mathew Marwa.....	Ndiyo
Mhe. Gimbi Dotto Masaba.....	Hapana
Mhe. Hassan Elias Masala.....	Ndiyo
Mhe. Stephen Julius Masele.....	Ndiyo

Mhe. Augustino Manyanda Masele.....	Ndiyo
Mhe. Susanne Peter Maselle.....	Hapana
Mhe. Yahaya Omary Massare.....	Ndiyo
Mhe. Janeth Maurice Massaburi.....	Ndiyo
Mhe. Flatei Gregory Massay.....	Ndiyo
Mhe. Aisharose Ndogholi Matembe.....	Ndiyo
Mhe. Silafu Jumbe Maufi.....	Ndiyo
Mhe. Lucy Thomas Mayenga.....	Ndiyo
Mhe. Kiza Hussein Mayeye.....	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mhe. Mussa Bakari Mbarouk.....	Ndiyo
Mhe. James Francis Mbatia.....	Hapana
Mhe. Prosper Joseph Mbena.....	Ndiyo
Mhe. Janet Zebedayo Mbene.....	Ndiyo
Mhe. Richard Philip Mbogo.....	Ndiyo
Mhe. Taska Restituta Mbogo.....	Ndiyo
Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria.....	Ndiyo
Mhe. Neema William Mgaya.....	Ndiyo
Mhe. Godfrey William Mgimwa.....	Ndiyo
Mhe. Suzana Chogisasi Mgonokulima.....	-
Mhe. Joseph Kizito Mhagama.....	Ndiyo
Mhe. Mboni Mohamed Mhita.....	Ndiyo
Mhe. Esther Lukago Midimu.....	Ndiyo
Mhe. Rehema Juma Migilla.....	-
Mhe. James Kinyasi Millya.....	Ndiyo
Mhe. Desderius John Mipata.....	-
Mhe. Nimrod Elirehema Mkono.....	Hayupo
Mhe. Joseph Michael Mkundi.....	Ndiyo
Mhe. Martha Moses Mlata.....	Ndiyo
Mhe. Goodluck Asaph Mlinga.....	Ndiyo
Mhe. Ester Michael Mmasi.....	Ndiyo
Mhe. Timotheo Paul Mnzava	Ndiyo
Mhe. Ally Keissy Mohamed.....	Ndiyo
Mhe. Twahir Awesu Mohammed.....	Hapana
Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali.....	Ndiyo
Mhe. Amina Saleh Mollel.....	Ndiyo
Mhe. Justin Joseph Monko.....	Ndiyo
Mhe. Daimu Iddi Mpakate.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda.....	Ndiyo
Mhe. Maryam Salum Msabaha.....	Ndiyo (<i>Makofi</i>)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi.....	Ndiyo
Mhe. Martin Mtonda Msuha.....	Ndiyo
Mhe. Shamsia Aziz Mtamba.....	Ndiyo (<i>Makof!</i>)
Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu.....	Ndiyo
Mhe. Abdallah Ally Mtolea.....	Ndiyo
Mhe. Daniel Edward Mtuka.....	Ndiyo
Mhe. Maulid Said Mtulia	Ndiyo
Mhe. Muhammed Amour Muhammed.....	Hapana
Mhe. Prof. Sospeter Mwitarubi Muhongo.....	Ndiyo
Mhe. Phillipo Augustino Mulugo.....	Ndiyo
Mhe. Mary Deo Muro	Hapana
Mhe. Benardetha Kasabago Mushashu.....	Ndiyo
Mhe. Mussa Hassan Mussa.....	Ndiyo
Mhe. Joseph Kasheku Musukuma.....	Ndiyo
Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata.....	Ndiyo
Mhe. Fredy Atupele Mwakibete.....	Ndiyo
Mhe. Edward Franz Mwalongo.....	Ndiyo
Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa.....	Ndiyo
Mhe. Venance Methusalah Mwamoto.....	Ndiyo
Mhe. Zainabu Nuhu Mwamwindi.....	Ndiyo
Mhe. Charles John Mwijage.....	Ndiyo
Mhe. Hasna Sudi Mwilima.....	Ndiyo
Mhe. Capt. Abbas Ali Mwinyi.....	Ndiyo
Mhe. Maftaha Abdallah Nachuma.....	Ndiyo (<i>Makof!</i>)
Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu.....	Ndiyo
Mhe. Shamsi Vuai Nahodha.....	Ndiyo
Mhe. Suleiman Masoud Nchambi.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile.....	Ndiyo
Mhe. Deogratias Francis Ngalawa.....	Ndiyo
Mhe. Eng. Edwin Amandus Ngonyani.....	Ndiyo
Mhe. Oran Manase Njeza.....	Ndiyo
Mhe. William Dua Nkurua.....	Ndiyo
Mhe. Nape Moses Nnauye.....	Ndiyo
Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwanko.....	Ndiyo
Mhe. Albert Obama Ntabaliba.....	Ndiyo
Mhe. Mussa Rashid Ntimizi	Ndiyo
Mhe. Nassor Suleiman Omar.....	Hapana
Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo.....	Ndiyo
Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed.....	Ndiyo
Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab	Ndiyo

Mhe. Shally Josepha Raymond.....	Ndiyo
Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza.....	Hapana
Mhe. Machano Othman Said.....	Ndiyo
Mhe. Magdalena Hamis Sakaya.....	Ndiyo (<i>Makofi</i>)
Mhe. Masoud Abdallah Salim.....	Hapana
Mhe. Mattar Ali Salum	Ndiyo
Mhe. Ahmed Ally Salum	Ndiyo
Mhe. Salum Khamis Salum.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum.....	Ndiyo
Mhe. Deo Kasenyenda Sanga.....	Ndiyo
Mhe. Edwin Mgante Sannda	Ndiyo
Mhe. Joseph Roman Selasini	Hapana
Mhe. Oliver Daniel Semuguruka.....	Ndiyo
Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby.....	Hayupo
Mhe. Rashid Abdallah Shangazi	Ndiyo
Mhe. Shaabani Omari Shekilindi.....	Ndiyo
Mhe. Prof. Norman Adamson Sigalla King.....	Ndiyo
Mhe. Njalu Daudi Silanga.....	Ndiyo
Mhe. Margaret Simwanza Sitta.....	Ndiyo
Mhe. Joyce Bitta Sokombi.....	Hapana
Mhe. Jitu Vrajlal Soni.....	Ndiyo
Mhe. Rose Kamil Sukum.....	Ndiyo (<i>Makofi/Vigelegele</i>)
Mhe. Khalifa Salum Suleiman.....	Ndiyo
Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Charles John Tizeba.....	Ndiyo
Mhe. Fatma Hassan Toufiq.....	Ndiyo
Mhe. Salim Hassan Turky.....	Ndiyo
Mhe. Rose Cyprian Tweve.....	Ndiyo
Mhe. Martha Jachi Umbulla.....	Ndiyo
Mhe. Ally Seif Ungando.....	Ndiyo
Mhe. Khamis Ali Vuai.....	Ndiyo
Mhe. Anastazia James Wambura.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf.....	Hapana
Mhe. Selemani Jumanne Zedi.....	Ndiyo
Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto.....	-
Mhe. Luhaga Joelson Mpina.....	Ndiyo
Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kigwangalla.....	Ndiyo
Mhe. Capt. (Mst.) George H. Mkuchika.....	Ndiyo
Mhe. George Boniface Simbachawene.....	Ndiyo
Mhe. Mohammed Juma Khatib.....	Hapana

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mhe. Omary Tebweta Mgumba.....	Ndiyo
Mhe. Salome Wycliffe Makamba.....	Hapana
Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel.....	Ndiyo
Mhe. Vedasto Edgar Ngombale.....	<i>Abstain</i>
Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa.....	Hayupo
Mhe. Susan Limbweni Kiwanga.....	Hapana
Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki.....	Hapana
Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe.....	Ndiyo
Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare.....	<i>Abstain</i>
Mhe. Upendo Furaha Peneza.....	Hapana
Mhe. Lucy Simon Magereli.....	Hapana
Mhe. Selemani Said Bungara.....	Hayupo

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:
Mheshimiwa Spika zoezi la kupiga kura limekamilika.

WABUNGE FULANI: Hapana, hapana.

SPIKA: Yeyote ambaye hajapiga kura naomba asimame pale alipo twende mmoja mmoja tuanze kule mwisho.

Mhe. Desderius John Mipata.....Ndiyo

SPIKA: Taratibu, ahsante tayari Mipata.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Nilisema ndiyo lakini sikuwashwa microphone naomba jina langu lirudiwe.

SPIKA: Mheshimiwa Lubeleje mumhesabu kwamba alisema ndiyo.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:
Mheshimiwa Spika, eee tumemsikia eeee

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge mwingine yoyote.

MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA: Mheshimiwa Spika, nilisema hapana lakini *microphone*...

SPIKA: Unataja na jina.

MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA: Mheshimiwa Spika, Suzana Mgonokulima.

SPIKA: Suzana Mgonokulima.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, Chogisasi.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, huku, hajaitwa eeeh.

SPIKA: Ndio Mheshimiwa Shamsi.

Mhe. Shamsi Vuai Nahodha.....Ndiyo

MBUNGE FULANI: Jina basi. (*Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Shamsi Nahodha, kura yake ni ndiyo. Kama tayari Makatibu nawapa mwingine. Tunaendelea.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE: Yule mama.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED Mheshimiwa Spika, nilisema Ndio lakini sikuwasha *microphone*. (*Makofi/Vigelegele*)

SPIKA: Taja na jina na kura yako ili viende pamoja kwa ajili ya hansard.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Spika, naitwa Rukia Kassim Ahmed nilisema NDIYO lakini sikuwasha *Speaker*. (*Makofi/Vigelegele*)

Mhe. Rukia kassim Ahmed.....Ndiyo

SPIKA: Mheshimiwa Rukia, kura yake ni ndiyo.

SPIKA: Tumekamilisha?

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, hapania. Nipo Lusinde hapa, Ndiyo. (*Makofi/Vigelegele*)

SPIKA: Mheshimiwa Livingstone Lusinde kura ya ndiyo.

Mhe. Livingstone J. Lusinde.....Ndiyo

SPIKA: Mheshimiwa *Chief Whip*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shabiby kidogo leo tumbo lake halipo vizuri lakini anaingia sasa hivi. Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

SPIKA: Nimekusikia vizuri, kama atatuwahi kabla hatujahesabu basi dakika mbili tatu, nne, tano ili Katibu aweze kufanya *tallying* na kutupatia majibu hapa hapa.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, nimepewa taarifa na....

SPIKA: Ndiyo, nani anaongea na yupo wapi?

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, nipo hapa, Edwin Amandus Ngonyani, nimepewa taarifa na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa amelazwa Benjamin Mkapa, anakuomba sana wewe unafahamu um-*record* kama amesema ndiyo, amenipa hiyo taarifa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU: Mheshimiwa Spika, Ahmed Shabiby amekwishakuungia Ukumbini.

Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby.....Ndiyo

SPIKA: Ahsante sana Makatibu m-*record* hiyo Ahmed Shabiby kura yake ndiyo. Umeshachelewa, Mheshimiwa Zitto Kabwe piga kura.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto.....Hapana

SPIKA: Mheshimiwa Leah Komanya yupo?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, hayupo na mpaka sasa tunamtafuta kwenye simu hapatikani.

MBUNGE FULANI: Amepatikana.

MBUNGE FULANI: Ameshapatikana?

MHE. FELISTER BURA: Nimempata anakuja yuko *toilet*.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa kesho nitaomba yaani tatu juu ya alama kila mtu awe amekaa, kwasababu kwa hakika tutafunga mlango wale waliozoea kuchelwa chelewa basi watajikuta wamebakia nje. Kwasababu kesho ni siku muhimu, ina shughuli nygingi tuna wageni wengi sana, hatuwezi ku-*avoid mistake*. Kwa hiyo, lazima awe *sited by* tatu juu ya alama.

MBUNGE FULANI: Baridi imezidi.

SPIKA: Wahusika baridi kali, wameamua kuwaaga Wabunge kwa baridi kali, kwa kiyoyozi, ndiyo maana imebidi Spika apate kikombe cha kahawa maana yake baridi kali sana.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

Mhe. Leah Jeremia Komanya.....Ndiyo

SPIKA: Nani naomba kujua jina, Katibu Leah Komanya ndiyo ameshatoka *toilet*, ndiyo. (*Kicheko*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge naomba usikivu wenu ili Katibu aweze kusoma matokeo.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

Mheshimiwa Spika, Wabunge waliokuwepo Bungeni walikuwa ni 371, na kwa idadi ya ambao hawakuwepo ni 13, Wabunge waliopiga kura ni 371, idadi ya kura za hapana ni 63, na idadi ya kura za ndiyo 304. (*Makofi/Vigelegele*).

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa kura hizo basi naomba kutangaza rasmi kwamba bajeti ya Serikali imepitishwa rasmi na Bunge hili, kwa kura 304, ni kura nydingi *record/haijapata kutokea, niwapongeze wote mliopiga kura na kura zenyewe zimeonyesha kwamba yajayo...!* (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Yanafurahisha!

SPIKA: Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha timu yako yote Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa ambayo mmeefanya miaka yote mitano hongera sana Mheshimiwa Philip Mpango na Naibu wako hongereni sana. (*Makofi*)

Kwa kweli kipindi kama hiki cha bajeti cha kuanzia Aprili mpaka sasa yaani huwa mnachapa kazi kwa kiwango ambacho hapa Bungeni mnaitwa leo, mnaitwa kesho, mnaitwa usiku, mnaitwa asubuhi, mchana, mara Kamati hii, mara Kamati ile ikabaki Kamati ya Bajeti ndiyo usiseme, Wajumbe wa Kamati ya bajeti hongereni sana, poleni kazi kwa kazi hata usuku wa kuamkia leo sijui mmelala saa ngapi Wajumbe wqa Kamati ya Bajeti, nawapongezeni sana sana. Mungu atawalipa kwa mema yote mliyotufanyia hatuna cha kuwapa watanzania mmejitahidi sana, hongereni sana. (*Makofi*)

Basi bado tunaendelea Mheshimiwa Waziri wa Fedha hatujamaliza na wewe kwa sababu hatujamaliza na wewe kwasababu kuna *finance* mbele, tutaongea kidogo hapo mbele, lakini kwa sasa Katibu shughuli inayofuata.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuidhinisha jumla ya shilingi trilioni 34,879,792,957,999 kwa matumizi ya Serikali kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2021, kutumia fedha zilizoidhinisha kwa mwaka huu, kuruhusu kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo, (*A Bill for an Act to Apply a sum of thirty four Trillion, eighty hundred seventy nine billion, seven hundred ninety two million, nine hundred fifty seven thousand, nine hundred ninety nine shillings out of the consolidated fund to the service of year ending on the 30th day of June twenty, twenty one to appropriate the supply gradient to was that year to authorized the reallocation of certain appropriations and provide for matters connected with those purposes*).

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba usikivu wenu kama nilivyosema mwanzoni kwamba Muswada huu wa *appropriation* huwa hauchapishwagi kwenye gazeti la Serikali kabla haujaletwa hapa Bungeni. Lakini Muswada huu huwa haupelekwi kwenye Kamati yoyote ya Kudumu wala Kamati ya Bunge zima, na masharti kuhusu Miswada kusoma hayatumiki, na unapitishwa mfululizo kwa hatua zake zote. Kwa hiyo, Katibu tena, narudi kwako.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2020 (The Appropriation Bill 2020)

(Kusomwa Mara ya Pili)

SPIKA: Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuidhinisha jumla ya shilingi trillioni 34,879,792,957,999 kwa matumizi ya Serikali kutoka katika Mfuko Mkuu Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka huo kuhusu kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo, (*A Bill of an Act to Apply a sum of thirty four Trillion, eighty hundred seventy nine billion, seven hundred ninety two million, nine hundred fifty seven thousand, nine hundred ninety nine shillings out of the consolidated fund to the service of the year ending on the 30th day of June twenty, twenty one, to appropriate the sum specified for that year to authorize the reallocation of certain appropriations and provide for matters connected with those purposes*).

(Kusomwa Mara ya Tatu)

SPIKA: Ahsante sana Katibu Muswada huu umeshapitishwa katika hatua zake zote tatu, nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge, tunawatachia Serikali utekelezaji mwema wa Muswada huu, tumeshawapa nguvu za kuwa-appropriate, tayari.

Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(Kusomwa Mara ya Pili)

**MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2020
(THE FINANCE BILL, 2020)**

SPIKA: Ahsante sana karibuni sana mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2020 (*The Finance Act, 2020*) pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri kuhusu vyanzo mbalimbali vya mapato yatokanayo na kodi kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati. Aidha, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao walichangia katika hotuba ya bajeti ya Serikali iliyopitishwa hapa Bungeni leo tarehe 15 Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wataalamu wake wa uandishi wa Sheria kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake, wadau mbalimbali katika Sekta ya Fedha, Biashara na Sekta Binafsi na wananchi kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao.

Mheshimiwa Spika, lengo la Muswada huu ni kufanya marekebisho sheria mbalimbali za kikodi na nyinginezo ili kuwezesha utekelezaji wa kisheria wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 niliyoiwasilisha Bungeni tarehe 11 Juni mwaka huu 2020.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudia kuzifanya marekebisho Sheria 18 zinazohusu masuala ya fedha, kodi, ushuru, tozo na mawasiliano kwa lengo la kuweka, kurekebisha, kupunguza au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali na kuboresha ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazofanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu, kwanza ni:-

- (i) Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji Fedha Haramu, Sura 423;
- (ii) Sheria ya Makampuni, Sura 212;
- (iii) Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, Sura 306;
- (iv) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147;
- (v) Sheria ya Ushindani, Sura 285;
- (vi) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332;
- (vii) Sheria ya Ardhi, Sura 113;
- (viii) Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290;
- (ix) Sheria ya Madini, Sura 123;
- (x) Sheria ya Usajili wa Magari, Sura 124;
- (xi) Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura 282;
- (xii) Sheria ya Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro, Sura 284;
- (xiii) Sheria ya Mamlaka ya Mapato, Sura 393;
- (xiv) Sheria ya Usimamizi wa Kodl, Sura 438;
- (xv) Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370;
- (xvi) Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini, Sura 318;
- (xvii) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148; na
- (xviii) Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji Stadi, Sura 82.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 19 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza inahusu masuala ya utangulizi inayojumuisha jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii ambapo sheria itaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2020.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha vifungu vya 3 na 15 vya Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura 423 ili kwanza kumtambua ndani ya sheria mnufaika wa mwisho kwa lengo la kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa; na pili, kuhakikisha taarifa sahihi za wanufaikaji wa mwisho zinapatikana, zinathibitishwa, zinahifadhiwa na kutambulika. Hatua hii itasaidia udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu pamoja na marekebisho yake inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Makampuni, Sura 212 ili:-

- (i) Kumtambua ndani ya Sheria mnufaika wa mwisho katika kampuni;
- (ii) Kuweka sharti la kuwasilisha taarifa za wanufaika wa mwisho wakati wa kusajili Kampuni au mabadiliko yanapotokea;
- (iii) Kuondoa sharti la kugongewa muhuri na Kamishna wa Kiapo ili kuonesha takwa la kisheria limetimizwa wakati wa kufungua au kuhuisha usajili;
- (iv) Kurejesha utaratibu wa kutoa hisa fichi (*warrant share*);
- (v) Kuweka wajibu kwa makampuni kuwa na rejista inayojumuisha wanufaika wa mwisho;
- (vi) Kuweka wajibu kwa rejista za kampuni kuwa na taarifa za wanufaika wa kampuni ambazo ni pamoja na majina kamili, tarehe ya kuzaliwa, namba za simu, uraia, makazi, sehemu za kazi na taarifa nyingine muhimu kwa ukamilifu; pamoja na kuweka sharti la kuwasilisha kwa Msajili wa Makampuni mabadiliko yoyote ya wanufaika wa mwisho wa kampuni ndani ya siku thelathini tangu kutokea kwa mabadiliko hayo;
- (vii) Kuweka sharti kwa kampuni yenye wanufaika wa mwisho kuhifadhi taarifa/kumbukumbu za wanufaika; na
- (viii) Kuweka sharti kwa Msajili wa Makampuni kuwa na rejista kwa ajili ya wanufaika wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne, kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, Sura 306 kwa kurekebisha Kifungu cha 26 kwa kuongeza kifungu kidogo cha (7) ili kampuni za mawasiliano zinazomilikiwa na Serikali

kwa kiwango cha asilimia 100 au asilimia 25 na zaidi na kampuni zinazohusika na ukodishaji wa minara ya mawasiliano zisiwe sehemu ya makampuni yanayotakiwa kuorodheshwa kwenye soko la hisa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 kwa kurekebisha Jedwali la Nne ili kuongeza kwenye orodha ya bidhaa zitazotozwa ushuru wa bidhaa; bia za unga na juisi za unga kwenye *HS Code 2106.90.99* zinazoingizwa nchini ili kupanua wigo wa kodi, kuleta uwiano na bidhaa nyiningine kama hizo na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita inapendekeza marekebisho kwenye Kifungu cha 60 cha Sheria ya Ushindani, Sura 258 ili kuweka wigo katika ukokotoaji wa adhabu kwa kuhusisha mauzo yaliyopatikana Tanzania pekee na siyo duniani kote kama ilivyo sasa. Lengo ni kuleta uwiano baina ya makosa na adhabu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba kama ilivyorekebishiwa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo: -

- (i) Kuongeza tafsiri ya maneno, '*associate*', '*beneficial owner*', '*representative assessee*', '*agent of a non resident person or of a beneficial owner*' na '*business connection*' ili kuwatambua washirika na wanufaika wa mwisho katika mfumo wa kodi kwa lengo la kupata taarifa za kikodi na kurahisisha utozaji wa kodi;
- (ii) Kuweka sharti la kumtoza kodi mwakilishi mkazi ambaye kuititia kwake mtu ambaye sio mkazi anapokea mapato ambayo anastahili kulipa kodi nchini;
- (iii) Kutambua mapato anayopokea mwakilishi mkazi au mnufaika wa mwisho kwa niaba ya mtu ambaye sio mkazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini anastahili kulipa kodi Tanzania kutokana na mapato anayopata nchini;

- (iv) Kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kutoa msamaha wa kodi ya mapato kwenye miradi ya kimkakati yenyenye jumla ya kodi ya mapato isiyozidi shilingi bilioni moja kwa kipindi chote cha utekelezaji wa mradi pasipo kuomba ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Lengo la hatua hii ni kurahisisha utekelezaji wa miradi ya kimkakati;
- (v) Kuweka ukomo wa kiwango cha asilimia 70 cha madai ya hasara inayotokana na ubadilishanaji fedha za kigeni wakati wa urejeshaji wa mikopo ya nje isiyokuwa na riba ili kulinda wigo wa kodi;
- (vi) Kuweka utaratibu wa kupunguza michango ya hiari kwenye Mfuko wa Ukimwi na Serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu (*Covid -19*), wakati wa ukokotoaji wa kodi. Lengo ni kuhamasisha uchangiaji wa hiari ili kusaidia mapambano dhidi ya magonjwa hayo;

SPIKA: Waheshimiwa mnaosimama simama kwa muda mrefu, kwenye makorido, mnaongea, mmempa mgongo Spika na kadhalika. Nawaomba tumsikilize Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Mheshimiwa Waziri wa Fedha endelea.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

- (vii) Kuweka ukomo wa asilimia 70 ya hasara inayoruhusiwa kusogezwa mbele kwa walipa kodi wenyenye hasara ya kikodi kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo au zaidi. Hata hiyo, marekebisho haya hayahusishi makampuni yanayojihuisha na kilimo, afya na elimu. Lengo la marekebisho ni kulinda wigo wa kodi;
- (viii) Kufuta msamaha wa kodi ya mapato kwa wanufaika wa Mfuko wa Udhamini;
- (ix) Kufanya marekebisho ya kiuandishi kwenye Kifungu cha 69 kwa kufuta kipengele kidogo cha (1) na kukiandika upya ili kurekebisha dosari zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria;

- (x) Kutambua mapato ya mtu ambaye sio mkazi au mnufaika wa mwisho yenyenye chanzo nchini yatakayotozwa kodi kwa mwakilishi mkazi ili kulinda wigo wa kodi;
- (xi) Kuweka sharti la kutoza kodi mawakala wa shughuli za kibenki na mawakala wa malipo kwa njia ya mtandao ili kuweka uwiano sawa katika utozaji wa kodi;
- (xii) Kuweka sharti la kutoza kodi ya ongezeko la mtaji kwenye uhamishaji wa leseni au haki ya kutumia ardhi tengefu kwa lengo la kupanua wigo wa kodi;
- (xiii) Kuongeza kiwango cha chini cha pato la mtu binafsi kisichotozwa kodi kutoka shilingi 2,040,000/= mpaka shilingi 3,240,000/= kwa mwaka, sawa na kutoka shilingi 170,000/= mpaka shilingi 270,000/= kwa mwezi. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu wa kodi ya mapato kwa wafanyakazi; na
- (xiv) Kuongeza kiwango cha mapato kisichotozwa kodi kutoka shilingi milioni 50 hadi shilingi milioni 100 kwa Vyama vya Ushirika vya Msingi ili kuongeza kiwango kinachosamehewa kodi; kutoa unafuu kwa Vyama vya Ushirika vya Msingi; na kufuta msamaha wa Kodi ya Mapato kwa wazalishaji wa bidhaa za ndani ya Kanda Maalum ya Kiuchumi (*Special Economic Zone*) wanaozalisha kwa ajili ya masoko ya ndani na nje ya nchi ili kuleta uwiano kati ya wazalishaji wa ndani ya Kanda Maalum ya uzalishaji na walio nje ya Kanda Maalum ya Uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura 113 kwenye Kifungu cha 33 ili kuweka sharti mtu yeyote anayehodhi ardhi iliyopimwa na aliyeshindwa kufanya maombi ya Hati ya Umiliki kwa Kamishna wa Ardhi...

Mheshimiwa Spika, samahani, naomba nirudie. Sehemu ya Nane kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura 113 kwenye Kifungu cha 33 ili kuweka sharti, mtu yeyote anayehodhi ardhi iliyopimwa na aliyeshindwa kufanya maombi ya Hati ya Umiliki kwa

Kamishna wa Ardhi ndani ya siku 90 kuanzia tarehe ya kuidhinishwa kwa michoro ya upimaji, kulipa Kodi ya Ardhi. Lengo ni kuhamasisha wananchi wanaohodhi ardhi bila kumiliki kukamilisha taratibu za umiliki wa ardhi. Hata hivyo, sharti hili halitahusisha taasisi na mamlaka za Serikali zinazojihusisha na upimaji na uuzaji wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 kama ifuatavyo: -

(i) Kubainisha wafanyabiashara wanaopaswa kulipa tozo ya huduma (*Service Levy*) kuwa ni wale wenye pato ghafi linalozidi shilingi 4,000,000/=; na

(ii) Kumpa mamlaka Waziri wa TAMISEMI kukadiria na kukusanya tozo ya huduma kwa Kampuni za Simu na kuandaa Kanuni ambazo zitaweka utaratibu wa kugawanya tozo hizo kwa Halmashauri za Wilaya ambako Kampuni za Simu zinaendesha shughuli zake. Lengo ni kuondoa kero kwa baadhi ya Halmashauri kukosa mapato kwenye chanzo hiki na kupunguza usumbufu wa ufuatiliaji kwa kila Halmashauri kwenye Makao Makuu ya Kampuni.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi kama ilivyorekebishesha inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Madini, Sura 123 katika vifungu vya 49(2), 54(2), 56, 73, 75(3), 80(1) na 82 ili kuongeza masharti kwa mwombaji wa leseni au anayetaka kuhuisha leseni ya uchimbaji madini kuwa na namba ya utambulisho wa mlipa kodi (*TIN*) na Cheti cha Kodi (*Tax Clearance*) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania. Lengo ni kuongeza uwajibikaji katika ulipaji kodi kwa hiari. Hata hivyo, sharti la kuwa na Cheti cha Kodi (*Tax Clearance*) halitahusisha wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Moja inapendekeza Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Magari, Sura 124 katika Jedwali la Kwanza ili kuanzisha usajili wa magari kwa kutumia namba maalum kwa kodi ya shilingi

500,000/= ambayo ni nyongeza ya kodi ya kawaida ya usajili wa gari. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura 282 kama ifuatavyo:-

- (i) Kuipa Mamlaka ya Mapato Tanzania jukumu la kukusanya maduhuli ya Hifadhi za Taifa na kuyawasilisha Mfuko Mkuu wa Serikali; na
- (ii) Kuweka utaratibu wa masuala ya kifedha na uandaaji wa bajeti ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tatu inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro, Sura 284 kama ifuatavyo:-

- (i) Kuipa Mamlaka ya Mapato Tanzania jukumu la kukusanya maduhuli ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na kuyawasilisha Mfuko Mkuu wa Serikali; na
- (ii) Kuweka utaratibu wa masuala ya kifedha na uandaaji wa bajeti ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na nne inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato, Sura 393 katika Sehemu B ya Jedwali la Kwanza kwa kuiongeza Sheria ya Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro, Sura 284 na Hati ya kuanzisha TAWA ya mwaka 2014 ili kuipa Mamlaka ya Mapato Tanzania jukumu la kukusanya maduhuli ambayo kwa sasa hukusanywa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na TAWA.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tano inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 kama ifuatavyo:-

- (i) Kufafanua watu wanaoruhusiwa kisheria kuwawakilisha walipakodi ili kurahisisha usimamizi wa kodi;

- (ii) Kuweka ukomo wa siku 14 kwa walipakodi kuwasilisha taarifa kwa Kamishna Mkoo ili kuhakikisha utoaji wa maamuzi ya kikodi;
- (iii) Kuondoa katika wigo wa maamuzi yanayostahili kukatiwa rufaa, maamuzi ambayo mlipakodi amekubaliana nayo kwa mkataba, kukiri na kuridhia na lengo ni kurahisisha usimamizi wa kodi;
- (iv) Kuweka ukomo wa kuwasilisha nyaraka zinazoombwaa na Kamishna Mkoo ili kuwezesha utatuza wa mapingamizi kwa wakati na lengo ni kurahisisha usimamizi wa kodi; na
- (v) Kuweka ukomo wa muda wa uwasilishaji wa nyaraka zinazoombwaa na Kamishna Mkoo wakati wa utatuza wa mapingamizi. Aldha, marekebisho haya yanapendekeza kuweka ukomo wa miezi sita kwa Kamishna kushughulikia utatuza wa mapingamizi. Lengo la hatua hii ni kuwezesha utatuza wa mapingamizi kwa wakati na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Sita inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370 katika Kifungu 10A (1) ili kuruhusu Ofisi ya Msajili wa Hazina kkusanya asilimia 70 ya fedha za ziada kutoka kwenye Mashirika, Taasisi au Wakala yoyote itakayokuwa na ziada. Lengo ni kuwezesha usimamizi mzuri wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Saba inapendekeza marekebisho ya vifungu vya 1A, 2 na 15 vya Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura 318 ili: -

- (i) Kumtambua mnufaika wa mwisho kwa lengo la kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa;
- (ii) Kuweka sharti la kuwasilisha taarifa za mnufaika wa mwisho wa udhamini wakati wa usajili wa Mfuko wa Udhampini ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa zake; na

(iii) Kuweka sharti kwa Mfuko wa Udhamini kuwasilisha taarifa za wanufaika wa maslahi ya mfuko ambao siyo wakazi au wanufaika wa mwisho (*beneficial owner*) kwa Kabidhi Wasihi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nane, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kurekebisha kifungu cha 59(3)(e) ili kuruhusu utozaji wa kodi ya ongezeko la thamani kwa asilimia sifuri (0%) kwenye huduma zinazotolewa kwenye mizigo inayosafirishwa kwenda nje ya nchi kupitia hapa nchini kwa kipindi cha ziada ambacho Kamishna wa Forodha ataruhusu. Lengo ni kuwapa unafuu waagizaji wa mizigo kupitia bandari zetu pale ambapo mizigo hiyo inachelewea kuondoka nchini kwasababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika,pili ni kurekebisha kifungu 68(3) ili kufuta kifungu kidogo cha aya (d). Lengo ni kuwawezesha wauzaji wa bidhaa ghafi nje ya nchi kuendelea kujirudishia kodi ya ongezeko la thamani iliyolipwa kwenye gharama za huduma au bidhaa katika shughuli hizo, ili bidhaa hizo ziweze kushindana katika masoko ya nje. Hatua hii inalenga kuendana na msingi wa utozaji kodi ya ongezeko la thamani kwa kuzingatia mahali bidhaa inapotumika.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kurekebisha Sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Kwanza ili kutoa msamaha kwenye bima za kilimo cha mazao kwa lengo la kupunguza gharama na kutoa unafuu katika bima za kilimo ili kuwawezesha wakulima kuziwekea bima shughuliza kilimo na kuvutia wananchi kutumia huduma za bima kwa ajili ya kujikinga na majanga mbalimbali yanayoathiri shughuli zao za kilimo mfano, ukame, mafuriko nakadhalika.

Mheshimiwa Spika,Sehemu ya Kumi na Tisa, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi, Sura 82 kwa kufanya marekebisho katika kifungu cha 14 ili kupunguza kiwango cha tozo ya ufundi stadi

kutoka asilimia 4.5 hadi asilimia 4.0. Lengo la hatua hii ni kuwapunguzia waajiri mzigo na gharama za uendeshaji wa shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua zilizobainishwa katika Hotuba ya Bajeti zitatekelezwa na Mawaziri husika kupidia Kanuni na Matangazo ya Serikali (*Government Notices*) kwa mujibu wa matakwa ya Sheria husika. Hatua hizo ni pamoja na:

- (i) Kupunguza tozo inayotozwa na Bodi ya Sukari;
- (ii) Kupunguza ada zinazotozwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;
- (iii) Kurekebisha tozo kwenye sekta ya mifugo na uvuvi;
- (iv) Kupunguza ada ya mabango ya matangazo kwenye magari ya wazalishaji wa bidhaa yanayotumika kusafirisha bidhaa toka viwandani kwenda kwa wasambazaji;
- (v) Kupunguza tozo ya elimu kwa umma inayotolewa na OSHA; na
- (vi) Kurekebisha hati iliyoanzisha TAWAili kuipa Mamlaka ya Mapato Tanzania jukumu la kukusanya maduhuli.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, mengi ya marekebisho ninayopendekeza ni utekelezaji kisheria wa mapendeleko ya Serikali kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye mkubali kuupitisha ili kuwezesha Serikali kutekeleza bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Kwa kuwa Muswada huu ulifuata taratibu za kawaida za Miswada ya Sheria ulipelekwa katika Kamati ya Bajeti na kwa hiyo tutapata maoni ya Kamati ya Bajeti, lakini tutapata maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Kwa ratiba ya leo nitawapa dakika 15 *each*, Kamati ya Bajeti dakika 15 na Kambi Rasmi ya Upinzani dakika 15.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti mwende *straight* kwenye mapendekezo, maoni na nini mjitahidi mtumie dakika 15.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2020 (*The Finance Bill*, 2020).

Mheshimiwa Spika, tarehe 11 Juni, 2020, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kueleza hatua mblimbali za kodi za kiutawala zitakazochukuliwa na Serikali zenye lengo la kuongeza mapato, kuimarisha usimamizi wa kodi pamoja na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti kwa nyakati tofauti ilifanya vikao kwa ajili ya kuufanya kazi Muswada huo ukiwa ni pamoja na kupokea maoni ya wadau mbalimbali wanaoguswa na Muswada huu pamoja na masuala mengine ya kikodi. Wadau waliofika mbele ya Kamati ni kama walivyoorodheshwa kwenye taarifa yangu hii na ninaomba sana taarifa hii iingie yote kwenye kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, tuliweza pia kupokea maoni kwa maandishi kutoka kwa wadau mbalimbali kama ambavyo wameorodheshwa lakini Kamati ilipitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhuhi ya kila kifungu na kupendekeza marekebisho katika maeneo ambayo yanahitaji maboresho. Baada ya kujiridhisha na maudhuhi ya Muswada siku ya Jumapili tarehe 14 Juni, 2020 Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na watendaji wa Wizara yake kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya sheria 29 zilizopo kwenye Muswada huu. Aidha, majadiliano hayo yalihusisha pia Wizara na Taasisi zote za Serikali ambazo zimeguswa na Muswada huu ikiwa ni pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara ikiongozwa na Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya* na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikiongozwa na Naibu Waziri pia Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula. Aidha, taasisi walizoongozana nazo ni Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni, Msajili wa Hazina, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Ufilisi na Vizazi na Vifo, Benki Kuu ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria wa Fedha wa mwaka 2020. Baada ya majadiliano ya kina baina ya Kamati na Serikali Kamati tunatoa maoni na mapendekezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu, Sura ya 423; mabadiliko yanayopendekezwa yanatoa tafsiri ya maneno *beneficialowner* ili kutatua changamoto ya kubaini wamiliki halisi wa makampuni na Asasi za Kiraia ili kuhakikisha kwamba wanalipa kodi stahiki na kulinda Taifa dhidi ya watu walitolikia mema ambao hawataki kujulikana na badala yake wanatumia Asasi za kiraia kutimiza lengo lenye nia ovu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipendekeza kwa Serikali kufanya mabadiliko ya kimaudhuhi na kiuandishi katika Ibara ya 4 ya Muswada inayopendekezwa kufanya marekebisho katika kifungu cha 3 cha sheria kwa kuongeza tafsiri mpya

za maneno mbalimbali ikiwemo neno *arrangement* na *beneficial owner*. Kamati ilipendekeza maboresho ya kimaudhui na kiuandishi kwenye tafsiri za maneno hayo ili yasije kusababisha kuharibu mazingira bora ya biashara na uwezekaji yaliyopo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile ushauri wa Kamati ulikusudia kuondoa mwanya wa kifungu hicho kutumiwa vibaya na baadhi ya Maafisa wa Serikali katika ukiukwaji wa haki za msingi za binadamu. Aidha, Kamati pia haikuona umuhimu wa kuwapa wajibu watu wasiohusika na utoaji wa taarifa za wanufaika wa makampuni na Asasi za Kiraia kama inavyopendekezwa na Ibara ya 5 ya Muswada inayopendekeza kuongeza fasili mpya ya 1(a) katika kifungu cha 15 cha sheria hiyo na badala yake Kamati inapendekeza wajibu huo wapewe watu mahususi wanaohusika na utoaji wa taarifa. Aidha, Kamati illkubaliana na mabadiliko mengine yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Sheria ya Makampuni, Sura ya 212; Kamati ilibaini changamoto katika mapendekezo ya marekebisho katika sheria hii hususani suala la kufuta hisa fiche, *sharewarrant* za makampuni. Utaratibu wa kuwa na hisa fiche unatumika kote duniani hasa kwa makampuni ya umma na Makampuni binafsi yanayotengeneza faida. Hisa ni nzuri kibiashara kwa kuwa zinauzika kirahisi nakuwa chanzo kizuri cha mapato ya Serikali. Kamati ilishauri Serikali kufanya mabadiliko kwenye Ibara ya 10 ya Muswada inayopendekeza kufuta aina hiyo ya hisa ili kuendelea kutumia utaratibu uliopo sasa, lakini ukiwa na maboresho. Kamati ilishauri Serikali kufanya maboresho ili Sheria ya Makampuni iendelee kuruhusu kampuni ambazo zinakusudia kutoa *share warrant* kwa kuweka masharti yafuatayo:-

(i) Hisa za kampuni husika ziwe zimelipiwa kikamilifu yaani *full paid up*;

(ii) Kampuni ipate idhini ya Serikali kufanya hivyo; na

(iii) Hisa hizo zitozwe kodi ya ushuru wa stempu (*stamp duty*) kwa kiwango kitakachowekwa na Serikali kwa madhumuni hayo ili kuiwezesha Serikali kupata mapato.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki; Bunge lako Tukufu lilitifanya marekebisho ya sheria hii mwaka 2016 kwa kuweka masharti ya kuyataka makampuni yote ya mawasiliano nchini kujirodhesha kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam na kuuza hisa zao kwa umma kwa angalau asilimia 25. Hata hivyo, kumekuwa na mwamko hafifu kwa makampuni ambayo yako kwenye sekta hiyo ambapo hadi hivi sasa ni kampuni moja tu ya *Vodacom* iliyoweza kutimiza masharti hayo.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo katika Muswada huu yanalenga kuyaondoa makampuni ya aina mbili katika utaratibu wa kujirodhesha katika soko hilo. Makampuni hayo ni yale yanayomilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 au yale ambayo Serikali ina hisa angalau asilimia 25 pamoja na makampuni yanayotoa huduma ya ukodishaji wa minara. Pendekezo la kuondoa makampuni hayo yanayotoa huduma ya ukodishaji wa minara yana lengo la kuondoa sharti ili kuleta makampuni mengine kwenye sekta ya minara ya mawasiliano na kuondoa ukiritimba yaani *monopoly* ambapo hivi sasa tuna kampuni moja ambayo inamiliki asilimia 90 ya minara yote nchini.

Mheshimiwa Spika, kampuni hiyo imekuwa ikitoza kiasi cha dola za Marekani 2,400 kwa mwezi kwa kampuni moja iliyopanga wakati gharama ya kuendesha minara hiyo ni dola za Marekani 3,200 kwa mwezi. Hatua hii itasaidia kuvutia uwekezaji katika sekta hii ambayo itapelekea kupungua kwa gharama za ukodishaji wa minara na hivyo kupunguzia wananchi mzigo mkubwa wa gharama za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147; Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi ambaou umeufanya kwa miaka miwili mfululizo sasa wa kutokuongeza ushuru wa bidhaa japo kifungu cha 124(2) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kinatoa fursa hiyo. Hata hivyo, Kamati

inaishauri Serikali kuangalia upya viwango na utozaji wa ushuru wa bidhaa kwa sekta ya mawasiliano ambapo kiwango ni kikubwa asilimia 17 na kiwango hicho kinatozwa kwa makampuni wanapokuwa wanaauza bidhaa za mawasiliano kwa wasambazaji. Wasambazaji nao pia wanatoza kiwango hicho wnapouza bidhaa za mawasiliano kwa watumiaji yaani *final consumers* na hivyo kufanya huduma hizo ziwe za ghali kwa walaji.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushindani, Sura ya 285; Kamati imekubaliana na Serikali kuhusu mapendekezo ya kutoza faini ya asilimia 10 kwenye pato ghafi kwa makampuni ambayo yatashindwa kutekeleza matakwa ya Sheria ya Ushindani kwa kampuni zilizopo Tanzania Bara tu. Sharti la awali lilikuwa linataka faini ya asilimia 10 itozwe kwenye mapato yote ya kampuni hata makampuni mama yaliyopo nje ya nchi ambayo yana kampuni tanzu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana naSheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332; mabadiliko yanayofanyika katika sheria hii yana malengo makuu yafuatayo:-

(i) Kwanza ni kuweka mazingira ya kumpata mnufaika wa mwisho (*beneficial owner*) katika biashara au uwekezaji na kumtoza kodi ipasavyo;

(ii) Pili ni kuziba mwanya wa muunganiko wa wadhamini yaani *trust* kutumika kama eneo la kukwepa kodi kwa kugawana mapato yanayozidi kiwango kinachohitajika ambayo yanatokana na shughuli za uwekezaji wa udhamini; na

(iii) Kutoa katazo la kuondoa asilimia 70 ya hasara kwa mwaka wa tano kwa kampuni ambazo zinatengeza hasara kwa miaka minne mfululizo na kupunguza hasara zao kwenye mapato ghafi kwa asilimia 70 tu na asilimia 30 itatozwa kodi ya mapato.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri Serikali kuiandika upya Ibara ya 33 ya Muswada inayofanya mabadiliko katika

kifungu cha 52(2) cha sheria hiyo kwa sababu kikiachwa jinsi kilivyo kinaleta mkanganyiko katika utekelezaji wake. Aidha, Kamati imeishauri Serikali kuangalia upya Ibara ya 32 ya Muswada inayofanyiwa mabadiliko katika kifungu cha 19(2) kwa sababu maudhui yanayofafanua na hayo yanayopatikana katika kifungu cha 4 na kifungu cha 19 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo lilijadiliwa kwa muda mrefu ni mabadiliko ambayo yanapendekezwa kwenye Ibara ya 36 ya Muswada ambayo inakusudia kufanya mabadiliko katika kifungu cha 83(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ambayo inaanizisha kodi ya zuio kwa Mawakala wa Mabenki wanapokuwa wanalipwa kamisheni na mabenki. Pendekezo hili lilionekana kwamba linatoza kodi ya zuio mara mbili katika hatua ya awali benki inalipa kodi ya zuio wakati inamlipa wakala na katika hatua ya pili wakala analipa kodi ya zuio anapotoa huduma kwa mwananchi. Hatua hii inaweza kusababisha ongezeko la gharama kwa watumiaji wa huduma ya mawakala ambao wengi ni wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri Serikali kufanya mabadiliko katika Ibara ya 31 ya Muswada kipengele (e)kinachoruhusu mapato yatakayotumika katika mapambano ya *Covid-19* kuondolewa wakati wa ukokotoaji wa mapato ya kampuni. Aidha, katika Ibara hiyo Kamati kuongeza aya mpya ya (f)ambayo itatoa mwanya wachangiaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa mashine na vifaa vya kupima usalama wa damu ambazo zimekuwa changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, lengo la mapendeleko hayo ni kuvutia sekta binafsi kuchangia katika ununuziwa mashine hizo ambazo ni muhimu kwa kuhakikisha tunakuwa na damu salama. Vilevile nitumie fursa hii kwa kuipongeza Serikali kwa kufanya mabadiliko katika jedwali la kwanza la sheria hii kwa kupanua wigo wa kiwango cha mapato ambacho hakitozwi kodi kwa sababu limekuwa pendekezo la Kamati kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, mapendekezo ya marekesbisho katika Sheria hii yanakusudia kuweka masharti ya kumtaka mwombaji aliyekwisha kupewa ardhi, kuwasilisha maombi ya kupatiwa hatimiliki ndani ya siku 90 toka upimaji ulipokamilika. Kamati ina maoni kuwa ni vema suala hili likafanyiwa kazi kiutendaji badala ya utaratibu unaopendekezwa katika Muswada kwakuwa utatuzi wa changamoto ya utoaji wa hati upo ndani ya uwezo wa Wizara kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290; wadau wa sekta ya mawasiliano wamekuwa wakilalamikia utaratibu uliokuwa unatumika wakufanya malipo kwa halmashauri moja moja na wamekuwa wakiomba Serikali malipo hayo yafanyike sehemu moja. Kamati inakubaliana na mapendekezo haya ya Serikali, jambo la kusisitiza ni kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa kwa wakati na kwa usahihi. Aidha, Kamati inakubaliana na Serikali kwa kuweka sharti la mauzo yasiyozidi shilingi milioni nne kama msingi wa kutotoza ushuru wa huduma. Hatua hii pia inalenga kuondoa utata na mkanganyiko kwa mamlaka za Serikali za Mitaa wakati wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini, Sura ya 123; mapendekezo ya Muswada katika sheria hii yanakusudia kuweka masharti ya kuwa na Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (*TIN*), pamoja na Cheti cha Kodi (*Tax Clearance Certificate*) wakati wa maombi mapya ya leseni au uhuishaji wa leseni. Kamati inakubaliana na mapendekezo haya yenye lengo la kuwaleta wahusika katika wigo wa kodi (*tax net*) ili nao wachangie katika pato la Serikali. Angalizo la Kamati ni kuangalia uwezekano wa kuwaondolewa wachimbaji wadogo wenyewe leseni za *primary mining license*, wafanyabiashara wadogo (*brokers*), sharti la kuwa na cheti cha kodi kwa sababu kimsingi wanakuwa hawajafanya biashara, hatua ya kuwataka wale na namba ya mlipa kodi na cheti cha kodi inaweza kuwakimbiza wengi katika kundi hili...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante. Malizia Mwenyekiti muda hauko upande wako.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, naomba taarifa hii yote ingie katika Kumbukumbu za Bunge na naomba basi nihitimishe.

Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru sana kwa kunipa fursa kuwasilisha taarifa ya maoni ya Kamati ya Muswada wa Fedha mwaka 2020. Nawashukuru pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini na umahiri na uvumilivu wao na wameorodheshwa katika taarifa yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile nimshukuru sana ndugu Stephen Kagaigai pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kutuwezesha kufanya majukumu yetu kama inavyostahilli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2020 (*THE FINANCE BILL, 2020*)- KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016 naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2020 (The Finance Bill, 2020).

Mheshimiwa Spika, tarehe 11 Juni, 2020, Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, na kuelezea hatua mbalimbali za kodi na kiutawala zitakazochukuliwa na Serikali zenyelengo la kuongeza mapato, kuimarisha usimamizi wa kodi pamoja na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini. Baada ya wasilisho hilo, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipewa jukumu la kuuchambua Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2020 pamoja na kushauriana na Serikali kisha kutoa maoni na mapendekezo kuhusu muswada huo.

1.1. Uchambuzi wa Muswada

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti, kwa nyakati tofauti ilifanya vikao kwa ajili ya kuufanya kazi muswada huo ikiwa ni pamoja na kupokea maoni ya wadau mbalimbali wanaoguswa na Muswada huu pamoja na masuala mengine ya kikodi. Wadau waliofika mbele ya Kamati ni pamoja na:-

- a) Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (*Tanzania Private Sector Foundation-TPSF*);
- b) Tanzania Cigarette Company -(TCC);
- c) Tanzania Hunting Operators Association-(TAHOA);
- d) Chama cha Wanasheria Tanzania Bara (Tanganyika Law Society TLS);
- e) Chama cha Wasindikaji wa Maziwa Tanzania (Tanzania Milk Processors Association -TAMPA)
- f) Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (*Confederation of Tanzania Industries -CTI*);

g) Baraza la Kilimo Tanzania (Agricultural Council of Tanzania); na

h) Financial Deepening Trust – (FSD).

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipokea maoni kwa maandishi kutoka Wadau wafuatao:-

a) Wadau wa Michezo ya Kubahatisha;

b) Wazalishaji wa mafuta ya Alizeti;

c) Umoja wa Mawakala wa Forodha (TASAA);

d) Umoja wa Mabenki Nchini (TBA);

e) Jumuiya ya Wazalishaji wa Vyuma (SMA); na

f) Wadau wa Sekta ya Bima.

Aidha, vikao vingine na wadau vilifanyika kupitia mtandao wa kidigitali wa Zoom ikiwa ni pamoja na wadau wa Vifaa vya Zimamoto, Kampuni ya Ukaguzi ya KPMG na Wadau wa Mabango.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui ya kila kifungu na kupendekeza marekebisho katika maeneo ambayo yanahitaji maboresho. Baada ya kujiridhisha na maudhui ya Muswada, siku ya Jumapili tarehe 14 Juni, 2020 Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Watendaji wa Wizara yake kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria Ishirini na tisa (29)zilizopo kwenye Muswada huu. Aidha, majadiliano hayo yalihusisha pia Wizara na Taasisi zote za Serikali ambazo zimeguswa na Muswada huu ikiwa ni pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara ikiongozwa na Naibu Waziri Mhe. Eng. Stella Manyanya, Mb na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikiongozwa na Naibu Waziri Mhe. Dkt. Angelina Mabula, Mb. Aidha, taasisi walizoongozana nazo

ni Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (Business Registration and Licencing Authority-BRELA), Msajili wa Hazina (Treasury Registrar), Mamlaka ya Mapato Tanzania (Tanzania Revenue Authority-TRA), Mamalaka ya Ufilisi naVizazi na Vifo (Registration of Insolvency and Trustee Agency - RITA), Benki Kuu ya Tanzania (Bank of Tanzania - BoT), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

2.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2020.

Mheshimiwa Spika, Baada ya majadiliano ya kina baina ya Kamati na Serikali, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo: -

2.1. Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu Sura 423 (*The Anti-Money Laundering Act Cap.423*).

Mheshimiwa Spika, mabadiliko yanayopendekezwa yanatoa tafsiri ya maneno "*Beneficial Owner*" ili kutatua changamoto ya kubaini wamiliki halisi wa Makampuni na Asasi za Kiraia ili kuhakikisha wanalipa kodi stahiki na kulilinda Taifa dhidi ya watu wasiolitakia mema ambao hawataki kujulikana na badala yake wanatumia asasi za kiraia kutimiza lengo yenye nia ovu. Kamati ilipendekeza kwa Serikali kufanya mabadiliko ya kimaudhui na kiuandishi katika Ibara ya 4 ya Muswada inayopendekeza kufanya mrekebisho katika kifungu cha 3 cha Sheria kwa kuongeza tafsiri mpya za maneno mballimbali ikiwemo neno "*arrangement*" na "*beneficial owner*". Kamati ilipendekeza maboresho ya kimaudhui na kiuandishi kwenye tafsiri za maneno hayo ili yasije kusababisha kuharibu mazingira bora ya biashara na uwekezaji yaliyopo hapa nchini.

Vilevile, ushauri wa Kamati ulikusudia kuondoa mwanya wa kifungu hicho kutumiwa vibaya na baadhi ya maafisa wa Serikali katika ukiukwaji wa haki za msingi za binadamu. Aidha, Kamati pia haioni umuhimu wa kuwapa wajibu watu wasiohusika na utoaji wa taarifa za wanufaika wa

makampuni na asasi za kiraia kama inavyopendekezwa na Ibara ya 5 ya Muswada inayopendekeza kuongeza fasili mpya ya (1A) katika kifungu cha 15 cha Sheria hiyo na badala yake Kamati inapendekeza wajibu huo wapewe watu mahsus wanaohusika na utoaji wa taarifa. Aidha, Kamati imekubaliana na mabadiliko mengine yanaopendekezwa na Serikali katika sheria hiyo.

2.2. Sheria ya Makampuni, Sura 212 (The Companies Act, (Cap.212)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini changamoto katika mapendeleko ya marekebisho katika Sheria hii hususani suala la kufuta hisa fiche (*Share warrant*) za makampuni. Utaratibu wa kuwa na hisa fiche unatumika kote duniani hasa kwa makampuni ya umma na makampuni ya binafsi yanayotengeneza faida. Hisa ni nzuri kibiashara kwa kuwa zinauzika kirahisi na kuwa chanzo kizuri cha mapato ya serikali. Kamati iliishauri Serikali kufanya mabadiliko kwenye ibara ya 10 ya Muswda inayopendekeza kufuta aina hiyo ya hisa ili kuendelea kutumia utaratibu uliopo sasa lakini ukiwa na maboresho. Kamati iliishauri serikali kufanya maboresho ili Sheria ya Makampuni iendelee kuruhusu kampuni ambazo zinakusudia kutoa *Share Warrant* kwa kuweka masharti yafuatayo: -

- i. Hisa za kampuni husika ziwe zimelipiwa kikamilifu (fully paid up);
- ii. Kampuni ipate idhini ya Serikali kufanya hivyo; na
- iii. Hisa hizo zitozwe kodi ya Ushuru wa Stempu (Stamp Duty) kwa kiwango kitakachowekwa na Serikali kwa madhumuni hayo ili kuiwezesha Serikali kupata mapato.

2.3. Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, Sura 306 (The Electronic and Postal Communication Act, (Cap. 306)

Mheshimiwa Spika, Bunge lako tukufu lilitanya marekebisho ya Sheria hii mwaka 2016 kwa kuweka masharti ya kuyataka

makampuni yote ya mawasiliano nchini kujiorodhesha kwenye Soko la Hisa la Dar-esalaam na kuuza hisa zao kwa umma kwa angalau **asilimia 25**. Hata hivyo, kumekuwa na muamko hafifu kwa makampuni ambayo yako kwenye sekta hiyo ambapo hadi hivi sasa ni kampuni moja tu ya Vodacom iliyezea kutimizq masharti hayo. Mapendekezo katika Muswada huu yanalenga kuyaondoa makampuni ya aina mbili katika utaratibu wa kujiorodhesha katika soko hilo. Makampuni hayo ni yale yanayomilikiwa na Serikali kwa **asilimia 100** au yale ambayo Serikali ina hisa ya angalau **asilimia 25** pamoja na makampuni yanayotoa huduma ya ukodishaji wa minara.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la kuondoa makampuni ambayo yanatoa huduma ya ukodishaji wa minara yana lengo la kuondoa sharti hili ili kuleta makampuni mengine kwenye sekta ya minara ya mawasiliano na kuondoa ukiritimba (monopoly) ambapo hivi sasa tuna kampuni moja ambayo inamiliki **asilimia 90** ya minara yote nchini. Kampuni hiyo imekuwa ikitoza kiasi cha **dola za marekani 2,400**kwa mwezi kwa kampuni moja iliyopanga wakati gharama ya kuendesha minara hiyo ni **dola za marekani 3,200** kwa mwezi. Hatua hii itasaidia kuvutia uwekezaji katika sekta hii ambayo itapelekea kupungua kwa gharama za ukodishaji wa minara na hivyo kumpunguzia mwananchi mzigo mkubwa wa gharama za mawasiliano.

2.4. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147, (*The Excise (Management and Tariff) Act (Cap 147)*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuza ambao imeufanya kwa miaka miwili mfululizo sasa wa kutokuongeza ushuru wa bidhaa japo kifungu cha 124(2) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kinatoa fursa hiyo. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya viwango na utozaji wa ushuru wa bidhaa kwa sekta ya mawasiliano ambapo kiwango ni kikubwa (**Asilimia 17**) na kiwango hicho kinatozwa kwa makampuni wanapokuwa wanauzu bidhaa za mawasiliano kwa wasambazaji na wasambazaji nao pia wanatoza kiwango hicho hicho wanapouza bidhaa za

mawasiliano kwa watumiaji (Final Consumers) na hivyo kufanya huduma hizo ziwe ghali kwa walaji.

2.5. Sheria ya Ushindani SURA 285, (*The Fair Competition Act, (Cap 285)*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na Serikali kuhusu mapendeleko ya kutoza faini ya **asilimia 10** kwenye Pato ghafi kwa makampuni ambayo yatashindwa kutekeleza matakwa ya Sheria ya Ushindani kwa kampuni zilizopo Tanzania Bara tu. Sharti la awali lilikuwa linataka faini ya **asilimia 10** itozwe kwenye mapato yote ya kampuni hata makampuni mama yaliyopo nje ya nchi ambayo yana kampuni tanzu hapa nchini.

2.6. Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 (*The Income Tax Act, (Cap 332)*)

Mheshimiwa Spika, Mabadiliko yanayofanyika katika Sheria hii yana malengo makuu yafuatayo: Kwanza ni kuweka mazingira ya kumpata mnufaika wa mwisho (Beneficial Owner) katika biashara au uwekezaji na kumtoza kodi ipasavyo., Pili ni kuziba mwanya wa Muunganiko wa Wadhamini (Trust) kutumika kama eneo la kukwepea kodi kwa kugawana mapato yanayozidi kiwango kinachohitajika ambayo yanatokana na shughuli za uwekezaji wa Udhamini. Tatu ni kutoa katazo la kuondoa asilimia 70 tu ya hasara kwa mwaka wa tano kwa kampuni ambazo zinatengeneza hasara kwa miaka minne mfululizo na kupunguza hasara zao kwenye mapato ghafi kwa asilimia 70 tu na asilimia 30 itatozwa Kodi ya Mapato.

Mheshimiwa Spika, Kamati ililshauri Serikali kuiandika upya ibara ya 33 ya Muswada inayofanya mabadiliko katika kifungu cha 52(2) cha Sheria hiyo kwa sababu kikiachwa jinsi kilivyo kinaleta mkanganyiko katika utekelezaji wake. Aidha, kamati imeishauri Serikali kuangalia upya ibara ya 32 ya muswada inayofanya mabadiliko katika kifungu cha 19(2) kwa sababu maudhui yanayofanua na hayo yanapatikana

katika kifungu cha 4 na kifungu cha 19 cha Sheria ya Kodi ya mapato hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo lilijadiliwa kwa muda mrefu ni mabadiliko ambayo yanapendekezwa kwenye ibara ya 36 ya muswada ambayo inakusudia kufanya mabadiliko katika kifungu cha 83(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ambayo inaanzisha kodi ya zuio kwa mawakala wa mabenki wanapokuwa wanalipwa kamisheni na mabenki. Pendekezo hili ilionekana kwamba linatoza kodi ya zuio mara mbili katika hatua ya awali benki inalipa kodi ya zuio wakati inamlipa wakala na katika hatua ya pili wakala analipa kodi ya zuio anapotoa huduma kwa wananchi. Hatua hii inaweza kusababisha ongezeko la gharama kwa watumiaji wa huduma ya mawakala ambao wengi ni wa kipato cha chini hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, kamati imeishauri Serikali kufanya mabadiliko katika Ibara ya 31 ya muswada kipengele (e) kinaruhusu mapato yatakayotumika katika mapambano ya **COVID - 19** kuondolewa wakati wa ukokotoaji wa mapato ya kampuni. Aidha, katika ibara hiyo Kamati inapendekeza kuongeza aya mpya ya (f) ambayo itatoa mwanya wachangiaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa mashine na vifaa vya kupima usalama wa damu ambazo zimekuwa changamoto kubwa. Lengo la mapendekezo hayo ni kuvutia sekta binafsi kuchangia katika ununuzi wa mashine hizo ambazo ni muhimu kwa kuhakikisha tunakuwa na damu salama. Vile vile, nitumie fursa hii kuipongeza Serikali kwa kufanya mabadiliko katika Jedwali la Kwanza la Sheria hii kwa kupanua wigo wa kiwango cha mapato ambacho hakitozwi kodi kwa sababu limekuwa pendekezo la Kamati kwa muda mrefu na viwango hivyo vilikuwa vimepitwa na wakati.

2.7. Sheria ya Ardhi Sura 113, (*The Land Act, (Cap. 113)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisho katika Sheria hii yanakusudia kuweka masharti ya kumtaka muombaji aliyekwisha kupiwa ardhi kuwasilisha maombi ya

kupatiwa hati miliki ndani ya siku tisini toka upimaji ulipokamilika. Kamati ina maoni kuwa ni vema suala hili likafanyiwa kazi kluetendaji badala ya utaratibu unaopendekezwa katika muswada kwa kuwa utatuzi wa changamoto ya utoaji wa hati upo ndani ya uwezo wa Wizara kwa sasa.

2.8. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, (*The Local Government Finance Act, (Cap 290)*)

Mheshimiwa Spika, Wadau wa Sekta ya Mawasiliano wamekuwa wakilalamikia utaratibu uliokuwa unatumika wa kufanya malipo kwa Halmashauri moja moja na wamekuwa wakiomba Serikali malipo hayo yafanyike sehemu moja (*centralized*). Kamati inakubaliana na mapendekezo haya ya Serikali jambo la kusisitiza ni kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa kwa wakati na kwa usahili. Aidha, Kamati inakubaliana na Serikali kwa kuweka sharti la mauzo yasiozidi **shilingi milioninne** kama msingi wa kutotoza ushuru wa huduma. Hatua, hii pia ina lenga kuondoa utata na mkanganyiko kwa Mamlaka za Serikali za mitaa wakati wa utekelezaji wake.

2.9. Sheria ya Madini, SURA 123, (*The Mining Act (Cap 123)*)

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Muswada katika Sheria yanakusudia kuweka masharti ya kuwa na Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN-Tax Identification Number) pamoja na Cheti cha Kodi (Tax Clearance Certificate) wakati wa maombi mapya ya leseni au uhuishaji wa leseni. Kamati inakubaliana na mapendekezo haya yenye lengo la kuwaleta wahusika katika wigo wa kodi (Tax net) ili nao wachangie katika pato la Serikali. Angalizo la kamati ni kuangalia uwezekano wa kuwaondolea wachimbaji wadogo wenye leseni za *Primary Mining Licence – PML* na wafanyabiashara wadogo (brokers) sharti la kuwa na Cheti cha Kodi kwasababu kimsingi wanakuwa hawajafanya biashara, hatua ya kuwataka wawe na namba ya Mlipakodi (TIN) na Cheti cha Kodi inaweza kuwakimbiza wengi.

2.10. Sheria ya Usajili wa Magari, Sura 124 (*The Motor Vehicle (Tax on Registration and Transfer Act, (Cap. 124).*

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali yenye lengo la kuanzisha chanzo kipy Cha mapato kwa Serikali. Hii ni fursa kwa wananchi kupata namba za vyombo vyaya usajili kwa namna wanayotaka mfano T 2020 CCM au T 2020 JPM.

2.11. Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura 282 (*The National Parks Act (Cap.282)na Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi za Wanayama Pori, Sura 284 (*The Ngorongoro Conservation AREA (Cap 284).**

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kuzifanyia marekebisho Sheria husika kwa lengo la kuipa Mamlaka ya Mapato Tanzania jukumu la kisheria la kukusanya maduhuli ambayo kwa sasa hukusanya na mamlaka hizo. Sababu kuu ambazo Kamati ilielezw na Serikali ni pamoja na kuleta uwajibikaji wa matumizi wa fedha zinazokusanya na Mamlaka husika, uwajibikaji katika utendaji kazi lakini pamoja na kuzirudisha Mamlaka hizo katika hali ya kiuchumi iliyokuwepo kabla ya mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19 ambao limeathiri sana uendeshaji wa shirika. Kamati inatambua umuhimu wa uhifadhi na ina heshimu hatua zinazochukuliwa na Serikali kwa Mashirika haya, hata hivyo Kamati inaushauri ufuataao:-

- i. Serikali kuweka utaratibu mzuri wa kukidhi bajeti za uendeshaji wa Mamlaka husika ikiwa pamoja na kuweka uzio (ringfencing) kwenye bajeti za matumizi ya Mashirika hayo kwa utaratibu wa kuzitoa fedha hizo kwa kipindi cha robo mwaka badala ya mwezi mmoja mmoja ili Mamlaka hizo zitekeleze wajibu wa uhifadhi ipasavyo;
- ii. Kwa kuwa mapato ya Mamlaka hizo yanakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali hivyo Kamati inashauri TANAPA isitozwe asilimia 15 ya Mapato Ghafi; na
- iii. Serikali ihakikishe inazingatia utaratibu wa uhifadhi na kupeleka fedha kwa wakatia kwenye Mamlaka husika.

**2.12. Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania SURA 399
(Tanzania Revenue Authority Act (Cap 399)**

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kufanya mabadiliko katika jedwali la Pili la Sheria ya Mamlaka ya Mapato ili kujumuisha Sheria za Mamlaka ya Ngorongoro, TANAPA na TAWA ili kuhamisha jukumu la kukusanya ada, tozo na ushuru mbalimbali uliokuwa unakusanywa na Mamlaka hizo sasa kukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

2.13. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438, (The Tax Administration Act, (Cap 438)

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuweka sharti la kumtaka mlipa kodi kuwasilisha nyaraka zote ambazo atazitumia katika kuwasilisha pingamizi kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, utaratibu huo pia unaweka katazo la mlipa kodi kuwasilisha nyaraka nyingine ambazo hakuziwasilisha kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato wakati wa pingamizi.

2.14. Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370, (The Treasury Registrar (Powers and Function (Cap 370)

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na Mapendekezo ya Serikali yenye nia ya kuruhusu Ofisi ya Msajili wa Hazina kukusanya asilimia 70 ya fedha za ziada kutoka kwenye Mashirika, Taasisi au Wakala yoyote itakayoonekana kuwa na ziada. Lengo la hatua hizi ni kuongeza udhibiti wa fedha za Serikali. Nia hii ni njema ya Serikali pamoja na kupanua wigo wa mapato pia itahakikisha kwamba kunakuwa na nidhamu ya matumizi katika Taasisi za umma ambazo baadhi yake zimekuwa na matumizi mabaya ya ziada hii.

2.15. Sheria ya Muunganiko wa Wadhamini Sura ya 318 (The Trustee Incorporation Act (Cap 318)

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mabadiliko yanayopendekezwa katika Sheria hii kwasababu kimsingi yanaleta muktadha wa mabadiliko yaliyofanyika kwa

kuweka tafsiri na matumizi ya maneno mnufaika wa mwisho *"Beneficiary Owner"*. Hata hivyo, Kamati iliishauri Serikali kufanya maboresho ya mapendekezo ya marekebisho katika sheria hii kwa kuzingatia ushauri uliotolewa katika sehemu ya pili ya muswada.

2.16. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 (*Value Added Act, (Cap 148)*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kurekebisha kifungu cha 59 lbara ya (3) cha Sheria ya Kodi ya VAT ili kumruhusu Kamishna Mkuu kusamehe kodi husika kwenye huduma kwa mizigo inayopitia Tanzania ambayo itakuwa imekaa zaidi ya muda unaotakiwa kutokana na sababu mbalimbali. Kamati imekubaliana na hatua hii njema ambayo ipo katika kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini na kuvutia mizigo mingi kupitia nchini.

Vilevile, marekebisho yanapendekezwa katika Jedwali la Kwanza na kutoa msahama kwa bima ya mazao. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ambayo itapelekea wakulima wengi kukatia bima mazao yao huku ikiongeza mapato ya Serikali.

2.17. Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia hatua zinazopendekezwa katika Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Mwaka 2004 na kubaini kwamba kwa kiwango kikubwa Mabadiliko hayo yamelenga maeneo makuu manne: -

- i. Kuwezesha upatikanaji wa vifaa tiba kama vile barakoa, PPE, pamoja na mashine za kusaidia kupumua kama hatua muhimu za kupambana na mafua makali yanayosababishwa na virusi vya Corona;
- ii. Upatikanaji wa Vifungashio ili kuchochea uzalishaji wa viwandani na usindikizaji wa bidhaa za kilimo na chakula;

iii. Kulinda uzalishaji wa viwanda mbalimbali vya ndani kama maziwa, nondo, magunia, nguo na mbogamboga; na

iv. Kuhamasisha uzalishaji wa mazao mbalimbali kwa kuyawekea mazingira rafiki kama mazao ya Kahawa.

2.18. Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundisti, Sura ya 82 (*Vocational Education and Training Act, (Cap 82)*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kupunguza tozo ya mafunzo na maendeleo ya ufundisti kwa sababu kimekuwa kilio cha muda mrefu cha Sekta Binafsi. Kamati inaamini hatua hii itaongeza mishahara kwa watumishi hasa wa sekta binafsi kwa kiwango kilichopunguzwa, waajiri katika sekta binafsi hawatarajiwi kupunguza kiwango cha mishahara ya waajirwa wao kwa kiwango kilichopunguzwa cha **asilimia 0.5** kufanya hivyo kutakuwa kinyume na kusudio la Serikali.

Mheshimiwa Spika; Kamati inapongeza hatua hizo muhimu kwa maendeleo ya sekta ya Kilimo, Viwanda na Biashara baina ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na mataifa mengine. Hata hivyo, kamati inaendelea kusitiza kwamba ni vema hatua hizi zikawa zinapata maoni ya Bunge kwa sababu kuna baadhi ya mapendekezo ya muda mrefu ili kuvisaidia viwanda vya ndani yamekuwa hayawasilishwi katika jumuiya hiyo kwa ajili ya maamuzi.

3.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA

Mheshimiwa Spika, masuala mengine yaliyojadiliwa katika Kamati wakati wa kuitisha muswada wa Sheria ya fedha: -

3.1. Vifungashio kwa ajili ya Mvinyo unaozalishwa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mitano sasa tumekuwa tukiwasilisha maombi Serikalini ya kuondoa Ushuru wa Bidhaa kwa chupa zinazotumika kwa ajili ya kufungashia mvinyo unazalishwa nchini. Hivi sasa chupa zinazoingizwa nchini zinatozwa ushuru wa bidhaa kwa **asilimia 25**, pamoja na tozo

nyingine za Serikali. Hali hii inasababisha mvinyo unaozalishwa nchini unakuwa aghali kuliko ule unaozalishwa nje. Wadau wameitaarifu kamati kwamba mataifa mawili yaliyoko katika jumuiya ya Afrika mashariki yameanza kulima zao la zabibu. Jambo la msingi la kujuliza ivi kwa hatua hizi tunalitakia mema zao hili ambalo linalimwa Dodoma katika Mji mkuu wa Tanzania.

3.2. Utozaji wa Kodi ya Stempu za Kieletroniki (ETS) Kwa kampuni ya Sigara TCC.

Mheshimiwa Spika, Kamati haipingi mfumo wa stempu za kodi za kieletroniki kwa sababu umeonekana kuwa na manufaa makubwa. Jambo la msingi ni tofauti kubwa wa ushuru wa stempu hizo kwa kampuni ya sigara (TCC) na makampuni mengine, mfano makampuni ya bia yanatozw **Dola za marekani 8.55** kwa kila stempu 1000. Jambo ambalo halikuweza kupata majibu ya uhakika ni kwanini kampuni ya sigara ambayo inamiliikiwa na Serikali na Watanzania kwa asilimia 100 inatozwa **dola za marekani 20** kwa kila stempu 1000 kiwango ambacho ni karibia mara tatu ya kile wanachotozwa wengine. Aidha, ieleweke wazi kwamba tozo ya ETS sio ushuru wa bidhaa kwamba unatozwa kwa kiwango tofauti na bidhaa tofauti. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezo kuleta usawa katika utozaji wa ada hiyo.

3.3. Uanzishwaji wa Ofisi ya Mpokea Malalamiko ya Walipa Kodi “Tax ombudsman”

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2016 tulifanya mabadiliko kwenye Sheria ya Usimamizi wa Kodi na Kuanzisha Ofisi ya Mpokea malalamiko ya walipa kodi ambayo ingekuwa nchini ya Wizara ya Fedha na Mipango. Lengo ilikuwa ni kutoa fursa kwa walipa kodi kuwasilisha malalamiko yao wakati wote na sio kusubilia mikutano ya Mhe.Rais ambao huandaliwa na Baraza la Biashara Tanzania. Hadi hivi sasa mwaka umekwisha pita na Ofisi hiyo bado haijaanzishwa, Kamati inaitaka Serikali kuanzisha Ofisi hiyo haraka iwezekanavyo ili iweze kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa.

3.4. Kufuta faini na tozo kwa Makampuni ambayo hayajasaliwa katika mfumo wa sasa wa Usajili wa Makampuni kwa wakati Maalumu ili kutoa fursa kwa Makampuni hayo kujisajili;

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usajili wa Makampuni (BRELLA) imeanzisha utaratibu mpya wa usajili wa makampuni ambapo uitwao ORS (Online Registration System) mfumo huu unaunganisha namba ya usajili wa makampuni na ile ya mlipa kodi. Mfumo huu umeweza kusajili makampuni **141,593** yaliyoko katika kanzi data, yaliyosajiliwa katika mfumo wa ors hadi mwezi februari **17,939** tu na kati ya Makampuni hayo yaliyowasilisha Taarifa kwa usahihi ni makumpuni **11,505**. Hatua hii inasababisha Makampuni ambayo yamechelewesha kuleta taarifa kudaiwa faini **Shilingi 303,173,216, 833**. Kiwango hichi kinaonekana ni kikubwa kwa sababu takwimu sahihi ya makampuni ambayo yameanzishwa na kufanya kazi hayajulikani ni mangapi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwa Waziri wa Fedha kwa kushirikina na Waziri wa Viwanda na Biashara ili kufuta madeni hayo kwa muda maalumu na kuruhusu kampuni ambazo zipo na zinafanya kazi ila zinashindwa kuhuisha Taarifa zake kutokana na madeni hayo. Hatua hii itasaidia Serikali kujua idadi kamili ya Makampuni yaliyopo nchini na kuyatoza kodi kikamilifu.

3.5. Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa vifaa, vifungashio na mitambo muhimu katika Sekta za Kilimo na maji.

Mheshimiwa spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuondoa kodi ya Ongezeko la thamani kwenye sekta ya Kilimo ili kuhamasisha usindikaji na uwekezaji katika Sekta hiyo. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuondoa kodi hiyo kwa mitambo ya kuchimba visima, vifaa vyta kuhifadhia maziwa (Tanks and Cans). Aidha, inapendekezwa kuondoa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mitambo inayotumika kuchimbia mabwawa ili ipatikane kwa wingi na kusaidia Serikali katika juhudzi zake za

upatikanaji wa maji kwa binadamu na mifugo. Vile vile utaratibu wa VAT *deferment* unaweza kuangaliwa hasa ukisingatia kwamba bidhaa nyingi za Kilimo hazitozi VAT (Vat exempt).

3.6. Kutengeneza Mazingira wezeshi kwa Sekta ya Elimu

Mheshimiwa Spika, Sekta ya elimu ni moja ya sekta ambayo imeathirika kwa kiasi kikubwa na hatua ya Serikali kufunga mashule ili kupunguza maambukizi ya virusi vya **COVID-19**. Walimu zaidi ya 9,000 wamepoteza ajira zao lengo ikiwa ni waajili kukwepa kulipa kodi ya mapato (PAYE) kwa waalimu ambaao kimsingi hawafanyi kazi. Shule zilizoendelea na waalimu bila kuwapa barua ya kusitisha ajira walilazimika kulipa kodi ushuru na tozo nyingine za Serikali zinazoendana na malipo ya mishahara. Muswada huu wa Sheria ya Fedha haukutoa ahueni ya aina yoyote kwa sekta hii ambayo kimsingi inatoa huduma kwa umma na ndio maana Serikali inaweza kuchukua (Take over) ya shule yoyote ya Binafsi. Kamati inaishauri serikali kwanza kuangalia uwezekano kuruhusu Shule binafsi kuanzisha mifuko ya uwekezaji (Endowment Funds) pili ni kuweka mazingira ya mpito walau kwa mwaka mmoja kwa shule binafsi ili zirejje karika hali yake ya awali.

4.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kwanza kwa kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka 2020/21 mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili nimshukuru Mhe Dkt. Tulia Akson, Mb - Naibu Spika kwa ushirikiano wake. Aidha napenda nimshukuru Dkt. Philip Isidor Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijiji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Ndg. Doto James Katibu Mkuu, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango

na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kuchambua Muswada hadi kufikia hatua hii. Kamati pia inawashukuru wadau wote wa masuala ya kodi waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwakushuruku Wajumbe wa kamati ya Bajeti kwa umakinii, umahiri na uvumilivu wao wakati wa kipindi chote cha Bajeti hasa ukizingatia kwamba muda haukuwa rafiki sana. Ni matumaini yangu kwamba tutarejea wote ili kuendelea kuwatumikia wananchi wa Tanzania. Wajumbe hao ni: -

1. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb Makamu Mwenyekiti Mjumbe
2. Mhe. David Ernest Silinde, Mb Mjumbe
3. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb Mjumbe
4. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb Mjumbe
5. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb Mjumbe
7. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb Mjumbe
8. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb Mjumbe
9. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb Mjumbe
10. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb Mjumbe
11. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb Mjumbe
12. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb Mjumbe
13. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb Mjumbe
14. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb Mjumbe
15. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb Mjumbe
16. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mb Mjumbe
17. Mhe. Abdallah M. Bulembo, Mb Mjumbe
18. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb Mjumbe
19. Mhe. Stephen Julius Masele, Mb Mjumbe
20. Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb Mjumbe
21. Mhe. Andrew John Chenge, Mb Mjumbe
22. Mhe. Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mb Mjumbe
23. Mhe. Suleiman A. Sadiq, Mb Mjumbe
24. Mhe. Shally J. Raymond, Mb Mjumbe
25. Mhe. Joseph Kakunda, Mb Mjumbe
26. Mhe. Jummane Kibera Kishimba, Mb Mjumbe
27. Mhe. Dkt. Raphael Chegeni, Mb Mjumbe

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Ndg. Michael Kadebe, Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti, Ndg. na Makatibu wa Kamati Ndg. Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi na Lilian Masabala pamoja na wanasheria wa Ofisi ya Bunge akiwemo Ndg. Stephano Seba Mbutu na Ndg. Matamus Anangisye Fungo kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mashimba Mashauri Ndaki (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI

15 Juni, 2020

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Kama nilivyo sema awali nakushukuru sana, pamoja na Wajumbe wako kwa kufanya kazi kubwa sana, kwa niaba yetu Bunge, mmeifanya kazi yetu kuwa rahisi sana kwa sababu mengi mmeyaongea ndani ya Kamati na Serikali imeyapokea mengi, itayafanya kazi na mengine ni sehemu kubwa sana ya akiba ya vitu ambavyo wataendelea kuvifanya kazi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, karibu sana, una robo saa, jitahidi.

MHE. CATHERINE N. RUGE - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara

ya Fedha na Mipango, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2020. Kabla sijatoa maoni hayo naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuweza kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii, kumshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe (Mbunge) kwa kuniamini na kunithea kwa Naibu Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Fedha na Mipango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Mara na hususan wananchi wa Jimbo la Serengeti kwa kunipa heshima kubwa waliyonipa na ushirikiano wanaondelea kunipa toka nimekuwa Mbunge mpaka sasa. Nina imani Wananchi wa Jimbo la Serengeti watanipa ridhaa ya kuwa Mbunge wao katika uchguzi Mkuu wa Oktoba, 2020. Aidha, naishukuru familia yangu kwa upendo wao kwangu na pia kwa kunivumilia ninapokuwa mbali nao kwa muda mrefu kutohana na majukumu yangu ya Kibunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo desturi ya utekelezaji wa bajeti ya Taifa, Serikali imeleta mbele ya Bunge lako tukufu Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 ili kuomba ridhaa ya Bunge kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi ikiwemo baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya sheria mbalimbali na kurekebisha taratibu za ukusanyaji na usimamiaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni kama zilivyoanishwa hapo chini.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni kwamba Muswada huu umejengwa katika msingi wa kufikirika jambo ambalo litapelekea

utekelezaji wa sheria inayopendekezwa kuwa mgumu na hivyo kutofikia lengo la makusanyo ya mapato kama ilivyokusudiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu licha ya Serikali kukiri kuwa pato la Taifa litapungua kutokana na athari za covid-19 pamoja na madhara ya hali mbaya ya hewa kama vile mafuriko yaliyoikumba nchi yetu katika kipindi cha mvua za masika na kuathiri sekta kadhaa za uchumi hususani sekta ya kilimo na uchukuzi na licha ya uhalisia kwamba mlipuko wa ugonjwa wa COVID -19 umeendelea kutikisa uchumi wa dunia jambo ambalo ni dhahiri litaathiri mapato yetu yatokanayo na mikopo na misaada ya kibajeti. Bado Serikali imeendelea kuweka makisio makubwa ya makusanyo ya mapato bila kujali mazingira ya sasa ambayo yanaashiria kuyumba kwa uchumi wa dunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Maoni mahususi kuhusu Vifungu vya Muswada; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepitia Muswada huu kifungu kwa kifungu na kutoa mapendekezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148; Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sehemu ya 18 ya Muswada huu ambapo Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bima ya kilimo cha mazao itasamehewa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haipingi mapendekezo ya Serikali ya kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bima ya kilimo cha mazao kwani msamaha kwani msamaha huo unavutia wawekezaji wakubwa, na hasa sekta binafsi kuwekeza zaidi katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wawekezaji wakubwa wenye uwezo wa kulipia bima ya shughuli zao za kilimo ni wachache; hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuona namna ya kuwapa motisha ya kodi (*tax incentive*) wakulima wadogo wadogo wanaowakilisha takribani asilimia 80 ya Watanzania wanaojishughulisha na

kilimo ambao ndio wenyewe mchango mkubwa wa pato la Taifa linalotokana na shughuli za kilimo.

Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332; mapendeko ya Serikali kwenye kifungu cha 38 cha kupandisha kima cha chini cha watumishi wanaotakiwa kuachwa kwenye wigo wa kulipa kodi ya mshahara kupanda kutoka shilingi 170,000 hadi shilingi 270,000.

Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa kima cha chini kiwe shilingi 419,000 badala ya kinachopendekezwa na Serikali. Kiwango hiki ndicho kima cha chini kwa daraja la chini kabisa kwa watumishi wa Serikali, kwa mfano; walimu wanaoingia kwenye ajira kwa mara ya kwanza (*TGSTS B1*) kupandisha kiwango hicho hadi shilingi 419,000 itasaidia idadi kubwa ya watumishi kubaki na fedha za kutosha ili kumudu gharama za maisha na hivyo kuongeza uwezo wa kununua bidhaa za huduma ambazo zina makato ya kodi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza katika sehemu ya saba ya Muswada huu, kufanya marekebisho ya jedwali la pili kwa kufuta msamaha wa Kodi ya Mapato kwa wazalishaji walio ndani ya maeneo maalum kwa manaa ya *Special Economic Zones*) wanaozalisha bidhaa na kuuza ndani ya nchi kwa asilimia 100. Hatua hii inalenga kuweka usawa katika utozaji wa kodi ya mapato baina ya wazalishaji wa bidhaa walio nje na wa ndani ya maeneo maalum ya kiuchumi. Ushauri wa kufuta misamaha ya kodi kwenye maeneo maalum ya uwekezaji yaliwahi kutolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni miaka tisa iliyopita kuititia maoni ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wakati wa Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2011. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika maoni hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilirejea utafiti uliofanywa na Mtaalam Kankesu wa Australia, kuhusu tathmini ya maeneo maalumu ya uwekezaji kiuchumi yaani *Export Processing Zones* na *Special Economic Zones* uliochapishwa mwaka 2003 ukionyesha dhahiri kuwa nchi zinazoendelea bado hazifaidiki na uwekezaji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, miaka 10 iliyopita, Kambi Rasmi ya Upinzani ilipendekeza kufutwa kwa msamaha wa kodi katika vifungu 15, 19, 25 na 31 vya Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2011 vifutwe, lakini Serikali ilikataa kuchukua mapendekezo hayo leo miaka tisa baadaye Serikali ndio imeelewa na kuona umuhimu wa kufuta misamaha hiyo ya kodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332 inafanyiwa marekebisho kumpa Mamlaka Waziri wa Fedha kutoa msamaha wa kodi ya mapato kwenye miradi ya kimkakati yenye jumla ya kodi ya mapato isiyozidi shilingi bilioni moja bila kuwasilisha mapendekezo kwenye Baraza la Mawaziri. Aidha, Waziri mwenye dhamana ya fedha atafanya mashauriano na Mamlaka ya Mapato kabla ya kutoa msamaha wa kodi husika.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapinda mapendekezo haya na inalisihi Bunge lako Tukufu kukataa kupitisha mapendekezo haya kwa kuwa yana kila dalili ya kufungua mianya ya rushwa, ujisadi na ubadhifuru wa fedha za umma ikiwa tutakuwa na Waziri wa Fedha na Maafisa wa Mamlaka ya Mapato ambao sio waadilifu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hivyo, Kifungu hiki kama kinavyopendekezwa na mtoa hoja na kwa kauli yake mwenyewe kuwa nafasi yake na mazingira mengi na makubwa ya ushawishi ya kupokea rushwa hivyo inahitaji mtu muadilifu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasilitiza umuhimu wa kujenga mifumo imara itakayowadhibiti hata wale viongozi wasio waadilifu.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290; katika sehemu ya Tisa ya Muswada huu, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 kwa kuongeza kifungu kipywa cha 9(a) katika sheria mama ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya masuala yanayohusu Serikali za Mitaa kukusanya tozo ya huduma au *Service Levy*

ya asilimia 0.3 ya mapato ghafi kwenye sekta ya mawasiliano kwa niaba ya halmashauri, na kuyagawa mapato hayo kwa halmashauri zote ndani ya siku 14 baada ya kukusanya. Aidha, kwa mujibu wa Waziri wa Fedha, Waziri wa TAMISEMI ataandaa kanuni ambazo zitaweka utaratibu wa ukusanyaji na ugawaji wa mapato kwa kutumia kikokotoo maalum kwa kuzingatia kiasi cha Tozo ya Huduma kutoka sekta ya mawasiliano kwa kila halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, mapendekezo haya ni mwendelezo wa Serikali Kuu kudhibiti vyanzo vya Mapato ya Halmashauri jambo ambalo limezifanya halmashauri nyingi nchini kuwa maskini na kushindwa kuijendesha kutokana na vyanzo vyake vya mapato kuchukuliwa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutoa ahadi kuwa makusanyo ya tozo hiyo yatarudishwa kwenye Halmashauri husika ndani ya siku 14 lakini hakuna uhakika wa kufanya hivyo kwa kuwa masharti hayo ya kurejesha fedha hayakutajwa kwenye sheria pendekezwa isipokuwa Waziri atakuwa na hiari ya kuyaweka kwenye kanuni ikiwa atajisikia kufanya hivyo. Kitendo cha kumlimbikizia Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa mamlaka yote kuhusu hatima ya halmashauri na Serikali za Mitaa, bila kushirikisha mamlaka hizo kwenye maamuzi kinazifiedhehesha Mamlaka za Serikali za Mitaa na kinayafanya mahusiano katika Serikali za Mitaa na Serikali Kuu kuwa wa Mtumwa na Mtwana.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; kwa mujibu wa Waziri wa Fedha, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 ili kuziongeza Taasisi za Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*); Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (*TFRA*), Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (*GPSA*), na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*) kwenye orodha ya taasisi zinazochangia gawio au asilimia 15 ya mapato ghafi kwenye Mfuko wa Hazina. Pamoja na kwamba mapendekezo haya hayapo kwenye Muswada huu, lakini kwa kuwa Waziri wa Fedha alishayaeleza katika hotuba yake wakati akiwasilisha

bajeti ya Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani inayachukua kama sehemu ya sheria pendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina mgogoro na utoaji wa gawio kwa Taasisi mbalimbali kwenda Mfuko Mkuu wa Hazina. Hata hivyo, hatukubaliani na pendekezo la Serikali la kuchangia mapato ghafi, kwa kuwa ikiwa taasisi zitatoa gawio kutoka kwenye mapato ghafi kuna hatari ya taasisi hizo kubaki bila fedha ya kutosha kuweza kuijendesha. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba gawio hilo litolewe kwenye mapato halisi au *net revenue* baada ya kutoa gharama mbalimbali za uendeshaji ili kuziwezesha taasisi hizo kubaki na fedha za kuweza kufanya uwekezaji na uendeshaji wa vitega uchumi vyake na hivyo kuongeza mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370; Serikali inapendekeza kufanya Marekebisho ya Kifungu cha 10(a) cha Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370 kwa kuondoa maneno "*not financed through Government Budget*" ili kuruhusu Ofisi ya Msajili wa Hazina kukusanya asilimia 70 ya fedha za ziada kutoka kwenye Mashirika, Taasisi au Wakala yoyote itakayoonekana kuwa na ziada.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba mapendekezo haya yatadumaza Mashirika, Taasisi na Wakala za Serikali na yatapunguza kasi na ari ya mashirika hayo kufanya kazi kwa bidii ya kukusanya mapato na kuwa na ziada kwa kuwa ziada hiyo haitayanufaisha. Kitendo ambacho Serikali inakifanya hapa ni kuziamisha taasisi, mashirika na wakala kuwa ni dhambi kuwa ni dhambi kuwa na fedha za ziada.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalishauri Bunge kukataa mapendekezo hayo na badala yake taasisi, mashirika na wakala wa fedha ziruhusiwe kuwa na fedha za ziada ili ziweze kuendelea kufanya uwekezaji na biashara mbalimbali ili kupata mapato zaidi. Ikumbukwe kwamba mashirika na taasisi hizi tayari yanakatwa asilimia

15 ya mapato ghafi. Kuongeza makato mengine ya asilimia 70 ya fedha za ziada ni kuyaua mashirika na taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, SURA 82; Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Mafunzo na Ufundi Stadi ili kupunguza kiwango cha tozo kwa ajili ya maendeleo ya ufundu stadi kutoka asilimia 4.5 hadi asilimia 4. Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa kwa namna Sheria mama ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ilivyopitishwa huku kukiwa na ubaguzi katika tozo ya maendeleo ya ufundu ambapo ni watumishi wa sekta binafsi tu wanaotozwa na kuwaacha watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba, badala ya kupunguza asilimia tano ya tozo hili kama inavyopendekezwa kimsigi haimpi nafuu yoyote mwajiri. Serikali ipunguze tozo hiyo mpaka asilimia mbili ili kupunguza mzigo kwa walipaji na hasa kipindi hiki ambapo taasisi nyingi zimeathiriwa na janga la Corona.

Aidha, Serikali ipanue wigo wa tozo hii ili ilipwe pia na taasisi za Serikali zinazoajiri. Chimbuko la pendekezo hili ni kuweka usawa kwa waajiri wote katika kuchangia maendeleo ya ufundu kwa manufaa ya Taifa.

Hitimisho; Sheria hii inayopendekezwa ndio mwongozo wa utekelezajiwa bajeti ya Mwaka 2020/2021. Hata hivyo, yapo baadhi ya marekebisho yaliyopendekezwa na Serikali ambayo yanaweza kuwa kikwazo katika utekelezaji bora wa Sheria hii.

Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuitia upya maeneo yote ambayo tumeonyesha kasoro na kuyafanyia marekebisho kabla Muswada huu haujapitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, KUHUSU
MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA
MBALIMBALI NA.3 WA MWAKA 2020 (THE WRITTEN LAWS
(MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2020)
(Chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge,
Toleo la Januari, 2016) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

- 1. Mheshimiwa Spika**, Kama ilivyo kawaida yetu waungwana, naomba kuanza hotuba yangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa uzima na nguvu nydingi za kuendelea kuwatumikia Watanzania nikiwa na utimamu wa mwili na akili, ninawiwa kushukuru kwa kuwa wapo wengi ambaao walitamani kumaliza Bunge hili wakiwa na afya njema lakini kwa mapenzi yake, hawakuweza.
- 2. Mheshimiwa Spika**, Katika muendelezo huo nitoe pongezi za dhati kwa kwa uongozi mzima wa Chama changu (**CHADEMA**) kwa kufungua pazia kwa Watanzania na wanachama wetu wenyе sifa na vigezo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria za nchi yetu, kujitokeza kuonesha nia ya kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nawapongeza ambaao tayari wameshatumia haki yako ya Kikatiba na wale ambaao bado, naamini mtakuwa mnakamilisha maandalizi binafsi ili mtangaze nia zenu rasmi.
- 3. Mheshimiwa Spika**, Kwa kipekee kabisa, nitoe wito kwa wanawake wenyе sifa za kugombea nafasi ya Urais kujitokeza na kutangaza nia zao. Ninaamini kwamba kuititia Mwenyekiti na Katibu wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA waliopewa dhamana ya kuongoza Baraza la Wanawake CHADEMA, wataongoza wanawake wa chama chetu wenyе uwezo katika mchakato huu wa ndani ya chama wa kuomba ridhaa ya chama chetu kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- 4. Mheshimiwa Spika**, napenda kuwakumbusha Waheshimiwa viongozi wote mliomo humu ndani ya ukumbi

wa Bunge kwamba baada ya Bunge hili kumaliza uhai wake wa miaka mitano, Taifa hili linatarajia kuingia kwenye Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba, 2020. Kwa mantiki hiyo naomba kuwakumbusha kuhusu utawala wa sheria ambao hautoi fursa kwa baadhi ya viongozi kuvunja Katiba na kuandaa mazingira ya kujivekea kinga ya kutochukuliwa hatua za kushitakiwa. Katika hilo naomba niwakumbushe matakwa ya Ibara ya 13(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inasema kwamba; "*Watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki, bila ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria*"

5. Mheshimiwa Spika, Kwa nukuu hii ya Katiba naomba viongozi tutafakari upya utaratibu wa sasa ambao unakua kwa kasi wa kutunga sheria kwa lengo la kuwekeana kinga za kisheria kwa uvunjifu wa Katiba ambao viongozi watafanya, badala ya kutunga sheria za kuwawajibisha sasa tunatunga sheria za kuwalinda viongozi wetu dhidi ya makosa wanayotarajia kufanya.

B. MAONI KUHUSU VIFUNGU MBALIMBALI VYA SHERIA ZINAZOPENDEKEZWA KUFANYIWA MAREKEBISHO:

6. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa utangulizi huo wa pongezi na kuwatakia kheri wanachama wanaoanza safari ya kuomba ridhaa ya chama chetu katika mchakato wa kumpata mgombea wa nafasi ya Urais, naomba sasa niangalie hoja iliyo mbele yetu inayohusu marekebisho ya sheria mbalimbali zilizoletwa kupitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 3 wa Mwaka 2020 (**THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2020**)

7. Mheshimiwa Spika, muswada huu unaopendekezwa unazifanya marekebisho jumla ya sheria kumi na tatu (13) ambazo ni:

- i. Sheria ya Ustawi wa Wanyama, Sura ya 154;
- ii. Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu wa Msingi, Sura ya 3;

- iii. Sheria ya Chuo cha Elimu ya Biashara, Sura ya 315;
- iv. Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi, Sura ya 223;
- v. Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54;
- vi. Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1;
- vii. Sheria ya Uendeshwaji wa Mahakama, Sura ya 237;
- viii. Sheria ya Maboresho ya Sheria Kuhusu Ajali Mbaya na Masharti Mengineyo, Sura 310;
- ix. Sheria ya Serikali ya Urekebu wa Sheria Mbalimbali, Sura ya 4;
- x. Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania, Sura ya 425;
- xi. Sheria ya Uendeshaji wa Bunge, Sura ya 115;
- xii. Sheria ya Masuala ya Rais, Sura ya 9; na
- xiii. Sheria ya Uhifadhi wa Wanyama pori, Sura ya 283.

8. Mheshimiwa Spika, sababu za mapendekezo ya marekebisho ya sheria tajwa hapo juu, zinaleezwa kuwa ni maboresho yaliyochochewa na wakati kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezwaji wake. Kwa sababu hizo, maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni yatajikita katika sheria zifuatazo;

i. SHERIA YA USTAWI WA WANYAMA, SURA YA 154

9. Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 4 cha muswada kinarekebisha kifungu cha 9 cha sheria kwa kuongeza kifungu kipyä cha 9A, kinachohusu mahusiano katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Wizara. Kifungu kipyä cha 9A(2) kinasema kuwa; “.....upon consultation with the Minister responsible for Finance and the Minister responsible for Local Government Authorities, suspend such local government authority from

collecting revenues sourced from the livestock sector". Kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba mbali na mashauriano kati ya Waziri wa Fedha na Waziri mwenye dhamana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamisha mamlaka husika ya Serikali za Mitaa kuacha kukusanya mapato yatokanayo na sekta ya mifugo.

10. Mheshimiwa Spika, jambo hili la halmashauri kusitishwa kukusanya mapato yatokanayo na sekta ya mifugo kwa hoja kuwa mapato yaliyokuwa yanapatikana yameshindwa kusimamiwa vizuri kuendeleza sera ya mifugo na Halmashauri husika. Hoja hiyo ni dhaifu sana kwani sheria na taratibu za kinidhamu dhidi ya wahusika ziko wazi kabisa na hakuhitajiki kuziadhibu Halmashauri kwa kosa la mtendaji mmoja tu ambaye ni Mkurugenzi au Mkuu wa Idara husika.

11. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona dhana nzima ya kifungu hiki kinachoongezwa ni mwendelezo wa nia ovu ya Serikali kupoka vyanzo vya mapato vya Halmashauri na kuvirejesha Serikali Kuu na hivyo kuua kabisa dhana nzima ya ugatuaji wa madaraka (D BY D). Kwa muktadha huo Kambi Rasmi inashauri kifungu hicho kipycha cha 9A kifutwe.

**ii. SHERIA YA UTEKELEZAJI WA HAKI NA WAJIBU WA MSINGI,
SURA YA 3**

12. Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kuifanya marekebisho Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu wa Msingi, Sura ya 3, kwa kufanya marekebisho katika Kifungu cha 4 ili kuweka masharti yanayotaka mtu ye yeyote anayekusudia kufungua shauri lolote la Kikatiba chini ya Ibara za 12-29 zinazohusu haki za msingi kuidhihirishia mahakama ni kwa kiasi gani mlalamikaji ameathiriwa na ukiukwaji wa haki anayolalamikia.

13. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7 cha muswada huu ambacho kinarekebisha kifungu cha 4 cha sheria mama kwa kuongeza Kifungu cha 4(2) ambacho kinamtaka mpeleka maombi mahakamani kueleza katika hati ya kiapo ni kwa namna gani ameathiriwa na uvunjwaji wa haki za binadamu

kama zilivyoainishwa katika Ibara ya 12-29 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

14. Mheshimiwa Spika, Ni muhimu Bunge hili tukufu liweze kutofautisha kati ya uvunjifu wa Ibara ya Katiba na uvunjifu wa haki za msingi za Kikatiba. Uvunjifu wa ibara ya Katiba unaweza kupingwa na kila mtu kwa kuwa unahusu ulinzi wa Katiba na uvunjifu wa haki za msingi unaweza kupiganiwa na mtu ambaye haki zake za msingi zimekiukwa.

15. Mheshimiwa Spika, Mabadiliko ya vifungu hivyo yanakiuka Ibara za 26(2) ambayo inasema; "*Kila mtu ana haki, kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria, kuchukua hatua za kisheria kuhakikisha hifadhi ya Katiba na sheria za nchi*" Sasa kwa kuwa Katiba haisemi mtu huyo lazima awe ameathirika na jambo hilo; sheria hii ikipitishwa na Bunge lako tukufu itakutana na mkwamo wa matakwa ya Ibara ya 64(5) za Katiba ambayo inasema; "*Bila ya kuathiri kutumika kwa Katiba ya Zanzibar, kwa mujibu wa Katiba hii kuhusu mambo yote ya Tanzania Zanzibar yasiyo mambo ya Muungano, Katiba hii itakuwa na nguvu ya Sheria katika Jamhuri nzima ya Muungano na endapo sheria nyngine yoyote itakiuka masharti yaliyomo katika Katiba hii, Katiba ndiyo itakuwa na nguvu, na Sheria hiyo nyngine, kwa kiasi inachokiuka Katiba itakuwa batili.*"

16. Mheshimiwa spika, Ikiwa Bunge hili tukufu litapitisha mabadiliko ya vifungu hivyo, ni dhahiri kwamba vifungu hivyo vyta sheria vitakuwa batili kwa kukinzana na Katiba, kwa sababu Kifungu cha 4(2) kinachopendekezwa kipo kinyume na Katiba na kinakinzana na Ibara za 26(2)ambayo nimeirejea hapo juu, na 30(3) inayosema; "*Mtu ye yoyote anayedai sharti lolote katika sehemu hii au katika sheria yoyote inayohusu haki yake au wajibu kwake, limevunjwa, linavunjwa au inaelekea litavunjwa na mtu ye yoyote popote katika Jamhuri ya Muungano, anaweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu*". Ni wito wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba Bunge lisifanye marekebisho katika vifungu vyta sheria vinavyopendekezwa kwa kuwa kwa maoni yetu vinakiuka Katiba na hivyo vitakuwa batili.

- 17. Mheshimiwa Spika**, kila kiongozi wa umma anapoingia madarakani anaapa kuilinda Katiba pamoja na sheria. Ibara ya 26(1) ya Katiba inatoa wajibu kila mtu kufuata Katiba na kutii sheria za Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Dhana ya Ibara ya 26(2) ni kwa ajili ya uwajibikaji na kuilinda Katiba yenewe. Kwa kutaka kwa anayetaka kwenda mahakamani kutaka tafsiri ya uwajibikaji itakuwa ni kuivunja Katiba yenewe na pia kuondoa dhana ya uwajibikaji hasa kwa viongozi wanaotakiwa kusimami ana kulinda Katiba na sheria.
- 18. Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 7 cha muswada kinaongeza pia kifungu cha 4(3). Hata hivyo Ibara mbili za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinazotajwa, yaani Ibara za 26(2) na 30(3) za Katiba zinalezea msingi wa kufungua shauri katika mazingira tofauti. Wakati Ibara ya 26(2) inaruhusu mtu ye yeyote kwenda mahakamani ***kwa ajili ya kuilinda na kuitetea Katiba dhidi ya uvunjifu*** na hivyo kuruhusu mashauri yenye maslahi kwa umma; Ibara ya 30(3) inazungumzia msingi wa mtu ye yeyote kufungua shauri ***kwa sababu ya uvunjifu wa hakizake*** za msingi ambazo zipo katika Ibara za 12 – 29 za Katiba. Ibara ya 30(3) haihusiani na uvunjifu wa Ibara za Katiba.
- 19. Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Ibara hizo mbili zime weka mazingira ya aina mbili tofauti, na ambazo haziwezi kutekelezwa kwa pamoja na mtu mmoja, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba; Kifungu cha 4(3) kifutwe kwa kuwa hakina maana yoyote zaidi ya kufanya kutaka Ibara ya 26(2) itekelezwe sawa na Ibara ya 30(3) jambo ambalo kisheria haliwezekani.
- 20. Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 7 cha muswada kinarekebisha kifungu cha 4 cha sheria mama kwa kuingiza kifungu kidogo cha 4(4). Pamoja na kwamba Mwanasheria Mkuu ni mshirika katika mashauri yote ya madai mahakamani yanayohusu Serikali, ni muhimu kwa wadaiwa kuhusishwa wao wenyewe na si kutenda makosa halafu akashitakiwa mtu mwengine ambaye ni Mwanasheria Mkuu. Pia kwa kuweka kipengele hiki inaondoa dhana nzima ya uwajibikaji

na kiapo cha mhusika. Aliyeapa lazima awajibike kwa matendo yake.

21. Mheshimiwa Spika, Nje ya kuondoa msingi wa uwajibikaji ulioelezwa katika aya ya 15 ya hotuba hii, kifungu hiki kinakinzana na Ibara ya 26(1) ya Katiba ambayo inamtaka kila mtu kuheshimu Katiba na wale wavunjifu wa Katiba wanaweza kupelekwa mbele ya mahakama chini ya Ibara ya 26(2) na 64(5) ya Katiba. Kuwashtaki maafisa au watumishi wa umma waliohusika na uvunjifu wa haki au Katiba unalenga kuhimiza uwajibikaji na uwazi kwa watumishi wa umma. Hakuna sababu ya msingi juu ya mapendekezo ya kifungu cha 4(4) na hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba kifungu hicho kifutwe.

22. Mheshimiwa Spika, Kiujumla, marekebisho haya yanapoka uhuru wa wananchi kufungua mashauri ya Kikatiba, mashauri yanayohusu haki za binadamu na hivyo kufunga milango ya Mahakama kwa wananchi kudai haki zao za msingi. Hii pia ni kinyume na Ibara ya 26 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inayompa mamlaka kila mmoja kufungua shauri katika Mahakama.

23. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba Serikali ya Tanzania ilizuia asasi za kiraia pamoja na raia kufungua mashauri katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwa kujitoa pamoja na kuwa mahakama hiyo ipo Tanzania, Serikali sasa inatunga sheria ya kuzuia raia wake kudai na kupigania haki kwa njia za amani katika mahakama zake za ndani.

24. Mheshimiwa Spika, Kuwazuia raia kutafuta haki zao katika mahakama za haki na taratibu zilizowekwa Kikatiba hupelekea watu kutafuta njia mbadala kuhakikisha wanapata haki zao hasa matumizi ya nguvu na kujichukulia sheria mkononi. Ni kwa mantiki hiyo basi, mifumo ya haki inapaswa kufanya kazi kwa kuheshimu haki, sheria na Katiba ili kusaidia kukuza amani katika nchi. Hivyo hivyo mifumo ya haki inayolenga kuzuia watu wasitafute haki hupelekea machafuko katika nchi.

25. Mheshimiwa Spika, Bunge hili tukufu linawajibu wa kutunga sheria za nchi ambazo hazipaswi kutungwa kuwalenga watu fulani. Ikiwa tutatunga sheria kwa kuwalenga watu, itakuwa ni kinyume na taratibu za utungaji sheria. Hoja hii inajionesha katika dhana ya kutaka watu waoneshe maslahi binafsi au namna gani wao binafsi wameathirika ni kushawishi na kuendeleza uvunjaji wa haki.

26. Mheshimiwa Spika, Marekebisho katika kifungu cha 7 cha muswada yanapendekeza mashauri yote ya madai dhidi ya Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Spika, Jaji Mkuu na Naibu Spika yafunguliwe dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Marekebisho haya ni kinyume na misingi ya mgawanyo wa mamlaka baina ya mihimili mbalimbali katika nchi lakini tayari kuna maamuzi mbalimbali ya Mahakama ambayo yameshaamua kuwa Rais pamoa na viongozi wengine nao wanaweza kushtakiwa ikiwa watavunja Katiba.

27. Mheshimiwa Spika, Baadhi ya maamuzi hayo ni; Addo Shaibu dhidi ya Joseph Pombe Maguful na Mwenzake Misc. Civil Cause. Na. 29 ya 2018; Zitto Zuberi Kabwe dhidi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mwenzake Misc. Civil Cause Na. 1 ya 2020; na shauri la Paul Revocatus Kaunda dhidi ya Spika na wenzake Misc. Civil Cause Na. 10 ya 2020. Wakati maamuzi haya yakikaribishwa kwa mikono miwili na wapenda haki, sasa mbele yetu kuna muswada wa kuondoa uvezekano huo wa kuwashitaki.

iii. SHERIA YA UENDESHAJI WA MAHAKAMA, SURA YA 237

28. Mheshimiwa Spika, Muswada huu katika sehemu ya nane, unapendekeza kuifanya marekebisho Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama, Sura ya 237, kwa kufanya marekebisho ya kuongeza kifungu kipyaa cha 65A kwa lengo la kuweka masharti ya kinga dhidi ya mashtaka kwa Jaji Mkuu, Majaji na Maafisa wengine wa Mahakama katika utekelezaji wa majukumu yao ya kimahakama.

29. Mheshimiwa Spika, Kinga dhidi ya Majaji na Mahakimu ni muhimu lakini kuwakinga watumishi wengine dhidi ya makosa katika utekelezaji wa majukumu yao ya kimahakama itatoa

uhuru zaidi wa kukwamisha utoaji haki mfano kupoteza mafaili au makosa mengine. Kinga kwa watumishi wa mahakama ni kinyume na Katiba na Sheria za Kimataifa kwani binadamu wote ni sawa na hakuna aliye juu ya sheria na kila mmoja anapaswa kutendewa kwa haki. Ni wito wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Bunge hili kutafakari pia uwepo wa sheria nyingine za Kimataifa tunapotekeleza majukumu ya Kibunge.

30. Mheshimiwa Spika, Hata hivyo maneno ya kifungu kipywa cha 65A hakielezi maneno “maafisa wengine wa mahakama” ni watu gani hasa na ukakasi huu utaleta changamoto ya utekelezwaji wa sheria hii. Kwa mfano kwa mujibu wa Sheria ya Mawakili, Mawakili wote pia ni maafisa wa mahakama, swali la kujiuliza hapa ni kama kwa sheria hii sasa wanawekewa kinga katika muktadha huo.

31. Mheshimiwa Spika, Kwa mtazamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, mtumishi au mwajiriwa wa Idara ya Mahakama ni mtumishi wa umma kama alivyo mtumishi wa Bunge au mtumishi yejote wa ofisi ya umma. Hivyo kufanya ubaguzi wa kuwawekea kinga wale ambaa ni waajiriwa wa Idara ya Mahakama ni kuleta ubaguzi na pia kutoa hisia kuwa watumishi hao kuna kitu ambacho wanafanya kinyume na maadili yao ya utumishi na hivyo muda ukifika au kwa msemo kuwa za mwizi ni arobaini, ndio maana wanawekewa kinga. Kinyume na hapo hakuna sababu yoyote ya msingi ya kuwawekea kinga inayohalalisha uzembe na kutokuheshimu kazi zao katika utendaji wa kila siku.

iv. SHERIA YA MABORESHO YA SHERIA KUHUSU AJALI MBAYA NA MASHARTI MENGINEYO, SURA YA 310

32. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa ya muswada huu inapendekeza kuifanya marekebisho sheria ya maboresho ya sheria kuhusu ajali mbaya na masharti mengineyo, Sura ya 310 kwa kuongeza Kifungu kipywa cha 18A.

33. Mheshimiwa Spika, uzoefu wa kuwaunganisha maafisa wa umma wanaohusika na uvunjifu wa haki ililenga kuongeza ufanisi, uwajibikaji na uwazi katika sekta ya umma. Kifungu

hicho kinapaswa kufutwa ili kuongeza uwajibikaji kwa matendo yanayohusu uvunjifu wa haki za raia au Katiba lakini pia kuongeza uwazi katika sekta ya umma.

34. Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 18A, kinakinzana na Ibara ya 26(1) inayotaka kila mmoja kuheshimu Katiba ya nchi na yeoyote anayekiuka misingi ya Katiba basi atafikishwa Mahakamani chini ya Ibara ya 26(2) na 64(5). Kwa kuwekewa kinga Katiba haitaheshimiwa kwa kisingizio cha kuwekewa kinga. Hata hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inapata mashaka pale inapoona sheria nyingi zikiwasilishwa ili kuongeza kinga kwa baadhi ya viongozi, wakati vipindi vilivyopita viongozi wetu walikuwa na kinga kiasi, kwa maoni yetu, tunaona kuna uvunjifu mkubwa wa Katiba unatarajiwa kujitokeza huko mbeleni na haya ni maandalizi ya kutowawajibisha wahusika. Pia tuangalie kwenye mazingira ya kupata kiongozi mbovu huko mbeleni tutamdhiliti vipli? Kila mtu anatakiwa kuwajibika kwa matendo yake.

v. SHERIA YA SERIKALI YA UREKEBU WA SHERIA MBALIMBALI, SURA YA 4;

35. Mheshimiwa Spika, Dhana nzima ya marekebisho yanayopendekezwa na Serikali, kwa mtazamo wetu yana nia ya kupoka madaraka na majukumu ya Bunge ya kuwa chombo pekee kwa mujibu wa Katiba chenye mamlaka ya kutunga sheria katika nchi hii.

36. Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 39 kinachofanyia marekebisho kifungu cha 4 cha sheria, katika kifungu kidogo kipya cha 3 na 4 vinavyosomeka kwamba;

"(3) Notwithstanding any other provision to the contrary, the Attorney General may require the Chief Parliamentary Draftsman to carry out a specific revision of any written laws. (4) Notwithstanding the provision of section 12(1), the written laws revised in terms of subsection (3) shall come into operation on such date as the Attorney General may, by notice published in the Gazette, appoint.;"

37. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa ina wajibu mkubwa wa kulinda na kutetea Katiba Ibara ya

4(1) inayosema kwamba; “..... *vyombo vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma vitakuwa ni Bunge na Baraza la Wawakilishi*” ; Ibara ya 63(3)(d) inayosema kwamba; “**Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake Bunge laweza kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwapo sheria**”- na Ibara ya 64(1) inayosema kwamba; “*Mamlaka yote ya kutunga sheria juu ya mambo mengine yote yahusuyo Tanzania Bara, yatakuwa mikononi mwa Bunge*” .

38. Mheshimiwa Spika, Mujibu wa marekebisho yanayopendekezwa na Serikali yanaondoa mamlaka ya Bunge kutunga sheria na badala yake kuyapeleka kuwa chini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali akimtumia Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Bunge-CPD na kumpelekea Rais aipitishé ili ianze kutumiwa na Mhimili wa Mahakama, rejea kifungu cha 41 cha muswada. Aidha, kama jambo hilo litapitishwa maana yake Miswada ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (*Written Laws-Miscellaneous Amendments*) litakuwa ni jukumu la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu akishirikiana na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Bunge - Chief Parliamentary Draftsman-CPD. Jambo hilo ni kinyume na pia ni uvunjifu wa Katiba yetu.

39. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii yafutwe kwani yanaenda kinyume na Katiba na hivyo kupora mamlaka ya Bunge kuwa ndio chombo pekee cha kutunga Katiba.

vi. SHERIA YA SHULE YA SHERIA TANZANIA, SURA YA 425

40. Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 43 cha Muswada kinarekebisha kifungu cha 2 cha Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania, ili kuwezesha sheria hiyo kutoa msamaha kwa baadhi ya wanasheria kutopitia kwenye mafunzo ya Shule ya Sheria.

41. Mheshimiwa Spika, Mapendekezo haya yanaanzisha mjadala mpya wa nini hasa lengo la kuanzishwa kwa shule hiyo. Ukiangalia kwa undani utagundua hoja ya Serikali ni uzoefu wanaoupata wanasheria hao ambaa sasa

watapaswa kupata msamaha wa kutopita Shule ya Sheria. Ni kwa nini sasa vijana wanaohitimu shahada za sheria wasipelekwe Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mahakani au Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kipindi fulani ili kupata uzoefu na baadaye wakawa mawakili ili kuokoa wanansheria wengi walioko mitaani kwa sababu ya kukosa ada za kusoma shule hiyo ya sheria?

42. Mheshimiwa Spika, Ikiwa si kwa lengo la kubagua basi msamaha huo upanue wigo zaidi ya wanasheria wa Serikali ili pia wanasheria waliostaafu utumishi wa umma, wanasheria kutoka sekta binafsi na wanasheria wengine wenye sifa waweze kunufaika na utaratibu huu. Kwa hali ilivyo sasa, marekebisho haya, yanaweka matabaka na sheria hiyo itakuwa kinyume cha Katiba hususani Ibara ya 13(1),(2) na (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

vii. SHERIA YA UENDESHAJI WA BUNGE, SURA YA 115;

43. Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 45 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 5 cha sheria mama kuhusu uundwaji wa idara na vitengo kama ambavyo Tume ya Huduma za Bunge itakavyoona inafaa katika utendaji bora wa Bunge. Lakini marekebisho yanayoletwa na Muswada huu ya kufanya marekebisho kifungu cha 5(1) kwa kuweka ulazima wa marekebisho hayo yaridhiwe na Rais.

44. Mheshimiwa Spika, Bunge ni muhimili unaojitegemea kwa mujibu wa Katiba na kwa dhana hiyo unatakiwa uwe na mamlaka kamili katika utendaji kazi wake. Kitendo cha kuhitaji ridhaa au idhini ya Rais katika maamuzi yake ni kuondoa **autonomy** ya mhimili wa Bunge, na hivyo ni dhahiri kuwa Bunge litakuwa chini ya Serikali na itakuwa kinyume cha Katiba na dhana nzima ya mgawanyo wa madaraka.

45. Mheshimiwa Spika, Serikali kutoa fedha za uendeshaji wa Bunge haina maana kuwa maamuzi ya Bunge litakavyokuwa linafanya kazi ni lazima yatoke au yatolewe na Serikali. Kama ni hivyo basi haitakuwa na maana yoyote ya uwepo wake, kwani maamuzi yote ya Bunge ni lazima yapate baraka za

Serikali kwa maana ya Rais. ***Check and balance*** itatoka wapi kama Bunge litaendelea kupo rwa madaraka yake?

46. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa mapendekezo yanayoletwa na Serikali yatupiliwe mbali na sheria iendelee kubaki kama ilivyo. Tunaamini kuwa Bunge lina rasilimali watu yenyeye utaalal na maadili ya kutosha kuweza kufanya yale yote ambayo Tume inakuwa imeyatolea uamuizi.

viii. SHERIA YA MASUALA YA RAIS, SURA YA 9

47. Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 49 cha Muswada kina mapendekezo ya marekebisho ya Kifungu cha 6 ili mashauri dhidi ya Rais kwa mambo anayodaiwa kuyatenda yeye binafsi kama raia na ambayo yameruhusiwa kufunguliwa dhidi yake kwa mujibu wa Ibara ya 46(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yafunguliwe baada ya kutoka madarakani. Ni dhahiri kwamba kifungu hiki kitakuwa kinakinzana na matakwa ya Katiba kwa kuwa kifungu cha 46(2) kimeshaweka utaratibu wa namna ya kufanya.

48. Mheshimiwa Spika, kama kifungu hiki kitarekebishwa kitakuwa kinakinzana na matakwa ya Ibara ya 46(2) na kwa vyovoyote vile sheria ya kawaida haitaweza kufanya kazi mbele ya Ibara ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

49. Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 7(1) cha Sheria ya Masuala ya Rais ambacho kinapendekezwa kurekebisa ili mashauri yoyote dhidi ya Rais yafunguliwe dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, Kambi ya Upinzani inapenda kufahamu kwani kifungu kinasema kwamba; “**(1) Proceedings against an act or omission by the President other than those referred to in section 6.....**” wakati kifungu cha 6 cha sheria mama kinatamka utaratibu wa kumshtaki Rais katika “**personal capacity**”. **Sasa haya makosa mbali ya yale yake binafsi yaliyoainishwa, ni makosa gani yatakayohitaji aunganishwe na AG ni yapi? Je, kama ni makosa yake binafsi kwa nini atumike Mwanasheria Mkuu wa Serikali? Kwa nini asimtumie mwanasheria wake binafsi?**

50. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani tunapendekeza kifungu hiki kifutwe na badala yake sheria iruhusu mtu aliyehusika katika uvunjfu wa Katiba au haki za kiraia kuwajibika katika Mahakama.

51. Mheshimiwa Spika, sababu za mapendekezo haya ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni kuongeza uwazi na uwajibikaji katika utumishi wa umma na usawa mbele ya sheria.

C. HITIMISHO

52. Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha ni kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge na Bunge hili tuangalie kwa tafakuri pana marekebisho ya sheria zinazoletwa na Serikali ili kupata ridhaa ya kuwa sheria.

53. Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba mambo mengi ambayo yanakuwa na hila mara nyingi yanaletwa kuititia miswada hii ya marekebisho ya sheria mbalimbali, kwani kwa ujumla mapendekezo kama haya ya kufanya mabadiliko ya sheria kwa dharura hayatofautiani na mapendekezo yaliyoletwa katika vipindi mbalimbali na uzoefu unaonesha kwamba sheria zote zilizopita kwa utaratibu huu zimekuwa ni sheria mbaya kabisa. Sheria zote zinazotungwa zinapaswa kuendana na Katiba. Tukipitisha sheria hii kama ilivyo tutaingia kwenye historia ya Tanzania kama Bunge lililoua utawala wa sheria na dhana ya uwajibikaji. Tutageuka mfano wa wanazuoni duniani katika tafiti zao katika masuala ya utawala bora, kinga za viongozi, uwajibikaji, utawala wa sheria na konstituisional supremacy.

54. Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha!

.....
SALOME WYCLIFFE MAKAMBA (MB)
MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI
KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

09 Juni, 2020

SPIKA: Ahsante sana, ahsante sana. Tunaingia kwenye uchangiaji kwa utaratibu wa dakila tano tano. Tunaanza na Mheshimiwa Jitu Soni atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu dakika tano nenda *straight* kwenye unachotaka kusema ni nini ukichelewa tu dakika tano zinakwisha.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nashukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kuleta Muswada huu wa *Finance Bill* ambao ni mzuri sana na umelenga sehemu kubwa kwa sekta ya kilimo kwa msaada mkubwa wa kuondoa tozo nyingi na ada mbalimbali lakini pia ombi letu kwamba Serikali iendelee kutekeleza ile *blue print* na jambo ambalo ni muhimu kwa sisi wote. Ule muda ambao tunajadili ile *budget cycle* tungeomba badala ya kuwa ile Julai - Desemba na wanapopokea maoni ya kubadilisha tozo na ada mbalimbali ibadilishwe iwe Januari -J uni ili kipindi cha pili basi kuwe na utekelezaji na wote anaopanga bajeti zao katika ngazi za halmashauri na wizara mbalimbali wajue nini kinachotakiwa kupanda au kushuka.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tulikuwa tunaomba ni upande wa *BRELA*; tunaiomba Serikali iendelee kuondoa tozo na *penalty* ambazo zipo kwenye *land submission* za Kampuni mbalimbali ili kwenye *database* wakati wanapotaka kuingia kwenye mfumo wa kielektroniki na kutumia mfumo wa digitali basi iweze kukubalika kwasababu sasa hivi mpka walipe madeni ndiyo mfumo huu uweze kukubalika.

Mheshimiwa Spika, tuipongeze Serikali kwa kuondoa tozo nyingi kwa upande wa *horticulture* kwenye upande wa *killing* na upande wa *refrigerator trucks* tungeomba basi msamaha huo pia uendelee kwa upande wa Nyama, Samaki, Maziwa kwasababu bidhaa ni hizo hizo zinazotumika ili iweze kufanyakazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tulikuwa tunaomba Serikali ifikirie namna ya kuondoa msamaha wa *EF moving*

equipment (mitambo ya kuchimba maji na kutengeneza mabwawa) ambapo sekta zingine zinapata msamaha huo kwa kupitia msamaha wa kodi ambapo bidhaa zao huwa zina kodi. Kwa upande wa kilimo kwasababu bidhaa nyingi hazina VAT basi msamaha huo wanashindwa kuupata.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo jingine ambalo pia tumependekeza ni kwamba, *solar water pumps* ziweze kusamehewa kodi ili ziweze kutumika maeneo mbalimbali bchini zitapunguza gharama za upatikanaji wa maji zikiletwa kama umwagiliaji haina kodo lakini zikiletwa kwa matumizi mengine ya maji zina kodi kwa hiyo, pia tungepata msamaha huo ingeweza kusaidia sana kupunguza gharama za maji hasa huko vijiji mabapo bili za umeme mahali tulipopata umeme asilimia kubwa sasa hivi tunatumia umeme zitapunguza gharama hiyo na zitasaidia Serikali kupunguza gharma hizo za upatikanaji wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuipongeze Serikali kuondoa tozo mbalimbali kwa upande wa *Fire*. Nilikuwa naomba pia jambo moja lilitosahaulika kwasababu liko kwenye Kanuni basi Serikali iweze kuangalia namna ya kuondoa *Fire* katika kilimo ile ambayo tunalipa kwa hekari. Wanaolipa ni yale Makampuni tu ambayo yamesajiliwa lakini kwa wakulima wengine haipo kwahiyio wangeondoa hiyo pia ingekuwa inaondoa tozo moja ambayo ni usumbufu.

Mheshimiwa Spika, tuipongeze Serikali pia kwa upande wa *SDL* kupunguza kutoka asilimia 4.5 kurudi mpaka asilimia nne.

Ombi letu ni moja kwamba asilimia mbili ya ile fedha inakwenda kwenye *loans board*. Tulikuwa tunaomba asilimia zote nne zirudi sasa iende kwenye *vocational training* kwa sababu VETA nyingi sasa zinajengwa.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia 100. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jitu Soni. Nilishakutaja Mheshimiwa Balozi utafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Ruge halafu Mheshimiwa Magdalena Sakaya ajiandae.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Spika, ningependa sana kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu ambao ni muhimu snaa ili kuweza kukazia Bajeti ambayo tumeipitisha leo hii.

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja nitakwenda wkenye vifungu ambapo nitaanza na kifungu cha utakatishaji fedha (*Anti-money lorrying*) ambacho kimeletwa kwa ajili ya mabadiliko. *Para ya nne ambayo inabadilisha kifungu cha tatu cha neno la "beneficial owner".* Mabadiliko haya yanamfanya mnufaika wa mwisho aweze kuhakiki taarifa zake ambazo zinaweza kupatikana kwa usahihi lakini mabadiliko haya ni mazuri ila tulitoa angalizo kwamba mnufaika wa mwisho na ambaye ameingizwa kwenye *anti-money lorrying registration* Serikali lazima itenganishe huyu mtu wa mwisho ambae kwa hisia nyingine inawezekana kuna *criminality* iko pale na pia kuna muwekezaji ambaye yuko pale ambaye Sheria yote imewajumuisha kwa pamoja mpaka kwenye Sheria za Makampuni ya biashara.

Mheshimiwa Spika, sasa ni vizuri Serikali ikatenganisha ili iweze kuona huyu Muwekezaji inamuweka kwenye mazingira mazuri ya kibashara badala ya kujumisha yote kwa upande mmoja na suala hili Serikali ilikubali na ikasema kwamba italifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwenye Sheria ya *electronic and postal communication act* ambalo linaondoa Kampuni za Serikali ambazo zina hisa 100 au ambazo Makampuni ambayo yana hisa pamoja na Serikali ya asilimia 25 sasa badiliko hili ni zuri ambalo linaamuru uwekezaji wa hisa. Kama utakumbuka kwamba Serikali iliamua Makampuni ya simu yote yajiorodheshe kwenye soko la hisa la Dar es Salaam *stock exchange* lakini ni Kampuni moja tu ambayo imejiorodhesha ambayo ni ya *Vodacom* sasa haieleweki ni

kwanini Makampuni mengine hayajapa muwamko wa kuweza kujiorodhesha kwenye soko la hisa.

Mheshimiwa Spika, lakini ni vizuri kwamba Serikali imeamua kutoa haya Makampuni ambayo yana hisa na Serikali au yenye asilimia 25 sasa hii itaongeza biashara kwasababu biashara ya Makampuni ya minara ambayo kwa asilimia kubwa yanamilikiwa na Mtu mmoja, Kampuni moja ya Helois sasa itafanya *competition*ili watu wengine waweze kuingia kwenye biashara hiyo ya minara.

Mheshimiwa Spika, lingine ni *amendments*ya *National parks* ambapo kifungu cha 56 mpaka 59 na pia kifungu hicho pia kimekwenda kwenye Sheria ya Ngorongoro *Conservation Act* kwa kifungu 60 mpaka 63 na Sheria ya *Wildlife Management Conservation Authority*. Sasa sheria hizi zinataka kuondoa mamlaka hizizisiweze kukusanya mapato ambayo wanapata na kuipa mamlaka *TRA* kwa ajili ya ukusanyaji wake.

Mheshimiwa Spika, suala hili lilileta hofu kwamba uchukuwaji huu wa *TRA* basi huenda ikapararazi mamlaka hizi za *Ngorongoro*, *TANAPA* pamoja na *Wild Life* na kuweza kufanya *operations* ambazo zinafanyika kule kila mara kukwama, tukitilia maanani kwamba utalii kwa kweli ni sekta ambayo inachangia karibu asilimia 17.5.

Mheshimiwa Spika, suala hili tumelijadili kwa kina na Serikali imekubali na imeona umuhimu wake na ikaamua kwamba huenda fedha zote ambazo zitakusanywa na *TRA*, basi zitakuwa *ring-fenced* ili kuweza kuhakiki; kwamba itaanzisha kituo maalum na kuweka Maofisa maalum ambao watashughulikia mapato yote yanayoshughulika na mamlaka hizi ili kuhakikisha kitu hiki hakiwezi kukwama. Kama suala hilo litashughulikiwa itaondoa ile hisia na hofu ambayo ipo mionganoni mwa wengi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi, nakushukuru sana. Mheshimiwa Catherine na Mheshimiwa Magdalena jiandae.

MHE. CATHEINE N. RUGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia Muswada ulioko Mezani. Mchango wangu utajikita zaidi kwenye Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Taifa (*The National Park Act*) pamoja na *The Ngorogoro Conservation Area Act*.

Mheshimiwa Spika, wote tunatambua umuhimu wa Sekta ya Utalii na jinsi gani ambavyo sekta hii imekuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa kwenye uchumi lakini pia kwenye ajira katika nchi hii. Serikali imeleta Marekebisho ya Sheria ili kuwapa *TRA* uwezo wa kukusanya mapato kwa niaba ya hizi hifadhi.

Mheshimiwa Spika, tunatambua siku zote hifadhi hizi zimekuwa zikiweza kukusanya mapato na kujiendesha lakini mmekuja na hii sheria kwa kusema sababu ni *Covid 19*, lakini nadhani *Covid 19* imetumika kama kichaka tu, kwa sababu Waziri alisema kwamba hakuna madhara makubwa yaliyosababishwa na *Covid 19* kwenye uchumi lakini pia tumeambiwa watalii wanaingia na kama kweli ni *Covid* mngeweza kuwapa *subsidize*.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwendelezo wa kuendelea kunyang'anya taasisi na Wakala wa Serikali mapato na kuzifanya zisiweze kujiendesha. Serikali hii imekuwa ina vivu kwa kuona taasisi zinazojiendesha na zinakusanya mapato kwa wingi mnaamua kuzinyang'anya ili sasa Serikali Kuu iweze kwenda kupanga matumizi. Nahisi pesa hizi zikienda kule zitakwenda kwenye matumizi mengine mfano kujenga reli, kujenga *Stiegiler's Gorge* na kununua ndege na hazitarudi kwa *National Parks*. Kwa sababu tumeona ni pesa nyngi sana ziko *ring-fenced* lakini hazirudi. Mlianza na Halmashauri, mmekuja kwenye korosho na sasa mmekuja kuua Hifadhi za Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunatambua hifadhi ni nne tu ambazo zinaendesa hifadhi nyingine zote, sasa leo mnaenda kuchukua mapato kurudisha Serikali hii. Mnachokifanya mnakwenda ku-*demoralized* kwanza wafanyakazi wasiweze kufanya kazi kwa sababu watakuwa hawana uhakika wa hizo pesa kama zitarudi au la. Pia tuliona *issue* ya *centralization* haifanyi kazi; Halmashauri zimekuwa paralysed, kwa nini tunaendelea kuchukua kila kitu? Kwa nini tunafanya *monopoly* ya kila kitu? Nashauri Hifadhi za Taifa ziachwe ziendelee kukusanya mapato na ziweze kujidoresha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nado kuna sheria inayompa mamlaka Msajili wa Hazina aweze kukata asilimia 70 ya mapato ya ziada (*net revenue*), bado kuna asilimia 15 ya pato ghafi. Hivi hiyo asilimia 15, 70 na 85; hiyo asilimia 15 inaenda kufanya nini? *I can assure you*, hizi Hifadhi za Taifa zinakwenda kufa, haziwezi kuwa *effective*, haziwezi kuwa *efficient* kwa sababu hata kwa shughuli za kawaida watashindwa kujidoresha.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzungumzia Sheria ya Kodi ambayo inakwenda kubadilisha *threshold* ya *payee*. Wafanyakazi ambao wanapata shilingi 270,000/= wasiweze kupata kodi. Kwenye taarifa yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani tumependekeza, badala ya shilingi 270,000/= basi *minimum threshold* ya mshahara ambao wafanyakazi hawatakatwa kodi iwe ni shilingi 419,000/=. Kwanza kwa miaka mitano mfululizo Serikali hii imeshindwa kuongeza mishahara kwa wafanyakazi, bado *minimum threshold* inabaki shilingi 270,000/=. Shilingi 419,000/= ni mshahara wa Mwalimu wa Daraja III ambaye anaanza kazi.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Spika, dakika moja. Akikatwa yale makato mengine, anabaki na shilingi

300,000/= . Hivi kweli shilingi 300,000/= *how do you survive?* Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aweze ku-*consider* hii *minimum threshold* kutoka shilingi 270,000/= kwenda shilingi 419,000/=.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Catherine. Kama nilikusikia vile unaenda Serengeti! Mimi mwenyeji Serengeti. Kwa jina hilo, inabidi uangalie jina; wale jamaa sijui kama watachagua hilo jina lako la pili. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kidogo kwenye Muswada ulipo mbele yetu. Naomba nianze na Marekebisho ya Sheria ya Ardhi Sura ile ya 113 ya kumtaka mtu aliyepimiwa ardhi awasilishe maombi ndani ya siku 90 na hapo hapo aanze kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, sheria imeeleza na Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hili halitahusu taasisi za Serikali ambazo zinapima maeneo na kuza. Nataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba kuna zaidi ya Taasisi za Serikali, ziko taasisi na makampuni binafsi mengi tu zaidi ya 100 ambayo yanashikiliwa na Serikali kwa ajili ya kupima maeneo na kuza. Sasa haya hayapo. Kwa hiyo, haoni kwamba hii ni *double standard?* Kwa yale ambayo yalikuwa yanasaidia sana wananchi ardhi kuweza kupimwa na wanauzu, sasa wao wanaingia kwenye utaratibu wa kulipa *immediately* badala ya siku 90. Kwa hiyo, naomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba wananchi wanapenda sana wamiliki maeneo yaliyopimwa na kumiliki kisheria; na wanapenda hata mashamba yao yamilikiwe kisheria, kiutaratibu kwa maana ya umiliki. Shida ni kwamba Wizara ya Ardhi haijawezesha kikamilifu kuhakikisha kwamba kila kipande kinapimwa na kumilikiwa kihalali na kwa wananchi wote. Ndiyo maana leo ukienda kwenye Idara za

Ardhi zote, hata hapa Dodoma nenda hapo Manispaa, utakuta kuna foleni kila siku kwa sababu kila mtu anatembea na *documents* zake, lengo lake ni kwamba ahakikishe anamiliki ardhi iliyopimwa, amiliki kihalali na ali pe kodi stahiki ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali kwamba tatizo siyo wananchi, kwa hiyo, tusianze kuwapa utaratibu ambao utawakwaza wananchi wakati wananchi wote tunapenda kumiliki maeneo yaliyopimwa. Kwa hiyo, naomba niungane na Kamati kwamba huu utaratibu wa umilikishaji uweze kuwa *solved* ndani ya Wizara na ndani ya Serikali, wasianze kuwa-*punish* wananchi kwa sababu wote tunapenda kumiliki eneo ambalo liko kisheria na tulipe kodi ambazo ni stahiki.

Mheshimiwa Spika, linge la pili ni hii Sheria ya Hifadhi ya Taifa Na. 283 lakini pia ya Ngorongoro 284 pamoja na ile ya *TAWA* ambayo imeanzishwa 2014. Kwa mara nyingine tunashauri kwa sababu tunalipenda Taifa letu, kwa sababu tunajua uhifadhi unahitaji kitu gani? Uhifadhi hausubiri ukaombe *OC* irudi ije. Wakati unasubiri *OC*, tayari huku umeshaharibikiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikumbuke kwamba huko nyuma wamewahi kumiliki mashirika yakawashinda kama Serikali, wameyabinafsisha kwa sababu walishindwa; ni ngumu. Baada ya kubinafsisha, yako mengine ambayo yamefanya vizuri. Serikali inapata kile ambacho ni stahili yake; kodi na tozo nyingine.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Serikali hapa imeeleza kupitia Mheshimiwa Waziri, akisema kwamba lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba taasisi hizi zinatumia utaratibu wa kibajeti wa kiserikali pamoja na kuongeza ufanisi. Nasema kwamba hakuna taasisi ya Serikali yoyote ambayo inafanya shughuli zake bila kufuata mfumo wa Serikali na utaratibu, ninakataa. Kwa hiyo, nina imani kabisa *TANAPA, TAWA na Ngorongoro*, wanafanya *budgeting* na wanaidhinishiwa na

mamlaka iliyoruhusiwa ndani ya taasisi hizo na watumia kibajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba na Serikali pia ina uwezo wa kuweka watu ndani ya hayo mashirika kufanya *cost and balance au check and balance* kama kuna fedha inakwenda vipi inatumika vibaya. Lengo letu kama Taifa, kama Wabunge ni kuhakikisha kwamba taasisi hizi zinakwenda kufanya kazi kwa ufanisi kama zilivyokuwa zinafanya. Kwa utaratibu huu, kuchukuwa fedha kupeleka kwenye Mfuko Mkuu wakasubiri *OC*, mwisho wa siku tumeomba hapa angalau kuwepo na *retention* angalau asilimia 20 au 25% ili wakati wanasubiri *OC* ya Serikali, shughuli huku zinakwenda.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema kwamba hata kwenye Muswada imekuja vile vile. Sasa hii kweli ni dhamira ya Serikali? Wameshahamua wabadilike lakini tutapata majibu siyo chini ya miaka miwili juu ya hifadhi zetu, juu ya hizi *WMA* zote, za *TAWA* zote na Ngorongoro, tutapata majibu tu. Juzi nimesema hapa, leo ni miezi miwili ya *Corona*; watu hawana mshahara, wanaisubiri Serikali. Basi Serikali ingeangalia basi, ingejuwa kwa sababu kuna *Corona* na kwa sababu walikuwakuwa wanapata ile 15 percent, wangeenda kulipa watumishi. Nninaapoongea, hawajapata fedha ya mshahara au kwamba matumizi yote yanaenda Serikalini?

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri asije akaacha kitu ndani ya nchi hii ambacho watu watamkumbuka kwa mabaya. Amefanya mazuri mengi, tunaomba aache *legacy*, mashirika haya ya hifadhi yafanye kazi kwa ufanisi, yaweze kujitegemea. Serikali isipende kumkamua ng'ombe mpaka inywe na damu, iridhike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, uhifadhi wenyewe, utalii unachangia asilimia 17, lakini bado kuna tozo mbalimbali na hifadhi zinakwenda vizuri, tusizipoteze...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya, naona unavyoongea kwa uchungu. Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima, atafuatia Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Mbaraka Dau, utatufungi.

MHE. HASNA S. MWILIMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuleta Muswada huu wa Sheria ya *Finance Bill*. Nina mambo machache tu madogo. La kwanza ni hii Sheria ya Ardhi ambayo mzungumzaji aliyetoka kuzungumza amesisitiza. Hofu yangu ni hizi siku 90 ambazo zimebekwa kwenye hii Sheria Sura Na. 113.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wanapenda wapimiwe maeneo yao lakini changamoto ambazo tunazo huko chini hatuna watumishi wa kutosha kwenye Halmashauri zetu. Kwa hiyo, kinachotokea, tunapotaka kuomba kupimiwa maeneo, mara nydingi, hata Halmashauri zetu wanasesma ngoja wawatafute wale wapimaji binafsi. Sasa kwa sheria hii, mtu tayari ameshahangaika anaambiwa siku 90 hajapata hati ina maana ataanza sasa kubanwa kisheria kwamba ardhi ile ichukuliwe na hatimaye irudi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa nafikiri kama ambavyo Kamati imeshauri, kwa sababu hili suala la utoaji hati liko katika Wizara husika. Basi tuwaacie Wizara husika na tumeona Mheshimiwa Waziri wa Ardhi amejikita sasa hivi kuweka wale Makamishna wa Ardhi kwenye kila Mkoa; kwa hiyo, nafikiri hii sheria tukiipitisha kidogo inaweza ikawa ina changamoto zake.

Mheshimiwa Spika, lingine ni hii Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura Na. 290. Sina tatizo na suala la hawa wadau wa Sekta ya Mawasiliano kuomba kwamba sheria

ibadilike na badala yake walipe moja kwa moja, yaani walipe eneo moja badala ya kulipa kwenye Halmashauri zetu. Hofu yangu tu ni hiki chanzo cha Halmashauri. Halmashauri zetu vyanzo vingi vimechukuliwa na Serikali Kuu. Sasa kwa sheria hii Na. 290, hiki chanzo kikilipwa moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ina maana: Je, marejesho yale yatakuwa yanarejeshwa kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, naona hata kwenye Taarifa ya Kamati imeonesha msisitizo wa hizi pesa ambazo zitakuwa zinalipwa kwenye chanzo kimoja kwa maana ya Mfuko Mkuu wa Serikali, basi tumwombe Mheshimiwa Waziri, marejesho yawe yanafanyika kwa usahihi katika Halmashauri zetu ili chanzo cha mapato kwenye Halmashauri zetu yasiweze kupungua.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania Sura Na. 390 hii ambayo inahusu kujumuisha Sheria ya Mamlaka ya Ngorongoro, *TANAPA* na *TAWA*.

Mheshimiwa Spika, nimeona tunataka kufanya mabadiliko ya sheria hii ili sasa makusanyo yafanywe na *TRA*. Hofu yangu ni moja tu. Wote tunajua kwamba *TANAPA*, Ngorongoro pamoja na *TAWA* haya makusanyo Ada, Tozo mapato yao ndiyo yanatusaidia kule chini; unaomba Zanahati, wanatuchangia, wanajenga Zahanati; madaraja yamebomoka, wanatusaidia wanajenga; barabara kiwango fulani hakipitiki, wanatusaidia. Sasa hofu yangu ni moja tu, *TRA* wakichukua hivi vyanzo wakakusanya wao, watakumbuka kurejesha? Hatuoni kwamba sasa *TANAPA*, Ngorongoro, *TAWA* tutaanza kukosa ile misaada ya kijamii? Hofu yangu ilikuwa ni hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie moja, hili ambalo Kamati imeshauri namna ambavyo uanzishwaji wa Ofisi ya Mpokeaji wa Malalamiko ya Walipakodi. Naunga mkono hoja ya Kamati kwa sababu nami nipo kwenye Kamati. Kuna malalamiko mengi sana ya Walipakodi wanashindwa namna ya kuyafikisha kwa Serikali na badala yake wanasubiri

Mheshimiwa Rais awaite wadau ndio wapate fursa ya kulalamika pale mbele ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hili *desk* la walalamikaji, wale ambao wana malalamiko mbalimbali, labda wamedhulumiwa. Labda kodi wamelipa visivyo; basi waweze kuanzisha ili walipakodi wote wapate eneo ambalo watakuwa wanalamika badala ya kumsubiri Mheshimiwa Rais ndiyo waanze kulalamika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na pia naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, sana. Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Mbaraka Dau utakuwa wa mwisho, baadaye Mheshimiwa Lukuvi.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba *Covid 19* imeathiri sana Sekta ya Utalii na ndiyo maana kwa maeleo yao, Serikali imeamua kuchukua hatua hii ambayo wameichukua wakiamini kwamba watakwenda kusaidia mamlaka zinazohusika na hifadhi zetu na mamlaka nyingine zote ambazo ziko kwenye eneo la Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, madhara ambayo yatasababishwa na hatua hii inayochukuliwa kama jinsi ambavyo yameelezwa na Waheshimiwa Wabunge wengine ni makubwa sana. Kwa sababu sote tunafahamu kwamba fedha ikishaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina na ikishakusanya na Mamlaka ya Mapato itakuwa ni vigumu sana fedha hii kuweza kurudi kwenye Mamlaka hizi na kuweza kufanya kazi ambayo inatakiwa.

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi, umekuwa Mjumbe wa Bodi ya Ngorongoro, unafahamu. Umekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili kwa muda mrefu, unafahamu kazi ambazo Mamlaka hizi kama *TANAPA* na

Ngorongoro na kadhalika ambazo wanafanya. Ukishaweka urasimu wa mapato yao kukusanya na Mamlaka ya Mapato; na hii hadithi ya *Ring-fencing* haipo, haijawahi kufanya kazi nchi hii! Haipo kabisa, ni kujidanganya, ni *self-deceit*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nadhani kuna haja kubwa sana ya Bunge hili kumwomba Waziri wa Fedha pendeleko hili lisitelezwe. Lisiwepo kwenye sheria kwa sababu ni pendeleko ambalo litakuwa na madhara makubwa. Pendeleko ambalo naomba Wizara ya Fedha ilitazame ni namna gani ya kuokoa Sekta ya Utalii kwa kupitia kwenye Sheria ya Fedha. Waziri wa Maliasili na Utalii alliambia Bunge hapa kwamba jumla ya watu 480,000 kwenye Sekta ya Utalii wapo kwenye hatari ya kupoteza kazi baada ya *Covid 19* kuikumba dunia.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, kuna makampuni ya Utalii ambayo yanakwenda kuafilisika. Baadhi ya Makampuni yameshapokea fedha kutoka kwa wateja wao ambao wame-cancel/safari zao, lakini Mamlaka ya Mapato tayari imekwenda kwenye akaunti za hiso Kampuni na kuchukua fedha. Kiasi kwamba Makampuni haya hayawezi kulipa, kurejesha fedha za Wateja ili kurejesha amani na imani kwa Tanzania ili waweze kuja wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba tusiichezee Sekta ya Utalii. Sekta hii ndiyo kuku anayetaga mayai ya dhahabu. Inaingiza nchini asilimia 27 ya mapato ya fedha za kigeni. Kwa hiyo, *measures* ambazo tulipaswa kuziona kwenye bajeti ni *measures* za kuisaidia Sekta angalau iwe katika hali ya kuweza kuamka huko ambako tunakwenda. Kwa hiyo, ni muhimu sana kama TANAPA na Ngorongoro wameingia kwenye mgogoro, wana matatizo ya fedha, Serikali iwapatie fedha, lakini isiende kuchukua vyanzo hivi vyaa mapato. Kwa sababu kuvirudisha itakuwa ni kazi ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwenye korosho, *export /levy* ya korosho ilipochukuliwa. Ni kwamba Serikali

inachungulia ni wapi kuna fedha nyingi? Inaingiza mikono na ni lazima iharibu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018 hapa tulikuwa tuna mgogoro mkubwa wa korosho, Serikali ikatuambia kwamba imefanikiwa kuuza tani 120,000 za korosho. Taarifa ambayo Waziri wa Fedha ameisoma hapa Bungeni juzi tarehe 11 inaonesha kumbe waliuza tani 70,000 tu katika korosho tani 313,000 ambazo wananchi walivuna wakati ule. Tani laki mbili na ushee ziko wapi Serikali ilizimwaga baharini, ilizichoma kwa sababu rekodi ya taarifa ya hali ya uchumi inaonesha ni tani 70,000 tu ambazo ziliuzwa. Kitu ambacho kimesababisha hasara ya dola za Kimarekani milioni 357 katika fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, sasa mambo kama haya hatuwezi kuyaacha tu yaende, kwamba iharibiwe korosho tukae kimya, uharibiwe utalii, naomba jambo hili liweze kufanyiwa marekebisho ambayo yanapaswa kufanywa ili kuiokoa Sekta ya Utalii na tusiangushe Ngorongoro na *TANAPA* na wenzao, waweze kufanya kazi yao ya uhifadhi sawasawa, wahudumie watalii sawasawa na tuhakikishe ya kwamba baada *Covid 19* mashirika haya yataweza kufanya kazi yake vizuri na nchi yetu tutaweza kurudi katika hali nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mbaraka Dau, baada ya hapo Waziri Lukuvi, dakika tano tano jamani, muda leo ni dhahabu.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia Muswada huu wa Fedha. Nitaanza na hili ambalo wengi wamekuwa wakizungumza hapa, mabadiliko ya sheria kuhusu Sheria ya Hifadhi ya Taifa, Sura 282 ambapo naona kwa kiasi kikubwa sana kumekuwa na upotoshaji na ni vizuri tukaweka kumbukumbu sawasawa. Mzungumzaji aliyepita Mheshimiwa Zitto, namheshimu sana, lakini kwa makusudi kabisa amekuwa akipotosha. Katika jambo ambalo

amelisisitiza zaidi ya mara mbili kwamba eti kitendo cha kufanya *ring fencing* hakijawahi kufanya kazi popote nchi hii, huu ni upotoshaji wa dhahiri kabisa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, leo tumesambaza umeme *almost* Tanzania yote, kigezo kikubwa ni hii hii inayoitwa *ring fencing*, sasa leo anasimama Mbunge anasema kwamba *ring fencing* haijawahi kufanya kazi sehemu yoyote nchi hii, huo ni upotoshaji wa hali ya juu. Kana kwamba hiyo haitoshi Mfuko wa Maji tumeona umekuwa *ring fenced* na mambo yanakwenda vizuri, usambazaji wa maji unaendelea katika nchi yote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge ama Mheshimiwa Zitto kwa makusudi ameamua kulipotosha Bunge au pengine hakumsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anawasilisha. Waziri wa Fedha amesema waziwazi kabisa kwamba fedha hizi zitakapokuwa *ring-fenced* na mifano wakatoa, akatoa mfamo wa TAA, akatoa mfano wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama na akatoa mfano wa TRA. Sasa lini TRA wame-suffer mishahara? Lini TAA wame-suffer mishahara? Lini vyombo vyetu na ulinzi na usalama vimekosa mishahara kwa sababu fedha zimekwenda katika Mfuko Mkuu. Haya mambo ni vizuri tukayaweka katika muktadha wake wa kiukweli. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nataka tu kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Sheria namba 664 ya Mwaka 1986, hii inapiga *bang* ya ku-export mkaa. Tumekutana na wadau ambao wanafishaa kule eneo la *Stiegler's Gorge* ambapo baadaye itakuja kujengwa bwawa pale kwa ajili ya kuzalisha umeme. Yale magogo wamepewa na Serikali waweze kuyachoma na wapate mkaa ili waweze kuuza, kufidia fidia ya kusafisha lile eneo na wao wenye wapate chochote. Kubwa zaidi kuna fedha zaidi ya trilioni 2.7 kwenye ile biashara ambayo ndani yake kutakuwa na kodi za Serikali, kutakuwa na tozo za Serikali, kutakuwa na mapato ya Serikali. Sasa leo wale wadau wanaondolewa linaingizwa jeshi kwa ajili ya kusafisha. Hatuna tatizo kwa kuingiza jeshi, lakini ushauri na hili tumelizingumza kwenye Kamati kama wanaamua

kuliingiza jeshi basi wapeleke hata watu wa Nyumbu au wapeleke Suma JKT badala ya kusafisha kwa maana ya ku-*destroy* wasafishe kwa maana ya kuvuna, Serikali yenyewe sasa ichome mkaa na iuze nje kwa sababu kuna pesa nyngi na inaweza ikaisaidia nchi yetu. (*Makofj*)

Mheshimiwa Spika, muda si rafiki sana na sikupata bahati kwenye kuchangia bajeti kuu, naomba kwa dakika moja tu nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wangu wa Mafia kwa heshima kubwa waliyonipa. Kwa muda wa miaka mitano tumefanya mambo mengi sana, tumejenga gati, kivuko tayari cha kwanza, kivuko cha pili kinakuja baada ya miezi miwili, tumejenga jengo la halmashauri pale kwa bilioni tano, tumepata Kituo cha Afya Kirongwe, tumefanya ukarabati mkubwa wa hospitali ya wilaya, tumepata mradi wa maji Jibondo...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimalizie kusema kwa sekunde tano tu, msanii maarufu wa Zanzibar Sitti Binti Saad anasema Zanzibar ni njema, atakaye aje na mimi nasema Mafia ni njema atakaye aje, tukutane site. (*Makofj*)

SPIKA: Ahsante sana Mbaraka Dau, umetukumbusha habari za Sitti Binti Saad.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara

ya Fedha na Mipango kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napongeza kwa Waziri wa Fedha kwa kuleta muswada mzuri ambao umelenga pia hatua za kupambana na janga la Covid-19. Pia hatua ya punguzo la *SDL* kwa waajiri ni muhimu katika kulinda na kuzalisha ajira na pia punguzo la *PAYE* kwa wafanyakazi ni faraja kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika mapendelekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ardhı Sura 113, nakubaliana na Kamati kuwa hili ni la kiutendaji zaidi na linaweza kuzoretsha upimaji na mipango miji kwa vile wananchi walitikia hatua za Serikali za kuboresha mipango miji. Napendekeza kuboresha utoaji wa hati mara tu baada ya upimaji kuidhinishwa na kama ilivyo kwa taasisi za Serikali, makampuni ya kibashara ya ardhi yasilazimike kupewa hati mpaka pale watakapopata wateja wa kumiliki viwanja husika.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la mabadiliko ya Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332, Ibara ya 36 unakusudia kubadilisha kifungu namba 83(1) cha zuio la kodi kwa mawakala wa mabenki. Hatua hii inakinzana na hatua za kibenki katika kukabiliana na janga la Covid-19 na hata Sera ya Serikali ya *Financial Inclusion* hasa kwa maeneo ya vijijini. Zuio hili la kodi litasabibisha kuongezeka kwa gharama za huduma za kibenki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Waziri Lukuvi, halafu Waziri wa Fedha. Waziri wa Fedha jiandae robo saa tu manake hoja zako nyingi zimekubaliwa.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ili nichangie Muswada huu lakini katika eneo la Sura 113 ya marekebisho ya ardhi. Kwanza nataka nimtoe hofu Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, halafu ndugu yangu

Mwilima, Catherine na Mama Sakaya. Kwamba marekebisho haya yana nia nje ya Sura hii ya 113. Serikali imefanya kazi kubwa sana ya kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi. Kwenye bajeti ya safari hii mmetuongeza nguvu ya pesa na vifaa vya kufanya kazi hiyo na sisi wenyewe tumekuwa tunatoa fedha hata kwenye halmashauri. Mamlaka za upangaji halmashauri wamefanya kazi kubwa sana na tumeongeza nguvu hata kwenye kampuni binafsi.

Mheshimiwa Spika, *process* ya kupanga na kupima, mwisho wake tunataka mtu awe na eneo lililo salama kwa kupata hati, yaani *process* hii ya upimaji inakupelekea mwisho kwenye hati. Ukipanga ardhi na ukipima bila kuchukua hati hujafanya lolote. Hivi sasa ninavyoongea sisi tumeshapanga nchi hii, hivi sasa tuna vipande vya ardhi vilivyopangwa, viko *surveyed* mchoro umeshaidhinishwa tumeshaweka na yale mawe 900,000, wenyewe hawajachukua hati mpaka leo, kwa kipindi tofauti. Kwa nini? Kwa sababu ukipanga na kupima kuchukua hati ni hiyari, kwa hiyo mtu anakaa miaka mitano au sita, mpaka ule mchoro unakuja kuvurugika. Mamlaka za upangaji halmashauri wengine wametumia pesa zao kupanga na kupima, lakini yule waliyempimia hataki kwenda kuchukua hati, hamna muda ambao unamwelekeza kwamba katika kipindi hiki lazima achukue ile hati.

Mheshimiwa Spika, Ubungo, tumefanya kazi ya urasimishaji kwa gherama za Serikali, tumepima vipande 6,000 lakini mpaka leo waliokwenda kuchukua hati hawafiki hata 100.

Kwa hiyo ndugu zangu hakuna *process* ya kupanga na kupima bila kumilikisha. Umilikishaji huu kama tungekuwa tumemilikisha vipande hivi 900,000 tungekuwa tuna uwezo wa kupata zaidi ya shilingi bilioni 100 kila mwaka kutoka kwenye hivi vipande 900,000 ambavyo vimeshapangwa na kupimwa na kuwekwa kila kitu. Kwa hiyo hapa tunataka kuwapa ulinzi salama wamiliki. Tunaposema kupanga kila kipande cha ardhi bila wamilikaji, mchoro peke yake haukupi usalama wa miliki yao. Kwa hiyo, tunataka tuwahakikishie tu wananchi kwamba hapa tunashughulika na *surveyed plots*.

Mheshimiwa Spika, naomba nimweleze Mheshimiwa mama Mwilima kwamba, hatuendi kwenye mashamba ya wananchi ambayo hatujaweka mawe, hatuendi huko, tunakwenda kwenye *surveyed plots* ambapo kila mwananchi ameomba kupimiwa, mamlaka ya upangaji halmashauri zenu zimepanga, lakini hati ile ni hiyari ya mtu kwenda kuchukua. Hawachukui, ule mchoro baada ya miaka miwili au mitatu, watu wanavamia, unavurugika, unatakiwa tena ku-resurveyeneo lile lile. Kwa hiyo hii ina nia njema, tuwasaidie wananchi vipande vyao vya ardhi vipate hati, kwa sababu zile hati ndizo zinazoleta usalama wa ardhi zao na ndizo zinazokwenda benki kukopa pesa, sio mchoro ule na mawe yale ya kwenye *site*, kwa hiyo tuwasaidie. Sisi hatuji kunyanganya maeneo yenu ya mjini ambayo hatujayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, leo tumenunua vifaa vya zaidi ya shilingi bilioni tatu na nusu, tumevisambaza kila mkoa na tunaanza kununua vifaa vingine vya upimaji ku-support halmashauri kwa ajili ya kuanza kupima na kupanga. Hata hivyo, kuna faida gani kama unamwekea mtu mpaka mawe anayachungulia lakini haendi kuomba hati? Haimsaidii yeye wala haiisaidii Serikali. Kwa hiyo hili ni jambo lile lile lakini tunataka tushirikiane ili kuhakikisha kwamba ardhi ya mwananchi inalindwa kwa kuwa na hati iliyo salama. Tufikishe mwisho, tupange, tupime, halafu tumilikishe, kila mtu awe na ardhi iligomillikishwa iwe salama zaidi.

Mheshimiwa Spika, nataka tu kutoa hofu hiyo, hii ina nia njema kwa Serikali, tutapata mapato lakini na ulinzi na usalama wa mwenye ardhi yake. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama nilivyosema mambo mengi yako upande wako, basi robo saa inakutosha ili tuingie katika Bunge Zima, shughuli hii ya Muswada huu ningependa tuimalize asubuhi hii kusudi jioni tukianza moja kwa moja, baada ya muda mfupi, tumkaribishe Waziri Mkuu kwa hotuba yake. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia na kutoa mapendelekezo na maoni kwenye Muswada huu. Yote ni heri kwa ajili ya kujenga nchi yetu na kuhakikisha tunatunga sheria ambayo itawezesha utekelezaji wa bajeti yetu tulioipitisha hivi sasa, kwa hiyo nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, napenda nitolee ufanuzi katika baadhi tu ya maeneo. Kwanza Kamati ya Bajeti nawashukuru sana, tulikuwa na mjadala mkali kweli, jana mpaka usiku na yaliyo mengi ambayo walikuwa wametushauri tumeyaweka kwenye marekebisho (*schedule of amendments*) kwa hiyo kweli tunawashukuru sana kwa kuboresha kile ambacho tulikuwa tumewasilisha awali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kurekebisha tafsiri ya maneno *beneficial*/ambayo kwenye *Anti Money Laundering Act*, napenda niseme tu kwamba lengo la tafsiri tulioleta ni kuwatambua wanufaika katika makampuni ili tuweze kuzuia utakatishaji wa fedha haramu ili tuweze kudhibiti ufadhilii wa ugaidi na ukwepajji wa kodi. Kama tukibadilisha marekebisho ya tafsiri hii, itaondoa dhana iliyokusudiwa na hivyo tunaweza tukashindwa kufikia lengo. Kwa kuwa tafsiri hii inatumika duniani kote, nadhani sisi tunavyoona ni kwamba matumizi yake yatawezesha Serikali kupata taarifa za kikodi za Mataifa mengine ambayo tayari tunafanya nayo makuballiano. Kwa hiyo tunadhani kwamba hii tafsiri ni vyema ikabaki kama ambavyo tumeweka.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na suala la msamaha kwenye vifungashio na mitambo muhimu katika upande wa kilimo na maji, Mheshimiwa Jitu, mapendelekezo nafikiri ni mazuri, ni ya kufikiriwa, lakini ushauri wa Serikali na wa Bunge zima ni kwamba, ni vyema haya mapendelekezo ili yachambuliwe vizuri na aina ya mitambo, kwa sababu mitambo iko ya aina nyingi, ni vizuri ikawa inawasilishwa mapema ili ichambuliwe vizuri kwenye kikosi kazi cha maboresho ya kodi na baadaye pia *think tank* ili pande zote basi tupate muda wa kuyachambua na kuleta maboresho

ambayo hayatatuletea matatizo pia katika utekelezaji hasa upande wa Mamlaka ya Mapato.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba tutakuwa tunatoza mara mbili kodi ya zuio pale ambapo tunawatoza mawakala wa huduma za kifedha zinazotumia mifumo ya kieletroniki. Kwa kweli pendekезo hili sisi tunalenga kuleta usawa kati ya hawa mawakala, lakini na wengine ambaao tayari wanatumia huduma hizi, kwa sababu tayari wao wanalipa kodi ya zuio. Kwa hiyo ni muhimu hawa ambaao walikuwa bado wameachwa nje, nao kwa vile wanatoa huduma hizo hizo kwa njia ya kieletroniki nao wajumuishwe ndio lengo la marekebisho ambayo tumeleta.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutoa pia motisha ya kodi ya VAT kwa wakulima, napenda tu niseme kwamba Serikali imekuwa inatoa ahueni kwenye pembejeo za kilimo mbegu, mbolea na vifaa vingine vya kilimo kama matrektka.

Kwa hiyo tutaendelea kuboresha tunavyokwenda na nadhani tungeshauri zaidi kama nilivyokwishesema kwamba hivi vifaa ambavyo ni *specific* kwa ajili ya kusaidia wakulima wadogo, basi viletwe mapema kwa ajili ya uchambuzi stahiki, vina *complication* kubwa kwa maana ya kusimamia utawala wa kodi, kwa sababu vifaa vingine vinatumika sehemu mbalimbali na ni muhimu tuweze kuvitenganisha kwamba kweli hivi vinakwenda kusaidia wakulima wetu wadogo au hivi vingine vinaingia tu kwenye soko la kawaida.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongeza ule wigo kipato cha chini ambacho watumishi hawatozwi kodi kwenda 419,000 kama ilivyopendekezwa. Niseme tu kwamba tutaendelea kufanya maboresho ya aina hii ya kupandisha viwango vya kodi kadri hali ya kibajeti inavyoruhusu, kwa sababu tumefanya hesabu maana hapa lazima *u-balance*, kwamba wakati huo huo ni kweli tunataka kutoa ahueni kwa wafanyakazi katika utumishi wa umma, lakini wakati huo huo ni lazima *tu-safeguard* mapato ya Serikali na hasa katika kipindi hiki ambacho kutegemea tena huko misaada siyo sawa. Kwa hiyo ni suala la *ku-balance* na sisi hesabu tulizopiga

zilituonyesha hapa hili pendekazo tuliloleta ndio tunaloweza kulimudu kibajeti kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupunguza tozo ya elimu ya mafunzo ya ufundi mpaka ifike asilimia mbili, tumeanza mbali sana mpaka hapa tulipofika. Kwa hiyo kwa kweli hali ya kibajeti itakavyoruhusu tutaeendelea kuwapunguzia mzigo waajiriwa. Naliomba tu Bunge lako Tukufu liridhike na hatua ambayo tumefikia hivi sasa kuendelea kupunguza hii tozo ya elimu ya mafunzo ya ufundi.

Mheshimiwa Spika, wakati nikihitimisha Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali nimetumia muda kidogo kuelezea jinsi ambavyo Serikali imejipanga. Kwanza kwa nini tunaleta haya mabadiliko ambayo yanagusa hifadhi zetu za Taifa. Nipende tena kusisitiza dhamira ya Serikali kamwe haiwezi kuua uhifadhi. Nimesisitiza hapa kwamba kwanza ilikuwa ni suala kwamba, je, tukipata changamoto kama ilivyotokea kwenye *covid* na siyo lazima iwe *covid* peke yake hata huko mbele ikafika mahali kwamba taasisi hizi za uhifadhi sasa haziwezi tena kujendesha kama ilivyo sasa, *TANAPA* wameshindwa kulipa mishahara, kukarabati miundombinu ni shughuli vilevile haiwezekani.

Kwa hiyo ili ku-*safeguard* hiyo kwenda mbele huko, tukija tukapata madhara mengine, ni lazima Serikali iweze kuhakikisha kwamba kuna uendelevu wa hifadhi na kwa hiyo utaratibu tunaouchukua ndio huo kwamba kwanza tunabeba sasa mzigo wa kulipa mishahara ya watumishi wote wa taasisi hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile tumefanya *commitment* kwamba tutahakikisha miundombinu yote ya uhifadhi inapewa fedha *promptly* kutoka Serikalini. Limeelezwa vizuri, namshukuru sana mchangiaji aliyelieleza wazi kabisa, *ring fencing* inafanya kazi, Mheshimiwa Zitto ulishasikia jeshi wanalamika juu ya posho zao, *they are in fence*, wala Polisi, *TRA* umewasikia wanalamika? *TANROADS* tunatenga fedha na Kamati ya Bajeti kila mara imekuwa inahoji na kufuatilia. Mfuko wa Barabara fedha yake ipo, Mfuko wa Maji fedha

yake ipo, Mfuko wa *REA* fedha yake ipo; kwa nini tushindwe *ku-ring fence* fedha kwa ajili ya hifadhi zetu ambalo ni jambo muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda nilihakikishie Bunge lako tukufu kwamba tutahakikisha kwamba fedha kwa ajili ya uhifadhi zinakuwa *ring fenced* kama ambavyo tunatoa kwa taasisi zote nyeti kila mwezi tunazipatia *one twelfth* ya *OC* yake bila kukosekana, kwa hiyo hakuna sababu kwa nini tushindwe hata kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Iakini nimerudia tena kusisitiza kwamba ni muhimu sasa *Central Government* iwe na *control* ya ajira katika taasisi za hifadhi. Watumishi 3,000 kuwa nje ya *the main payroll* ya Serikali haliwezi kuwa sawasawa. Kwa hiyo, ni muhimu pia, maana kama nilivyoeleza tumefanya sana ukaguzi wa taasisi hizi na tumeona madhaifu makubwa sana katika mifumo ya ukusanyaji wa mapato. Tumeona mapungufu makubwa sana katika matumizi ya hizi taasisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni lazima tusahihishe haya, hizi bado ni taasisi za Umma, ni lazima tuhakikishe kwamba fedha ya Umma inakwenda kweli kutumika kadri inavypaswa. Kwa hiyo nimelisitisiza sana hili toka mwanzo, nafikiri mdogo wangu, Mheshimiwa Zitto, alikuwa hajaingia ukumbini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya *TR*, kwamba ile asilimia 70 itakwenda kupunguza uwezo wa taasisi; napenda nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba Ofisi ya Msajili wa Hazina tunaendelea kuiimarisha na katika kipindi kifupi, kama nilivyoeleza wakati na-*wind up*, imefanya mambo makubwa sana katika kuimarisha taasisi na mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, usimamizi madhubuti wa mapato na matumizi ni muhimu na tutafanya uchambuzi makini wa mahitaji ya taasisi zote ili kuhakikisha kwamba bado uwezo wao wa kufanya shughuli zao za kisheria unatekelezwa ipasavyo. Lakini haiwezekani tuendelee kuwaacha zile taasisi

ambazo tunaona zina ziada ziendelee kuogelea tu kwenye fedha wakati yako maeneo mengine yana uhitaji mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na kwamba kama hili la kuruhusu Waziri wa Fedha aweze kutoa msamaha kwa kuwekewa *cap* ya bilioni moja kwa *duration* yote ya mradi. Pamekuwa na malalamiko muda wote wa Bunge hili kwamba miradi inachelewa kwasababu Waziri wa Fedha amebanwa, hawezi kutoa msamaha wa Kodi ya Mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulichofanya ni kusema walau tuweke *cap* fulani ya bilioni moja aruhusiwe kutoa msamaha ili tuweze kwenda haraka zaidi. Sasa ntashangaa kama Bunge hili linaludi tena kusema hapana. Na kama lengo letu ni kuondoa huu ucheleweshaji, lakini tumeweka *safeguards*, Waziri wa Fedha asiamue peke yake, Waziri wa Fedha lazima *a-consult TRA*, na sipendi kuamini kwamba itatokea wakati basi *Commissioner General*wa *TRA* na Waziri wa Fedha wanaingia njama za kuhujumu nchi yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ni *system* kwa hiyo, ni muhimu sana kwamba Bunge likubali kumpatia Waziri wa Fedha *at least level*hiyo ya *ku-approve* hiyo miradi bila kupitia ule mlolongo mrefu, mapendekezo haya yaende *Cabinet Secretariat*, yaende *IMTC* ndiyo yaende kwenye Baraza, inachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, labda nisemee la mwisho ambalo lilichangiwa na Mheshimiwa Dau kuhusu kuzuia usafirishaji wa mkaa, hususani kwenye ule mradi wetu mkubwa kule Rufiji. Jambo hili tulilionia uzito wake na ninaomba kama Watanzania wazalendo mfikirie changamoto kubwa tullyokuwa nayo ya wenzetu huko nje amba walikuwa wanapinga mradi wetu usiendelee kwasababu ya *concerns* zao za mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo la kwanza ambalo tulihangaika nalo tukasema haiwezekani na kubwa zaidi tuliona kwamba mradi ule utachelewa kwasababu taasisi

zinazohusika zilikuwa zinapishana na tenda zenyewe zilivokuwa zinaandaliwa tukaona hili haliwezekani. Kwa hiyo, maamuzi yaliyofikiwa ilikuwa ni kwamba ili mradi wetu usichelewe tulipeleka, tulifanya maamuzi kwamba Jeshi liende likafanye *clearing* ya ile site na hivi sasa ndiyo majadiliano yanaendelea kati ya *Tanzania Forest Services*, Wizara inayohusika na idara nyingine ndani ya Serikali ili tuweze kuona sasa yale matumizi ya ule mkaa unakuaje *internally*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya ufanuzi wa mambo hayo, naomba kutoa hoja na ninaomba kabisa kwa dhati Bunge lako Tukufu liridhie kuitisha Muswada huu wa Sheria ya Fedha ili tuendelee kutekeleza bajeti ambayo mmeipitisha. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Wziri wa Fedha, ahsante sana. (*Makofi*)

Sasa Waheshimiwa tunaongeza muda ili tumalize jambo hilli, halitatuchukua muda mrefu hata kidogo, ili jioni tuweze kwenda na utaratibu mzuri zaidi. Tukilaza kiporo hapa itatusumbua.

Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2020
(The Finance Bill, 2020)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wajumbe, tukae. Katibu!

Ibara ya 1
Ibara ya 2

Ibara ya 3
Ibara ya 4

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 11

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa)

Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15

Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

Ibara ya 18

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 19

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 21

Ibara ya 22

Ibara ya 23

Ibara ya 24

Ibara ya 25

Ibara ya 26

Ibara ya 27

Ibara ya 28

Ibara ya 29

Ibara ya 30

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 32

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 34

Ibara ya 35

Ibara ya 36

Ibara ya 37

Ibara ya 38

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 39

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 40

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara mpya ya 41

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 42

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 43

Ibara ya 44

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 45

Ibara ya 46

Ibara ya 47

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 48

*(Ibara illyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 49

Ibara ya 50

Ibara ya 51

Ibara ya 52

Ibara ya 53

Ibara ya 54

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 55

*(Ibara illyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 56

Ibara ya 57

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 58

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 59

Ibara ya 60

Ibara ya 61

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 62

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 63

Ibara ya 64

Ibara ya 65

Ibara ya 66

Ibara ya 67

Ibara ya 68

Ibara ya 69

Ibara ya 70

Ibara ya 71

Ibara ya 72

Ibara ya 73

Ibara ya 74

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 75

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 76

Ibara ya 77

Ibara ya 78
Ibara ya 79
Ibara ya 80
Ibara ya 81
Ibara ya 82
Ibara ya 83

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

NDG. NENELWA MWIHAMBI – KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza
kazi yake.

(Bunge lilitrudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae; Mheshimiwa
Waziri, taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika,
naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima
imepitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2020 (*The
Finance Act, 2020*) kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja
na marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba
taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi na Bunge lako; naomba
kutoa hoja.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika,
naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

SPIKA: Tunashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, Sheria hii ya Fedha imepitishwa rasmi, inahitimisha sasa shughuli zetu za bajeti kwa kweli kadri tulivyozianza mwezi Aprili mpaka leo, hii ndiyo inahitimisha ile shughuli nzima ya Bunge la Bajeti. (*Makofii*)

Sisi tumetimiza wajibu wetu, tumejadili mengi, tumesema mengi na mengi yako ndani ya *Hansard*. Waheshimiwa Wabunge, mkitaka kujua umuhimu wa *Hansard* muwe mnachukua *Hansard* hata ya miaka ya 1970, ya miaka ya 1960, ya miaka ya 1980 kuhusu jambo lolote kubwa muhimu mkaona majadiliano yalivyoenda wakati huo na nini kilikubalika na nini kinaendelea leo. Mtakuta majadiliano ya Bunge ya kwenye *Hansard*, yana utajiri mkubwa sana wa *information*, mkubwa sana. Na ni kumbukumbu muhimu sana kwa vizazi vinavyokuja kuona kwa nini jambo fulani lilitifikiwa hapo hivyo lilitifikiwa, na ndiyo umuhimu wa nyumba hii.

Kwa hiyo, kwenye bajeti ya mwaka huu Wabunge wamesema sana; Waheshimiwa Mawaziri mmewasikia Wabunge walichosema, kuna maeneo tumekubaliana, kuna maeneo hatukukubaliana, lakini *time will tell*. Mwisho wa siku ukija kusoma *Hansard* utakuta vitu vingi vilizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge na walishauri kwa nia njema kabisa kwasababu ya kuipeleka mbele nchi yetu.

Kwa hiyo, tunawaomba msisahau kupitia *Hansards* na ninyi pia, mtakuta baadhi ya mambo, labda wakati huo wa kujadiliana hukubaliana jambo fulani lakini baadaye unagundua kwa kweli *this is the right path*. Tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa bajeti hii ya 2020/2021.

Sasa ili kukamilisha kabisa taratibu zetu, nakuita Katibu tena usome ile *third reading* ili tukamilishe kabisa.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kutunga Sheria Itakayotoza au Kubadilisha baadhi ya Kodi, Ushuru, tozo na Ada mbalimbali kufanya Marekebisho kwenye Sheria

Mbalimbali zinazohusu Ukusanyaji na Usimamizi wa Mapato ya Umma (*A Bill for an Act to Impose and Alter Certain Taxes, Duties, Levies, Fees and to Amend Certain Written Laws Relating to the Correction and Amendment of Public Revenues*)

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Nakushukuru sana.

Basi tutakaporudi, ili mambo yetu yaende vizuri ningeshauri turudi saa kumi kamili juu ya alama. (*Makofi*)

Leo ni siku ya mwisho Waheshimiwa, msiwe na wasiwasi, twende kwa utaratibu huo ili Mheshimiwa Waziri Mkuu hotuba yake aitoe katika wakati mzuri wakati Watanzania wote wanamsikiliza.

Waheshimiwa Wabunge, tukirudi saa kumi na moja itabidi atoe kwenye giza giza hivi kwasababu kuna mambo ya kuanza nayo ikiwemo shughuli ya Kanuni ambazo Kanuni hizo zitatumika kwenye Bunge linalofuata la Kumi na Mbili. Sisi tunapaswa tutekeleze wajibu wetu wa kuzikamilisha Kanuni hizo ili wenzetu watakapokuja wataanza kuzitumia moja kwa moja Kanuni hizo mpya.

Basi kwa hatua hiyo naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili leo jioni.

(*Saa 7.21 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa Kumi Jioni*)

(*Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Karibuni tena Waheshimiwa Wabunge kwa session yetu ya jioni hii ya leo, siku muhimu sana katika historia ya Bunge letu.

Katibu.

NDG. NENELWA M. WANKANGA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

**Azimio la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kanuni za Bunge
Kuhusu Marekebisho ya Kanuni za Bunge**

SPIKA: Ahsante sana. Naomba nikukaribishe Mheshimiwa Naibu Spika, *you have the flow.*

MHE. DKT. TULIA ACKSON - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA KANUNI ZA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba yako kama MwenyeKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kanuni, naomba kuwasilisha Azimio la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kanuni za Bunge kuhusu Marekebisho katika Kanuni za Kudumu za Bunge. Maeleo haya yanatolewa chini ya Kanuni ya 155 fasili ya (1) na ya (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 155 fasili ya (1) na ya (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio la Bunge kuhusu Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kwa sababu ya muda, naomba maeleo yangu yote yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukupongeza kwa dhati kwa utayari na juhudzi zako zilizowezesha Kamati ya Kudumu ya Bunge kuitia kanuni zetu na kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya baadhi ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Mapendekezo hayo yanalenga kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa kipindi ambacho kanuni hizo zimekuwa zikitumika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, nitumie fursa hii kukupongeza kwa dhati kabisa kwa maono na ubunifu wako katika kubuni mbinu mbalimbali za uendeshaji wa shughuli za Bunge na hasa katika mazingira ambayo kanuni zetu ziliikuwa kimya. Ni ukweli usiofichika kwamba ubunifu

wako umetuwezesha kukabiliana na changamoto mbalimbali za uendeshaji wa Bunge, hasa wazo lako la Bunge Mtandao. Kuna wakati huwa najiuliza, usingekuja na wazo la Bunge Mtandao, Bunge letu tungeendesha vipi kipindi hiki cha *Covid-19?* (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yako, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati yako ya Kudumu ya Bunge na Sekretarieti ya Kamati chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai, kwa uzalendo na moyo wao wa kujituma uliofanikisha zoezi la kuanda Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Bunge ambayo leo ninayawasilisha kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa na Bunge. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, nitumie fursa hli kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, pamoja na Serikali kwa ujumla kwa ushirikiano waliotupatia sisi viongozi wa Bunge na Wabunge wenzetu katika kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, binafsi namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuonesha imani yake kwangu kwa kunitfea kuwa Mbunge na hatimaye kuchaguliwa na Wabunge wenzangu kuwa Naibu Spika wa Bunge hili. Nafasi hli imeniwezesha siku ya leo kuwasilisha mbele ya Bunge hoja hii muhimu katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua pia fursa hii ili kuwashukuru sana wananchi wenzangu wa Mkoa wa Mbeya kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa na wanaendelea kunipa wakati ninapotekeleza majukumu yangu kwa kipindi chote cha Ubunge wangu. Hakika ninajivunia mafanikio ambayo tumeyapata kwa pamoja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kipekee naishukuru familia yangu, hasa mume wangu James Andilile Mwenyekule na watoto

wetu kwa kunivumilia katika kipindi chote cha Ubunge wangu na kwa kunitia moyo wakati wa utekelezaji wa majukumu yangu. Nasema kweli, bila upendo, sala na uvumilivu wao kazi hii ingekuwa ngumu sana. Itoshe tu kusema, nawapenda sana na ninawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitoe maelezo ya maeneo yanayohitaji maboresho ya msingi katika kanuni zetu. Katika kuboresha uendeshaji wa shughuli za Bunge, Kamati imebaini kuwepo kwa maeneo machache yanayohitaji kufanyiwa marekebisho ya kanuni kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni utaratibu wa kumwita au kumrejesha nchini Mbunge au Mjumbe katika vyombo vingine vyta uwakilishi aliyechaguliwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mikataba inayoanzisha vyombo mbalimbali vyta uwakilishi, Bunge limepeewa mamlaka ya kuchagua Wabunge au Wajumbe kwenda kwenye vyombo hivyo vyta uwakilishi, kama vile *SADC PF, IPU, PAP, EALA, CPA*, na kadhalika. Pamoja na Bunge kuwachagua Wajumbe au Wabunge hao kuwakilisha nchi yetu, Kanuni za Bunge hazijaweka masharti ya kuwezesha Bunge kumwita au kumrejesha Mbunge au Mjumbe anayeweza kuwa:-

- (a) Ameshindwa kumudu majukumu yake kwa sababu za ugonjwa;
- (b) Amekuwa na mwenendo usiofaa na unaodhalilisha nafasi anayoitumikia; au
- (c) Ameshindwa kutetea na kuzingatia maslahi ya nchi wakati akitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, ili kupatikana kwa suluhisho la upungufu huu inapendekezwa iwepo kanuni inayoweka utaratibu wa kumwita au kumrejesha Mbunge au Mjumbe ili Mbunge au Mjumbe husika aweze kuchukuliwa hatua za kinidhamu ambapo akipatikana na hatia Bunge liweze

kumpa adhabu ya karipio au kumwondoa Mjumbe au Mbunge husika kwenye nafasi ya Uwakilishi kwa Azimio la Bunge. Inatazamiwa kuwa utaratibu huu utasaidia kudumisha nidhamu na uzalendo kwa Wabunge ama Wajumbe wanaochaguliwa na Bunge na pia utalipa Bunge uwezo na sauti juu ya Uwakilishi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, ni masharti kuhusu makosa ya kinidhamu:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha uhai wa Bunge hili la Kumi na Moja tumeshuhudia ongezeko kubwa la vitendo vyta makosa ya kinidhamu kwa baadhi ya Wabunge.

Aidha, vitendo hivyo vilijirudiarudia, hivyo kuathiri taswira na kushusha hadhi ya Bunge kwa ujumla wake. Kutokana na hali hiyo, inapendekezwa eneo la amani na utulivu Bungeni liboreshwe kwa makosa na adhabu kugawanywa katika makundi matatu kwa kuzingatia aina ya kosa na adhabu anayoweza kupewa Mbunge anayetenda makosa, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Utovu wa Nidhamu. Kosa hili litachukuliwa kama ni kosa dogo. Mfano wa kosa la utovu wa nidhamu ni Mbunge:-

(i) Kutishia kutumia nguvu kwa Mbunge au mtu mwingine ndani ya Ukumbi wa Bunge au kwenye Kamati;

(ii) Kukiuka Muongozo wa Spika uliotolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 64 Fasili ya 2; au

(iii) Kukiuka masharti ya Kanuni za Bunge ambayo kwa maoni ya Spika kitendo hicho ni utovu wa nidhamu.

Mheshimiwa Spika, adhabu; inapendekezwa Mbunge anayetenda kosa la utovu wa nidhamu aadhibiwe na Spika kwa kupewa onyo au kutolewa nje ya Ukumbi wa Bunge au Mbunge kusimamishwa kuhudhuria Vikao vyta Bunge visivyozidi 10.

(b) Mheshimiwa Spika, Utovu Mkubwa wa Nidhamu. Kosa hili litachukuliwa kama ni kosa kubwa zaidi ya kosa la utovu wa nidhamu uliotajwa awali. Mifano ya kosa la utovu mkubwa wa nidhamu ni Mbunge:-

- (i) Kudharau uamuzi au maelekezo ya Spika.
- (ii) Kufanya au kusababisha vurugu wakati shughuli za Bunge zinaendelea;
- (iii) Kufanya kosa ambalo alishaadhibiwa kwa mujibu wa Kanuni ya 73;
- (iv) Kupiga kura zaidi ya mara moja ya uamuzi wa hoja;
- (v) Kukataa kufafanua au kuondoa maneno yasiyo ya Kibunge au kukataa kuomba radhi, licha ya Spika kumtaka kufanya hivyo.
- (vi) Kutenda kosa la utovu wa nidhamu wakati wa hotuba ya mgeni mashuhuri;
- (vii) Kumshambulia, kumtukana au kutoa ishara ya matusi dhidi ya Mbunge mwingine au wageni wanaotembelea Bunge au mtu mwingine ndani ya Ukumbi wa Bunge au Kamati;
- (viii) Kujaribu au kuvuruga msafara wa Spika anapoingia au kutoka Ukumbini; na
- (ix) Kufanya kitendo chochote kinachoshusha hadhi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, adhabu; inapendekezwa Mbunge anayetenda kosa la utovu mkubwa wa nidhamu asimamishwe kuhudhuria vikao visivyo zidi 15 iwapo ni kosa la kwanza. Au kusimamishwa vikao visivyo zidi 20 ikiwa ni kosa la pili au kupewa adhabu nyingine yoyote itakayopendekezwa na Kamati ya Maadili.

(c) Mheshimiwa Spika, Utovu wa Nidhamu Uliokithiri. Kosa hili litahesabiwa kuwa ni kosa kubwa zaidi ya makosa hayo mengine. Mifano ya kosa la utovu wa nidhamu uliokithiri ni Mbunge:-

- (i) Kujaribu kumshambulia au kumshambulia Spika au mgeni mashuhuri Bungeni;
- (ii) Kujaribu kuondoa au kufanya kitendo chochote cha kuondoa Siwa mahali pake;
- (iii) Kutukana au kutoa ishara ya matusi kwa Spika au mgeni mashuhuri;
- (iv) Kusababisha vurugu ambazo zitasababisha shughuli za Bunge kuahirishwa; na
- (v) Kurudia kutenda kosa la utovu mkubwa wa nidhamu zilizoainishwa chini ya Kanuni ya 74.

Mheshimiwa Spika, adhabu; inapendekezwea Mbunge aliyetenda kosa la Utovu wa Nidhamu uliokithiri apewe adhabu au achukuliwe hatua zifuatazo:-

- (i) Kusimamishwa kuhudhuria mikutano isiyopungua miwili na isiyozidi mitatu.
- (ii) Adhabu nyingine itakayopendekezwa na Kamati;
- (iii) Bunge kuazimia kwamba shauri hilo lishughulikiwe kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambapo Mbunge husika anawenza kupewa adhabu ya kufukuzwa Ubunge.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Usimamizi wa Amani na Utulivu kwenye Vikao vya Kamati. Kanuni zilizopo hazijaweka utaratibu wa kudhibiti amani na utulivu kwenye vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge. Hii ni changamoto kubwa katika kusimamia nidhamu na utulivu kwenye vikao. Inapendekezwa utaratibu wa kikanuni uwekwe ili kusimamia

amani na utulivu kwenye Kamati kwa kuweka makosa na adhabu kama zilivyo wakati wa Vikao vya Bunge. Utaratibu unaopendekezwa kufuatwa ni uongozi wa Kamati kuwasilisha jina la Mbunge aliyefanya makosa hayo ili hatua zichukuliwe dhidi yake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Utaratibu wa Kujadili na Kuridhia Mikataba ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 63(a) ya Katiba inalipa Bunge madaraka ya kujadili na kuridhia mikataba yote ya Kimataifa inayohusu Jamhuri ya Muungano. Kanuni zetu hazijaweka utaratibu wa utekelezaji wa jukumu hili muhimu, kama ilivyo katika utungaji wa sheria, upitishaji wa bajeti, uulizaji wa maswali kwa Waziri, na kdhalika

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kuweka utaratibu wa kikanuni wa kuridhia Miktaba ya Kimataifa inayohitaji kuridhiwa na Bunge. Kanuni zifafanue namna ya kuwasilisha Hoja ya Kuridhia Mkataba, mchakato wa mijadala kwenye Kamati, Bunge na uwasilishaji na upitishaji wa Azimio husika. Japokuwa suala hili halikuwepo kwenye kanuni, huo ndiyo utaratibu ambao tumekuwa tunautumia kwa muda wote katika kupitisha Azimio la Kuridhia Mkataba.

Mheshimiwa Spika, jambo la tano ni utaratibu wa kushughulikia Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Muda Mrefu.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 94 inaweka utaratibu wa kushughulikia Mapendekezo ya Mpango wa Muda Mfupi pekee, bila kueleza namna ambavyo Bunge litashughulikia Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Muda Mrefu kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba. Hii imekuwa ikileta changamoto ya kushughulikia Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Muda Mrefu. Hivyo, inapendekeza kuboreshwa Kanuni ya 94 kwa kuweka utaratibu wa kushughulikia Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Muda Mrefu ambao utajadiliwa mapema iwezekanavyo katika

Mkutano wowote wa Bunge mara baada ya Mkutano wa Kwanza wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, jambo la sita ni maboresho mengine ya kimaudhui katika Kanuni. Mbali na maboresho hayo, Kanuni inapendekeza maboresho mengine yafanyike katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kuboresha utaratibu wa kushughulikia malalamiko dhidi ya uamuzi wa Spika kwa kuweka sharti la ukomo wa muda wa kuwasilisha malalamiko ya Mbunge dhidi ya uamuzi wa Spika. Inapendekezwa Mbunge awasilishe malalamiko yake ya maandishi kwa Katibu wa Bunge ndani ya siku moja tangu uamuzi ulipotolewa.

(b) Kuboresha utaratibu wa Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge kwa kuondoa sharti la kutaka karatasi ya kura kuwa na majina sita na badala yake Kamati ya Uongozi itakiwe kuwasilisha majina ya Wagombea yasiyo zidi sita. Sharti hilo limekuwa na changamoto ya utekelezaji hasa pale wanapo jitekeza Wagombea wachache kuliko idadi iliyotajwa na kanuni.

(c) Kuweka masharti ya Mjumbe kukoma kuwa Mjumbe katika vyombo vingine vya Uwakilishi. Inapendekezwa kanuni itaje sababu zinazoweza kusababisha Mjumbe kukoma Uwakilishi wake, ikiwa ni pamoja na Mjumbe kutiwa hatiani na kuadhibiwa na Bunge kwa kosa la utovu mkubwa wa nidhamu au utovu wa nidhamu uliokithiri.

(d) Kuweka utaratibu wa Bunge kutoa taarifa kwa Bunge la Afrika Mashariki inapotokea Mjumbe wa Bunge hilo kakosa sifa za kuendelea kuwa Mjumbe. Inapendekezwa Spika awe anatoa taarifa kwa Spika wa Bunge la Afrika Mashariki pale ambapo Mjumbe wa Bunge hilo kutoka Tanzania atakosa sifa za kuendelea kuwa Mjumbe kwa mujibu wa Ibara ya 67 na 71 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(e) Kuweka utaratibu wa kujaza nafasi ya Mjumbe katika Bunge la Afrika Mashariki au chombo kingine cha uwakilishi. Kwa kuweka utaratibu wa kujaza nafasi ya Mjumbe wa Bunge la Afrika Mashariki mara itakapokuwa wazi, utaratibu ambao haupo kwenye kanuni zetu kwa sasa.

(f) Kuboresha kwa kubadili jina la Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Inapendekezwa Kambi ya Wabunge ambao vyama vyao haviundi Serikali ijulikane kama Kambi Rasmi ya Walio Wachache badala ya Kambi ya Upinzani Bungeni ili kuendana na utamaduni wa baadhi ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola kama vile Kenya.

Hii itasaidia kuondoa dhana ya Wabunge wa Kambi hiyo kupinga kila kitu kinacholetwa na Serikali badala ya kutoa mawazo mbadala na yenye tija kwa Taifa. (*Makofii*)

(g) Kuboresha kiapo cha Mbunge. Kwanza ni kuondoa neno "Uti" kwenye Kiapo cha Ubunge na badala yake kuweka neno "Uaminifu" ambalo lipo kwenye Katiba na Sheria ya Viapo vya Viongozi. Pili, ni kuweka utaratibu wa kumwezesha Mbunge Mteule wa Rais na Mbunge anayeshinda katika uchaguzi mdogo au kuteuliwa, kuapishwa mara moja na kuanza kutekeleza majukumu yake ya Kibunge bila kulazimika kusubiri mpaka Bunge likutane ndipo aapishwe. Baada ya Spika, kumwapisha Mbunge, atatoa taarifa Bungeni kuhusu Mbunge aliyepishwa na kumtambulisha Mbunge husika. (*Makofii*)

(h) Kuboresha utaratibu wa kuwasilisha jina la Mbunge anayependekezwa na Rais kushika nafasi ya Waziri Mkuu kwa kueleza namna Taarifa ya Rais inayotaja jina la Mbunge anayependekezwa kuwa Waziri Mkuu itakavyomfikia Spika, ambapo inapendekezwa taarifa hiyo iwasilishwe na Mpambe wa Rais au mtu mwagine atakayetumwa na Rais kuingia ukumbini na kumkabidhi Spika taarifa hiyo.

(i) Kuweka utaratibu wa Maswali kwa Mawaziri yanayohusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza wakati huo katika jamii. Inapendekezwa kanuni ziruhusu Bunge kutenga

siku maalum ambayo Mawaziri wataulizwa maswali na Wabunge kuhusu masuala yaliyojitokeza kwa wakati huo. Utaratibu huu utasaidia kupunguza maombi ya miongozo ya Wabunge kwenye masuala yaliyojitokeza mapema kwenye jamii. (*Makofi*)

(j) Kuboresha masharti kuhusu muda wa kusema Bungeni kwa kupunguza muda wa kusema Bungeni kutokana na changamoto ya ufinyu wa muda na ongezeko la idadi ya Wabunge. Inapendekezwa muda wa kuchangia upunguzwe kutoka dakika 15 hadi dakika 10. Muda wa Waziri kuhitimisha hoja upunguzwe kutoka dakika 60 hadi dakika 30 na muda wa kuwasilisha Maoni ya Upinzani upunguzwe kutoka dakika 30 hadi dakika 15. Mapendekezo haya yanalenga kutoa fursa kwa Wabunge wengi zaidi kuchangia hoja. (*Makofi*)

(k) Kuboresha masharti ya malipo ya mshahara na posho kwa Mbunge aliye mahabusu na anayetumikia kifungo Gerezani kwa kuweka masharti kwa Mbunge aliye mahabusu kulipwa nusu mshahara na posho zinazoambatana na mshahara wake na Mbunge anayetumikia kifungo kutokulipwa mshahara wala posho zinazoambatana na mshahara wake. Msingi wa mpendekezo haya ni Mbunge kutofanya kazi ya Mbunge kwa wakati huo anapotumikia adhabu.

(l) Kuboresha utaratibu wa kutangaza Muswada kwenye gazeti la Serikali kwa kuondoa sharti la kutangaza Muswada wa sheria kwenye gazeti mara mbili na badala yake utangazwe mara moja. Sharti la awali limepitwa na wakati.

(m) Utaratibu wa kuunda Kamati ya Pamoja na Kamati Maalum kwa kuweka utaratibu wa kuunda Kamati ya Pamoja na Kamati Maalum, utaratibu wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati hizo na utaratibu wa kufanya kazi Taarifa za Kamati hizo. Kamati hizo zitaundwa na kufanya kazi kwa maelekezo ya Spika kama ilivyokuwa ikifanyika awali.

(n) Kuboresha utaratibu wa ukusanyaji na utoaji wa habari za Bunge kwa kueleza misingi ya ukusanyaji na utoaji wa habari za Bunge, matangazo ya moja kwa moja ya Bunge kurushwa na *Studio* ya Bunge. Masharti ya upigaji picha ndani ya ukumbi wa Bunge, inapendekezwa chombo au Mwandishi wa Habari atakayekiuka masharti yaliyowekwa apewe onyo, kusimamisha kuchukua na kutoa habari za Bunge au kufutiwa kibali cha kufika Bungeni.

Mheshimiwa Spika, maboresho ya kimpangilio, kiuandishi na kisarufi. Mbali na niliyoyaeleza, inapendekezwa yafanyike maboresho ya mpangilio kiuandishi na kisarufi katika Kanuni za Bunge ili kuondoa makosa madogo madogo ya kiuandishi na kwa ajili ya kurahisisha rejea na kuweka mtiririko mzuri wa maudhui. Kanuni zilizofanyiwa maboresho ya kiuandishi na kisarufi ni kama zinavyoonekana kwenye Taarifa hili pamoja na Nyongeza ya Kwanza, ya Pili, ya Tatu, ya Tano na ya Nane.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; baada ya maelezo haya naomba sas anichukue fursa hii kuwasilisha Azimio la Mabadiliko ya Kanuni za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 155(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili Bunge lako Tukufu lijadili na kuitisha Azimio la kufanya Mabadiliko ya Kanuni yanayopendekezwa na Kamati ya Kudumu ya Kanuni za Bunge kwa kadri itakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, hili ni Azimio la Bunge la kufanya mabadiliko ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

KWAKUWA changamoto za mara kwa mara za matumizi ya Kanuni za Bunge zimekuwa zikijitokeza pamoja na vitendo vya baadhi ya Wabunge vya ukiukwaji wa Kanuni hivyo kuhitaji kuwekewa utaratibu wa kikanuni;

NA KWA KUWA Kamati ya Kanuni za Bunge ilikutana kujadili na kuandaa mapendekezo kwa lengo la kufanya marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016;

NA KWA KUWA mabadiliko yanayopendekezwa yanalenga kuboresha uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa kutatua changamoto zilizojitekeza wakati wa utekelezaji wa shughuli za Bunge;

NA KWA KUWA Kanuni nyingi bado zina maudhui thabiti na yanayojitosheleza isipokuwa maeneo machache ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi na kuboreshwa na machache mengine yanahitaji maboresho ya kiuandishi;

NA KWA KUWA mabadiliko yanayopendekezwa yataingizwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge ili kuanza kutumika katika Bunge la Kumi na Mbili;

NA KWA KUWA Kanuni ya 155(1) inatoa madaraka kwa madaraka kwa Bunge kufanya mabadiliko ya Kanuni za Bunge;

NA KWA KUWA Kanuni ya 155(1) inaitaka Kamati ya Kanuni za Bunge kuandaa na kuwasilisha Bungeni mapendekezo ya mabadiliko ya Kanuni za Bunge;

NA KWA KUWA Kamati ya Kanuni imeandaa mapendekezo ya mabadiliko ya Kanuni;

NA KWA KUWA Kanuni ya 155(2) inataka mapendekezo hayo yawasilishwe Bungeni kwa Azimio na Naibu Spika nimewasilisha mapendekezo ya mabadiliko hayo kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Kanuni za Bunge. (*Makof*)

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia manufaa yatakayopatikana kutokana na mabadiliko yanayopendekezwa, Bunge linaazimia kwamba linakubali na kuitisha mapendekezo ya kufanya mabadiliko katika Kanuni za Kudumu za Bunge kama yalivyowasilishwa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 155(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunashukuru sana kwa uwasilishaji mzuri wa ufasaha wa mapendekezo ya Kanuni za Bunge lijalo. Watakaobahatika ndiyo wataweza kutumia baadhi ya Kanuni hizi, ni kwa juhudi. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha tayari ya wachangiaji na nitaenda kwa orodha hiyo niliyokuwa nimepewa. Nianze na Mheshimiwa Mwakasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Makamba na Mheshimiwa Hamidu Bobali kama atakuwa amefika, anaafuatia.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye Azimio la Marekebisho ya Kanuni. Namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika kwa uwasilishaji wake mzuri wa mapendekezo ya baadhi ya mabadiliko ya Kanuni.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kushukuru uongozi wa Awamu ya Tano wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa ushirikiano mkubwa ambao amekuwa akiutoa kwa Bunge hili kupitia kwako kiongozi wetu, kwa kweli Bunge hili sasa tunaelekea mwisho lakini tukiwa na mafanikio mengi. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ushirikiano wake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nina mapendekezo machache lakini pia na hoja ambazo naona ni vizuri ningeziongelea kuhusu Kanuni. Kwa haraka haraka naomba nianze na suala moja ambalo limekuwa likiendelea.

Mheshimiwa Spika, nchini Uingereza ambako ndiyo uendeshaji wetu wa Bunge hata sheria nyingi tumezichukua huko, Waziri Mkuu wa Uingereza ndiyo Mtendaji Mkuu wa Serikali kwa maana ya kwamba yeye ndiyo Kiongozi wa Serikali moja kwa moja, kitu ambacho hapa kwetu sisi Mheshimiwa Rais ndiyo Mtendaji Mkuu wa Serikali kwa maana ya kwamba maamuzi mengi yako chini ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, hapa Bungeni anayemwakilisha Mheshimiwa Rais katika shughuli za Serikali ni Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kuna utata ambao nauona katika Kanuni, ni hili suala la masuala ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu. Mimi kwa mapendekezo yangu, kwa wenzetu wale wanaokuja na hata sisi wengine tutakaokuja nadhani haya maswali kwa mapendekezo yangu, ya Waziri Mkuu yatoke yasiwemo kwenye Kanuni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba, tunampa stress Waziri Mkuu ambazo hazina mashiko kwa sababu yeye sio moja kwa moja muamuzi wa shughuli za Serikali. Mawaziri nadhani wanatosha kabisa kufanya majukumu ambayo au maswali ambayo angekuwa anaulizwa Waziri Mkuu hapa. Mawaziri wengine wa Kisekta waliopo wa Wizara mbalimbali wanaweza kuyajibu kuliko Mheshimiwa Waziri Mkuu moja kwa moja akayajibu. Kwa hiyo, naomba nitoe mapendekezo, maswali ya moja kwa moja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yasiwepo kwenye Kanuni zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni nidhamu Bungeni. Mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili, pamoja na wenzangu. Moja ya shida tulioipata au changamoto iliyopo ni zile adhabu ambazo tumekuwa tukitoa mara kwa mara pale mtu anapopatikana na kosa.

Sasa nimekuwa nikijuliza adhabu zile na mapokeo yake, sio tu hizi za Kikanuni za Bunge lakini adhabu yoyote hata kama ni ya Mahakama nje ya Bunge mapokeo yanakuwa tofauti. Kwa mfano, kuna Waheshimiwa Wabunge ambao wao zile adhabu unaona ni Mbunge yule yule anarudia makosa. Sasa nikawa najuliza, hizi adhabu hazitoshelezi au anayepewa ile adhabu haimuumizi ndiyo maana anarudia kosa mara kwa mara?

Mheshimiwa Spika, nimeangalia nakuta Kanuni hizi ambazo zinaongoza kwa mfano kwenye Kamati ya Maadili Kanuni ambazo zinatumika ni za miaka mingi, zimekuwa *copy and paste* watu wamezizoea, Waheshimiwa wengi ambao wanafanya makosa hizi adhabu wanaziona ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, napendekeza,kwa Bunge lijalo, Kanuni hizi ziongezewe makali kwa maana ya kwamba adhabu ziongezeke ili watu wasirudie makosa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye Kanuni haiongelei moja kwa moja kuhusu Mbunge kwa Mbunge. Kuna masuala ambayo hayamo kwenye Kanuni na yanatendeka...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Muda wako umeisha Mheshimiwa.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, naomba kidogo dakika moja tu samahani. Kuna hili suala linaendelea la Wabunge wenyewe kuchafuana. Ukiona kwa mfano *Parliamentary* ni nembo ya Bunge inabeba ule mtandao, lakini Wabunge wanatukanana matusi machafu sana. Mambo yao ya binafsi wanaingiza mle, wanachafuana sana na hilo jambo halijakaa vizuri. Kama inawezekana kitu kama hicho, kiingizwe hata kwenye Kanuni.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hili wazo na niunge mkono kuhusu mabadiliko ya Kanuni. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwakasaka. Nilikwishamtaja Mheshimiwa Salome.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na niseme mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Kanuni.

Kwa kuwa wewe ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kanuni za Bunge na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Spika ndiye Makamu Mwenyekiti na Kwa kuwa Kamati hii imesheheni watu na wajuzi wa sheria mbalimbali na Wabunge wengi wazoefu, Kamati hii ilifanya mjadala mpana sana ambao ulikuwa na lengo la kuboresha Kanuni za Bunge

ili ziweze kwenda kuwasaidia Wabunge watakaorudi kwenye Bunge ijalo waweze kwenda vizuri ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa niseme mpaka sasa mimi mjumbe wako wa Kamati sijaiona walau rasimu ya kwanza ya mapendekezo ya Kamati ambayo ndiyo tuliyoshauri kwenye Kamati yetu. Mapendekezo yamekuja kuibukia humu Bungeni, nimewaita wasaidizi wanioneshe angalau niiione hotuba hiyo, mpaka sasahivi sijaiona, naisikia Mheshimiwa Naibu Spika anaisoma ndani ya Bunge hili tukufu.

Mheshimiwa Spika, kama huo ndiyo msimamo wa Kamati, mimi Salome Makamba naomba niseme wazi, haya mapendekezo yaliyoletwa ndani ya Bunge hili ni mapendekezo yako wewe na Mheshimiwa Naibu Spika na Wajumbe wengine watakaokubaliana lakini mimi na Kambi Rasmi ya Upinzani...

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: ... mimi na Mheshimiwa, Mlowe hatujayaona mapendekezo ambayo tuliyatoa kwenye Kamati ambayo tulisema sekretarieti iende ikachapishe rasimu tuje tuone kama...

SPIKA: Kuna Taarifa unapewa Mheshimiwa Salome.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, naomba kumpa Taarifa Mheshimiwa Salome. Kwanza nashangaa yaani hii kauli kaitoa wapi kwa sababu Mheshimiwa Salome kama alivyosema ni Mjumbe kwenye Kamati ya Kanuni na tulikuwa naye na anafahamu yote haya. Sijaona kitu chochote ambacho ni kipyä aseme leo kwamba ni wewe pamoja na Naibu ndiyo mmeamua. Kitu hiki sio cha kweli na analiambia Bunge kitu ambacho ni cha uongo, alikuwepo mpaka tulipomaliza kule.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

SPIKA: Subiri kidogo. Mheshimiwa Salome kaa kidogo. Unajua ndiyo moja ya mapendekezo hapa kwamba jina upinzani lina matatizo! Yaani mtu anakuwa na hali ya kupinga tu, yaani iko kwenye damu. Kwa sababu ni Mjumbe mwanzo mwisho. (*Kicheko*)

Sawa hiyo ya mwisho hukuiona, sema katika mapendekezo haya, lipi limepandikizwa la Ndugai ambalo hamkujadili kwenye Kamati, ndiyo itakuwa *point*, lakini kwa sababu wewe hukuona kitu fulani, basi! (*Makofi*)

La pili, ni utamadumi wa Mabunge yetu haya kutomtuhumu Spika isipokuwa kwa jambo ambalo kwa kweli unadhani ni vizuri kumtuhumu hadharani. Sio mambo tu yaani unatamani tu! Haiendi hivyo! Sema Kipengele fulani mmekiweka humo hatukujadili, hiyo ni hoja, lakini unakurupuka tu mimi, mimi, sasa kwa hiyo wewe ndiyo Kamati ya Kanuni? Au mimi peke yangu ndiyo Kamati ya Kanuni? Wenzako wote wamefanya hii kazi na ndiyo maana imeletwa hapa, kazi ya Kamati! Lipi ambalo limezungumzwa humu ambalo halikuwemo? Labda wewe siku hiyo hukuwepo, kwa hiyo, habari ya kutuhumiana hebu epuka Salome, tumalzie vizuri tunamaliza kesho au *panic* kwamba mambo magumu kule? (*Kicheko*)

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kanuni za Bunge ndiyo Kamati inayotegemewa kufuata Kanuni hizi kwa sababu ndiyo Kamati ambayo inalea Kanuni za Bunge. Kiutaratibu na wewe utanisaidia kama nakosea, kiutaratibu Kamati ikishatoa mapendekezo kwa Wajumbe, Sekretarieti itaenda kutengeneza Rasimu na Rasimu ile italetwa kwa wajumbe ili waweze kusema hiki ni sawa au hiki sio sawa.

SPIKA: Nimekuuliza, kipyta kilichoko humu ni nini unaanza *story*. Una dakika tano tu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, kipyta kilichomo humu mapendekezo yaliyokubaliwa na Wajumbe

kwenye Kamatihayajathibitishwa na Kamati kama mchakato unavyotaka na hiyo ndiyo changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Hebu kaa chini...

MHE. SALOME W. MAKAMBA: ... mimi siwezi kuwa...

SPIKA: Nasema mara ya pili, kaa chini.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: ... ni sawa hamna shida!

SPIKA: Huyu mtu kichwa chake kikoje huyu? Mnalewa pombe, mnakuwaje?

MBUNGE FULANI: Unajua Wahehe ni wabishi sana!

SPIKA: Haya Salome, *out!* Mtu umeshiriki mwanzo mwisho, kila kitu ndiyo hiki hapa. Sema kitu gani ambacho kimepandikizwa hapa, hakuna!

Wewe! Askari hebu shughulika na huyu na nisikuone hapa mpaka baada ya siku saba. Kama siku saba utanikuta mimi hapa. (*Makofi*)

(Hapa Mhe. Salome W. Makamba Alitoka Ukumbini)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Sijui ni bangi, sijui ni nini? Umeshiriki kila kitu tangu mwanzo mwisho. Sema kitu gani kimepandikizwa, hakuna! Kilicho...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, Faru John, Faru John!

SPIKA: Watu wa ajabu sana hawa na posho zote umevuta, unakuja hapa unajishauashaua tu! (*Makofi*)

Hili ndiyo tatizo, mnadanganya Watanzania kila wakati wahisi kwamba kuna watu wanaonewa. Kuna kitu gani kinaonea mtu hapa? Sema kitu fulani mimi niliwaza tofauti, Kamati wamewaza tofauti, bado nalistawishi Bunge liwaze hivi. Hiyo ni hoja! Sikusaba ndiyo uje unitafute. (*Makof/ Kicheko*)

Mheshimiwa Hamidu Bobali, hayupo, tunaendelea. Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kutambua mchango wako mkubwa katika *jurisprudence* ya Bunge hili. Tunapozungumzia sayansi ya Bunge hili ufahamu/*knowledge* ya Bunge hili, tunakutaja wewe pamoja na Maspika waliotangulia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na Taarifa ya Kamati ambayo ni nzuri na mimi naifiki moja kwa moja, naomba niongezee tu pale ambapo mzee Mwakasaka amezungumzia. Hii ni misingi ya Ibara ya 52 ya Katiba yetu, Ibara ya 52(3) ya Katiba inamtaja Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba katika utekelezaji wa shughuli za Serikali, ye ye hatakuwa mtu wa mwisho moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 53(2) inamtaja Mheshimiwa Rais kwamba ye ye ndiye mwenye mamlaka ya mwisho kabisa. Hizi ni katika Ibara ambazo zinazungumzia majukumu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo naafikiana na Mheshimiwa Mwakasaka kwamba zile tamaduni ambazo tumekuwa tunaziiga kwa wenzetu wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola hususan wenzetu Waingereza basi tuangalie utaratibu mzuri zaidi kama ambao umewasilishwa na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuzingatia misingi ya Ibara ya 52 pamoja na Ibara ya 53. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Taifa letu sasa linajikita katika misingi ile ya ujamaa na kujitegemea na hii ni sababu kubwa ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa akitekeleza baadhi ya majukumu yake kwa kujitegemea sisi wenywewe, utekelezaji wa miradi mikubwa na masuala mengine.

Naomba Bunge lako Tukufu kuendelea kuzingatia fikra za kuondoa kabisa fikra za kitumwa, kitwana, kikoloni pamoja na kibaguzi katika Kanuni zetu kwa kuzingatia pengine matumizi ya Kanuni ambazo zinakwenda kuweka mila na desturi na hapa naomba nizungumzie kidogo tu kwenye eneo hili la mavazi.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiiga tamaduni za wazungu katika kucaa tunapoingia hapa Bungeni hususan uvaaji wa makoti wakati umevaa kanzu. Nikuombe kama utaridhia na Bunge litaridhia basi tuangalie mchakato wa uvaaji wa mavazi ndani ya Bunge. Pengine kwa kutumia Wizara inayojihusisha na masuala ya sanaa kwa kuandaa vazi rasmi kabisa la Kitanzania ambalo pengine Wabungewanaweza kuingia humu Bungeni wakiwa wamevaa na wamependeza vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia kwa mavazi yale ya kanzu, unapoweka kanzu ukaweka baghalashee na suti, lile si vazi rasmi; lile ni vazi ambalo wenzetu wa Jumuiya ya Ulaya wamekuwa wakilivaa. Kwa hiyo, tuangalie uwezekano katika Kanuni zetu tuweze kuondoa wakati unapovaa kanzu, ukivaa kanzu na baghalashee ijitosheleze pengine liwe ni vazi rasmi kwa Mbunge ye yote kuweza kuingia Bungeni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama inawezekana pia tuangalie uwezekano wa matumizi ya mavazi kutokana na mila na desturi zetu ili tuendelee kulinda mila na desturi zetu, tunaweza kuangalia vazi la baadhi ya makabila ambalo linaweza kuwa ni vazi la staha ili tuweze kuwasilisha Taifa letu kwasababu misingi ya Taifa letu sasa Serikali ya Awamu ya Tano lakini Bunge la Kumi la Moja limejikita sana katika misingi iliyopo katika Ibara ya 9 ya Katiba, ibara inayozungumzia ileile misingi ya ujamaa na kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapozungumzia ujamaa na kujitegemea tunzungumzia zaidi kuhusu mila na desturi zetu. Kwa hiyo, naomba nifanye ushawishi kwa Waheshimiwa Wabunge kuona uwezekano wa kuangalia mavazi ambayo yanaendana na mila na desturi zetu kwa

Wamasai, Wasukuma wale ambao wana mavazi yanayoendana na vile, basi waruhusiwe kuingia Bungeni na ille liwe ni vazi rasmi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namba kuwasilisha lakini pia naafikiana na mapendekezo yote yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa kutoka kwa nani, endelea kuongea jitambulische.

TAARIFA

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, nashukuru, nilikuwa nataka nimpe tu taarifa mzungumzaji aliyeppita kuhusiana na kuiomba Wizara tuangalie namna ya kuwa na vazi ambalo litavaliwa...

SPIKA: Aah Mheshimiwa Waziri

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: ...ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba sisi kama Wizara tayari tupo kwenye mchakato wa kuandaa vazi ambalo tunataka tuliletie ndani ya Bunge lako Tukufu ili liwe linavaliwa angalau mara moja kwa wiki.

Kwa hiyo, mchakato huo umefika vizuri, ni imani yetu kwamba tutakaporudi hapa ndani ya Bunge lijalo, tutaleta hilo vazi ndani ya Bunge ili liweze kupitishwa na Wabunge wote waweze kulivaa angalau kwa siku moja tu ya wiki ndani ya Bunge, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante hayo watakutana nayo waliojaaliwa, Mheshimiwa Mchengerwa kidogo tu kuhusu vazi la kanzu na kadhalika...

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Spika, ndiyo.

SPIKA: Asili ya kuwekwa mavazi haya ni kwamba mtu asichakachue mavazi ndiyo asili yake kwamba ukivaa suti ya Kiingereza basi uivae kwa utaratibu uleule wa suti ya Kiingereza, usipachike pachike vitu. Ukivaa kanzu basi uvae kanzu kwa ukamilifu wake kwamba utavaa balaghashia, kanzu, koti na utavaa makobadhi pale chini miguuni; huwezi kuvaan kanzu na kiatu umevunga gidamu namna hiyo. Kwa hiyo, Kanuni zipo hivyo zinaangalia vazi lakini katika ukamilifu wake, siyo nusunusu. (*Makofi*)

Ahsante Mheshimiwa Mchengerwa, Mheshimiwa Raphael Chegeni atafuatiwa na Mheshimiwa Almas Maige.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuweza kuwasilisha vizuri mapendekezo haya kwa ajili ya Kanuni zetu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba niwarejeshe Wabunge wenzangu wafahamu kwamba Kanuni hizi zilirekebishwa mara ya kwanza 2006 na msimamizi wa kurekebisha Kanuni hizi ulikuwa ni wewe. Kwa hiyo, nakupongeza sana kwamba ulianzisha mchakato mzuri ukiwa msimamizi wamarekebisho ya Kanuni hizi 2006.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba sisi Bunge letu linaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni za Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Na kwasababu vitu vingi tunafanya kama ilivyo, naomba tu kwenye Kanuni tuzingatie yafuatayo; suala la Waziri Mkuu nadhani Mheshimiwa Mwakasaka amelizungumza vizuri zaidi. Sioni haja ya kuendelea kumuuliza maswali ya papo kwa papo, kwa sisi siyo mtendaji Mkuu wa Serikali, yeye ni msimamizi wa shughuli za Serikali Bungeni.

Kwa maana hiyo, nadhani itakuwa vizuri zaidi Mawaziri kwasababu wanapewa nafasi ya kuulizwa maswali na Wabunge moja kwa moja au kujadili hapa Bungeni

itakuwa ni fursa nzuri ya kuweza kupata majibu ya kina zaidi kuliko kwa Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda niwaombe Wabunge wenzangu katika Kanuni hizi tukubaliane, maswali tunayouliza yanakuwa ni mrefu mmoja, majibu yanayojibowi na yenyewe ni mrefu mno, nadhani tuwe na utaratibu wa Kikanuni maswali yaulizwe kwa mujibu wa taratibu wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola (*CPA*) na majibu yafuate vilevile kwa sababu urefu wa swali ndiyo urefu wa majibu. Na naomba pengine Waheshimiwa Mawaziri wanapojobu maswali haya, wajikite katika kujibu maswali yaliyoushwa kuliko kuweka porojo nyingi; amechangia huyu mzuri na kadhalika, wapiga kura wanatujua vizuri...

MHE. ESTER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Naomba msema taarifa ni sauti ya kike nimesikia

MHE. ESTER N. MATIKO: Ester Matiko

SPIKA: *Okay*, Mheshimiwa Matiko.

TAARIFA

MHE. ESTER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Chegeni amesema vyema kwamba tunafuata taratibu za Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Na kwa mfano Uingereza tunaona Waziri Mkuu akiulizwa amaswali. Waziri Mkuu tunamuuliza maswali ya Kisera, Mawaziri wakija hapa tunawauliza maswali ya kiutendaji zaidi. Sasa nikupe tu taarifa kwamba ni vyema tuendelee kumuuliza Waziri Mkuu maswali na tunafuata jinsi Jumuiya ya Madola wanafanya. (*Makofii*)

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, sijaipokea taarifa yake kwasababu nadhani amejichangaya. Jumuiya ya Madola ukikuta Waziri Mkuu anapouliwa maswali kwa mfano Uingereza yule mtendaji mkuu wa Serikali, *is*

Executive Prime Minister, huyu siyo Mtendaji Mkuu wa Serikali, ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni; naomba tusiwe tunachanganya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni Mwenyekiti wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola Tawi la Tanzania, ninachokizungumza nakielewa. Naomba ukitaka nitakuja nikueleze zaidi kwa muda wako. (Makofi/Kicheko)

MBUNGE FULANI: Akufate wapi?

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Atanifuata popote.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme suala zima la taarifa za Kamati halikuingia kwenye Kanuni. Kamati hizi zinafanya kazi kubwa sana za kuchambua mambo mbalimbali lakini wakati wa kutoa taarifa hapa Bungeni muda unakuwa ni mchache sana, unakuta kamati mbili au tatu kwa siku moja; huu muda hautoshi kujadili masuala ya msingi. Kwa hiyo, ningeomba kupitia Kanuni hizi tutenge muda wa kutosha kuzipa kamati muda wa kutafakari na kuweza kutoa taarifa sahihi Bungeni na Wabunge wapate kuchangia kwa kirefu zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile suala jingine ni muda wa kuchangia, kwa kweli nakubaliana na ile Kanuni kwamba tunguze dakika 15 mpaka dakika 10 kwasababu Wabunge wote tunaweza kuchangia humu ndani, dakika tano tumia kupongeza, kushukuru na kufanya nini yote nadhani tukiyapunguza haya yata-save muda. Na kwasababu tupo wengi tupate muda wa kuongea kama ambavyo Kanuni inavyopendekeza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala jingine ni suala la Vikao vya Kamati, nimeshukuru sana kuna pendekezo kwamba kwenye vikao vya Kamati viendeshwe kwa utaratibu sasa ili kusudi kama kuna baadhi ya Wajumbe wa Kamati wanashindwa kutii misingi ya Kamati basi Kanuni iweze kuchukua muda wake. Na hii itasaidia sana kujenga nidhamu kwenye Kamati kama ilivyo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, lingine...

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Chegeni

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Almas Maige.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kuniruhusu nichangie Azimio hili la kubadilisha/kuboresha Kanuni za Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa mmoja ya watu ambao wamepata tabu sana kutumia Kanuni hizi na kama unavyoja uliniweka kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na tullanza na Mheshimiwa Mkuchika. Tumepata tabu sana kwa ababu makosa yote yaliyotokea tuliponea Kanuni ya 74(3) mpaka (4) ambayo ndiyo ilikuwa kama ndiyo mwarobaini wa kutoa adhabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wale tuliowapa adhabu waliturudia tena na mimi sikosei nikintaja Mheshimiwa Heche ambaye alinifuata ndani ya canteen nimekaa na Wabunge wa Tabora na akaniambia wewe lizee ngoja tu, wewe ndiyo nongwa sana hapa na Kanuni ya kuweza kujitetea. Mabadiliko haya yanaleta mwelekeo wa kupata adhabu nyingine kwa watu ambao wafanya makosa haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile Kanuni ambayo tulikuwa nayo ilikuwa kimya sana kwenye maeneo chungu mzima. Tulipata tatizo la kutoa au kutoakutoa adhabu kwa mmoja wetu waliyekwenda kuwakilisha nchi hii nje ya nchi na jinsi ya kumrekebisha ikawa vigumu sana. Kulikuwa na makosa walifanya watu nje kulikosea Bunge, wote tunaenda kujietetea kutumia Kanuni ya 74, haikuwa sahihi.

Mheshimiwa Spika, ni mmoja wa watu waliofurahia sana mabadiliko haya ya leo na naunga mkono kabisa Azimio

hili ambalo kwa kweli litakuja kuwa na manufaa kwa watumiaji wote wa Bunge, nakushukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa tunapoendelea kujadili mapendekezo haya msije mkapata picha kama vile lile la maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu limeondolewa na mapendekezo haya, halimo katika mapendekezo yaani lipo kama liliivyokuwa zamani. Kwa hiyo, mawazo yanayotolewa ni mawazo ya wanaochangia mmoja mmoja wanavyoona wao, kwa hiyo msije mkalihesabu hivyo. Ndilo hayo nilikuwa nasema ya Mheshimiwa Salome anafikiri kuna kitu kimechomekewa, hakuna kilichochohomekewa hata kimoja. (*Makofii*)

Sasa Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Gidarya

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Kwa sababu leo ni mara ya mwisho kusimama ndani ya Bunge lako na kuchangia basi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeneweza kuwepo hapa. Nimshukuru Mungu kwa kunipa kibali, kunibariki, kunilinda na kuniongoza vyema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili; naomba nishukuru Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kuniamini kunitfea na kunipa ridhaa ya kuwa Mbunge kwasababu bila CHADEMA nisingekuwepo humu ndani. Na *through* CHADEMA nimeweza kuwa mwanasiasa sikuwa na *knowledge/skills* za kuwa mwanasiasa. Kwa hiyo, nawashukuru kwa kunipa hiyo *platform* na *opportunity*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia naomba nilishukuru Bunge lako, wewe mwenyewe, Naibu Spika na timu yako nzima, mmetupa mwongozo mzuri kwa miaka hii minne *point* tano na mpaka sasa hivi tunaenda kuhitimisha. Sina budi pia kushukuru uongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yako yote nashukuru sana. Sina budi kumshukuru Katibu wa Bunge na timu yake yote,

wametuwezesha Wabunge kuweza kutimiza majukumu yetu ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, itakuwa sitendi vyema pia kutotoa shukrani kwa vyombo vy ya ulinzi na usalamakwa kutuhakikishia kwamba tupo sawa, watoa huduma wa kutunza mazingira na usafi ni wa muhimu sana na hata watoa huduma wa chakula Bungeni kwasababu nafikiri muda mwangi kama hatupo humu ndani Waheshimiwa Wabunge tupo *canteen*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sisi binadamu si wakamilifu, tumekuwa tukikoseana labda kwa kupanga au kutokupanga kwa kutofautiana na fikra basi naomba tusameheane kwasababu nafikiri wote tulikuwa hapa katika kujenga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo ni dhahiri kwamba nimepiga kura ya ndiyo, nimeenda kinyume na upande niliopo ukizingatia *issues za three-line whip* ndiyo hiyo ilikuwa ni kuashiria kwamba ninaunga mkono bajeti ya Serikali na Serikali ipo chini ya CCM. Basi kwa hatua hiyohiyo ninaomba ridhaa ya kuwa chini ya uongozi wa Serikali ya CCM... (*Makofi/Vigelegele*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, bado watano tulishasema bado watano.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Ahsante sana Sware kalamakito mwanawito...

(*Hapa baadhi ya Wabunge waliiimba wimbo wa CCM na Mheshimiwa Juma S. Nkamia aliiimba kilugha*)

SPIKA: Mliowasha *mic it is not fair*, msiwashe *mic*.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, nimefikia maamuzi haya kwa kufuata nafsi yangu inavyonituma kwa kumtegemea Mungu na nimewezeshwa kufikia maamuzi haya kwa sababu uliniwezesha kuwa kwenye

Kamati yako ya Bajeti. Na kwa kupitia Kamati ya Bajeti nimeweza kujifunza kwelikweli majukumu ya Mbunge ni nani katika kuishauri na kuismamia Serikali na nimejifunza kuwa Mbunge maana yake nini na nguvu ya chama katika Mbunge katika kufanya maamuzi au katika kushauri ikoje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, basi ninaomba ridhaa hiyo kuwa chini ya uongozi wa CCM ili niweze kuendelea kutoa mchango wangu katika kulijenga Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kwa kuwa pia mada iliyopo mezani ni kuhusu Kanuni za Bunge, ninaziunga mkono ili hao wabunge watakaokuja kwa hilo Bunge la Kumi na Mbili waweze kuwa *channeled* vizuri na kutekeleza majukumu yao salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi. (*Makofi*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, ahame kiti. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu, naomba Mheshimiwa Anna Gidarya achangie hoja iliyo mbele yetu.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kuwa sehemu ya Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani ya miaka minne na nusu.

Mheshimiwa Spika, binafsi nikushukuru wewe mwenyewe, nimshukuru Naibu Spika wa Bunge...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawaombe tusikilizane anapoongea mwenzetu.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Spika, pia niwashukuru watendaji wakuu wa Serikali ambaao ni Mawaziri wote, tumeshirikiana kwa hali na mali katika kutatua matatizo kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kwasababu mtoto anazaliwa na anakua, katika ukuaji kuna waliochangia hatua zake za ukuaji. Nishukuru Chama Cha Demokrasia na Maendeleo kwa kunipa nafasi ya mimi kuwa Mbunge ndani ya miaka minne ambayo kesho Bunge likivunjwa nitakuwa nimekoma katika ukomo wa nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninatambua juhudini kubwa inayofanywa na Serikali na leo nimepiga kura ya ndiyo kwa nia ya dhati na kwa makusudi, Watanzania walio wengi wanatuangalia sisi kwa ajili ya maendeleo yao. Kwa hiyo, kwa dhamira ya dhati ya moyo wangu siumii na wala sishuhudii maumivu kwamba nimefanya makosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, basi kwa misingi hiyo naomba pia niwashukuru wananchi wangu wa Mkoa wa Manyara kwa muda wote ambaao tumeshirikiana katika kutekeleza na kutatua kero zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijawa Mbunge wa CHADEMA nilikuwa mtumishi ndani ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, basi kwa tamko hili la leo, mrudi kwao si mtumwa. Kesho Bunge likivunjwa ninarudi rasmi kwa baba yangu. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, bila kupoteza muda, mwisho kabisa niseme uamuzi huu ni uamuzi wangu mwenyewe bila kushurutishwa na mtu na nina amini kwa upande wa CHADEMA hautakuwa umeumiza chama lakini na mimi pia sitegemei maumivu kupitia wao. Ahsante. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Yajayoo! (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Yanafurahisha! (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Sasa naomba nimkaribishe Mheshimiwa Latifah Chande Hassan Kigwalilo.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mtukufu, Mwingi wa Rehma, kwa kunifikisha leo hii nikiwa mzima mwenye afya njema kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nakushukuru wewe, Mheshimiwa Naibu Spika, Katibu wa Bunge na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mkubwa walionipa kwa kipindi hiki chote nikiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, pili, nakishukuru chama changu na Uongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuwa Mbunge mpaka leo hii nimesimama hapa kama Mbunge. Tatu, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano wao na mshikamano wao katika kipindi hiki chote nikihudumia kama Mbunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nne, naishukuru familia yangu kwa ushirikiano mkubwa walionipatia na kwa kipekee zaidi namshukuru mume wangu kwa *support* kubwa aliyonipa katika kazi yangu ya kibunge kwa uvumilivu na ustahimilivu pamoja na ushauri mkubwa alionipatia; bila kuwasahau wazazi wangu ambao wameniweka kwenye maombi usiku na mchana ili niweze kutekeleza majukumu yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa nia yake ya dhati na thabiti ndani ya maono mazito ya kuifikisha nchi yetu katika uchumi wa kati na uchumi wa viwanda. (*Makofii*)

Ndugu zangu, mwenye macho haambiwi ona. Sote tumejionea kwa macho yetu kazi kubwa iliyotukuka ambayo Serikali ya Awamu ya Tano imeifanya tangu ilipoingia madarakani rasmi Novemba tarehe 5, 2015. Nawapongeza

Mawaziri, Watendaji wote wa Serikali wa ngazi zote kwa moyo wa kufanya kazi na kuifanya ndoto ya Rais na Jemedari wetu Mkuu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli idhihirike mbele ya macho yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama mwanasiasa kijana, msomi, mwenye uelewa na uwezo wa kuona na kupambania mambo mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya wananchi, basi hadi kufikia leo nimepata muda wa kutosha wa kutafakari kwa kina na siku ya leo tarehe 15 Juni, 2020 ninatangaza rasmi kukihama Chama cha Demokrasia na Maendeleo, naomba ridhaa ya kujunga na Chama cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti wake, Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ili niweze kufanya mambo mengine katika kujenga nchi yetu. (*Kicheko/Makof!/Vigelegele*)

MBUNGE FULANI: Yajayo! (*Makof!*)

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: Mheshimiwa Spika, kwa wale wote ambao kwa namna moja au nydingine naweza nikawa nimewakwaza naomba mniwie radhi, nami vilevile nawasamehe wote ambao walinikwaza kwa namna moja au nydingine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki nimejifunza mengi na mpaka leo hii nimefikia hatua hii nawashukuruni wote na ninaahidi mtakaponipokea nitajumuika na nyie kwa utiifu na nitashiriki kikamilifu katika kujenga nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa mara nydingine tena, nawashukuru wote. Napenda kuunga mkono hii hoja iliyotolewa hapa. Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Latifah. Karibu nyumbani. (*Makof!*)

Sasa kabla sijamuita Naibu Spika kuhitimisha hoja yake, nawaomba kwa kifupi sana; Mheshimiwa Najma kwa dakika mbili tatu na Mheshimiwa Andrew Chenge kwa dakika

hizo hizo mbili tatu, halafu nitamwita Mheshimiwa Naibu Spika kusema chochote. (*Makofi*)

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa *surprise* nzuri kama hii. Nitumie tu fursa hii ambayo umenipa kutoa shukrani za dhati kwanza kwako wewe mwenyewe; narudia tena mara ya pili, lakini siyo ya pili, ni mara nyingi sana kabla hujakuwepo mbele yangu au ukiwa hauko mbele yangu, nimekuwa nazungumza na vyombo nya habari, magazeti jinsi ambavyo tumekuwa tukishirikiana katika kazi ndani ya Bunge hili. Kwa hiyo, leo hii nikirudia tena hapa mbele yako na mbele ya Wabunge wote; na leo wako wengi sana, siyo mbaya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hapa nikiwa chini ya uongozi wako pamoja na timu yako nzima kwa namna ambavyo tumefanya kazi kwa kushirikiana vizuri kabisa, nimeweza kujijengea uwezo kupitia kwako pamoja na viongozi wengine wote katika hili Bunge. Nashukuru sana, nimeweza kufikia hatua nzuri kiasi kwamba naweza kujipongeza mwenyewe kusema kuwa kuna mambo ambayo nimejifunza ambayo bila ya kuwa chini yako nisingeweza kuyapata.

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru viongozi wote wengine akiwa Naibu Spika; *Chief Whip*, dada yangu au mdogo wangu; Mwanasheria Mkuu ambaye tuko naye saa zote kwenye Kamati ya Katiba na Sheria; na Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria. Tokea tumeanza mwanzo hadi mwisho, kwa kweli tumefanyakazi kwa ushirikiano mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile nawashukuru Wabunge wote bila ya kujali itikadi za chama jinsi ambavyo nimekuwa nikishirikiana nao kwa namna ya pekee kabisa. Wakati naingia hapa Bungeni nikiomba nafasi ya Uenyekiti kuna mmoja aliniuliza swali kwamba nitaweba vipi kudumisha mahusiano? Basi naomba kama kuna mtu ambaye anaona nimepotosha mahusiano, basi asimame aseme hapa ili ionekane kwamba kauli yangu ilikuwa siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, naamni kwamba mahusiano yangu yalikuwa mazuri na wote Wabunge humu ndani nami hashukuru kwa hilo. Naamini kwamba imani yenu ambayo mmenipa kwa muda wote huu, basi hata tukiwa nje ya Bunge kuanzia wewe timu yako yote ya Makatibu basi na huko nje mtanipa ushirikiano mzuri kama huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nawashukuru wote kwa ujumla, lakini niseme kwamba nawaombea kila lenye heri, kwa sababu mtu anaomba yenye heri. Naamini kwamba dua yangu kwenu ninyi nyote itakuwa ni yenye heri na Mwenyezi Mungu atatujaalia yaliyo mazuri mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Najma Giga ambaye ulikuwa Mwenyekiti wetu wa Bunge na mmoja wa wasaidizi wangu hapa Mezani. Sasa Mtemi.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii. Nami kupitia kwako nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupatia uzima. Pia nakishukuru sana Chama cha Mapinduzi kupitia Kamati yetu ya Uongozi hapa Bungeni kwa kupendekeza jina langu kuwa mionganoni mwa majina ya *Presiding Officers* wa kukusaidia wewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuniamini kupitia kura zenu nikaweza kuwa Mwenyekiti mionganoni mwa Wenyeviti wa Bunge kwa kipindi hiki cha miaka minne na miezi mitano na siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawashukuruni sana, mmenisaidia sana katika utumishi, katika kuhudumu kwa nafasi hiyo ya *Presiding Officer*. Nakushukuru wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wenzangu ambapo mmojawao sasa Mheshimiwa Zungu amekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais na Mheshimiwa Najma. Tumefanya kazi vizuri kwa ushirikiano mzuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe na Naibu Spika kwa wakati wote katuonyesha njia ya namna ya kuongoza shughuli za Bunge. Pia naishukuru sana Serikali kuititia Waziri Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yote ya Mawaziri, kwa kipindi hiki tumefanya kazi vizuri na yote haya ni kwa faida ya maendeleo ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hili suala la kanuni tumelifanyia kazi kuititia Kamati ya Kanuni ulioiteua. Kama mnavyoona Waheshimiwa Wabunge, kanuni ambazo tunazo mpaka uzitumie tena ndiyo utaona kama zinatufaa au la. Kwa hiyo, nasema hoja ambayo Mheshimiwa Naibu Spika ameiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, tuiunge mkono ili wenzetu Bunge iljalo waanze kuzitumia; na kama zitakuwa na upungufu tutaona. Nasema tutaona kwa sababu nami natarajia kwamba tutakuwa mionganoni mwa Wabunge ambaao tutarejea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumefanya mengi na nilisema juzi. Maana Bunge kazi yake ni kuwezesha Serikali ifanye mambo yake. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa hayo mazuri tuliyoyafanya kwa faida ya maendeleo ya nchi yetu. Yako mengi na wewe leo umesema vizuri sana wakati tunapitisha Muswada wa *Finance Bill* kwamba katika kipindi hiki yapo yale ambayo tuliyokubaliana na yapo mengine hatukukubaliana. Ndiyo maana ya Bunge! Mengine ukasema tutayatafakari na baadaye mnaona kwamba hapa tuta-converge tu, tutakutana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nisichukue muda wako mwingi, nimesimama kushukuru tu kwa unyenyekevu kwa heshima mliyonipatia ninyi Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Ahsanteni sana, niwatakie kila lililo jema tukutane tena katika jengo hili la Watanzania na Mwenyezi Mungu awapeni afya njema tukafanye kampeni za heshima kule kwenye Majimbo yetu. Ahsanteni sana.

SPIKA: Ahsante sana Mtemi Chenge, Mwenyekiti wa Bunge, nakushukuru tena kwa kunisaidia sana hapa Mezani.

Sasa kabla sijaenda kwa Naibu Spika, kwa dakika chache nimwombe Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, kuna jambo liliiongelewa sana hapa, kama unawenza ukapitia kidogo, maana yake ulikuwa katika timu ile iliyoasisi jambo hili. Karibu sana, karibu Mheshimiwa kwa ajili ya kupeana elimu tu.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nakushukuru sana kwa kweli. Hata mimi nimekwaruzwa kidogo na kauli za kwamba Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano hawezi kujibu maswali moja kwa moja kwa sababu ya hali ya *executive powers*, siyo sahihi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, tumelifanya kazi hili chini ya Uenyekiti wako kwenye Bunge la Kumi na ndiyo maana kuna umuhimu wa kurudi kwenye *records* kabla ya kufanya maamuzi yoyote. Mfumo wa demokrasia tunaoufuata hapa ni Demokrasia ya Kibunge (*Parliamentary Democracy*) ambapo mchezo mzima baada ya uchaguzi unahamia Bungeni ambapo vile vile sisi Mawaziri chini ya Waziri Mkuu tunawajibika moja kwa moja kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukisoma Ibara ya 53 (2) inasema: "Serikali ya Jamhuri ya Muungano chini ya mamlaka ya Rais ndiyo itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya Sera ya Serikali kwa ujumla. Katiba sasa inamfanya Rais sasa agawane madaraka na Waziri Mkuu kwenye utekelezaji, siyo Sera. Inasema na Mawaziri chini ya Uongozi wa Waziri Mkuu watawajibika kwa pamoja Bungeni kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waziri Mkuu wetu ana madaraka makubwa sana na Katiba yetu hii *haija-copy* kutoka kwenye Katiba nyingine za Jumuiya ya Madola. Ni *sui generis provision* zake nyingi hapa na ndiyo maana kulitokea dhana miaka ya 1960 (Profesa Kabudi unakumbuka) ya *constitutional doctrine* yaani tulitengeneza hii Katiba siyo kwa *ku-copy*; siyo *cut and paste*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna Waziri Mkuu mwenye mamlaka na ndio maana tunaendelea kumpa heshima kubwa sana Waziri Mkuu, ndio maana akisimama akisema geuka kushoto, sisi tunageuka kushoto. Msifikiri tunageuka tu kwa maneno tu, ni kwa sababu ana madaraka. Ana-share madaraka na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema, ukisoma Ibara ya 57, Waziri Mkuu akijiuzulu leo Mawaziri wote hatuna kazi. Sijui mnaelewa msingi wake ni nini? Msingi ni kwamba tunakaa na mtu hapa Bungeni hata kama ni kiongozi ambaye anajishusha sana, lakini tunakaa na kiongozi mwenye madaraka makubwa sana tena sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba, kama ulivyosema mwanzoni, hili suala liendelee kujadiliwa kwenye Bunge la Kumi na Mbili. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe. Bunge ni shule yaani unajifunza mambo mengi sana ukiwa Bungeni. Wale wa Bunge lile liliopita, mtakumbuka wakati Mheshimiwa Lowassa amesimama humu ndani ya Bunge na kujuzulu, kama mnakumbuka, Mheshimiwa Spika Sitta ilibidi aombe mwongozo kwa Wabunge; Jamani, sasa tunafanyaje?

Kwa nini hilo lilitokea? Mheshimiwa Waziri Mkuu akijiuzulu hapa, maana yake Serikali hakuna. Bunge lazima Serikali iwepo, yaani lazima Serikali iwepo na sisi tuwepo. Inapokuwa Serikali hakuna, kuna Bunge? Sasa ameshajiuZulu, Bunge hakuna, sasa Spika afanyeje pale? Yaani hata jinsi ya kuahirisha shughuli, sijui unafanyaje, kwa sababu Serikali haipo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni mjadala mzuri, mpana mrefu, pande zote zinazungumza vitu ambavyo ni *logical* sana. Tunadhani basi, hebu tuwaacie wenzetu watakuja kulitazama zaidi huko mbele. Ndiyo maana huku nyuma ikawa ni Maswali ya Sera tu peke yake. Pia nia yake ilikuwa

ni kuwapa Waheshimiwa Wabunge nafasi; wakati mwiningine Mbunge una jambo; na shida za maswali ya Wabunge huwa siyo maswali ya Wabunge, ni swali la wananchi. Yaani kuna jambo ambalo wananchi wako wakisikia tu Waziri Mkuu analijibu, yaani ni tiba tosha, Mbunge umesrafanya kazi yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni fursa tu, dirisha fulani, siyo kwa ajili ya Waziri Mkuu kufanya nini au nini, lakini ni fursa ya kutibu kidogo baadhi ya mambo ambayo yanaweza yakajibowi, lakini likijibowi na Naibu Waziri bado sawa, lakini bado kuna mwenyewe ambaye ndiyo Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika uhitimishe hoja yako, halafu baadaye nitakupa muda kwa lile lingine.

MHE. DKT. TULIA ACKSON - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA KANUNI ZA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuhitimisha hoja hii ambayo nimeileta Mezani ambayo inaangalia changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa kuendesha Bunge la Kumi na Moja katika kanuni hizi ambazo tumekuwa tukizitumia.

Mheshimiwa Spika, hoja hii imechangiwa na Wabunge wapatao 11 na wengi wao wamekubaliana na yale ambayo tumeyaleta kama Kamati. Nitoe ufanuzi kwa baadhi ya hoja zao japokuwa sitamtaja Mbunge mmoja mmoja isipokuwa kwa wale ambao labda hoja zao ni mahsus.

Mheshimiwa Spika, nianze na hoja ya kwanza ambayo umeitolea ufanuzi wewe na ninaamini kwamba Waheshimiwa Wabunge wanafahamu wewe ndiye Mwenyekiti wa Kamati hii. Kwa hiyo, yale ambayo pengine nitakuwa sijatoa ufanuzi, unaweza ukaongezea hapo.

Mheshimiwa Spika, nianze na hili ambalo amelitolea ufanuzi Mheshimiwa Mwakyembe na wewe umeshalitolea

ufafanuzi kwa hiyo sitalirejea jambo hilo la maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hata hivyo, katika wachangiaji lipo jambo ambalo amelizungumza Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, kuhusu nidhamu ya hapa Bungeni lakini pia wakati mwingine mazingira labda ya Mbunge na Mbunge kukoseana. Wakati akieleza kuhusu nidhamu ya hapa Bungeni ameelleza namna ambavyo wapo Wabunge ambaao wanarejea yale yale makosa au wanafanya mengine zaidi huku wakijua kwamba makosa ni kuzipungukia Kanuni za Mbunge.

Mheshimiwa Spika, katika Maboresho ambaao kanuni hizi zinafanyiwa siku ya leo sehemu mojawapo ni hiyo ya kuongeza aina za makosa ambayo Mheshimiwa Mbunge ambayo anaweza kuadhibiwa; lakini pia kuweka adhabu wazi kabisa kama Mheshimiwa Mbunge atakuwa anarudia rudia hayo makosa ambayo ameshawahi kuyafanya. Kwa hivyo, hoja hii ya nidhamu na kama makosa yanayorudiwa rudiwa kama adhabu hazitoshelezi adhabu sasa zitatosheleza kwa kadri tuliyopendekeza.

Mheshimiwa Spika, kwenye hoja hii kuna jambo la Wabunge wenyewe kuchafuana na pengine kwenye mazingira ya wao uso kwa uso ama kwa kuandikiana katika yale maeneo ambayo Wabunge wanaweza wakaandikiana. Kwenye hili mapendekezo haya tuliyoyaweka haliongelei hili jambo lakini nadhani utaratibu wa kawaida wa kisheria unaweza ukatumika kwa Mbunge ambaye anaweza kuwa ameumizwa na maneno ya Mbunge mwingine kama ni nje ya ule utaratibu wetu wa Kibunge; kwa maana ya kwamba kazi za humu ndani ama kwenye kamati, hawa watakuwa wapo tayari kwenye hizi kanuni namna ambavyo tulivyoziveka kwenye kwa maboresho hayo. Kwa wale walio koseana wao binafsi wanaweza kuchukua mkondo wa kisheria ili tusiingie huko kwenye hili Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo pengine ningetaka kilitolea ufanuzi ni alilochangia Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa kuhusu mavazi Bungeni. Mheshimiwa Naibu Waziri ameongelea mchakato wa Serikali

na nisingependa kwenda huko, lakini pia umetoa ufanuzi kuhusu jambo hili na ninadhani tukubaliane na huo ufanuzi ulioutoa kama kiongozi wa Kamati hii ya Kanuni.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Raphael Chegeni pamoja na mambo mengine ameuliza mambo ambao machache ambayo nataka niyazungumzie. Amezungumza kuhusu maswali kuwa mafupi na pia majibu kwamba yawe mafupi na pengine tungeyaweka vizuri kwenye kanuni. Kanuni zilizopo sasa zimeweka utaratibu mzuri pengine unavyotuungeza na pengine sisi tunavyokusaidia tutajaribu kuona namna bora ya kuyafanya hayo majibu na maswali yawe mafupi kwa sababu huwa yanapitiwa kabla hajapelekwa Serikali kabla yakujibwa kwa hiyo utaratibu ule uliopo sasa unao uwezo wa kutosheleza jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kamati kutoa kuongezewa muda wa kutoa taarifa Bungeni nadhani tunaweza kuangalia hizi kanuni zilivyobadilishwa sasa kwenye kuongeza muda; kwa maana waziri amepunguziwa muda kidogo na pia Wabunge wamepunguziwa muda kidogo kwa hiyo itatoa fursa kwa wajumbe wa Kamati kuweka nyama kwenye yale ambayo Kamati itakuwa imetoa ufanuzi hapa ndani. Vilevile pia kwa sababu kamati inaruhusiwa kuleta taarifa ndefu lakini ikasema yote iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, Wabunge wanaweza kupata fursa ya kusoma taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, mengine alikuwa akiunga mkono hoja. Wabunge wengine ambao nimesema sitawataja lakini niwataje wengine kwamakundi; Mheshimiwa Spika, hoja yako hii ambayo ni ya mabadiliko ya kanuni imekuja na mambo mengine kwa sababu nami natoka Chama cha Mapinduzi, ina mambo mazuri. Hoja hii imerejesha Wabunge watatu kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo kuhamia Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya ufanuzi huo nikushukuru tena kwa fursa kwa wote waliochangia hoja hii, lakini pia wajumbe wa Kamati kwa mawazo yao ambayo

yamepelekea hoja hii kukamiliaka na hata kuweza mapndekezo haya mbele ya Bunge. Aidha, ninawashukuru sana wote ambao wameweza kutoa changamoto ambazo zitawenza kufanyiwa kazi hapo baadaye ambapo kanuni zetu mpaka sasa zitakuwa hazizungumzi hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika hoja imetolewa na imeungwa mkono tayari mmeshapiga kura zinavyoonyesha walio wengi wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja illamuliwa na kuafikiwa)*

**Azimio la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kanuni za Bunge
kuhusu Marekebisho ya Kanuni za Bunge lilipitishwa na
Bunge**

SPIKA: Kwa hiyo kanuni hizi mpya zimeungwa mkono zitawekwa vizuri na katibu na zitachapishwa katika kijitabu maalum kabisa ambapo mionganini mwa *documents* ambazo Wabunge wapya watakafokika mwezi Novemba katika mkoba watakaopewa mmojawapo utakuwa na kanuni hizi mpya. Kwa hiyo hata wabunge ambao mtaendelea, na mimi naamini walio wengi mtaendelea, wakati huo ukifika ni vizuri kusizoma kanuni hizo mpya kwa sababu zina haya mabadiliko ambayo ni vizuri kuyazingatia ili tuweze kwenda vizuri kwa pamoja. (*Makofii*)

Kama tulivyosema, jambo hii tulilianza zaidi ya mwaka mmoja uliopita tukitoa wito kwenu wote, kila wakati nikilizungumza hapa kwamba jamani mwenye mapendekezo, mwenye maoni ya kutakana marekebisho popote kwenye kanuni tafadhali tuyapeleke marekebisho hayo. Tukakumbusha tena na tena na tena na tena mpaka Kamati ikaanza kukaa kwenye Bunge lilitopita ikaanza

kuchambua; na kwenye Bunge hili pia ikaendelea kuchambua; wakati fulani chini ya uwenyekiti wangu, wakati fulani chini wa Naibu Spika. Hata dada yetu Salome makamba amehudhuria vikao *almost* vyote vinavyohusika na mambo haya. Lakini ile tabia tu niliyoileza ya mtu lazima apainge kitu yaani haiwezakani lazima upinge tu.

Kwa hiyo vitu vidogo vidogo sikuona sikuju kitu gani cha dakika ya mwisho! Kitu muhimu unaangalia zile hoja muhimu zilivyokuja hapa kuna kipya? au ni yale yale tulijojadiliana. Lakini pili mambo ya Kamati si walio wengi wanaamua? Hata hivyo basi sema yaliyowachache kitu gani ambacho unaona hukubaliani nacho. Badala yake ni madongo ambayo hayana kichwa na mguu. Hizi tabia hizi zibadilike ndugu zangu, ndiyo mambo yanayokera katika Ubunge wetu. Yaani mtu anatamani kushambulia tu watu; na wanadhani hiyo ni ujiko. Si anaenda kugombea? Haya aende akaone, kama haya mambo ya ubabe ubabe na nini tena kwa mtoto kwa kike kama wanadhani yanalipa. Kitu kinacholipa uwe mtaratibu.

Sisi waafrika tuna utaratibu jamii inavyokutazama inakutazama hivyo. Mtoto wa kike ana heshima yake kwenye jamii, haruki rukii watu, anawafokea wanaume hadharani, tena wanaume wenyewe baba zake kichwani hamna kitu nani atakuchagua? Kwani unafikiri wale wasukumani wajinga? Wana mila na desturi. Halafu basi kwenye moyo wako uwe na haki ya kufanya hivyo, wala hujachokozwa. Hata hivyo tupo pamoja, utajua vizuri, na mimi si mnanifahamu? Bado nina mambo yake. Kama milioni mbili ilikuwa shughuli huku mbele itakuwa shughuli zaidi.

Sasa nikupae nafasi Mheshimiwa Naibu Spika kama dakika kumi na tano ili tuendelee. (*Kicheko*)

MHE. DKT. TULIA ACKSON: Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kabisa kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutujalia sisi sote uzima na afya. Pia ninakushuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kuzungumza machache ndani ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa shukrani za kipekee sana kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuniona na kunateua kuwa Mbunge kupitia taarifa iliyotolewa saa 12 asubuhi siku ya jumatatu tarehe 16 Novemba, 2015. Fursa aliyonipa Meheshimiwa Rais iliniwezesha kuomba na kupata nafasi hii adhimu ya kuwa Naibu Spika. Kwa heshima hii kubwa sana aliyonipatia ninamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hasan Makamu wa Rais ambaye amekuwa mfano kwa viongozi wanawake. Kupitia utumishi wake mimi na wanawake wengine tumepata mengi yakujifunza.

Mheshimiwa Spika, niuruhusu pia nimshukuru Mheshimiwa Kasim Majaliwa Majaliwa Mbunge na Waziri Mkuu na kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni amenipa mafunzo, ushauri na usaidizi mkubwa katika kipindi chote cha miaka mitano nikihudumu kama Naibu Spika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nirejee kwako mwenyewe. Nikushukuru kwa uongozi wako, mafunzo na fursa ulizoni patia ambazo zililenga kuboresha utendaji kazi wangu; ushauri wako umenifikasiha hapa, ninakukushuru sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nisingewezakupata nafasi hii na pia kutimiza majukumu yangu pasipo nguvu ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Wabunge hawa wamenifundisha mengi, wamenishaidia na wamenipa ushirikiano mkubwa katika kutumikia nafasi hii. Kila mmoja wao ana mchango wa aiana yake katika utumishi wangu kama Naibu Spika. Wabunge wa Chama cha Mapinduzi walismama na mimi wakati wote kupitia michango yao na katika kujenga ushirikiano chanya uliofanikisha kazi zetu kama Bunge. Kwa pamoja tulishirikiana katika kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa watani wetu wa jadi changamoto walizozibua chanya na hasi zote ziliniimaliza kiuongozi na kisiasa, na wao pia nina washukukuru sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuwashukuru sana Watanzania wenzangu kwa kufuatilia shughuli za Bunge lako Tukufu na kututia moyo chini ya uongozi wako. Katika kipindi cha utumishi wangu nimealikwa na kutembelea maeneo mengi ya nchi yetu; huko nimepokelewa kwa upendo sana.

Mheshimiwa Spika, mbali na jina langu la kila siku la Tulia nimeongezewa majina mengi mengine. Nitayataja baadhi tu maana orodha ni ndefu. Kanda ya Ziwa naitwa Sola Nyua, Kanda ya Kati naitwa Nzitu ama Liti, Kanda ya Pwani naitwa Ukti Salma, Nyanda za Juu Kusini naitwa Mbozo au Upendo. Kwa sehemu ya pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ninalo jina adhimu la Bi. Khadija. Majina yote haya ninayependa na nitayaenzei kwa bidii sana daima, nina washukukuru sana Watanzania wenzangu kwa upendo huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninazo salamu za mwaka 2020. Bunge la Kumi na Moja litafikia ukomo wake hizi karibu, fursa hii uliyonipa ya kuzungumza katika Bunge lako Tukufu inanipa nafasi ya kutambua na kupongeza kazi kubwa aliyoifanya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli akisaidiwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kasim Majaliwa Majaliwa ambaye ni Waziri Mkuu. Chini ya uongozi wake thabiti nchi yetu imepiga hatua kubwa katika Nyanja zote.

Mheshimiwa Spika, yaliyofanywa ni mengi lakini nitaje machache kwa mifano. Ujenzi wa Bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa reli mpya ya kisasa, ujenzi wa meli za abiria na mizigo katika maziwa yote nchini, ujenzi wa barabara, ufufuaji wa Shirika la Ndege na umalishaji wa safari za anga na ujenzi wa viwanda mbalimbali. Pamoja na hayo mabadiliko yaliyofanywa katika sekta za madini na uvuvi ni kielezo cha usimamizi madhubuti ya rasilimali za taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki ambacho dunia imekubwa na janga la corona Rais wetu amedhihilisha udhabitii wa maamuzi yake. Ametuhimiza tuendelee kuchapa

kazi huku tukizingatia miongozo ya Serikali, mambo ambayo tunayatekeleza kwa nguvu zote. Uongozi wake umetufanya tutoke salama katika janga hili, Watanzania tunampongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wengi wananzungumza kuhusu kazi nzuri uliyofanya katika Bunge letu Tukufu, lakini si wote watapata fursa ya kuyasema hayo; nami siku ya leo nipate fursa ya kuzungumza wewe kidogo. Sababu ni kwamba si rahisi mtu akajisemea yeye mwenyewe juu ya mambo mazuri aliyoafanya. Kwa hiyo naomba uniruhusu nikupongeze sana kwa kazi nzuri ulizozifanya.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha miaka mitano umetuongoza vyema, umetulea vyema hasa wale tulioingia Bungeni kwa mara ya kwanza na hatukuwa wachache wabunge wapya tulikuwa wastani wa asilimla 70. Pamoja na ulezi huu oongozi wako umeleta mabadiliko makubwa katika utendaji kazi wa Bunge letu hasa kwenye eneo la TEHAMA. Mabadiliko hayo yameokoa takribani bilioni hamsini kwa mwaka katika matumizi ya Bunge. Jana tu tarehe 14 Juni, 2020 uliweka alama nyingine ya uongozi wako, Bunge unaloliongoza lilikabidhi Serikalini shule ya wasichana ya Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Jimbo la Kongwa umeshirikiana vyema na wananchi wako wa Kongwa katika kuendeleza sekta zote za uchumi na kijamii. Kongwa ya leo si kongwa ya miaka mitano ilyopoita. Ninaamini kwa uchapakazi huo wakati ukifika ni kuchukua na kuweka. Itoshe kusema mchango wako hautasahaulika kwangu, kwa Wabunge, kwa wana Kongwa na kwa watanzania wote kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Wabunge wenzangu kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuwawakilisha wananchi waliowachangua. Wameitendea haki na nafasi yao ya uwakilishi, wameishauri na kuisimamia Serikali kikamilifu na wamefanya maamuzi sahihi yenye manufaa kwa Watanzania wote. Siku zote wameweka maslahi ya taifa

mbele. Wabunge hawa wamefanya kazi nzuri sana kwenye majimbo yao naamini wananchi wameziona kazi za Wabunge hawa Bungeni lakini pia majimboni. Sina shaka wengi wao watarejeshwa Bungeni kwa kishindo. Nawatakia kila kheri kwa yaliyo mbele yao hasa uchanguzi wa Oktoba, 2020. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kwa uwakilishi wa Wabunge wote nimataje Mheshimiwa Waziri Mkuu Kasim Majaliwa Majaliwa, amefanyakazi kubwa sana nchini, ametembelea maeneo mengi sana na kukagua miradi mingi. Amekuwa kiongozi mahiri wa shughuli za Serikali Bungeni na amewatumikia wananchi wa jimbo Lake Kikamilifu. Ninamuombea ushindi mmono Jimbo kwake Ruangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna kipekee nimtakie kheri Mheshimiwa Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mama yetu Mama Janeth Magufuli, ninawaombea uzima na afya na ushindi wa kishindo 2020 Oktoba. Namtakia pia kila la kheri Makamu wa Rais Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa yale yote yaliyombele yake. Mama huyu amekuwa mfano bora kwa wanawake wote nchi, sote tunamtakia kila kheri kama wanawake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninazo salamu binafsi za mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, safari yangu ya kisiasa ilianza nilipoteuliwa kuwa Mbunge. Kama nilivyoeleza hapo awali, baada ya kuingia Bungeni nilipata fursa hii ya pekee ya kuwa Naibu Spika, hii ni kazi ya utumishi. Kwa nafasi hiyo nimezungukia maeneo mengi ya nchi yetu kama ambavyo nimeshaeleza hapo awali. Nilifurahi sana kujumuika na kufanya kazi na Watanzania wenzangu katika maeneo hayo. Pamoja na ukweli huo chereko huanzia nyumbani, hivyo sikubaki nyuma katika kushirikiana na Watanzania wenzangu wa Mkoa wa Mbeya ambako ndiko chimbuko langu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka miatano cha uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph

Magufuli Mkao wetu umepiga hatua kubwa kimaendelea, hakuna sekta ilioachwa nyuma. Nikiwa mwana Mbeya ninafurahi kwamba nimepata fursa ya kuwa nao bega kwa bega katika kuchangia maendeleo ya Mkao wetu. (*Makofii/Vigelegele*)

Nachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa fedha alizozitoa katika maeneo ya elimu, afya, ujenzi, usafiri wa majini, umeme na maji; ametimiza ahadi zake zote. Nikitoa mfano katika sekta ya afya, Mkao wa Mbeya tumepata jumla ya shilingi billioni 23. Kutokana na fedha hizo tumepata vituo vya afya 16, hospitali za Wilaya tatu; yaani Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Halmashauri ya Busokelo na Wilaya ya Mbarali. Fedha hizi pia zimefanya na zinaendelea kufanya maboresho katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Wanawake Meta na maboresho katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya; ujezi wa jengo la radiolojia na vifaa tiba kama vile *CT scan, x-ray* za kisasa na mashine za *ultrasound*. Hospitali za Kanda Meta na Mbeya zinahudumia Mikoa yote ya Nyanda za Juu kusini, ikijumuisha Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Njombe, Iringa na Ruvuma. (*Makofii*)

Kwa upande wa Mbeya Jiji kwenye eneo la afya tumepata fedha kwa ajili ya vituo vya afya viwili, na upanuzi wa kituo cha afya cha Igawilo, kuwa hospitali ya Wilaya ya Mbeya Mjini. Wananchi kwa kushirikiana na Serikali tunaendelea na juhudhi za kuimarisha zahanati za Iganzo, Itesa, Tembela, Mwansekwa na Nanenane ili tuendelee kupata huduma bora za afya. Vilevile tuko mbioni kuhakikisha zahanati za Iziwa na Itagano zinapandishwa hadhi na kuwa vituo vya afya ili kusaidia wananchi walio mbali na huduma za afya kwa zaidi ya kilometra 10 kupata huduma. (*Makofii*)

Kama Mbunge na mwana Mbeya umenipa fursa mara kadhaa kuuliza maswali yaliyogusa maendeleo mkoani mwetu. Baadhi ya maswali hayo nilimuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji tarehe 2 Frebruari 2019. Kufuatia majibu ya Naibu Waziri wa Maji hatua zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mradi wa maji Mbalizi. Kukamilika kwa mradi huu kumetoa fursa kwa wakazi wa Mbeya Jiji kupata huduma

ya maji katika mitaa ambayo haikuwa na maji, hasa katika Kata za Mwansekwa, Igango, Iduda, Uyole, Nsalaga, Iwambi, Itagano, na Itende .*(Makof)*

Tarehe 27 Mei 2019 ulinipa nafasi ya kumuuliza Waziri wa Nishati swali kuhusu tatizo la umeme hasa kwa wananchi wa Kata zilizopo pembezoni mwa Jiji la Mbeya ambazo ni pamoja na Kata ya Itende, Iziwa, Msoho, Iwambi, Mwasanga, Itezi, Iduda, Isalaga, Kitagano na Mwazekwa. Kutokana na jibu na agizo la Mheshimiwa Waziri wa Nishati leo wananchi wanalipa kiasi cha shilingi 27,000 badala ya takriban laki tatu, kwani mazingira ya maeneo haya hayatofautiani na mazingira ya vijijini. Kwa niaba ya Mbeya niruhusu niishukuru Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa kusikiza kilio chao katika sekta ya maji na umeme. *(Makof)*

Mnamo tarehe 25 Aprili 2019 Mheshimiwa Rais alifanya ziara ya wiki moja Mkoani Mbeya. Katika wiki hiyo nikijumuika na wana Mbeya wenzangu tulimkaribisha Mheshimiwa Rais na tuliungana sote pamoja kutoa kilio chetu cha barabara. Mheshimiwa Rais alitoa agizo papo hapo kwamba Barabara Kuu ya TANZAM ianzee kujengwa, na kwa sasa imeshafanyiwa michoro na wakati wowote ujenzi utaanza. Barabara hii inaanzia Igawa, inapita Mbeya Jiji, inaelekea Tunduma.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais pia alitoa maelekezo kuhusu barabara ambayo inatoka Inyala - Simambwe mpaka Mbalizi. Barabara hii ni ya kilometra 40 na mpaka sasa awamu ya kwanza ni ya kilometra 16.5 na zimeshaanzwa kujengwa, na bilioni 7.5 zimeshatolewa. Barabara hii ya mchepuko itapunguza ajali nyingi zinazotokea Jijini Mbeya kutokana na malori ya mizigo kupita katikati ya Jiji.*(Makof)*

Nimalizie kwa kuwazungumzia Machinga wenzangu wa Jiji la Mbeya. Kwa niaba yao napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia eneo la uwanja wa ndege wa Mbeya kuwa eneo letu la kufanya biashara. Tumeshaanza kunufaika na eneo hili kwani biashara zimeanza; miundombinu inaendelea

kuwekwa ili kuwa na mazingira bora ya kibashara. Tunamshukuru Mkoo wa Mkoa wa Mbeya Ndugu Albert Chalamila, Mkoo wa Wilaya ya Mbeya Ndugu William Paul Ntinika na Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya Kamishna Msaidizi wa Polisi James Kasusura kwa kutuwekea mazingira mazuri na salama ya kufanya biashara, ikiwa ni pamoja na kutafuta wadau wakaosaidia kuongeza miundombinu bora katika eneo letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimewashukuru wengi katika hotuba hii. Shukrani za mwisho, lakini si kwa umuhimu ni kwa familia yangu ikiongozwa na mume wangu James Andilile Mwenyekule, na watoto wetu Daniel James na Ackson, wazazi wetu na ndugu zetu wote. Hao wamekuwa ni nguzo kuu katika maisha yangu, ninawapenda na kuwashukuru sana kwa kukubali niwe nje ya majukumu ya kifamilia wakati wa kufanya kazi zangu za ubunge na Naibu Spika.

Ninapowataenia kheri Waheshimiwa Wabunge wote kwa kipindi hiki na hasa kwa kuzingatia Uchaguzi Mkoo wa Octoba 2020, napenda kusema nami nimepata hamasa ya kujitosa. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, na Inshallah Mwenyezi Mungu atujalie uzima na afya yumkini nitakwenda mahali fulani kuomba ridhaa ya wananchi wenzangu ya kuwatumikia katika Bunge lako Tukufu. Kwamba nitaenda wapi *stay tuned*.

Mheshimiwa Spika, umenipa fursa ya kipekee kusema haya niliyoweza kuyasema, ninakushukuru, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuniskiliza, ahsante sana, nakutakia kila la kheri. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsate sana, Mheshimiwa Naibu Spika, tunakushukuru sana.

(Hapa baadhi ya Wabunge wakishangilia kwa kutamka Mbeya! Mbeya! Mbeya! Mbeya!)

SPIKA: Sasa, Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

SPIKA: Kesho tutakuwa na wageni wengi sana, ni mkutano ambao utakuwa na *record* ya wageni; na kutakuwa na wageni maarufu, wazee wetu na viongozi; kwa kweli wengi wameitikia wito wetu na tutakuwa nao. Kwa hiyo kama ilivyo ada basi nimuombe Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu; *Chief Whip* atupitishe kwenye hoja ya kutengua Kanuni.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa heshima ya Bunge lako nmba nitoe mawelezo ya Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 153 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari mwaka 2016. Kwa kuwa kesho tarehe 16 Juni mwaka 2020, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atalihutubia Bunge na kulifunga Bunge la 11 rasmi kwa mujibu wa Ibara ya 91 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kanuni ya 30 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, na kwa kuwa wamealikwa viongozi mbalimbali kuja kusikiliza Hotuba ya Mheshimiwa Rais, wakati akihitubia na kulifunga rasmi Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kwa kuwa Kanuni ya 139 (1) na Kanuni ya 143(f) zinalekezwa kwamba wageni wanaruhusiwa kuingia Bungeni watacaa maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili yao, na kwamba inabidi Bunge litengue Kanuni hizi ili kuruhi viongozi maalum walioalikwa na Mheshimiwa Spika kuja kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati akilihitubia na kulifunga rasmi Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuingia na kukaa ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi Bunge linaazimia kwamba Kanuni ya 139(1) na Kanuni ya 143(f), ambazo kwa ujumla wake zinawataka wageni wanaoingia ukumbini wakae maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili yao

zitenguliwe ili Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Zanzibar waruhusiwe kuingia na kukaa sehemu watazopangiwa ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa ajili ya kusikiliza Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akilihutubia Bunge na kulifunga rasmi Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono sana, nakushukuru sana *Chief Whip*, hoja hii inawaombea Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Mheshimiwa Jaji Mkuu Zanzibar na Mheshimiwa Jaji Mfawidhi hapa Dodoma akiwemo na Spika wa Baraza la Wawakilishi. Mtaona kwamba ugeni huu kwa kweli kwa historia ya Bunge haijapata kutokea. Pia tutakuwa na Marais wastaaifu kwenye *gallery*, tutakuwa na Mawaziri Wakuu wastaaifu wale watakaomudu kuweza kuja kuwa na sisi; na kwa kweli crème ya nchi itakuwa hapa. Kwa hiyo ni jambo kubwa na ni heshima kubwa sana kwetu.

Kwa hiyo tunaombwa tutoe kibali hicho naomba sasa niwahoji, kwa kusema wanaoafiki waseme ndiyo, wote wameafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

SPIKA: Nashukuru sana, Katibu kwanza.

NDG. NENELWA MWIHAMBI - KATIBU MEZANI:

SPIKA: Taarifa ya Katibu wa Bunge.

TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE

Kwa mujibu wa Kanuni ya 29(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye orodha ya shughuli za Mkutano wa 19 wa Bunge sasa zimemalizika. (*Makofi*)

SPIKA: Taarifa hiyo, kwamba shughuli za Mkutano huo wa 19 zote zimekamilika. Mkutano ulikuwa mgumu sana, kulikuwa na mitihani mingi sana, lakini tulisema mpaka tumalize kazi hii, Mungu ni mwema. (*Makofi*)

Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HOTUBA YA KUKAMILISHA SHUGHULI ZA MKUTANO WA KUMI NA TISA WA BUNGE

SPIKA: Hotuba ya kukamilisha shughuli za mkutano huu, sasa kwa heshima nimkaribishe Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa, karibu sana hapa mbele, karibu sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, karibu utuhutubie, ahsante. (*Makofi/Vigelegele*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kufika siku hii ya leo ambayo mimi naita kuwa ni siku ya historia kwetu. Nasema siku ya leo kuwa ni historia kwa sababu Bunge lako Tukufu linahitimisha shughuli za Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia tunahitimisha mkutanowa 19 wa Bunge ulioanza mwezi Aprili mwaka huu wa 2020.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu wa Bunge licha ya uwepo wa ugonjwa wa homa ya mapafu iliyosababishwa na virusi *corona*, (*COVID-19*), tumeweza kukaa hapa Dodoma kwa kipindi kilisichopungua miezi miwili na nusu. Aidha katika kipindi hicho tumeweza kutekeleza majukumu yetu yote kama ilivyokuwa imepangwa. Ama kwa hakika hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwani tunakamilisha maisha yetu ya kibunge kwa kipindi cha miaka mitano tangu Novemba 2015. Tumeshirikiana katika maeneo mengi nje na ndani ya Bunge kwa kila mmoja kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, siwezi kuanza kueleza yaliyojiri kwenye majukumu yetu bila kumshukuru Mwenyezi Mungu aliye niwezesha kuwa na afya njema na kunisimamia katika kila jambo na hasa nilipokuwa natekeleza majukumu yangu binafsi na majukumu ya umma kwa kipindi chote hadi sasa; Inshallah!ye ye ndiye msimamizi wa yote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwamoyo mkunjufu kabisa kabisa naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kitendo chake cha kunianimi na kunituea kushika wadhifa wenye dhamana kubwa ya kumsaidia kazi ya utendaji ndani ya Serikali kwa kipindi chote cha miaka mitano. Kwa niaba ya familia yangu na wana Ruangwa wote namshukuru sana kwa ukarimu, imani na upendo alionunesha kwetu, Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu, ulinzi, kheri na kila liliojema na aendelee kuliongoza taifa hili vyema na kwa mafanikio makubwa kama ambavyo Watanzania tumeendelea kushuhudia mafanikio makubwa katika kipindi hiki cha uongozi wake wa Awamu ya Tano. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, Rais wetu ametenda mema kwa Watanzania na watamlipa mema. Ninamwombea kheri pia kwauchaguzi mkuu ujao ashinde kwa kishindo, amina.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana pia Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan Makamu wa Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano wake mkubwa wakati wote nilipokuwa natekeleza majukumu ya Waziri Mkuu, vilevile ninashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa nilioupata kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa pamoja na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar pamoja na viongozi, watendaji na wananchi wote wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kukushukuru sana wewe binafsi kwa upendo uliouonesha kwangu kipindi chote cha uhai wa Bunge la Kumi na Moja (11). Kwa uzoefu ulionao katika kuendesha Bunge, umekuwa msaada sana kwangu kwa kunipa ushauri na ushirikiano wa dhati ulionifanya nijenge imani kubwa kwenye majukumu yangu ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu kukutakia kheri nyngi kwenye uchaguzi ujao, naamini Wana-Kongwa wasasikiliza na kutekeleza dua zetu za kuwa upite bila kupingwa kwenye jimbo lako, na ukirudi hapa basi chukua fomu ya Uspika ili upate kura zote za ndiyo uendelee kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Mbili (12). (*Makof/ vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, sitasahau tukio la tarehe 19 Novemba, 2015 siku ambayo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipowasilisha jina langu katika Bunge lako Tukufu na kupendekeza niwe Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof/*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena wewe na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa imani mlionionesha kwa kuridhia mapendekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli na kunipigia kura nyngi za ndiyo na mkaridhia tufanye kazi kwa pamoja katika kuwatumikia Watanzania. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, natambua, naheshimu na nathamini ushirikiano wa dhati mlionipa katika kipindi chote cha Bunge kwa kipindi hiki cha miaka mitano.

Nami nawaombea na nawatakia ushindi wa kishindo kwenye majimbo yenu ili mrudi tena hapa mwezi Novemba, 2020. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pia, nawashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Akson, Naibu Spika, najua naye ametamka hapa kwamba na ye ye anajipanga kwenda kugombea. Popote unapokwenda basi upate kura ny ingi za kutosha hapo unapogombea na uweze kuwa Mbunge na urudi tena kuwa Naibu Spika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Wenye viti wa Bunge, Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan ambaye mwishoni alipata uteuzi wa Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, kwa kuliongoza Bunge hilli kwa busara na umahiri mkubwa; nanyi najua kuwa mnakwenda kugombea kwenye maeneo yenu. Ninawatachia kila la kheri kwenye uchaguzi ujao mpate kura za kutosha.

Mheshimiwa Spika, vilevile, namshukuru sana Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha Bajeti za Serikali. Pia, nawashukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai na Watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika Mkutano huu na Mikutano yote iliyoendeshwa kipindi chote cha miaka mitano, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu hapa Bungeni napenda kutambua mchango wa Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayesimamia Sera, Uratibu, Bunge, Ajira, Kazi, Vijana na Watu wenye ulemavu. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mhagama kwa kunisaidia ipasavyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Uwaziri Mkuu sambamba na majukumu yake ya unadhimu

pamoja na uratibu wa shughuli za Serikali hapa Bungeni. Nakuombea sana kwa wananchi wa Peramiho, Maposeni, Mgazini, Mdunduwalo, wakupitishe upite bila kupingwa. (*Makof/vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, namshukuru sana Mheshimiwa Angela Kairuki (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji kwa kufuatilia na kusimamia hatua mbalimbali za kuimarisha na kuboresha mazingira ya uwekezaji hapa nchini. Mheshimiwa Waziri Kairuki amekuwa akitembelea maeneo mbalimbali na kukutana na wawekezaji, wadau wa sekta binafsi ili kusikiliza changamoto zao na kuzitatua na kuzipatia ufumbuzi. Juhudi zake hizo, zimekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha mazingira ya biashara na kuimarisha mahusiano ya sekta binafsi na Serikali hapa nchini. Nawe najua unakwenda kugombea, nakutakia kila la kheri huko uendako ili upate kura za kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa masuala ya maendeleo na uwezeshaji wa vijana napenda kumshukuru Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Mbunge kija wa Dodoma Mjini, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu kwa msaada mkubwa katika kusimamia vizuri masuala ya ajira na vijana. Kadhalika naye pia najua atagombea Dodoma Mjini kwa, hiyo wana-Dodoma naamini mtampa kura za kutosha. Namshukuru Dada yangu Mheshimiwa Stella Ikupa Alex (Mb), Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kusimamia vema masuala na maslahi ya Watu Wenye Ulemavu. Umetenda mema katika kuwasikiliza Walemavu hapa nchini na kutatua changamoto zao. Nawe pia najua unaingia kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi, nakutakia kila la kheri na ushindi mnono ili uweze kurudi tena hapa Bungeni. (*Makof/vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri; kwa pamoja Professor Adelardus Kilangi Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Balozi Mhandisi John William Kijazi Katibu Mkuu Kiongozi; Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu

wakiongozwa na Bw. Tixon Tuyangine Nzunda, Bw. Andrew Wilson Massawe, na Bibi Dorothy Aidan Mwaluko kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. Nawashukuru kwa ushirikiano wa dhati mlionipa katika kuratibu na kusimamia shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu; bila kuwasahau Watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Nina uhakika Mawaziri pamoja naNaibu Mawaziri wote mnarudi kwenye Majimbo yenu kuomba ridhaa kwa Wananchi waliowaleta hapa. Nawatakia kila la kheri muweze kushinda kwa kishindo kwenye Majimbo yenu. Kila la Kheri.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwashukuru Wakuu wa Vyombo vyta Ulinzi na Usalama akiwemo Jenerali Venance Mabeyo (Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama); Inspeksa Jenerali wa Polisi Simon Nyakoro Sirro; Brigedia Jenerali Suleiman Mzee (Kamishna Jenerali wa Magereza); Dkt. Anna Makakala (Kamishna Jenerali wa Uhamiaji); John William Hasunga Kamishna (Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji); Kamishna Diwani Athumani (Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa); Brigedia Jenerali John Mbung'o (Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa); James Kaji Kamishna (Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti) na Kupambana na Madawa ya Kulevyta.

Mheshimiwa Spika, wakuu hawawa Vyombo vyta Ulinzi na Usalama wametenda kazi yao vizuri kwakulinda mipaka na usalama wa ndani ya nchi, wameonesha nidhamu na uzalendo mkubwa katika kuhakikisha kwamba Nchi yetu, raia wake na mali zao wanakuwa salama.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Wakuu wa Taasisi mbalimbali za Serikali, wakurugenzi na watendaji wote Serikalini kwa ushirikiano mzuri walioutoa na utendaji wa pamoja wenye mafanikio makubwa. Aidha, tuendelee kutakiana mema na tuchape kazi hadi hapo utumishi wetu utakapokoma.

Mheshimiwa Spika, nimalizie salamu zangu za shukrani kwafamilia yangu ambayo inaniunga mkono, kunivumilia pale ambapo nawatumikia Watanzania na kunitia moyo siku hadi siku kwenye majukumu yangu. Bila kuwasahau Wana-

Ruangwa ambao walnipigia kura bila kujali vyama vyao na kuniwezesha kuingia Bungeni na hatimaye nikapata uteuzi wa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania. Nataka niwahakikishie Wana-Ruangwa kuwa bado tuko pamoja katika harakati za kuleta maendeleo. Nawashukuru sana. (*Makofii/kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wananchi na Watanzania wote kwa kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli na ushirikiano walioutoa kwa Serikali wakati wote wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ya taifa hili kwa ujumla bila kujali tofauti zao za kiitikadi au dini. Sambamba na kuonesha uzalendo, mshikamano na kudumisha amani na utulivu ulioiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi; na kwa mujibu wa taarifa zinazotolewa na taasisi ya *GLOBAL PEACE INDEX 2020* inayofuatilia masuala ya amani duniani, Tanzania ni nchi ya saba kwa amani na utulivu Afrika na ni nchi ya kwanza kwa amani na utulivu Afrika Mashariki. Naamini wananchi wataendelea kuiunga mkono Serikali yetu ili ifanye mambo makubwa zaidi katika kipindi cha pili cha Awamu ya Tano kwa amani na maendeleo yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu za shukurani nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa Iramba Magharibi kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria na Mheshimiwa Dkt. Godwin Aloyce Mollel Mbunge wa Siha kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Aidha, mkiwa viongozi mlioteuliwa, tambueni kuwa mnalo jukumu kubwa la kuwashudumia Watanzania, hususan katika kipindi hiki ambacho nchi yetu imekumbwa na changamoto mbalimbali likiwemo janga la Corona.

Mheshimiwa Spika, wakati tukiendelea na Mkutano huu wa 19, Bunge lako Tukufu lilipata pigo kwa kuondokewa na Wabunge wapendwa wenzetu akiwemo Mheshimiwa

Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, aliye kuwa Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa aliye kuwa Mbunge wa Jimbo la Sumve na Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga, aliye kuwa Mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho pia tuliondokewa na aliye kuwa Jaji Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Jaji Augustino Ramadhan. Aidha, niungane na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kuwapa pole majirani zetu, wanchi ya Burundi na wananchi wa Burundi kwa kifo cha aliye kuwa Rais wa nchi hiyo, Mheshimiwa Pierre Nkurunzinza. Tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu azipumzishe Roho za wapendwa wetu wote mahali pema. Amina.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Taifa letu lilikumbwa na majanga mballmbali ikiwa ni pamoja na mafuriko, Covid-19 na ajali za barabarani ambazo zilisababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Napenda kutoa salamu za pole kwa ndugu, jamaa na marafiki walipoteza wapendwa wao na wengine kupata majeraha kutokana na matukio hayo. Tumuombe Mwenyezi Mungu aziweke Roho za marehemu mahali pema na walipata majeraha awajalie nafuu na kupona mapema. Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano, na kwa namna ya pekee kabisanitumie fursa hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kutokana na fikra na uongozi makini katika ujenzi wa Taifa letu. Ni dhahiri kuwa maono yake katika kuongoza na kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020 na mipango ya Serikali, zimeleta mafanikio makubwa ambayo hivi sasa Watanzania wote tunayaona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nyote mtakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Rais na Makamu wake Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanawafikia Watanzania, wanawasikiliza na

kutatua kero zao. Lengo la ziara walizozifanya, pamoja na mambo mengine, ilikuwa ni kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 ikiwemo kukagua miradi ya maendeleo, kuzungumza na watumishi wa Umma na kuwafahamisha kuhusu falsafa ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Hapa Kazi Tu.

Mheshimiwa Spika, ziara hizo zimesaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha utendaji wa watumishi wa umma. Hivi sasa, wananchi wanapokwenda katika ofisi za umma wanapokelewa, wanasikilizwa na kuhudumiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, aidha, usimamizi wa miradi ya maendeleo umeimarika sambamba na kuakisi thamani halisi ya fedha katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, hapa Bungeni ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa maoni mliyokuwa mnayatoa, ushauri wenu na ushirikiano ambaa mmekuwa mkiutoa kwetu wakati wa ufuatiliaji wa shughuli za maendeleo sambamba na kusimamia Serikali yetu. Mambo mengi ya kujivunia yamefanywa na tumekuwa tukiyaeleza katika maeneo mbalimbali kuitia mikutano ya hadhara, vyombo vya habari, nyaraka mbalimbali, uwepo wa miradi mingi ya kimkakati hadi kwa wananchi wa kawaida kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, hapa nitatumia nafasi hii kuyaeleza yale majukumu muhimu yaliyotekelizwa na miradi michache ya kimkakati iliyotekelizwa kwa kifupi ili kuwakumbusha nini Serikali imefanya katika kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza lililosughulikiwa ni marekebisho ya nidhamu kwa utumishi wa umma na uwajibikaji Serikalini ili kuwawezesha watumishi kutambua majukumu yao ya kuwatumikia Watanzania. Na wakati wote watumishi waumma ni watumishi wa Watanzania. Ni vyema wakaendelea kutambua hilo ili kuendelea kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili, ni mapambano dhidi ya rushwa ndani na nje ya Serikali. Kazi hii ilifanywa kwa weledi mkubwa ili kulinda mali na fedha za umma, na hatua hii itakuwa endelevu. Lengo ni kung'oa mizizi ya rushwa iliyoshamiri hapa nchini; na kwa kufikia hatua hii tunaridhika kuona kwamba vitendo vya rushwa nya kuomba na kupokea vimepungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tulikuwa tunaimarisha vyombo vya ulinzi na usalama, kuhakikisha kwamba mihimili, ambapo tukianza na mhimili wa Bunge unajimarisha katika utendaji kazi zake na mhimili wa Mahakama unaimarika na kutenda kazi zake. Matakwa yetu ni kuhakikisha kuwa nchi inabaki salama na mihimili yote ifanye kazi yake kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia mapambano dhidi ya matumizi ya dawa za kulevyaa ili kujihakikishia kuwa tunakuwa na taifa lenye nguvukazi inayofanya kazi. Mapambano haya bado yanaendelea kwasababu bado tunao wanaaoendelea kuzalisha, kuuza na kusambaza. Tutaendelea kupambana na wazalishaji, wasambazaji, wauzaji na watumiaji wa dawa za kulevyaa. Tunataka tuhakikishe taifa hili linakuwa salama kwa kutokuwa na matumizi ya Dawa za kulevyaa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tumelifanyia kazi ni utambuzi wa watumishi hewa waliokuwa wanalipwa fedha za umma wakiwa hawapo mahali pa kazi. Katika zoezi hili tumepata mafanikio makubwa ambayo tumeweza kuokoa shilingi Bilioni 19.83 kwa kuwaondoa kwenye mfumo wa malipo watumishi hewa 19,708 na wenye vyeti nya kugushi 15,411. Masuala ya uhakiki wa watumishi hewa yanaendelea kupitia Wizara zetu, kila sekta inayosimamia watumishi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia jambo lingine ambalo tumelifanyia kazi ni ukusanyaji wa mapato ili kuwezesha Serikali kujenga miradi na kutoa huduma muhimu kwa Watanzania. Ukusanyaji wa mapato umeongezeka kutoka wastani wa shilingi Bilioni 800 kwa mwezi mwaka 2015 hadi

wastani wa shilingi triliuni 1.5 kwa mwezi katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020. Nafurahi kueleza Taifa kwamba Watanzania wengi sasa wanafahamu umuhimu wa kulipa kodi. Muhimu tuendelee kulipa kodi ili tuendelee kupata mapato zaidi kwaajili ya uendeshaji wa miradi yetu na huduma nyingine za Jamii.

Mheshimiwa Spika, Iakini pia tumeimarisha uwekezaji kwa kujenga viwanda. Hadi Aprili 2020 jumla ya viwanda vipyta 8,477 vikiwemo vidogo, vya kati na vikubwa vimeanzishwa katika maeneo mbalimbali nchini na hivyo kuwezesha ongezeko la ajira za viwandani zipatazo 482,601.

Mheshimiwa Spika, eneo jingne ni kuimarisha kilimo na masoko yake. Tumeimarisha kilimo cha mazao makuu, kama vile, korosho, pamba, chai, tumbaku, kahawa, michikichi na mkonge pamoja na mazao ya mengine ya chakula ili kuwa tuna uhakika wa usalama wa chakula nchini. Suala la masoko ya mazao ya kibiashara linaendelea. Wizara inaendelea kusimamia malipo mbalimbali kwawakulima na pale ambapo kuna mapungufu Wizara inaendelea kusimamia kila mkulima aendelee kupata stahiki yake.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuimarisha ushirika wa kilimo na upatikanaji wa pembejeo pamoja na huduma za ugani ili kuwafanya wakulima waweze kuzalisha kwa tija. Serikali inajipanga vizuri kwa kuhakikisha kuwa tunapeleka pembejeo za kilimo kwa wakati ili kila mkulima wa kila zao apate pembejeo angalau mwezi mmoja au miwili kabla ya kipindi cha msimu wa kilimo. Kazi hiyo inaendelea na Wizara wanashughulikia.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni marekebisho ya Sheria ya Madini yamefanyika sambamba na kuanzisha masoko ya madini 28 na vituo 12 vya ununuzi wa madini katika maeneo ya uchimbaji na hivyo kuongeza makusanyo ya Serikali. Kupungua biashara haramu na utoroshaji madini kwenda nje. Mwezi Machi hadi Septemba, 2019 jumla ya kilo za dhahabu 4,680.28 zenye thamani ya shilingi billioni 432.49

zimezalishwa na Serikali imeweza kukusanya shilingi bilioni 30.27 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingina ni kuhakikisha kwamba tunahamisha Makao Makuu na kuhamia Dodoma ambapo tayari Watumishi wapatao 15,361 wameshamia hapa Dodoma, na sasa fursa za uwekezaji zimeongezeka katika Jiji la Dodoma na wataumishi wote sasa wako Dodoma na shughuli za Serikali zimekamilika na shughuli zinaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuboresha miundombinu na taaluma kwenyesekta ya elimu kwa ngazi zote kuanzia awali hadi elimu ya juu. Eneo hili linaendelea kufanyiwa kazi ikiwemo ujenzi na ukarabati wa madarasa, maktaba, maabara, nyumba za walimu, mabweni na ukarabati wa shule kongwe ili kuzlongezea uwezo wa kupokea wanafunzi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, sera ya Elimu bila ada ambayo inatumia zaidi ya Shilingi Bilioni 20.8 kila mwezi kwa ajili ya fidia ya ada, posho ya madaraka kwa walimu wakuu, wakuu wa shule na waratibu kata kila mwezi toka 2016 na tutaendelea. Hii imesaidia kuongeza uandikishaji na mahudhurio shulenii.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuimarissha huduma za afya kwa kujenga zahanati, vituo vya afya, kujenga hospitali za wilaya, mikoa, kanda na za kitaifa, huduma za madawa na vifaa tiba. Tumeweza kujenga zahanati 1,198 vituo vya afya 487, hospitali za wilaya 71, hospitali za rufaa za mikoa 10, nahospitali za kanda nne. Kwenye Kanda ya Kusini – Mtwara, Kanda ya Magharibi – Tabora na Kanda ya Ziwa – Burigi na Hospitali ya Nyerere iliyoko Musoma Mjini; na hapa Dodoma tunaendelea kujenga Hospitali ya Uhuru. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi wa miradi ya maji vijijini na mijini tumeweza kufikisha asilimia 84 mijini na asilimia 70.1 vijijini; na kazi ya kupeleka maji katika vijiji vyote inaendelea; na kazi ya kusambaza kwa kupitia miradi

mikubwa kwenye miji mikubwa, midogo na ya kati inaendelea.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine niufufuaji wa Shirika la Ndege ambapo tumeweza kununua ndege kumi na moja (11) ambazo kwa sasa zinaendelea kutoa huduma mikoa yote yenye viwanja vya ndege. Pia tumeanzisha safari za nje ambazo zinaendelea kutoa huduma huko nje. Mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba kila mkoa kunakuwa na kiwanja cha ndege na kila mkoa ndege hizi zinatua kwa ajili ya kusafirisha abiria kutoka eneo moja mpaka lingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunaendelena na ukarabati wa viwanja vya ndege kwenye mikoa isiyokuwa na viwanja vya ndege, na tunaanza kujenga viwanja kwenye mikoa isiyokuwa na viwanja vya ndege; na tunaanza kujenga viwanja kwenye milka ambayo haina kabisa. Lengo kila mkoa lazima uwe na kiwanja cha ndege. Ununuzi warada nao umefayika katika kipindi hiki. Tumenunua rada nne mpya za kuongoza ndege za kiraia; na rada hizo ziko Mkoani Mwanza pale Uwanja wa Mwanza, Mbeya Songwe *Airport*, Dar-es-Salaam JNIA *Airport* na Kilimanjaro *KIA* zinaendelea kufanya kazi .

Mheshimiwa Spika, pia tumeshiriki ujenzi wa mradi mkubwa wa kufufua umeme (Mwalimu Nyerere Dam) utakaozalisha megawat 2115. Kwa sasa umeshafikisha asilimia 40. Ujenzi huu una gharama ya shilingi trillioni 6.5. Kazi inaendelea vizuri na tumepata fursa kutembelea mradi huo kuona maendeleo ya kazi hiyo na kazi inaendelea vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine ni ya usambazaji wa umeme vijiji kupitia Wakala wa Nishati Vijiji (REA). Serikali imefanya jitihada za kuhakikisha kwamba onapeleka umeme vijiji na sasa tumefikia asilimia 80 ya vijiji tulivyonavyo hadi kufikia mwezi Aprili 2020. Jumla ya shilingi trillioni 2.27 zimetumika na kufanikisha jumla ya vijiji 9,112 kati ya 12,268 vya Tanzania Bara kuunganishwa na umeme kutoka vijiji 2,118 mwaka 2015. (*Makofii*)

Pia katika kipindi hiki cha miaka mitano ujenzi wa Mradi wa Reli ya Kimataifa (*SGR*) wa Kilomita 300 kutoka Dar-es-Salaam mpaka Morogoro. Mradi unaendelea kujengwa na sasa umefikia asilimia 78. Kipande cha Morogoro hadi Makutupora mkoani Singida cha Kilomita 422 kinaendelea na ujenzi na mradi huo umefikia asilimia 30 ya kazi yake. Lengo ni kukamilisha mradi huu ifikapo Juni 2021 kwa gharama ya shilingi trillioni 7.5. Kipande cha Dar es Salaam Morogoro tayari kimeshaanza kufanyiwa majaribio kwa kutumia kiberenge kidogo ambacho kinafanya kazi kwenye eneo hilo ili kuonyesha kuwa aina hiyo ya reli ndio itakayotumika na aina hiyo ya mabehewa ndiyo yatakayotumika.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunaendelea na ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha lami kote nchini, zikiwemo barabara kuu, barabara za mikoa na sasa tunaenda kwenye barabara za Wilaya zenyet thamani ya zaidi ya shillingi trillioni 7.6. Pia Serikali inaendelea kujenga barabara ya njia nne kutoka kutoka Kimara hadi Kibaha (km 19.2), lakini pia tunaendelea kukamilisha barabara kwenye mikoa ya Kigoma, Tabora na maeneo mengine kote nchini. Malengo yetu ni kuhakikisha kwamba Makao Makuu yote ya Mikoa yanafikiwa kwa barabara ya lami. Kwa sasa ujenzi wa kwenda wilayani umeshaanza, malengo yetu wilaya zote zifikiwe kwa kiwango cha lami, na inawezekana, uwezo wa fedha tunao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ujenzi wa madaraja. Ujenzi wa daraja la juu la Mfugale (Dar-es- Salaam), maarufu TAZARA, daraja la Furahisha (Mwanza) na daraja la Magufuli (Mto Kilombero) umeshakamilika. Ujenzi wa barabara ya pete (*Ubungo interchange*) umefikia asilimia 77 na wananchi wa Tanzania mmeanza kuona eneo hilo daraja hilo linaanza kutumika; kwa shilingi bilioni 247. Aidha, ujenzi unaendelea kwa daraja la *New SelanderBridge* (Dar- es-Salaam) kwa shilingi Bilioni 270. Daraja la Kigongo- Busisi lenye urefu wa kilometra tatu kwa shilingi Bilioni 699.2.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunaendelea na ujenzi wa bandari zetu. Tunaendelea na uboreshaji na upanuzi wa

Bandari za Tanga, Dar-es-Salaam na Mtwara zenye thamani ya shilingi zaidi ya triliuni 1.2. Pia, ujenzi wa bandari ya kwenye maeneo muhimu kama vile Bandari ya Kigoma , Bandari ya Kalema kule Wilayani Katavi ili kuhakikisha kwamba tunajiunganisha na nchi jirani kwa kuasifirisha abiria na mizigo na shughuli nydingine za kibashara.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea pia na ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria na mizigo. Kwa sasa tunajenga meli ya kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo liliilo Ziwa Victoria na ujenzi wa chelezo, ukarabati wa meli ya MV Victoria na MV Butiama hapo hapo Ziwa Victoria ambapo katika kipindi cha mwaka 2015/2016 hadi Aprili, 2020 jumla ya shilingi bilioni 111.7 zimetumika. (*Makof*)

Vile vile, Serikali tunajenda meli na zimeshaanza kufanya kazi kule kwenye *Itungi Port Wilayani* Kyela kwa ajili ya kuunganisha Tanzania na Malawi; meli hizo zimeshaanza kufanya kazi. Vilevile Serikali imekamilisha ujenzi wa meli moja mpya, inaendelea na ujenzi wa meli kwenye Ziwa Tanganyika MT. Sangara ambalo pia nayo itakuwa inafanya kazi ya kubeba mafuta na mizigo mingine. Tunaendelea na ujenzi wa vivuko kama vile vya MV Kigamboni, MV Pangani, Kigongo -Busisi feri, *MV Sengerema* na sasa tunajenga Kivuko cha Nyamisati kitakachofanya safari zake hadi Mafia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tumeendelea na urejeshaji na usimamizi wa mali za ushirika zilizokuwa zimechukuliwa kinyume na utaratibu, kama vile, *Nyanza Cooperative Union*mali zake zote zimerejeshwa, *SHIRECU* mali zake zote zimerejeshwa, *KNCU* tunaendelea na urejeshaji wa mali hizo, Mamlaka ya Mkonge Tanzania tumerejesha mali zake na sasa mali hizo ziko kwenye ushirika huo. Lengo la zoezi hili ni kuimarisha ushirika na kujenga imani kwa Watanzania juu ya ushirika wao na mali zao ambazo walikuwa wamezizalisha kupitia mazao wanayoyauza.

Mheshimiwa Spika, pia tunaendelea kusimamia maboresho kwenye Sekta ya Uvuvi na Mifugo kwa kuvua na kufuga kisasa, kujenga viwanda na masoko yake lakini pia

kusimamia makusanyo ya mapato katika sekta hizi ambazo zimeshaanza kuonesha mafanikio makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kupitia Bunge lako Tukufu katika kipindi cha miaka minne imeidhinisha jumla ya shilingi trilioni 126.8 kwaajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kote nchini ikiwemo miradi ya kimkakati niliyoitaja hivi punde. Watanzania mmeshuhudia ujenzi wa miradi hiyo. Napenda nitumie nafasi hii tena kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote, Naibu Mawaziri wote, Makatibu Wakuu na Watendaji wa Wizara zote kwa utekelezaji mzuri usimamizi mzuri, na ufuatilaji wa miradi hii mbalimbali ambayo leo hii imeendelea kutupa faraja hapa nchini, kwamba Mtanzania anaendelea kutumia rasilimali hizo na miradi hiyo; hongera sana Waheshimiwa Mawaziri na Makatibu Wakuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo ya nchi yetu yalikumbwa na mafuriko kufuatia mvua nyngi zilizonyesha nchini. Mafuriko hayo yalisababisha madhara makubwa ikiwemo uhariifu wa miundombinu, mali na vifo. Serikali imeendelea kuchukua hatua za kurejesha hali ya miundombinu iliyoharibika na zoezi hilo ni endelevu. Mvua nyngi tulizopata msimu huu zimeleta neema ya mavuno, lakini pia katika baadhi ya maeneo mazao yameharibika. Hivyo, niendelee kusitiza kauli ya Waziri wa Kilimo wakati akiwasilisha Hoja ya Wizara yake hapa kuwa hali ya chakula nchini imeendelea kuimarika. Kwa msingi huo, hatutarajji kuwa na upungufu wowote wa chakula kwa msimu ujao. Muhimu kwetu ni kuongeza umakini wa matumizi kwa kuweka akiba ya chakula ili kiweze kutosheleza mahitaji ya familia hadi msimu ujao wa kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mapambano Dhidi ya Homa Kali ya Mapafu(*Covid-19*). Mwezi Machi 2020 baada ya Shirika la Afya Duniani (*WHO*) kutangaza kuwa Covid-19 ni janga la dunia, ambako nchi nyngi duniani zilipata maambukizi makubwa, Tanzania tulitangaza kisa cha kwanza tarehe 15 Machi, 2020. Nchi nyngi duniani zikiwemo nchi za Bara la Afrika ugonjwa huu ulianza kuingia. Kila nchi ilichukua

hatua kadhaa za kudhibiti maambukizi zikiwemo watu kutotoka ndani ya nyumba zao "*Lockdown*", kuzuia mikusanyiko kwa kufunga shule, vyuo, michezo, aina zote za usafiri wa ndani na nje, maeneo ya Ibada na shughuli za uzalishaji maeneo ya kazi, viwanda, nakadhalika vilifungwa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania nasi tulianza kuchukua hatua kadhaa ili kukabiliana na maambukizi kwa kuunda Kamati tatu za ngazi ya mawaziri, watendaji na wataalam wa afya kwa lengo la kufanya tathmini ya hatua za kuchukua kila hatua ilipokuwa inafikia ili kupunguza maambukizi na kulinda anguko la kiuchumi. Hatua zilizochukuliwa ni kupunguza misongamano kwa kufunga shule, vyuo, mikutano, kunawa maji, matumizi ya vitakasa mikono na kuvalaa barakoa.

Mheshimiwa Spika, siku ya tarehe 22 Machi, 2020 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa Jijini Dodoma na tarehe 03 Mei, 2020 akiwa Chato aliwataka Watanzania kuwa watulivu waondoe hofu ya ugonjwa huu kwa sababu ni ugonjwa kama magonjwa mengine, kama vile Malaria, UKIMWI, Kifua Kikuu, nakadhalika na kuwataka Watanzania kuchukua tahadhari na kuendelea na shughuli za uzalishaji mali, kufanya kazi ofisini, viwandani, mashambani na kutofunga nyumba za Ibada.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alihutubia taifa tarehe 16 Aprili, 2020 kwa kutoa maelekezo na kusositiza yafuatayo:-

i. Aliwasihii Watanzania kuondoa hofu kwa kuwa Mungu yupo nasi na hivyo waendelee kuchapa kazi ili kunusuru uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla na kuzingatia kanuni za afya.

ii. Watanzania watumie siku tatu kumuomba na kumlilia Mwenyezi Mungu kwani Mungu yu pamoja nasi na atatusikia huku akiendelea kusimamia kauli yake ya kuwataka Watanzania wafanye kazi kwa bidii na kumtegemea Mungu

bila kujali kauli za kebehi na ukosoaji kutoka pande mbalimbali za dunia;

iii. Alihimiza Watanzania kumtegemea Mwenyezi Mungu na kwamba Mwenyezi Mungu pekee ndiye atakayetuvusha na kutuepusha na janga hili.

iv. Aliwasihi Watanzania kutopuuza umuhimu wa tiba mbadala katika mapambano dhidi ya *Covid-19*. Kauli hii imekuwa chachu katika kuimarisha tafiti za dawa za asili ambazo zimekuwa na mchango mkubwa katika kupambana na maradhi mbalimbali ikiwemo *Covid-19* na Watanzania walianza kutumia lakini pia walianza pia na ile inayoitwa nyungu.

v. Tarehe 20 Mei, 2020 Mheshimiwa Rais akiwa Singida aliwaomba Watanzania watumle siku tatu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa maajabu aliyoyafanya kwa Taifa letu kwa kutuepusha kusambaa kwa virusi vya *Covid-19*. (*Kicheko*)

(Hapa picha mbalimbali zillioneshwa ndani ya ukumbi wa Bunge)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, hali iliyoko sasa, ni kuwa maambukizi yamepungua na wagonjwa wamepungua hospitalini. Kama kuna anayestahili sifa ni Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msimamo wake usiotetereka na maono ya mbali aliyokuwa nayo yaliyokuwa chachu katika kupunguza maambukizi ya *Covid-19* na kulinda uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameifanya Tanzania kuwa ya kupigiwa mfano duniani kwa namna alivyoshughulikia ugonjwa huu. Naomba tuangalie screen zetu ili tupate ujumbe wa video. (*Makofii*)

(Hapa video zilizoonesha hotuba mbalimbali za Mheshimiwa Rais zikitoa maelekezo juu ya mapambano dhidi ya Covid-19)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, pongozi maalum kwaviongozi wa dini kwa namna walivyoshirikiana na waumini katika mapambano ya ugonjwa wa *Covid-19*. Wakati wote viongozi hao wamekuwa wakiwapatia waumini Watanzania faraja pia na wagonjwa kwamba Mwenyezi Mungu atawaponya. Hatua hizo zimekuwa mhimili mkubwa wa upendo, umoja, mshikamano na ujasiri miongoni mwa Watanzania. Tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, taarifa iliyotolewa na Taasisi ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (*Organisation for Economic Cooperation and Development - OECD*) inabashiri kuwa kitendo cha kuwafungia watu ndani (*Lockdown*) kumesababisha vifo kwa njaa na kusinyaa kwa uchumi wa nchi zilizoendelea kwa asilimia 2 kila mwezi. Hivi sasa nchi nyingi zinakubaliana kuwa *Lockdown* si hatua sahihi ya kukabiliana na *Covid-19*. Vilevile, kisayansi inakadiriwa kuwa nchi ambazo ziliwafungia watu wake na mipaka yake zipo katika hatari ya kukumbwa na madhara makubwa ya ugonjwa huo pindi utakapotokea mlipuko wa pili na hata wa tatu.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, mtizamo na hatua zilizochukuliwa na Tanzania katika kupambana na *Covid-19* zinaonesha upekee tulionao nchini. Serikali inayo kila sababu ya kuwapongeza Watanzania ambao si tu walipokea maelekezo ya Serikali lakini pia walifanya hivyo kwa uaminifu mkubwa na kwa hiari yao wenyewe bila kushurutishwa na mamlaka yoyote ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwashukuru wataalamu wetu wa afya kwa kuwashudumia wagonjwa wa *Covid-19*. Wataalamu wetu hao walitekeleza majukumu yao bila kujali hatari ya virusi hivyo kwa maisha yao na wependwa wao. Vievile naishukuru sekta binafsi, mtu mmoja mmoja na wadau wote ambao waliitikia wito wa Serikali kwa kutoa michango ya hali na mali katika kufanikisha vita dhidi ya *Covid-19* nchini. Kipekee niwashukuru wamiliki wa viwanda ambao waliitikia wito wa Mheshimiwa Rais na kuanza

kuzalisha vifaa kinga hapa nchini badala ya kuagiza kutoka nje, na waendelee kufanya hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kwamba zile nchi zilizoondoa vizuizi sasa zinalo somo la kujifunza kutoka Tanzania. Aidha, suala la kudhibiti maambukizi ya *Covid-19* litaendelea kuwa kipaumbele cha Serikali kwa sasa sambamba na malengo ya muda mrefu ya kumaliza ugonjwa huo hususani katika kipindi hiki ambacho Shirika la Afya Duniani ambalo limebainisha kwamba *Covid-19* si gonjwa la kuondoka mara moja. Hivyo, watu na dunia kwa ujumla hatuna budi kujifunza namna ya kuishi na virusi hivyo kama ilivyo kwa UKIMWI na virusi vingine, huku tukifanya kazi ili kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 9 Juni, 2020 Bunge Iako Tukufu lilipitisha Azimio la Kumpongeza naKumuunga Mkono Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna alivyomudu kuivusha nchi katika janga la hili la *Covid-19*. Waswahili husema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Katika hili na mimi naomba niseme kidogo kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba zake zote zilizohusu ugonjwa huu ambapo alihimiza masuala muhimu kwa Watanzania katika kukabiliana na janga hili na zilitibu hofu kubwa iliyokuwa imetanda kwa Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, leo tunayo idadi ya wagonjwa waliolazwa wanaouguwa kuona kwamba inapungua sana. Kwa mfano, taarifa ya leo mpaka mchana, leo tarehe 15 Juni, 2020 kutoka katika vituo vyatolea huduma na hospitali za Serikali na Binafsi nchini, inaonesha kuwa tuna wagonjwa 66 katika mikoa 10 na mikoa 16 haina wagonjwa ikiwemo Mkoa wa Arusha, Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Mara, Mtwara, Manyara, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Simiyu, Songwe na Tabora; hatuna mgonjwa aliyelazwa kwenye hospitali yoyote ya Serikali wala binafsi. Pamoja na mwenendo huu, ninawaomba wananchi wote kuendelea kuchukua tahadhari zote za kiafya na miongozo yote

inayotolewa na wataalam wa afya pamoja na Serikali.
(Makof)

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu, pamoja na Katibu Mkuu, Mganga Mkuu wa Serikali, Watendaji wote wa Wizara ya Afya wakiwemo Madaktari, kwa kazi kubwa walioifanya usiku na mchana kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata elimu ya *corona* na kuhakikisha kuwa maambukizi yanapungua kwa kasi. Tunawashukuru sana kwa kazi hii walioifanya.*(Makof)*

Mheshimiwa Spika,Mheshimiwa Ummy Mwalimu amekuwa akiifanya kazi hii bila kujali familia, mchana na usiku umeweza kupata mawasiliano ya hatua mbalimbali, amekuwa akijenga tabia ya mawasiliano kwa viongozi lakini plia na Watendaji wetu, kwa kweli anastahili sifa na Mwenyezi Mungu atamwongoza. Hongera sanakwa Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa kazi hiyo na timu yake yote akiwemo Katibu Mkuu, Mganga Mkuu wa Serikali na Madaktari wote kwenye Wizara yake.*(Makof/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nieleze shughuli zilizotekeleza kwenye Bunge lako la Kumi na Moja toka mwaka 2015 mpaka 2020; wakati Bunge la Kumi na Moja likielekea kuhitimisha shughuli zake, limefanikiwa kutekeleza masuala mbalimbali ikiwemo kujibu maswali na hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge, kujadili na kuitishaMiswada ya Serikali, Maazimio mbalimbali yenye kuhusisha mikataba na Itifaki za Kikanda na Kimataifa, kupokea kauli za Serikali kuhusu ufanuzi wa mambo mbalimbali pamoja na kuunda Tume kwa ajili ya kufuatilia masuala muhimu yenye maslahi mapana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chote cha Bunge la Kumi na Mojinaloolekea kuhitimisha uhai wake tarehe 16 Juni, 2020 kesho, jumla ya maswali ya msingi 3,962 yameulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Aidha, maswali ya nyongeza 9,563 yameulizwa kutokana na maswali ya msingi na kujibiwa na Serikali. Vilevile, jumla ya maswali

178 ya kawaida na ya nyongeza 162 yameulizwa na Wabunge na kujibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuitia utaratibu wa maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kuitia Mkutano huu wa Kumi na Tisa, jumla ya maswali 471 ya msingi na mengine 69 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge kwa mfumo wa mtandao na kujibiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali imewasilisha jumla ya Miswada 60 ya Sheria ambayo imejadiliwa na kuitishwa na Bunge lako la Kumi na Moja, wakati Sheria 159 zimefanyiwa marekebisheso. Vilevile, jumla ya Maazimio 38 ya Bunge yamejadiliwa na kuridhiwa na Bunge lako Tukufu. Pia, Kauli 20 za Serikali zimetolewa ikiwa ni ufanuzi wa masuala mbalimbali yaliyowasilishwa na Mawaziri. Aidha, Kamati Maalum nne za Bunge zimeundwa katika Bunge la Kumi na Moja kwa ajili ya uchunguzi wa masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu unaoishia kesho, Bunge lako Tukufu lilipitisha kwa hatua zake Miswada ya Sheria sita ambayo ni:-

- (i) Muswada wa Sheria ya Marekebisheso ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2020.
- (ii) Muswada wa Sheria ya Afya ya Mimea, 2020.
- (iii) Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, 2020.
- (iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisheso ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2020.
- (v) Muswadawa Sheria ya Fedha za Matumizi, 2020.
- (vi) Muswada wa Sheria ya Fedha, 2020.

Mheshimiwa Spika, Maazimio ya Serikali; vilevile, Serikali iliwasilisha katika Mkutano huu Maazimio matano ya

Bunge. Maazimio hayo yaliyordhiwa na Bunge hili kama ifuatavyo:-

- (i) Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuuvi wa Mwaka 1995 F.
- (ii) Azimio la Bunge la kuitaka Serikali Kutobadili Uamuzi wa Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi na Shughuli za Serikali.
- (iii) Azimio la Bunge la Kumpongeza Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Mafanikio ya Bunge la Kumi na Moja.
- (iv) Azimio la Bunge la Kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, kwa namna alivyoliongoza Taifa katika Mapambano Dhidi ya Janga la Ugonjwa wa Corona.
- (v) Azimio la Bunge kuhusu Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambalo nalo pia lilipitishwa kwenye Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Mkutano huu pia, Kamati za Kudumu za Bunge 15 ziliwasilisha Bungeni taarifa za mwaka za kazi. Taarifa hizo zilisheheni uchambuzi wa kina, maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa Serikali. Nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na wajumbe wote wa Kamati hizo kwa kazi nzuri waliyoifanya kuanzia maandalizi ya kazi za Kamati hadi kuwasilisha taarifa zao katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, leo hii tarehe 15 Juni, 2020, Waheshimiwa Wabunge 304 kati ya Wabunge 371 wamepitisha kwa kishindo Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2020/2021 ya jumla ya shilingi trillioni 34.88. Kati ya fedha hizo, shilingi trillioni 21.98 ni za matumizi ya kawaida na shilingi trillioni 12.90 ni za miradi ya maendeleo sawa na asilimia 37 ya Bajeti yote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, kwa pamoja na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Mbunge wa Kondoa na Watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuwasilisha kwa umahiri mkubwa Hotuba ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2019 na Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021 na kuhitimisha hoja hiyo. Nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri wote ambao pia wameshiriki kuchangia hoja hiyo na pia wale wote ambao wamechangia na kuunga mkono Bajeti hiyo, tunawashukuru sana, matunda tutayaona.

Mheshimiwa Spika, kipekee niwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao ambayo imesheheni maoni na ushauri mzuri kwa Serikali wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara mbalimbali kwa mwaka 2020/2021, pamoja na mjadala kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2019 na Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021. Nalishukuru Bunge lako Tukufu kwa kuitisha Bajeti ya Serikali ya Mwaka ujao wa Fedha kwa kura nydingi za ndiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi shupavu wa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imejipanga vizuri kutekeleza mipango yote iliyowekwa katika Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Mwaka 2020/2021. Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kuendelea kushirikiana na Serikali katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu. Aidha, natoa wito kwa sekta binafsi, wadau wa maendeleo na wananchi wote kuendelea kutoa ushirikiano katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, sambamba na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu, utekelezaji wa kazi za Serikali utaendelea. Hivyo, Watumishi wote wa Umma wanashauriwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi, uaminifu na kutoa huduma bora kwa wananchi kwa ufanisi na tija wakati wote.

Aidha, katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021, napenda kutoa msisitizo katika maeneo yafuatayo:-

- (i) Serikali itaendelea kutekeleza Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021 kwa kuzingatia athari na changamoto za ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya *corona*.
- (ii) Serikali itakamilisha mchakato wa shughuli zilizobaki za maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Ubunge, Urais na Udiwani na kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kusimamia kikamilifu shughuli zote za uchaguzi huo kwa uhuru na haki.
- (iii) Serikali itatoa msukumo wa kipekee katika kukamilisha miradi ya kipaumbele na miradi ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano ili wananchi waendelee kupata huduma bora.
- (iv) Serikali itashirikiana na sekta binafsi kuleta mageuzi kwa kutekeleza kwa kasi mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Lengo ni kuhakikisha kuwa shughuli za uchumi na biashara zinashamiri na kuchangia kuondoa umaskini nchini.
- (v) Serikali itaendelea kuboresha huduma za jamii pamoja na kuhakikisha kwamba ulinzi na usalama unaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaendelea vema na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Hivi sasa, pamoja na mambo mengine Tume imekamilisha matakwa ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya kufanya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara mbili kati ya Uchaguzi Mkuu mmoja na mwingine.

Mheshimiwa Spika, zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura wa awamu ya kwanza lilianza rasmi tarehe 18 Julai, 2019 na kukamilika tarehe 23 Februari, 2020

kwa nchi nzima wakati awamu ya pili ilianza tarehe 17 Aprili, 2020 na kukamilika tarehe 5 Mei, 2020.

Mheshimiwa Spika, takwimu za awamu ya kwanza na ya pili, zinaonesha kuwa wapigakura wapya walioandikishwa ni 7,326,552, wapigakura walioboresha taarifa zao ni 3,548,846 na wapiga kura 30,487 wamepoteza sifa. Hadi sasa jumla ya Wapigakura halali kwa mwaka 2020 ni 29,804,992 ikilinganishwa na Wapigakura wa mwaka 2015 ambao walikuwa 23,161,440.

Mheshimiwa Spika, Tume inaendelea na uchambuzi wa taarifa za Wapiga Kura waliojiantikisha na baada ya zoezi hilo kukamilika, Daftari la mwisho litakalotumika katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 litaandalisha na kuwekwa wazi.

Mheshimiwa Spika, niwasih i viongozi na wanachama wa vyama vyote vya siasa na wananchi kwa ujumla kuendelea kulinda amani ya Taifa letu na kuendeleza mshikamano tulionao katika kipindi hiki na wakati wa uchaguzi mkuu. Natoa wito kwa Viongozi wa Vyama vya Siasa na Wadau wengine wa uchaguzi kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo katika uendeshaji wa shughuli za uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Michezo; kwa miaka hii mitano tunaendelea kuonesha upekee wa Mheshimiwa Rais wetu mbali ya kazi kubwa ya ujenzi wa miradi ya huduma za jamii, pia Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli amehamasisha masuala ya kijamii ikiwemo michezo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ni Mwanamichezo na ni Msanii ambaye amekuwa hasiti kuonesha kipaji chake cha matumizi ya ala ya ngoma. Aidha, wote ni mashahidi kila awapo palipo na wasanii wanaotoa burudani ya ngoma huwa lazima akaungane nao na kuonesha umahiri wake kwa kupiga ngoma. Naye anaingia kwenye orodha ya washiriki waliochomoza kuwa maarufu

kwa kumudu katika kutumia ala hiyo kwa kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo na burudani tunao Watanzania waliofanya vizuri kwenye eneo hilo katika kipindi cha miaka mitano. Ikumbukwe kuwa ninaowazungumzia hapa ni baadhi ya wanamichezo na wasanii waliolibeba Taifa letu na kupeperusha bendera ya Taifa huko nje ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, kwenye michezo ya riadha ni muhimu tukampongeza kijana wetu Alphonce Felix Simbu aliyetuletea medali ya fedha na kupeperusha vyema bendera ya Taifa kwenye mashindano ya mbio ndefu ya Majeshi ya Dunia yaliyofanyika nchini China. Wanamichezo wengine waliochomoza nje ya nchi ni pamoja na Mwanamasumbwi bingwa, Hassan Mwakinyo aliyemtwanga Sam Eggington wa Uingereza kwa *knock out* katika raundi ya pili na kupeperusha Bendera ya Taifa huko Uingereza.

Mheshimiwa Spika, eneo la sanaa na burudani hususani muziki wa *Bongo Flavour* limekuwa na mchango mkubwa katika kuitangaza nchi yetu lakini hata mapato. Natumia fursa hii kuwapongeza vijana wetu ambao ni wasanii wa muziki wa *Bongo Flavour* akiwemo Naseeb Abdul Juma maarufu kama *Diamond Platinumz* (Simba) pamoja na Rajabu Abdul Kahali maarufu kama *Harmonize* (Konde boy-Tembo). Tumekuwa tunashuhudia mapokezi wanayopata huko nje na wakitumbuiza muziki wetu na kupeperusha Bendera yetu kwenye Mataifa mbalimbali. Wako pia Wasanii wengine kama wakina Vanessa Mdee, Raymond Mwakyusa (Rayvanny), Ali Kiba (King Kiba) na kadhalika. Hawa nao pia wamefanyakazi ya kupeperusha bendera na kulipa sifa Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mchezo wa soka nao licha ya kuwa ndio mchezo unaoongoza kwa wapenzi hapa nchini pia umetoa vijana wengi nje walioilettea sifa nchi yetu. Kwa upande huu wa soka, sote tumpongeze kijana wetu Mbwana Samata anayelitangaza Taifa letu katika ligi kuu ya soka

Nchini Uingereza kwenye Timu ya *Aston Villa*. Pia tunawapongeza sana wachezaji wetu kama akina Simon Msuva, Hassan Kessy, Abdi Banda, Kelvin John na kadhalika ambaao wanaendelea kutangaza Taifa letu huko na ni matarajio yetu kwamba wapo watakaofuata nyayo zao ili kuliletea sifa Taifa letu. Soka la Vijana nalo limeendelea kuimarike ambapo Timu za Soka za Vijana wa umri wa miaka 17 na miaka 20 na Timu ya Wanawake (*Twiga Stars*) zimefanya vizuri katika michezo ya Kimataifa na kuleta makombe hapa nchini. *Taifa Stars* nayo katika kipindi cha miaka 39 imeweza kucheza *AFCON* mara ya pili katika kipindi hiki cha miaka mitano. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha miaka mitano, tumeshuhudia *Club* kongwe ikipeperusha Bendera ya Taifa nje ya nchi na ikitutoa kimasomaso katika medani za soka la kimataifa kwa kuweka historia ya Taifa letu kwa kucheza hatua ya robo fainali ya Mabingwa wa Afrika baada ya kufuzu hatua ngumu ya makundi nayo si nyingine bali ni *Simba Sports Club*, nayo siyo nyingine bali ni *Simba Sports Club*, *Clubambayo* inakaribia kutangaza ubingwa wa Tanzania... (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WABUNGE FULANI: Rudia, rudia, rudia.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge hawajakusikia kwa kweli. (*Vicheko*)

WAZIRI MKUU: Timu ambayo imeingia katika mashindano ya bingwawa Afrika baada ya kufuzu hatua ngumu ya makundi nayo siyo nyingine bali ni *Simba Sports Club*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *Simba Sports Club* ni *Clubambayo* inakaribia kutangaza ubingwa wa Tanzania kwa ligi ya ndani kwa mara ya tatu mfululizo ikiwa haijacheza michezo tisa. Kama inaweza kutangaza ubingwa ikiwa haijamaliza

michezo yote nini faida ya mkuki? Kama *Club* inaweza kutangaza ubingwa kabla haijamaliza michezo yote, nini faida ya mkuki? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kuonyesha ubora wa timu hiyo, mchezaji anayeongoeza kwa kufunga magoli mengi ni Medie Kagere aliyefunga magoli 19 kutoka *Simba Sports Club* na wachezaji wanaofuatia kwa magoli mengi ni Reliants Lusajo wa *Namungo FC* magoli 11; Yusuph Mhilu wa *Kagera Sugar* magoli 11; Bigirimana Bleiz wa *Namungo FC* magoli 10; na Paul Nonga wa *Lipuli FC*, magoli 10. Hatujaona timu ya wananchi iklongoza kwenye magoli. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hatua hii haiwezi kufikiwana timu yoyote kwa kuwa mikuki mingi nibutu, mkuki wenye ncha kali uko *Simba Sports Club*.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu muda bado uko upande wako

WABUNGE FULANI: Aaaah.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kurudia kwa kusema kwamba hatua hii haiwezi kufikiwa na timu yoyote kwa kuwa mikuki mingi nibutu na mkuki wenye ncha kali uko *Simba Sports Club*.

Mheshimiwa Spika, nihitimishe hotuba yangu kwa kumshukuru tena Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake makini uliolipatia Taifa letu mafanikio makubwa katika kipindi kifupi cha miaka mitano. Watanzania wanakuhitaji kulongozwa Taifa hili. Nitoe wito kwa Watanzania kujitokeza kwa wingi ili tumpigie kura za kutosha pale atakapokuwa anaomba kura kwa wananchi. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa mara nyingine tena niwashukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; pamoja na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa

Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia vema utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Vilevile, namshukuru sana Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ushirikiano ambao amekuwa akinipatia wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, narudia tena kukushukuru na kukutakia afya njema, uendelee kuwa mbunifufui katika kuendesha shughuli yako ya Uspika hapa na baadaye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Prof. Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania kwa ubunifufui wake wa kuendesha shughuli za Mahakama kwa njia ya mtandao katika kipindi cha ugonjwa wa *COVID-19*. Lakini pia namshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Eliezer Feleshi, Jaji Kiongozi, Waheshimiwa Majaji wote, Mahakimu na watendaji wote wa mhimili wa Mahakama kwa kazi nzuri ya kuwashudumia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nitumie tena fursa hii kuwashukuru tena Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Makatibu Wakuu pamoja na Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru washirika wa maendeleo zikiwemo Nchi rafiki, Taasisi na Mashirika ya Kimataifa, madhehebu ya dini na mashirika yasiyo ya kiserikali, kwa kuendelea kuunga mkono juhudzi za Serikali katika kujenga uchumi wa viwanda na kuilettea nchi yetu maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia, Viongozi wote wa dini na wanahabari wote kwa ushirikiano mkubwa

waliouonesha kwa Serikali katika kipindi chote cha miaka mitano. Mchango wenu wana habari umekuwa muhimu katika kuiwezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa kimaendeleo na kwa kutoa taarifa mbalimbali kulingana na mipango tuliyojiwekea lakini na utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha miaka mitano tumekuwa karibu sana na kupata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi wa Chama Cha Mapinduzi katika ngazi zote. Hivyo, niendele kumshukuru Mheshimiwa Philip Mangula, Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa pamoja na Dkt. Bashiru Ally, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi; nawashukuru sana Viongozi wangu wa CCM kwa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa llani ya Chama chetu. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijafika mwisho, niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano ambaa mmetupa kwa Serikali. Pia ninawashukuru Watumishi wote wa Bunge kwa huduma nzuri na msaada ambaa mmekuwa wakitupatia kipindi chote tulichokuwa hapa Bungeni. Aidha, ninawashukuru Watendaji wote wa Serikali na Taasisi mbalimbali kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi, umahiri na ufanisi mkubwa na hivyo kufanikisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na Bunge bila kuwasahau Wanahabari kwa uchambuzi na kuuhabarisha umma na Madereva wote walituhudumia wakati wote tukiwa tunakuja nan a kurudi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nitumie nafasi hii kuishukuru tena familia yangu ambayo imeweza kunivumilia wakati mwingu nilipokuwa nikitekeleza majukumu yangu ya kitaifa. Namshukuru sana mke wangu Mary Majaliwa na watoto wangu kwa kuniombea, na kunitia moyo wakati wote ninapokuwa nikitekeleza majukumu yangu. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu ya Waziri Mkuu inawezekana kabisa kwa namna moja au nyingine niliwakwaza baadhi ya viongozi na watendaji, lakini

yote ni katika kutekeleza majukumu ya Waziri Mkuu. Imani yangu ni kwamba tutaendelea kulijenga Taifa kwa pamoja hususan katika kipindi hiki tunachoelekea kwenye kinyang'anyiro cha Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mwisho wa Bunge hili, ndiyo kiashiria cha Bunge lijalo baada ya uchaguzi. Hivyo, nawaaga wote kwa kuamini kuwa wale waliofanya vema katika kipindi hiki wataaminiwa tena na wananchi na kurejea kwenye Bunge lijalo. Hivyo, tuombeane heri ili kila mmoja wetu atakayechukua fomu za kugombea tena apate ushindi na fursa ya kuwatumikia wananchi. (*Makofî*)

**HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB),
WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WAKATI WA KUHITIMISHA SHUGHULI ZA MKUTANO
WA KUMI NA TISA WA BUNGE – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kufika siku hii ya leo ambayo naiita kuwa ni siku ya kihistoria kwetu.
2. Nasema kuwa ni ya kihistoria kwa sababu Bunge lako Tukufu linahitimisha shughuli za Bunge la Kumi na Moja (11) la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia tunahitimisha Mkutano wa Kumi na Tisa (19) wa Bunge ulioanza mwezi wa Aprili mwaka huu wa 2020.
3. **Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano huu wa Bunge, licha ya uwepo wa ugonjwa wa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19), tumeweza kukaa hapa Dodoma kwa kipindi kisichopungua miezi miwili na nusu. Aidha, katika kipindi hicho tumeweza kutekeleza majukumu yetu yote kama ilivyokuwa imepangwa.
4. Ama kwa hakika hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwani tunakamilisha maisha yetu ya Kibunge kwa kipindi cha miaka mitano toka Novemba 2015. Tumeshirikiana katika

maeneo mengi nje na ndani ya Bunge kwa kila mmoja kutekeleza majukumu yake.

5. **Mheshimiwa Spika**, siwezi kuanza kueleza yaliyojiri kwenye majukumu yetu bila kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeiwezesha kuwa na afya njema na kunismamia katika kila jambo na hasa nilipokuwa natekeleza majukumu yangu binafsi na ya umma kwa kipindi chote hadi sasa. InshaAllah, yeye ndiye msimamizi wa yote.

6. **Mheshimiwa Spika**, kwa moyo mkunjufu kabisa naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kitendo chake cha kuniamini na kunitfea kushika wadhifa wenyewe dhamana kubwa ya kumsaidia kazi ya utendaji ndani ya Serikali kwa kipindi chote cha miaka mitano.

7. Kwa niaba ya Familia yangu na Wana-Ruangwa wote, namshukuru sana kwa ukarimu, imani na upendo alionunesha kwetu, Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu, ulinzi, kheri na kila lililo jema na aendelee kuliongoza Taifa hili vyema na kwa mafanikio makubwa kama ambavyo Watanzania tumeendelea kushuhudia mafanikio makubwa katika kipindi hiki cha Uongozi wake wa Awamu ya Tano.

8. **Mheshimiwa Spika**, Rais wetu ametenda mema kwa Watanzania na watamlipa mema. Ninamwombea kheri pia kwa Uchaguzi Mkuu ujao ashinde kwa ushindi wa kishindo. Amina.

9. **Mheshimiwa Spika**, ninamshukuru sana pia Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano wake mkubwa wakati wote nikitekeleza majukumu ya Waziri Mkuu. Vilevile, ninashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa nilioupata kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar pamoja na viongozi, watendaji na wananchi wote wa Zanzibar.

10. **Mheshimiwa Spika**, nitumie nafasi hii pia kukushukuru sana wewe binafsi kwa upendo uliouonesha kwangu kipindi chote cha uhai wa Bunge la Kumi na Moja (11).
11. Kwa uzoefu ulionao katika kuendesha Bunge, umekuwa msaada sana kwangu kwa kunipa ushauri na ushirikiano wa dhati ulionifanya nijenge imani kubwa kwenye majukumu yangu ndani ya Bunge.
12. **Mheshimiwa Spika**, nami niungane na wenzangu kukutakia kheri nyingi kwenye Uchaguzi ujao, naamini Wana-Kongwa watasikiliza na kutekeleza dua zetu za kuwa upite bila kupingwa, na ukirudi hapa chukua fomu ya Uspika ili upate kura zote za ndiyo uendelee kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Mbili (12).
13. **Mheshimiwa Spika**, sitasahau tukio la tarehe 19 Novemba, 2015 siku ambayo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipowasilisha jina langu katika Bunge lako Tukufu na kupendekeza niwe Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
14. **Mheshimiwa Spika**, nakushukuru tena wewe na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa imani mlionionesha kwa kuridhia mapendelekezo ya Mheshimiwa Rais na kunipigia kura nyingi za ndiyo na mkaridhia tufanye kazi kwa pamoja katika kuwatumikia Watanzania.
15. **Waheshimiwa Wabunge wenzangu**, natambua, naheshimu na nathamini ushirikiano wa dhati mlionipa katika kipindi chote cha Bunge. Nami nawaombea na nawatakia ushindi wa kishindo kwenye Majimbo yenu ili mrudi tena hapa mwezi Novemba, 2020.
16. **Mheshimiwa Spika**, pia, nawashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Akson, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan ambaye mwishoni alipata uteuzi wa Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa

Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa kuliongoza Bunge hili kwa busara na umahiri mkubwa.

17. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, namshukuru Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha Bajeti ya Serikali. Pia, nawashukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai na Watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mkubwa walilotupatia katika Mkutano huu na Mikutano ilioendeshwa kipindi chote cha miaka mitano.

18. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu hapa Bungeni, napenda kutambua mchango wa Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayesimamia Sera, Uratibu, Bunge, Ajira, Kazi, Vijana na Watu wenyewe ulemavu. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mhagama kwa kunisaidia ipasavyo katika kutekeleza majukumu yangu sambamba na majukumu yake ya unadhimu na uratibu wa shughuli za Serikali Bungeni. Nakuombea sana kwa wananchi wa Peramiho, Maposeni, Mgazini, Mdunduwalo, wakupitishe upite bila kupingwa.

19. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, namshukuru Mheshimiwa Angela Kairuki (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji kwa kufuatilia na kusimamia hatua mbalimbali za kuimarisha na kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini. Mheshimiwa Waziri Kairuki amekuwa akitembelea maeneo mbalimbali na kukutana na Wawekezaji wadau wa sekta binafsi ili kusikiliza changamoto zao na kuzitafutia ufumbuzi. Juhudi zake hizo, zimekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha mazingira ya biashara na kuimarisha mahusiano ya sekta binafsi na Serikali nchini. Nawe nakutakia kila la kheri huko uendako ili upate kura za kutosha.

20. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa masuala ya maendeleo na uwezeshaji wa vijana napenda kumshukuru Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Mbunge wa Dodoma

Mjini, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu kwa msaada mkubwa katika kusimamia vizuri masuala ya vijana na ajira. Kadhalika, namshukuru Dada yangu Mheshimiwa Stella Ikupa Alex (Mb), Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kusimamia vema masuala na maslahi ya Watu Wenye Ulemavu.

21. Nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri; Professor Adelardus Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Balozi Mhandisi John William Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi; Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wakiongozwa na Bw. Tixon Tuyangine Nzunda, Andrew Wilson Massawe, na Bibi Dorothy Aidan Mwaluko kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. Nawashukuru kwa ushirikiano wa dhati mlionipa katika kuratibu na kusimamia shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu. Bila kuwasahau Watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

22. **Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii pia kuwashukuru Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama akiwemo Jenerali Venance Mabeyo - Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama; Inspekta Jenerali wa Polisi - Simon Nyakoro Sirro; Brigedia Jenerali Suleiman Mzee -Kamishna Jenerali wa Magereza; Dkt. Anna Makakala - Kamishna Jenerali wa Uhamiaji; John William Hasunga - Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji; Kamishna Diwani Athuman - Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa; Brigedia Jenerali John Mbung'o - Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa; James Kaji - Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevyा.

Wakuu hao wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wameonesha nidhamu na uzalendo mkubwa katika kuhakikisha Nchi yetu, raia wake na mali zao wanakuwa salama.

23. **Mheshimiwa Spika**, nawashukuru pia Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na Watendaji wote Serikalini kwa ushirikiano mzuri walioutoa na utendaji wa pamoja wenye mafanikio makubwa. Aidha, tuendelee kutakiana mema na tuchape kazi hadi hapo utumishi wetu utakapokoma.

24. **Mheshimiwa Spika**, nimalizie salamu zangu za shukrani kwa Familia yangu ambayo inaniunga mkono, kunivumilia pale ambapo nawatumikia Watanzania na kunitia moyo siku hadi siku kwenye majukumu yangu. Bila kuwasahau Wana-Ruangwa ambao walnipigia kura bila kujali Vyama vyao na kuniwezesha kuingia Bungeni na hatimaye nikapata uteuzi wa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania. Nataka niwahakikishie Wana-Ruangwa kuwa bado tuko pamoja katika harakati za kuleta maendeleo. Nawashukuru sana.

25. **Mheshimiwa Spika**, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wananchi na Watanzania wote kwa kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Tano na ushirikiano walioutoa kwa Serikali wakati wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ya Taifa kwa ujumla bila kujali tofauti zao za kilitikadi au dini. Sambamba na kuonesha uzalendo, mshikamano na kudumisha amani na utulivu uliowezesha Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi, kwa mujibu wa taarifa zinazotolewa na taasisi ya GLOBAL PEACE INDEX 2020 inayofuatilia masuala ya amani duniani. Tanzania ni nchi ya saba kwa amani na utulivu Afrika na ni nchi ya kwanza kwa amani Afrika Mashariki. Naamini wananchi wataendelea kuiunga mkono Serikali yetu ili ifanye mambo makubwa zaidi katika kipindi cha pili cha Awamu ya Tano kwa amani na maendeleo yake.

26. **Mheshimiwa Spika**, baada ya salamu za shukurani nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa Iramba Magharibi kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria na Mheshimiwa Dkt. Godwin Aloyce Mollel, Mbunge wa Siha kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Aidha, mkiwa viongozi mlioteuliwa, tambueni kuwa mnalo jukumu kubwa la kuwashudumia Watanzania, hususan katika kipindi hiki ambacho Nchi yetu imekumbwa na changamoto mbalimbali likiwemo janga la Corona.

SALAMU ZA POLE

27. **Mheshimiwa Spika**, wakati tukiendelea na Mkutano huu wa 19, Bunge lako Tukufu lilipata pigo kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu akiwemo Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Sumve na Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga, aliyekuwa Mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria.
28. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hicho pia, tuliondokewa na aliyekuwa Jaji Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Jaji Augustino Ramadhan. Aidha, niungane na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kuwapa pole majirani zetu, wananchi wa Burundi kwa kifo cha aliyekuwa Rais wa Nchi hiyo, Mheshimiwa Pierre Nkurunzinza. Tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu azipumzishe Roho za wapendwa wetu wote mahali pema. Amina.
29. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Taifa letu likumbwa na majanga mbalimbali ikiwa ni pamoa na mafuriko, COVID-19 na ajali za barabarani ambazo zilisababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Napenda kutoa salamu za pole kwa ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza wapendwa wao na wengine kupata majeraha kutokana na matukio hayo. Tumucombe Mwenyezi Mungu aziweke Roho za marehemu mahali pema na walioapata majeraha awajalie nafuu na kupona mapema. Amina.

MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA TANO

30. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na fikra na uongozi makini katika ujenzi wa Taifa letu. Ni dhahiri kuwa maono yake katika kuongoza na kusimamia utekelezaji wa llani ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 na mipango ya Serikali, zimeleta mafanikio makubwa ambayo hivi sasa wote tunayaona.

31. **Mheshimiwa Spika**, nyote mtakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Rais na Makamu wake Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanawafikia Watanzania, wanawasikiliza na kutatua kero zao. Lengo la ziara hizo, pamoja na mambo mengine lilikuwa ni kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 ikiwemo kukagua miradi ya maendeleo; kuzungumza na watumishi na kuwafahamisha kuhusu falsafa ya Serikali ya awamu ya tano ya **Hapa Kazi Tu**.

32. **Mheshimiwa Spika**, ziara hizo zimesaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha utendaji wa watumishi wa umma. Hivi sasa, wananchi wanapokwenda katika ofisi za umma wanapokewa, wanasikilizwa na kuhudumiwa vizuri. Aidha, usimamizi wa miradi ya maendeleo umeimarika sambamba na kuakisi thamani halisi ya fedha katika utekelezaji wa miradi hiyo. Hapa Bungeni ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa maoni, ushauri na ushirikiano ambao mmekuwa mkiutoa wakati wa ufuutiliaji wa shughuli za maendeleo sambamba na kusimamia Serikali yetu.

Mambo mengi ya kujivunia yamefanywa na tumekuwa tukiyaeleza katika maeneo mengi kupitia mikutano ya hadhara, vyombo vyya habari, nyaraka mbalimbali, uwepo wa miradi mingi ya kimkakati hadi kwa wananchi wa kawaida.

33. Nitaeleza majukumu na miradi michache tena kwa kifupi ili kuwakumbusha nini Serikali imefanya katika kipindi hiki cha miaka mitano.

- Marekebisho ya nidhamu kwa utumishi wa umma na uwajibikaji Serikalini ili kuwezesha Watumishi kutambua majukumu yao na kuwatumikia Watanzania.
- Mapambano dhidi ya rushwa ndani ya Serikali na nje ya Serikali ili kulinda mali na fedha za umma. Hatua hii ni endelevu, lengo ni kung'oa mizizi ya rushwa nchini.

- Kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama, mhimili wa Bunge na Mahakama. Matakwa yetu ni kuhakikisha kuwa nchi inabaki salama na mihimili ifanye kazi yake.
- Mapambano dhidi ya matumizi ya dawa za kulevyia ili kujihakikishia kuwa tunakuwa na Taifa lenye nguvukazi inayofanya kazi. Mapambano bado yanaendelea. Tutapambana na wazalishaji, wasambazaji, wauzaji na watumiaji wa dawa za kulevyia.
- Utambuzi wa watumishi hewa waliokuwa wanalipwa fedha wakiwa hawapo. Katika zoezi hili tumepata mafanikio makubwa na kuokoa **shilingi Bilioni 19.83** kwa kuwaondoa kwenye mfumo wa malipo watumishi hewa 19,708 na wenye vyeti vya kugushi 15,411.
- Ukusanyaji wa mapato ili kuwezesha Serikali kujenga miradi na kutoa huduma muhimu. Ukusanyaji wa mapato umeongezeka kutoka wastani wa shilingi Bilioni 800 kwa mwezi mwaka 2015 hadi wastani wa shilingi trilioni 1.5 kwa mwezi katika kipindi cha Julai 2019 hadi Aprili 2020.
- Kuimarisha uwekezaji kwa kujenga viwanda. Hadi Aprili 2020 jumla ya viwanda vipyta 8,477 vikiwemo vidogo, vya katika vikubwa vimeanzishwa katika maeneo mbalimbali nchini na hivyo kuwezesha ongezeko la ajira viwandani za viwandani zipatazo 482,601.
- Kuimarisha kilimo na masoko. Tumeimarisha kilimo cha mazao makuu, kama vile, Korosho, Pamba, Chai, Tumbaku, Kahawa, Michikichi na Mkonge pamoja na mazao ya chakula ili kuwa na uhakika wa usalama wa chakula.
- Kuimarisha ushirika wa kilimo na upatikanaji wa pembejeo pamoja na huduma za ugani ili kuwafanya wakulima kuzalisha kwa tija.
- Marekebisho ya Sheria ya madini yamefanyika sambamba na kuanzisha masoko ya madini 28 na vituo 12 vya ununuzi wa madini katika maeneo ya uchimbaji na hivyo kuongeza

makusanyo ya Serikali, kupungua biashara haramu na utoroshaji madini kwenda nje. Mwezi Machi hadi Septemba, 2019 jumla ya kilo za dhahabu 4,680.28 zenyе thamani ya shilingi bilioni 432.49 zimezalishwa na Serikali kukusanya shilingi bilioni 30.27.

- Kuhamishia Makao Makuu Dodoma ambapo tayari Watumishi wapatao **15,361** wamehamia Dodoma na sasa fursa za uwekezaji zimeongezeka katika Jiji la Dodoma.
- Kuboresha miundombinu na taaluma Sekta ya Elimu kwa ngazi zote kuanzia awali hadi Elimu ya Juu ikiwemo ujenzi na ukarabati wa madarasa, maktaba, maabara, nyumba za walimu, mabweni na ukarabati wa shule kongwe ili kuziongezea uwezo wa kupokea wanafunzi wengi zaidi.
- Sera ya Elimu bila Ada ambayo inatumia zaidi ya Shilingi Bilioni 20.8 kila mwezi kwa ajili ya fidia ya ada, posho ya madaraka kwa walimu wakuu, wakuu wa shule na waratibu kata kila mwezi toka 2016 na tutaendelea. Hii imesaidia kuongeza uandikishaji na mahudhurio shulenii.
- Kuimarisha huduma za afya kwa kujenga Zahanati, Vituo vya Afya, kujenga Hospitali za Wilaya, Mikoa, Kanda na za Kitifa, huduma za Madawa na Vifaa Tiba. Tumejenga Zahanati **1,198** Vituo vya Afya **487**, Hospitali za Wilaya **71**, Hospitali za Rufaa za Mikoa **10**, na Hospitali za Kanda **03** za Kusini – Mtwara, Magharibi – Tabora na Kanda ya Ziwa - Burigi.
- Ujenzi wa miradi ya maji Vijijini na Mijini tumefikia asilimia **84** Mijini na asilimia **70.1** Vijijini.
- Ufufuaji wa Shirika la Ndege kwa kununua ndege kumi na moja (11) ambazo zinatoa huduma mikoa yote yenye Viwanja vya Ndege na nje ya nchi.
- Ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege kwenye mikoa isiyo na Viwanja vya Ndege unaendelea.

- Ununuzi wa Rada nne mpya za kuongoza Ndege za kiraia zilizo Mwanza, Mbeya, Dar-es-Salaam na Kilimanjaro.
- Ujenzi wa mradi mkubwa wa kufua umeme (Mwalimu Nyerere Dam) utakaozalisha Mg 2115 kwa sasa umefikia asilimia 40. Ujenzi una gharama ya Shilingi Triliioni 6.5
- Usambazaji wa umeme Vijiji kuititia Wakala wa Nishati Vijiji (REA) tumefikia Vijiji kwa asilimia 80% ambapo hadi Aprili 2020 shilingi trillioni 2.27 zimetumika na kufanikisha jumla ya vijiji 9,112 kati ya 12,268 vya Tanzania Bara kuunganishwa na umeme kutoka vijiji 2,118 mwaka 2015.
- Ujenzi wa Mradi wa Reli ya Kimataifa (SGR) wa Kilomita 300 Dar-es-Salaam–Morogoro. Mradi umefikia asilimia 78. Kipande cha Morogoro hadi Makutupora Kilomita 422 mradi umefikia asilimia 30 ya kazi. Lengo ni kukamilisha mradi huu ifikapo Juni 2021 kwa gharama ya Shilingi Triliioni 7.5.
- Ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha lami zikiwemo barabara kuu, barabara za mikoa na za wilaya zenye thamani ya zaidi ya Shilingi Triliioni 7.6. Pia serikali inaendelea kujenga barabara ya njia nne kutoka kutoka Kimara hadi Kibaha (km 19.2)
- Ujenzi wa madaraja: ujenzi wa daraja la juu la Mfugale (Dar-es- Salaam), daraja la Furahisha (Mwanza) na daraja la Magufuli (mto Kilombero) umekamilika; ujenzi wa barabara ya pete (*Ubungo interchange*) umefikia asilimia 77 kwa shilingi bilioni 247; Aidha, ujenzi unaendelea kwa daraja la New Selander (Dar- es-Salaam) kwa shilingi Bilioni 270. Daraja la Kigongo- Busisi shilingi Bilioni 699.2
- Ujenzi wa Bandari, uboreshaji na upanuzi wa Bandari za Tanga, Dar-es-Salaam na Mtwara kwa Shilingi zaidi ya Triliioni 1.2. Pia, ujenzi wa Bandari ya Kigoma na Kalema umeshatengewa fedha.
- Ujenzi wa Meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Victoria na ujenzi wa chelezo;

ukarabati wa meli ya MV Victoria na MV Butiama ambapo katika kipindi cha mwaka 2015/16 hadi Aprili, 2020 jumla ya shilingi billioni 111.7 zimetumika.

Vile vile, Serikali imekamilisha ujenzi wa meli moja mpya yenyewe uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo katika Ziwa Nyasa; na ukarabati wa meli ya mafuta ya MT Sangara katika Ziwa Tanganyika.

- Ujenzi wa Vivuko vya MV Kigamboni, MV Pangani, Kigongo -Busisi, MV Sengerema na Nyamisati.
- Urejeshaji na usimamizi wa mali za Ushirika zilizokuwa zimechukuliwa kinyume na utaratibu, kama vile, NYANZA, SHIRECU, KNCU, Mamlaka ya Mkonge Tanzania, n.k.
- Kusimamia maboresho kwenye Sekta ya Uvuvi na Mifugo kwa kuvua na kufuga kisasa, kujenga viwanda na masoko yake.

34. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kupitia Bunge lako Tukufu katika kipindi cha miaka minne imeidhinisha jumla ya **Shilingi Triliioni 48.075** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kote nchini ikiwemo miradi ya kimkakati niliyoitaja hivi punde. Aidha, jumla ya **Shilingi Triliioni 126.832** ziliidhinishwa zikiwa ni bajeti ya Serikali kwa kipindi hicho.

MVUA KUBWA ZILIZONYESHA NCHINI

35. **Mheshimiwa Spika**, baadhi ya maeneo ya Nchi yetu yalikumbwa na mafuriko kufuatia mvua nyngi zilizonyesha nchini. Mafuriko hayo yalisababisha madhara mbalimbali ikiwemo uharibifu wa miundombinu, mali na vifo. Serikali imeendelea kuchukua hatua za kurejesha hali ya miundombinu iliyoharibika na zoezi hilo ni endelevu.

36. **Mheshimiwa Spika**, mvua nyngi tulizopata msimu huu zimeleta neema ya mavuno lakini pia katika baadhi ya maeneo mazao yameharibika. Hivyo, niendelee kusisitiza kauli

ya Waziri wa Kilimo wakati akiwasilisha Hoja ya Wizara yake kuwa hali ya chakula nchini imeendelea kuimarika. Kwa msingi huo, hatutaraji kuwa na upungufu wowote wa chakula kwa msimu ujao. Muhimu kwetu ni kuongeza umakini wa matumizi kwa kuweka akiba ya chakula ili kitosheleze mahitaji ya familia hadi msimu ujao.

MAPAMBANO DHIDI YA HOMA KALI YA MAPAFU COVID 19

37. **Mheshimiwa Spika**, mwezi Machi, 2020, baada ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kutangaza kuwa COVID 19 ni janga la dunia, ambako nchi nyngi duniani zilipata maambukizi makubwa, Tanzania tulitangaza kisa cha kwanza tarehe 15 Machi, 2020.

38. Nchi nyngi duniani zikiwemo nchi za Bara la Afrika ugonjwa huu ulianza kuingia. Kila nchi illichukua hatua kadhaa za kudhibiti maambukizi zikiwemo watu kutotoka ndani ya nyumba zao “*Lockdown*”, kuzuia mikusanyiko kwa kufunga mashule, vyuo, michezo, aina zote za usafiri wa ndani na nje, maeneo ya Ibada na shughuli za uzalishaji maeneo ya kazi, viwanda, n.k. vilifungwa.

39. Tanzania nasi tulianza kuchukua hatua kadhaa ili kukabiliana na maambukizi kwa kuunda Kamati 3 za ngazi ya Mawaziri, Watendaji na Wataalam wa Afya kwa lengo la kufanya tathmini ya hatua za kuchukua ili kupunguza maambukizi na kulinda anguko la kiuchumi.

40. Hatua zilizochukuliwa ni kupunguza misongamano kwa kufunga shule, vyuo, mikutano, kunawa maji, matumizi ya vitakasa mikono na kuвая barakoa.

41. **Mheshimiwa Spika**, siku ya tarehe 22 Machi, 2020 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa Jijini Dodoma na tarehe 03 Mei, 2020 akiwa Chato aliwataka Watanzania kuwa watulivu waondoe hofu ya ugonjwa huu na ni ugonjwa kama magonjwa mengine, kama vile Malaria, UKIMWI, Kifua Kikuu, n.k. na kuwataka Watanzania kuchukua tahadhari na

kuendelea na shughuli za uzalishaji mali, kufanya kazi ofisini, viwandani, mashambani na kutofunga nyumba za Ibada.

42. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alihutubia tena Taifa tarehe 16 Aprili, 2020 kwa kutoa maelekezo na kusitiza yafuatayo:

Mosi: Aliwasihii Watanzania kuondoa hofu kwa kuwa Mungu yupo nasi na hivyo, waendelee kuchapa kazi ili kunusuru uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla na kuzingatia kanuni za afya.

Pili: Watanzania watumie siku tatu kumuomba na kumlilia Mwenyezi Mungu kwani Mungu yu pamoja nasi na atatusikia huku akiendelea kusimamia kauli yake ya kuwataka Watanzania wafanye kazi kwa bidii na kumtegemea Mungu bila kujali kauli za kebehi na ukosoaji kutoka pande mbalimbali za dunia;

Tatu: Alihimiza Watanzania kumtegemea Mwenyezi Mungu na kwamba Mwenyezi Mungu pekee ndiye atakayetuvusha na kutuepusha na janga hili;

Nne: Aliwahimiza Watanzania kutopuza umuhimu wa tiba mbadala katika mapambano dhidi ya COVID-19. Kauli hii, imekuwa chachu katika kuimarisha tafiti za dawa za asili ambazo zimekuwa na mchango mkubwa katika kupambana na maradhi mbalimbali ikiwemo COVID-19; na

Tano: Tarehe 20 Mei, 2020 akiwa Singida, aliwaomba Watanzania watumie siku tatu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa maajabu aliyoyafanya kwa Taifa letu kwa kutuepusha kusambaa kwa virusi vyta COVID-19.

43. Mheshimiwa Spika, hali iliyoko sasa, ni kuwa maambukizi yamepungua na wagonjwa wamepungua hospitalini. Kama kuna anayestahili sifa ni Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msimamo wake usiotetereka na maono ya mbali aliyokuwa nayo yamekuwa chachu katika kupunguza maambukizi ya

COVID-19 na kulinda uchumi wa Nchi. Mheshimiwa Rais ameifanya Tanzania kuwa ya kupigiwa mfano duniani kwa namna alivyoshughulikia ugonjwa huu.

44. **Mheshimiwa Spika**, pongezi maalum kwa Viongozi wa dini kwa namna walivyoshirikiana na waumini katika mapambano ya ugonjwa wa COVID-19. Wakati wote Viongozi hao wamekuwa wakiwapatia waumini (Watanzania) faraja pia na wagonjwa kwamba Mwenyezi Mungu atawaponya. Hatua hizo zimekuwa mhimili mkubwa wa upendo, umoja, mshikamano na ujasiri miongoni mwa Watanzania. Tunawashukuru sana.

45. **Mheshimiwa Spika**, taarifa iliyotolewa na Taasisi ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (Organisation for Economic Cooperation and Development - OECD) inabashiri kuwa kitendo cha kuwafungia watu ndani yaani "*Lockdown*" kumesababisha vifo kwa njaa na kusinyaa kwa uchumi wa nchi zilizoendelea kwa asilimia 2 kila mwezi.

46. **Mheshimiwa Spika**, hivi sasa, nchi nyingi zinakubaliana kuwa "*Lockdown*" si hatua sahihi ya kukabiliana na COVID-19. Vilevile, kisayansi inakadiriwa kuwa nchi ambazo ziliwafungia watu wake na mipaka yake zipo katika hatari ya kukumbwa na madhara makubwa ya ugonjwa huo pindi utakapotokea mlipuko wa pili na hata wa tatu.

47. **Mheshimiwa Spika**, kwa mantiki hiyo, mtizamo na hatua zilizochukuliwa na Tanzania katika kupambana na COVID-19 zinaonesha upekee tulionao kama nchi. **Serikali, inayo kila sababu ya kuwapongeza Watanzania ambao si tu walipokea maelekezo ya Serikali** lakini pia walifanya hivyo kwa uaminifu mkubwa na kwa hiari yao wenyewe bila kushurutishwa na mamlaka yoyote ya nchi.

48. **Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kuwashukuru wataalamu wetu wa afya kwa kuwashukuru wagonjwa wa COVID19. Wataalamu wetu hao, walitekeleza majukumu yao bila kujali hatari ya virusi hivyo kwa maisha yao na wapendwa wao. Vilevile, naishukuru sekta binafsi, mtu mmoja mmoja na

wadau wote ambao waliitikia wito wa Serikali kwa kutoa michango ya hali na mali katika kufanikisha vita dhidi ya COVID19 nchini. Kipekee, niwashukuru wamiliki wa viwanda ambao waliitikia wito wa Mheshimiwa Rais na kuanza kuzalisha vifaa kinga hapa nchini badala ya kuagiza nje waende kufanya hivyo.

49. **Mheshimiwa Spika**, ni matumaini yetu kwamba zile nchi zilizoondoa vizuizi sasa zinalo somo la kujifunza kutoka Tanzania. Aidha, suala la kudhibiti maambukizi ya COVID 19 litaendelea kuwa kipaumbele cha Serikali kwa sasa sambamba na malengo ya muda mrefu ya kumaliza ugonjwa huo hususan katika kipindi hiki ambacho Shirika la Afya Duniani (WHO) nalo limebainisha kwamba COVID 19 si gonjwa la kuondoka mara moja. Hivyo, watu na dunia kwa ujumla hatuna budi kujifunza namna ya kuishi na virusi hivyo kama ilivyo kwa UKIMWI na virusi vingine, huku tukifanya kazi ili kujiletea maendeleo.

50. **Mheshimiwa Spika**, tarehe 9 Juni Bunge lako Tukufu lilipitisha Azimio la kumpongeza na kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna alivyomudu kuivusha nchi katika janga la COVID-19. Waswahili husema ***mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni***. Katika hili, nami naomba niseme kidogo kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba zake zote zilizohusu ugonjwa huu ambapo alihimiza masuala muhimu kwa Watanzania katika kukabiliana na janga hili na zilitibu hofu kubwa iliyokuwa imetanda kwa Watanzania.

51. **Mheshimiwa Spika**, leo tunaona idadi ya wagonjwa wanaougua inapungua sana. Kwa mfano, taarifa ya leo, Jumatatu tarehe 15 Juni, 2020 kutoka katika Vituo vya kutolea huduma na Hospitali za Serikali na Binafsi nchini, inaonesha kuwa tuna wagonjwa 75 katika Mikoa 12 na Mikoa 14 haina wagonjwa ikiwemo Mkoa wa Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Mara, Manyara, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Simiyu, Songwe na Tabora. Pamoja na mwenendo huu,

ninawaomba wananchi wote kuendelea kuchukua tahadhari zote za kiafya na miongozo inayotolewa na Serikali.

52. Nampongeza sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu (Mb), kwa kazi kubwa aliyoifanya usiku na mchana kuhakikisha kuwa maambukizi yanapungua kwa kasi. Tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa hatua tuliyofikia. Pia, nawashukuru Katibu Mkuu, Mganga Mkuu wa Serikali na Watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa usimamizi wa tatizo hili na naamini mnaendelea vema. Hongereni sana.

SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA KATIKA BUNGE LA 11 (2015–2020)

53. **Mheshimiwa Spika**, wakati Bunge la 11 likielekea kuhitimisha shughuli zake, limefanikiwa kutekeleza masuala mbalimbali ikiwemo kujibu maswali na hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge; kujadili na kupitisha Miswada ya Serikali; Maazimio mbalimbali yenye kuhusisha Mikataba na Itifaki za Kikanda na Kimataifa; kupokea kauli za Serikali kuhusu ufanuzi wa mambo mbalimbali pamoja na kuunda Tume kwa ajili ya kufuatilia masuala muhimu yenye maslahi mapana kwa Taifa letu.

Maswali na Majibu

54. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi chote cha **Bunge la 11** linaloolekeea kuhitimisha uhai wake tarehe 16 Juni, 2020 jumla ya maswali ya msingi **3,962** yameulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Aidha, maswali ya nyongeza **9,563** yameulizwa kutokana na maswali ya msingi na kujibiwa na Serikali. Vilevile, jumla ya maswali **178** ya kawaida na ya **nyongeza 162** yameulizwa na Wabunge na kujibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia utaratibu wa maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu.

55. **Mheshimiwa Spika**, kupitia Mkutano huu wa Kumi na Tisa, jumla ya maswali **471** ya msingi na mengine **69** ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kupatiwa majibu na Serikali.

Miswada, Maazimio ya Bunge na Kauli za Serikali

56. **Mheshimiwa Spika**, hadi sasa Serikali imewasilisha jumla ya Miswada **60** ya Sheria ambayo imejadiliwa na kupitishwa na Bunge la 11 wakati Sheria 159 zimefanyiwa marekebisho. Vilevile, jumla ya Maazimio **38** ya Bunge yamejadiliwa na kuridhiwa na Bunge. Pia, **Kauli 20 za Serikali** zimetolewa ikiwa ni ufanuzi wa masuala mbalimbali yaliyowasilishwa na Mawaziri. Aidha, **Kamati Maalumu 4 za Bunge** zimeundwa katika **Bunge la 11** kwa ajili ya uchunguzi wa masuala mbalimbali.

57. **Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano huu, Bunge lako Tukufu lilipitisha kwa hatua zake zote Miswada ya sheria sita ambayo ni:

- (i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2020;
- (ii) Muswada wa Sheria ya Afya ya Mimea wa Mwaka 2020;
- (iii) Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu wa Mwaka 2020;
- (iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2020;
- (v) Muswa wa Sheria ya Fedha za Matumizi wa Mwaka 2020; na
- (vi) Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2020.

Maazimio ya Serikali

58. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Serikali iliwasilisha katika Mkutano huu Maazimio matano ya Bunge. Maazimio hayo yaliyordhiwa na Bunge ni kama ifuatavyo:

- (i) Azimio la Bunge la Kuridhia Mkatiba wa Kimataifa wa Utoaji Mafunzo na Vyeti vya Wafanyakazi wa Meli za Uvuvi wa Mwaka 1995 F;

- (ii) Azimio la Bunge la kuitaka Serikali Kutobadili Uamuzi wa Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi na Shughuli za Serikali;
- (iii) Azimio la Bunge la Kumpongeza Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Mafanikio ya Bunge la Kumi na Moja;
- (iv) Azimio la Bunge la Kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa namna alivyoliongoza Taifa katika Mapambano Dhidi ya Janga la Ugonjwa wa Corona (COVID-19);
- (v) Azimio la Bunge Kuhusu Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Kamati za Kudumu za Bunge

59. **Mheshimiwa Spika**, wakati wa Mkutano huu, Kamati za Kudumu za Bunge 15 ziliwasilisha Bungeni taarifa za mwaka za kazi. Taarifa hizo zilisheheni uchambuzi wa kina, maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa Serikali. Nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyevitii, Makamu Wenyevitii na wajumbe wote wa Kamati hizo kwa kazi nzuri waliyoifanya kuanzia maandalizi ya kazi za Kamati hadi kuwasilisha taarifa zao katika Bunge lako Tukufu.

UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2020/2021

60. **Mheshimiwa Spika**, leo hii tarehe 15 Juni, 2020 Waheshimiwa Wabunge **304** kati ya Wabunge **371** wamepitisha kwa kishindo Bajeti ya Serikali ya mwaka 2020/2021 ya jumla ya shilingi **trilioni 34.88**. Kati ya fedha hizo, shilingi **trilioni 21.98** ni za matumizi ya kawaida na shilingi **trilioni 12.90** ni za miradi ya maendeleo sawa na asilimia 37 ya bajeti yote.

61. **Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, kwa

kuwasilisha kwa umahiri mkubwa Hotuba ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2019 na Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021 na kuhitimisha hoja hiyo. Ninawapongeza pia Mheshimiwa Dkt. Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango; Katibu Mkuu; Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wa Wizara kwa kufanya kazi kwa ushirikiano. Matunda tunayaona.

62. **Mheshimiwa Spika**, kipekee niwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao ambayo imesheheni maoni na ushauri mzuri kwa Serikali wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara mbalimbali kwa mwaka 2020/2021 pamoja na mjadala kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2019 na Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021. Nalishukuru Bunge lako Tukufu kwa kupitisha Bajeti ya Serikali ya mwaka ujao wa fedha kwa kura nyingi za ndiyo.

63. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi shupavu wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imejipanga vizuri kutekeleza mipango yote iliyowekwa katika Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya mwaka 2020/2021. Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kuendelea kushirikiana na Serikali katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu. Aidha, natoa wito kwa sekta binafsi, wadau wa maendeleo na wananchi wote kuendelea kutoa ushirikiano katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

64. **Mheshimiwa Spika**, sambamba na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu, utekelezaji wa kazi za Serikali utaendelea. Hivyo, Watumishi wote wa Umma wanashauriwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi, uaminifu na kutoa huduma bora kwa wananchi kwa ufanisi na tija wakati wote. Aidha, katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021, napenda kutoa msisitizo katika maeneo yafuatayo:

Kwanza: Serikali itaendelea kutekeleza Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021 kwa kuzingatia athari na changamoto za ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona;

Pili: Serikali itakamilisha mchakato wa shughuli zilizobaki za maandalizi ya uchaguzi mkuu wa ubunge, urais na udiwani na kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kusimamia kikamilifu shughuli zote za uchaguzi huo kwa uhuru na haki;

Tatu: Serikali itatoa msukumo wa kipekee katika kukamilisha miradi ya kipaumbele na miradi ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa na Serikali ya awamu ya tano ili wananchi waendelee kupata huduma bora;

Nne: Serikali itashirikiana na sekte binafsi kuleta mageuzi kwa kutekeleza kwa kasi mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini (*yaani Blue Print for Business Environment*). Lengo ni kuhakikisha shughuli za uchumi na biashara zinashamiri na kuchangia kuondoa umaskini nchini; na

Tano: Serikali itaendelea kuboresha huduma za jamii pamoja na kuhakikisha kwamba ulinzi na usalama unaimarishwa.

UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020

65. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaendelea vema na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Hivi sasa, pamoja na mambo mengine Tume imekamilisha matakwa ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya kufanya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara mbili kati ya Uchaguzi Mkuu mmoja na mwingine.

66. **Mheshimiwa Spika**, zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura wa awamu ya kwanza lilianza rasmi tarehe 18 Julai, 2019 na kukamilika tarehe 23 Februari, 2020 kwa Nchi nzima wakati awamu ya pili lilianza tarehe 17 Aprili, 2020 na kukamilika tarehe 05 Mei, 2020.

67. **Mheshimiwa Spika**, takwimu za awamu ya kwanza na ya pili, zinaonesha kuwa wapiga kura wapya walioandikishwa ni **7,326,552**, wapiga kura waliloboresha taarifa zao ni **3,548,846** na wapiga kura **30,487** wamepoteza sifa. Hadi sasa jumla ya Wapiga Kura halali kwa mwaka 2020 ni **29,804,992** ikilinganishwa na Wapiga Kura **23,161,440** wa mwaka 2015.

68. **Mheshimiwa Spika**, Tume inaendelea na uchambuzi wa taarifa za Wapiga Kura waliojiandikisha na baada ya zoezi hilo kukamilika, Daftari la mwisho litakalotumika katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 litaandaliwa na kuwekwa wazi.

69. **Mheshimiwa Spika**, niwasih i viongozi na wanachama wa vyama vyote vya siasa na wananchi kwa ujumla kuendelea kulinda amani yetu na kuendeleza mshikamano katika kipindi hiki na wakati wa uchaguzi mkuu. Natoa wito kwa Viongozi wa Vyama vya Siasa na Wadau wengine wa uchaguzi kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo katika uendeshaji wa shughuli za uchaguzi.

MICHEZO

70. **Mheshimiwa Spika**, kwa miaka hii mitano tunaendelea kuonesha upekee wa Mheshimiwa Rais wetu mbali ya kazi kubwa ya ujenzi wa miradi ya huduma za jamii, pia Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli amehamasisha masuala ya kijamii ikiwemo michezo.

71. **Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Rais ni mwanamichezo na msanii ambaye amekuwa hasiti kuonesha kipaji chake cha matumizi ya ala ya ngoma. Aidha, wote ni mashahidi kila awapo palipo na wasanii wanaotoa burudani ya ngoma huwa lazima akaungane nao na kuonesha umahiri wake kwa kupiga ngoma. Naye anaingia kwenye orodha ya washiriki waliochomoza kuwa maarufu kwa kumudu kutumia ala hiyo kwa kipindi hiki cha miaka mitano.

72. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa michezo na burudani tunao Watanzania walifanya vizuri kwenye eneo hilo katika

kipindi cha miaka mitano. Ikumbukwe kuwa ninaowazungumzia hapa ni baadhi ya wanamichezo na wasanii waliollbeba Taifa letu na kupeperusha vema bendera ya Taifa nje ya Nchi.

73. **Mheshimiwa Spika**, kwenye michezo ya riadha ni muhimu tukampongeza kijana wetu Alphonce Felix Simbu aliyetuletea medali ya fedha na kupeperusha vyema bendera ya Taifa kwenye mashindano ya mbio ndefu ya majeshi ya Dunia yaliyofanyika nchini China. Wanamichezo wengine waliochomoza nje ya nchi ni pamoja na Mwanamasumbwi Hassan Mwakinyo aliyemtwanga Sam Eggington wa Uingereza kwa *knock out* katika Raundi ya 2 na kupeperusha Bendera ya Taifa huko Uingereza.

74. **Mheshimiwa Spika**, eneo la sanaa na burudani hususan muziki wa *Bongo Flavour* limekuwa na mchangi mkubwa katika kuitangaza nchi yetu. Natumia fursa hii kuwapongeza vijana wetu ambaao ni wasanii wa muziki wa *Bongo Flavour* akiwemo Naseeb Abdul Juma maarufu kama *Diamond Platinumz* (Simba) pamoja na Rajabu Abdul Kahali maarufu kama *Harmonize* (Konde boy-Tembo). Tumekuwa tunashuhudia mapokezi wanayopata huko nje na wakitumbuiza muziki wetu na kupeperusha Bendera yetu kwenye mataifa mbalimbali. Wako wengine wengi kama Vanessa Mdee, Raymond Mwakyusa (Rayvanny), Ali Kiba (King Kiba), n.k.

75. **Mheshimiwa Spika**, mchezo wa soka nao licha ya kuwa ndio mchezo unaoongoza kwa wapenzi hapa nchini pia umetoa vijana wengi nje wanaoiletea sifa nchi yetu. Kwa upande huu wa soka, sote tumpongeze kijana wetu Mbwana Samata anayelitangaza Taifa letu katika ligi kuu ya Soka nchini Uingereza kwenye Timu ya *Aston Villa*. Tunawapongeza sana wachezaji wetu kama Simon Msuva, Hassan Kessy, Abdi Banda, Kelvin John, n.k. ambaao wanatangaza Taifa letu nje ya nchi. Ni matarajio yetu wapo watakaofuata nyayo zao ili kuliletea sifa Taifa letu.

76. Soka la Vijana nalo limeendelea kuimarika ambapo Timu za Soka za Vijana wa umri wa miaka 17 na 20 na Timu ya Wanawake – *Twiga Stars*, zimefanya vizuri katika michezo ya kimataifa na kuleta makombe hapa nchini.

77. **Mheshimiwa Spika**, *Taifa Stars* nayo katika kipindi cha miaka 39 imeweza kucheza AFCON mara ya pili katika kipindi cha miaka mitano hii.

78. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki cha miaka mitano, tumeshuhudia Klabu kongwe ikipeperusha Bendera ya Taifa nje ya nchi na ikitutoa kimasomaso katika medani za soka la kimataifa kwa kuweka historia ya Taifa letu kwa kucheza hatua ya robo fainali ya Mabingwa wa Afrika baada ya kufuzu hatua ngumu ya makundi nayo si nyingine bali ni *SIMBA SPORTS CLUB*, Klabu ambayo inakaribia kutangaza ubingwa wa Tanzania kwa Ligi ya ndani kwa mara ya tatu mfululizo ikiwa haijakamilisha michezo 9.

79. **Mheshimiwa Spika**, kama inaweza kutangaza ubingwa ikiwa haijamaliza michezo yote hiyo nini faida ya mkuki. Mheshimiwa Spika, ili kuonesha ubora wa Timu mchezaji anayeongoza kwa kufunga magoli mengi ni Medie Kagere aliyefunga **magoli 19** kutoka *SIMBA SPORTS CLUB*na wachezaji wanaofuatia kwa magoli mengi ni Reliants Lusajo wa Namungo FC **magoli 11**; Yusuph Mhilu wa Kagera Sugar **magoli 11**; Bigirimana Bleiz wa Namungo FC **magoli 10** na Paul Nonga wa Lipuli FC **magoli 10**. Hatua hii haiwezi kufikiwa na Timu yoyote kwa kuwa mikuki mingi ni butu. Mkuki wenye ncha kali uko *SIMBA SPORTS CLUB*.

HITIMISHO

80. **Mheshimiwa Spika**, nihitimishe hotuba yangu kwa kumshukuru tena Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake makini uliolipatia Taifa letu mafanikio makubwa katika kipindi kifupi cha miaka mitano. Watanzania wanakuhitaji kuliongoza Taifa hili. Nitoe wito kwa Watanzania kujitokeza kwa wingi ili tumpigie kura za kutosha.

81. **Mheshimiwa Spika**, naomba kwa mara nyingine niwashukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhi Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia vema utekelezaji wa llani ya CCM.
82. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, namshukuru sana Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ushirikiano ambao amekuwa akinipatia wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.
83. **Mheshimiwa Spika**, narudia tena kukushukuru na kukutakia afya njema. Namshukuru pia Mheshimiwa Prof. Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania kwa ubunifu wake wa kuendesha shughuli za Mahakama kwa njia ya mtandao katika kipindi cha ugonjwa wa COVID-19. Namshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Eliezer Feleshi, Jaji Kiongozi, Waheshimiwa Majaji wote, Mahakimu na watendaji wote wa mhimili wa Mahakama kwa kazi nzuri ya kuwahudumia Watanzania.
84. **Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kuwashukuru tena Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Makatibu Wakuu pamoja na Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Wafanyakazi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.
85. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuwashukuru washirika wa maendeleo zikiwemo Nchi rafiki, Taasisi na Mashirika ya Kimataifa, madhehebu ya dini na mashirika yasiyo ya kiserikali, kwa kuendelea kuunga mkono juhudzi za Serikali katika kujenga uchumi wa viwanda na kuilettea Nchi yetu maendeleo. Ninawashukuru pia, Viongozi wote wa dini na wanahabari wote kwa ushirikiano mkubwa waliounesha kwa Serikali katika kipindi chote cha miaka mitano. Mchango wao umekuwa muhimu katika kuiwezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa kimaendeleo kulingana na mipango tuliojiwekea.

86. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki cha miaka mitano tumekuwa karibu sana na kupata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi wa Chama cha Mapinduzi katika ngazi zote. Hivyo, Mheshimiwa Philip Mangula, Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa pamoja na Dkt. Bashiru Ally, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi; nawashukuru sana Viongozi wangu wa CCM kwa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa llani ya Chama chetu.
87. **Mheshimiwa Spika**, kabla sjafika mwisho, niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano wao mkubwa katika kuishauri Serikali. Pia ninawashukuru Watumishi wote wa Bunge kwa huduma nzuri na msaada ambao wamekuwa wakitupatia kipindi chote tulichokuwa hapa Bungeni. Aidha, ninawashukuru Watendaji wote wa Serikali na Taasisi mbalimbali kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi, umahiri na ufanisi mkubwa na hivyo kufanikisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na Bunge bila kuwasahau Wanahabari kwa uchambuzi na kuuhabarisha umma na Madereva wote walituhudumia wakati wote wa shughuli za Bunge.
88. **Mheshimiwa Spika**, kipekee, nitumie nafasi hii kuishukuru tena familia yangu ambayo imeweza kunivumilia wakati mwiningi nilipokuwa nikitekeleza majukumu yangu ya kitaifa. Namshukuru sana mke wangu Mary Majaliwa na watoto wangu kwa kuniombea, na kunitia moyo wakati wote ninapokuwa nikitekeleza majukumu yangu.
89. **Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa majukumu ya Waziri Mkuu inawezekana kabisa kwa namna moja au nyingine niliwakwaza baadhi ya viongozi na watendaji, lakini yote ni katika kutekeleza majukumu ya Waziri Mkuu. Imani yangu ni kwamba tutaendelea kulijenga taifa kwa pamoja hususan katika kipindi hiki tunachoelekea kwenye kinyang'anyiro cha Uchaguzi Mkuu.
90. **Mheshimiwa Spika**, mwisho wa Bunge hili, ndiyo kiashiria cha Bunge Ijalo. Hivyo, nawaaga wote kwa kuamini kuwa wale waliofanya vema katika kipindi hiki wataaminiwa tena

na wananchi na kurejea kwenye Bunge iljalo. Hivyo, tuombeane heri ili kila mmoja wetu atakayechukua fomu za kugombea tena apate ushindi na fursa ya kuwatumikia wananchi.

91. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA AFYA NA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono kabisa na waheshimiwa Wabunge hote ahsante sana, ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa hotuba hii nzuri na muhimu sana. Hakika umetupitisha kwenye mambo mengi sana yanayoelekea kwenye kumaliza shughuli za Bunge la Kumi na Tisa na kesho atakapokuja Mheshimiwa Rais ye ye atahitimisha shughuli za Bunge la Kumi na Moja kwa hiyo shughuli za Bunge la Kumi na Tisa Mheshimiwa Waziri ametufungia hapa na ametoa hoja mmeiunga mkono japo hakusema hamehaiisha hadi lini? Itabidi waheshimiwa mnipe tarehe labda mwezi ujao tukutane tena lakini najua kafanya hivyo ahsante sana. (*Makofi*)

Niseme kidogo jambo la kwanza ambalo ningependa kusema ni ahsanteni sana, ahsanteni sana! Ahsanteni sana, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Nilitamani sana nimpe kila mmoja wenu zawadi siku ya leo iwe chini ya kitu cha kila mmoja wenu nikafikiri sana nikapata tabu niwape zawadi gani nikampigia simu rafiki yangu Mheshimiwa Joseph Kasheku Msukuma, kwamba niwape Wabunge zawadi gani akaniambia wape kila mmoja chini ya meza kila mpatie faru John moja ile kubwa. (*Makofi/ Kicheko*)

Nikasema huna maana msukuma wewe ushauri huo sijazingatia. Mheshimiwa Waziri Mkuu Kasim Majaliwa Majaliwa umekuwa kaka yangu, umekuwa mwenzangu, umekuwa kiongozi wangu, kwa kuwa mkuu wa shughuli Bungeni tusingewenza kufika popote bila ushirikiano wako

nasema ahsante sana, ahsante sana Mungu akubariki sana na nitashangaa kusikia wananchi wa Ruangwa wanavunja utamaduni wa *commonwealth* ambapo Waziri Mkuu jimboni kwake hapingwi ndani ya chama chake hiyo haijawahi kusikika sasa hata kwenye Chama Cha Mapinduzi vitu vingine watu wawe wanaambiwa hatutarajii hilo. (*Makofii*)

Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu mawaziri, waheshimiwa Wabunge wenzangu wote watanzania wenzangu katika maisha yangu katika kijana sikuwahi kuwaza wala kuota, wala kufikiri kwamba siku moja nitakuwa mwanasiasa, wala kwamba siku moja ninaweza kuwa mbunge, na kuwa Spika ndiyo kabisa haikuwahi kufikirika hata mara moja. Ni Mungu tu Mungu wa ajabu ambaye katika uumbaji wake hutujua na wakati mwingine hutupangia safari kadri anavyoona ni vema. (*Makofii*)

Kwa vile sikufikiria haya na leo nimefika hapa nilipo niseme ahsanteni wana Kongwa, ahsanteni chama changu cha Mapinduzi na ahsante sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Waheshimiwa Wabunge uwezi ukawa Spika wa Bunge tena ukafanikiwa kama huna *strong support* ya Rais haiwezekani! Rais asipokuunga mkono ufiki popote huo ndio ukweli wenyewe. Kwa hiyo, niseme ndugu zangu kuna wakati wanani pima hivi maji nilikuwa na *support, support* na ndiyo maana tumefika hapa leo. (*Makofii*)

Kwa hiyo, namshukuru mno mno. Huu ni mwaka wa tano ambao nimekaa na kusimama kwa nyakati mbalimbali kwenye kiti hiki mbele yenu kwa pamoja tukiendesha mambo ya Bunge na kwa hiyo, kabla ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt John Pombe Joseph Magufuli hajaja hapa kesho ili kufunga Bunge hili la kumi na moja nimeona vema niongee nanyi kiasi tu kwa nia ya kuagana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Mawaziri, Wabunge wenzangu na watumishi wa Bunge kusema kwa kheri si jambo rahisi sana hapa Bungeni nimetumia sehemu muhimu sana ya maisha yangu takribani miaka 20 sasa nimekutana na watu wengi wema sana na nimekutana na

changamoto nyingi sana maana idadi yetu inakaribia watu 400, watu 400 ni wengi sana mwalimu wangu mmoja enzi hizo akiniambia darasa moja huwa linakadiri wanafunzi 40 hivi, anakaniambia katika wanafunzi 40, hao hao 40 kuna watu wanatabia za Askofu, au wanatabia za Mufti, kuna watu wakawaida, katika ya 40 hawa kuna watu watakuwa walevu siku mmoja, katikati ya 40 hao kuna wezi uenda hata kuna majambazi katikati ya watu 40 hawa, unaweza ukakuta tabia za ajabu ajabu sembuse watu 400 ni watu wengi kwa hiyo, hapa ni tabia karibu zote za mwanadamu zipo.

Kwa hiyo, imekuwa ni fadhili tu kwangu kuhudumu kama kiongozi kuhudumu kwa miaka hii mitano sasa ahsanteni sana kwa kuniamini, na kwa ushirikiano mlionipa. (*Makofi*)

Naamini sote tutatembea kifua mbele kwa mafanikio ya Bunge la Kumi na Moja kwasababu bila msaada wenu tusingefika hapa, baadhi waniliuliza hasa waandishi wa habari hivi karibuni kuwa unajisikiaje kumaliza salama Bunge hili la Kumi na Moja jibu langu limekuwa na leo bado liko hivyo hivyo, kwamba Sifa apewe Bwana wa Majeshi. (*Makofi*)

Nimetokea Kongwa kuja hapa Bungeni huko ndiko nilikozaliwa na kukulia na kukulia ni eneo lenye nyanda kame lakini nyanda bora kwa malisho ya mifugo. Mkoa wa Dodoma ni Mkoa amba kwa kawaida huwa na mvua chache na kwa hiyo, maisha yake ya wananchi huwa na changamoto za kipekee sana na moja ya changamoto kubwa huwa ni masikini nakumbuka miaka niliyosoma, Shule ya msingi miaka ya sabini, shule ya msingi ya Sagara huko kwetu Kongwa nikitokea nyumbani kwetu kijijini Laikara hadi shulen. Kutoka kijijini kwetu hadi shulen ilikuwa kilometra 8. Kwa hiyo, tulikuwa tunasoma siku tano kwa wiki Jumatatu mpaka Ijumaa. Nilikuwa nikitembea kilometra 8 kwenda na kilometra 8 kurudi nyumbani, kilometra 16 kwa siku moja. $16 \times \text{siku } 5 = \text{kilometra } 80$.

Nimekulia maisha ya shida, dhiki na miaka mingine tukiwa na janga la njaa Mkoani Dodoma nilipitia maisha hayo. Nikiwa mdogo nililala kwenye kitanda cha kamba,

nillalilia ngozi ya ng'ombe na kwenye nyumba ya tembe na nilichunga sana ng'ombe. Lakini baadaye nikakua kwa kudra ya Mwenyezi Mungu nimesoma Vyuo vingi tu mbalimbali ndani na nje ya nchi. Lakini nakumbuka nilipokuwa Chuo cha Mweka Moshi, *College of African Wildlife Management* ambako tulikuwa wanafunzi wa kutoka nchi zote za Kiingereza Africa, South Africa, Zambia, Zimbabwe, Malawi wote Namibia, Egypt tulikuwa nao pale Nigeria, Ghana, *Sierra Leone everywhere*. Sudan, Uganda, Kenya *English Scheme* zote tulikuwa pale.

Nilikuwa mmoja wa wanafunzi maskini sana chuoni, baadhi ya likizo sikuwa na nauli ya kuweza kutoka kule Moshi kurudi Dodoma Kongwa. Kwa hiyo, tukakubaliana na Mkuu wa Chuo wakati huo kwamba niwe nabaki kutumikia tumikia pale kufyeka fyeka majani, kupanga panga vitabu stoo na kazi zingine ndogo ndogo. Wakati mwengine kuwasaidia Walimu katika *research project* zao, kukusanya *data* na unaweza ukakumbuka, nakumbuka jinsi ambavyo wakati wa likizo unapofika inabidi mimi nisiende nyumbani. Wenzangu wanapopanda magari kuondoka wengine wanatoka nchi za mbali wakienda *KIA* kupanda ndege kuondoka kwenda kwao na Watanzania baadhi yetu tuliokuwepo wachache wakipanda mabasi kuondoka. Mimi nilikuwa najificha kwa aibu ya kutokuulizwa swali moja tu na wenzangu, wewe kwa nini huendi kwenu? Kwasababu siwezi kujieleza siendi kwa sababu sina nauli. Mimi ni maskini!

Na kumbukeni nyumbani nilikuwa mtoto wa pekee wa mama yangu mmoja tu. *How I missed my mother!* Tunapomaliza Bunge hilli natamani ni-revenge sasa nirudi akanipokee lakini bahati mbaya Mungu ameshamchukua. Kwa hiyo, wakati mwengine mnisamehe huwa Napata hasira ninapokutana na mtu mjinga. (*Makof!*)

Ndio maana inapotokea na watu kama wakina Mheshimiwa Suzane yaani ananipa taabu tu kwasababu tumeshapita huko tumeshapata tabu sisi. Kama ni huo ukamanda sisi tumepita huo ukamanda kwa wiki kilometra

80. Wewe umekanyakaga 80 wewe kwa wiki, utakuwa kamanda kunizidi kweli.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wenzangu nyumba hii ni nyumba ya Watanzania mahala ambapo wananchi wanaiambia Serikali yao nini wanataka. Sheria ambazo wananchi wanazitaka zinatungwa hapa, mipango ambayo inaidhinishwa na Wananchi kwa maana ya nyinyi wawakilishi wao inapitishwa hapa. Bajeti ambayo inaenda kuhudumia wananchi inachujwa na kuitishwa hapa, Serikali inauliza maswali hapa, kwa maneno ya Katiba Serikali inasimamiwa hapa. Hiyo ndio kazi ambayo tumefanya kwa miaka mitano. (*Makofi*)

Nirudie kusema Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni wewe na timu yako ya Mawaziri wote tunasema ahsanteni sana! Ahsanteni sana, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Tunapofikia hapa mwisho nyinyi Wabunge mnaondoka, mwenzenu mtaniacha hapa hadi Novemba baada ya uchaguzi mkuu. Ili baada ya hapo kama tunamkabidhi mwenzetu mwingine haya, kama tunaendelea sisi haya. Kwasababu katika Uongozi hatuachi ombwe. Kwa hiyo, nitaendelea kuwepo kuandaa Bunge hilo la Kumi na Mbili ambalo naamini nyote mnarudi tuweze kuendelea kuitumikia nchi yetu. (*Makofi*)

Ahsanteni sana Kambi Rasmi ya Upinzani nawashukuruni sana, tumeshirkiana kwa mengi. Ahsante sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Mheshimiwa Rais, wabeja sana Ntemiwisee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Makamu wa Rais Samia Suluhu ahsante, Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Dkt. Shein ahsante, Mheshimiwa Jaji Mkuu Professa Ibrahim Juma ahsante, Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi ahsante, Wakuu wote wa Vyombo vyaa Ulinzi na Usalama ahsanteni sana. (*Makofi*)

Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wote ahsanteni sana, Makatibu Wakuu wote, Naibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na wengine wote Wizarani ahsanteni sana. Ahsante sana Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Bashiru Ally na Sekretarieti yote ambao ninyi ndio wenye llani ya Uchaguzi ambayo tumekuwa tukiitekeleza hapa. Ahsanteni sana Watanzania wote mlietuombea kwa namna mbalimbali, mlipiga magoti kutuombea, mlipiga simu kunitia moyo, mlietuombea dua, mliwasiliana nasi, ahsanteni sana. (*Makofii*)

Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Naibu wangu na Msaidizi wangu, ahsante sana. Ahsante sana Mtemi Andrew Chenge, Mwenyekiti kwa kunisaidia. Ahsante sana Mheshimiwa Najma Giga, Mwenyekiti, kwa kunisaidia. Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kunisaidia sana. Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagalgai na Wasaidizi wako wote, Watumishi wa Bunge ahsanteni sana, sana, sana. Bunge *Sports Club* chini ya Mheshimiwa Ngeleja, ahsanteni sana, sana, sana, mmetupeleka mpaka Misri, tunawashukuruni sana. (*Makofii*)

Nawashukuru sana timu yangu ya Wasaidizi wote wa Ofisi Binafsi ya Spika. Ahsanteni sana Wana-Kongwa kwa kuvumilia kutokuwepo kwangu mara kwa mara na sasa kuanzia kesho nakuja. (*Makofii*)

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, kwa miaka mitano sijawahi kuwaleta rafiki yangu kipenzi, rafiki yangu namba moja. Leo nimekuja naye. Ahsante sana mke wangu, Dkt. Fatma, lakini amekuja na wanetu; wanangu nanyi simameni. Huyu mke wangu ni Daktari wa binadamu na huyo kijana wetu wa kiume naye anasomea Udaktari wa binadamu huko China. (*Makofii*)

Mama umenivumilia sana kama mnavyojua nilipata *challenge* kubwa sana ya kuugua; na mama huyu alisimama kidete. Hata nilipokuwa kule India /ICU, kuna wakati alikuwa analala hapo pembeni ya kitanda changu masaa 24 amekaa kwenye kiti. Nilikuwa naumwa sana kiasi ambacho

kwa kawaida haruhusiwi mtu asiyekuwa mhudumu wa hospitali ile kwa maana ya wodi ile maalum akakaa mle ndani, lakini ilibidi yeye aruhusiwe kukaa mle ndani nami akilala kwenye kiti masaa 24 kwa siku kadhaa. Ulipata taabu sana. (*Makofi*)

Pia kwa sababu ni daktari, amekuwa ni daktari wangu muda wote ndiyo maana mnionia hapa vile nilivyo. Hakika wewe ni mke mwema. Kwa kukopa maneno ya Mheshimiwa Dkt. Mpango, ahsante sana kwa kunipa raha. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, hatujasikia huku nyuma. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Nakushukuru, maana hata suti ya leo umeninunulia wewe. Ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, bila kuwapotezea muda zaidi, naomba shukrani zote hizi tumpelekee Mungu wetu kwa rehema zake na neema zake. Kwa herini ndugu zangu, Mungu awabariki sana waumini wote, enendeni kwa amani. (*Makofi*)

Ahsante sana. Katibu.

NDG. NENELWA MWIHAMBI – KATIBU MEZANI: Wimbo Maalum wa Kuwaaga Waheshimiwa Wabunge.

SPIKA: Wimbo Maalum kutoka Kwaya ya Bunge. Wimbo Maalum wa kuwaageni Waheshimiwa Wabunge. Watumishi wetu wametuandalia Wimbo Maalum.

WIMBO MAALUM WA KUWAAGA WABUNGE ULIIMBWA NA KWAYA YA BUNGE

Mwanzo wa safari hatukujua kama tutafika salama, Pongezi twatoa kwa viongozi wetu wa Bunge tunasema hongera,

Pongezi kubwa kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Mheshimiwa Job Yustino Ndugai kwa uongozi wake uliotukuka,
Amekuwa nahodha shupavu, safari yetu imekuwa nzuri,
Ushirikiano wake na Bunge leo tumefika tulipo.

Kwa muda wa miaka mitano,
Mafanikio tumeyaona,
Ndani ya Bunge la Kumi na Moja kweli tumeona,
Kwa weledi pia na ustadi, juhudhi, maarifa, mabadiliko tumeyaona.

Bunge limefanya mambo makubwa sana na yakukumbukwa,
Ziara nydingi za Kamati za miradi yote kweli zilifanyika,
Kukagua miradi wakaweza kujifunza mambo mengi na kushauri Serikali ilivypaswa.

Kwa maono yake Spika Ndugai, twakupongeza,
Kamati za Madini ziliundwa, hongera sana,
Matokeo ujenzi wa ukuta,
Ili kulinda madini yetu, tusiibiwe,
Kule mereraani mambo safi, hongera sana,
Kwa maoni yake Spika wetu, twakupongeza
Sasa Bunge limepiga hatua

Hakuna kutumia karatasi tena, teknolojia sasa kutumika,
Kweli twasema hongera, Wabunge wote tunawapongeza

Hakuna kutumia karatasi tena, teknolojia sasa kutumika,
Kweli twasema hongera, Wabunge wote tunawapongeza

Miswada mbalimbali ya sheria, ilipitishwa,
Sheria za madini ziliwekwa, zikawezesha,
Kwa hakika kuleta faida kubwa.

Hongera Wabunge Wanawake, kujenga shule,
Kwa umoja wenu mmeweza, hongera sana,
Pia hongera kwa Bunge letu kwa zahanati,
Mmefanya kujali Watanzania

Hakika leo ile siku imefika ya kuagana na Waheshimiwa,
Wabunge wote kwaheri, tunawatachia safari njema

Hakika leo ile siku imefika ya kuagana na Waheshimiwa,
Wabunge wote kwaheri, tunawatachia safari njema.

*(Waheshimiwa Wabunge Wote Walisimama na Kucheza
Wakati Wimbo Ukiimbwa)*

SPIKA: Naomba tukae Waheshimiwa Wabunge.
(*Makofi*)

Ahsanteni sana Watumishi wa Bunge kwa kutuandalia
zawadi hii Waheshimiwa Wabunge wote ya kutuimbia wimbo
wa kutuaga, tunashukuru sana, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Basi kwaya yetu imetuhudumia sana katika kuimba
Wimbo wa Taifa hapa katikati na leo wametuimbia wimbo
wa kutuaga. Rafiki yangu Mheshimiwa Mkuchika alikuwa na
wasiwasi kidogo mwanzoni tulipoanza, lakini nimhakikishie
kwa kesho sasa Mheshimiwa Mkuchika, kesho ni *brass band*.
Maana kesho shughuli nzito sasa. (*Kicheko*)

Tunawashukuru sana sana sana, mwendelee
kuiboresha kwaya hii kwenye Bunge la Kumi na Mbili iwe ni
kwaya bora zaidi. Kwenye michezo ya Afrika ya Mashariki,
kwa sababu Uganda wana Kwaya yao ya Bunge na Kenya
wana Kwaya yao ya Bunge, naamini kwa sababu sasa na
sisi tunayo, tutaongeza *item* ya mashindano ya Kwaya za
Mabunge. Naamini tutachukua huo ushindi, maana yake
tuna wasanii wengine wamo ndani ya Bunge humu humu
ambao watawafundisha vionjo mbalimbali kiasi ambacho
tuna uwezo wa kushinda kabisa. Akina Vicky Kamata, akina
Mheshimiwa Mlata, ziko taarabu hapa. Ile ya Sugu na
mwenzake, ile hapana ile. (*Makofi/Kicheko*)

WABUNGE FULANI: Aaaaah! (*Kicheko*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Basi
kwa mambo yaliyopangwa hapa jioni ya leo yamekamilika,

niendelee kusisitiza tu kwamba tuwahi kwenye saa 3.00 kwa sababu mambo ni mengi, usije ukasukumwa sukumwa huko getini halafu ukasikia vibaya kidogo. Kuwahi ni vizuri, tuna ugeni mwingi sana, kwa hiyo, hapa patakuwa *tight* kidogo kuhakikisha kila mmoja wenu yuko salama na wageni wetu wako salama.

Kwa hiyo, Shughuli zetu zitaanza tu wakati wowote baada ya Mheshimiwa Rais kufika. Kwa jinsi hiyo basi, naomba nahirishe shughuli za Bunge hadi kesho *around* saa 4.00 hivi kwa maana ya hotuba kuanza hapa Bungeni, *around* hapo. Kwa hiyo, sisi tufike saa 3.00 ili wageni wetu wote waweze kuingia na kadhalika ili hotuba iweze kuanza mara moja.

Waheshimiwa Wabunge, basi naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa hizo nilizosema.

*(Saa 1.35 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 16 Juni, 2020 Saa Nne Asubuhi)*